ISO 9001:2015 Certified

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# RIPOTI KUU YA MWAKA YA UKAGUZI WA WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24



**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**MACHI 2025**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

NATIONAL AUDIT OFFICE
NAOT
ISO 9001:2015 Certified

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Mahakama, S.L.P. 950, 41104 Tambukareli, Dodoma. Simu: 255(026)2161200-9, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

**Kumb.Na.PA.319/421/01** **27 Machi 2025**

Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Ikulu,
S.L.P 1102,
1 Barabara ya Julius Nyerere,
11400 Chamwino,
**40400 DODOMA.**

**YAH: RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2023/24 kwa mujibu wa Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 34 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura 418.

Ripoti hii imeangazia matokeo ya ukaguzi na mapendekezo ya hatua stahiki za marekebisho zinazohusiana na kuchochea uwajibikaji katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali za umma.

Ninawasilisha,

Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

## Mamlaka

Majukumu na wajibu wa kikatiba wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yamebainishwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 na Kifungu Na. 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi, Sura 418.

**Dira**

Kuwa Taasisi yenye Kuaminika na ya Kisasa katika Ukaguzi wa Umma inayotoa Huduma za Ukaguzi za Viwango vya Juu zinazoimarisha Imani kwa Umma.

**Dhima**

Kutoa huduma za Ukaguzi zenye Kiwango cha Juu kwa njia za Kisasa zenye Kuimarisha Uwajibikaji na Uwazi katika Usimamizi wa Rasilimali za Umma.

**Kauli Mbiu**

Kuwa Taasisi yenye kuaminika na ya Kisasa katika ukaguzi wa umma

## Misingi ya Maadili

**Kufanya kazi kwa uhuru na bila upendeleo:** Sisi ni taasisi ya umma isiyo na upendeleo, inayotoa huduma za ukaguzi wa hali ya juu kwa wateja wetu kwa njia isiyo na upendeleo

**Kufanya kazi kwa uadilifu:** Tunazingatia na kudumisha viwango vya juu vya maadilina sheria katika utoajiwa huduma za ukaguzi

**Kufanya kazi kwa kuzingatia matokeo:** Tunazingatia katika kufikia malengo muhimu yenye kuaminika kwa wakati, usahihi na utumizi staiki

**Kufanya kazi kwa utaalam:** Tunatoa huduma za ukaguzi za hali ya juu kwa kuzingatia maarifa ya kitaaluma, ujuzi na mbinu bora

**Kufanya kazi kwa ubunifu na uvumbuzi** Tunahimiza, kuvumbua na kubuni mawazo ya kuongeza thamani kwaajili ya kuboresha huduma za ukaguzi

**Kufanya kazi kwa ushirikiano:** Tunathamini na kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje

## YALIYOMO

SURA YA KWANZA ........ 1
UTANGULIZI ........ 2
SURA YA PILI ........ 4
HATI ZA UKAGUZI ........ 5
SURA YA TATU ........ 8
MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA ........ 9
SURA YA NNE ........ 12
UTENDAJI WA KIFEDHA WA MASHIRIKA YA UMMA ........ 13
SURA YA TANO ........ 26
UFANISI WA MASHIRIKA YA UMMA KATIKA KUIMARISHA MAZINGIRA YA KIBIASHARA ........ 27
SURA YA SITA ........ 44
USIMAMIZI WA MAPATO NA FEDHA KATIKA MASHIRIKA YA UMMA ........ 45
SURA YA SABA ........ 55
USIMAMIZI WA MATUMIZI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA ........ 56
SURA YA NANE ........ 67
USIMAMIZI WA BAJETI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA ........ 68
SURA YA TISA ........ 78
USIMAMIZI WA MALI ........ 79
SURA YA KUMI ........ 86
USIMAMIZI WA MIKATABA NA UNUNUZI ........ 87
SURA YA KUMI NA MOJA ........ 106
TATHMINI YA UTAWALA NA USIMAMIZI WA VIHATARISHI ........ 107
SURA YA KUMI NA MBILI ........ 117
USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU ........ 118
SURA YA KUMI NA TATU ........ 130
USIMAMIZI WA KODI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA ........ 131
SURA YA KUMI NA NNE ........ 137
MWENENDO WA BENKI ZINAZOMILIKIWA NA SERIKALI, MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII NA TAASISI ZINGINE ZA KIFEDHA ........ 138
SURA YA KUMI NA TANO ........ 155
MAPITIO KATIKA SEKTA YA UTALII ........ 156
SURA YA KUMI NA SITA ........ 165
UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI ........ 166
SURA YA KUMI NA SABA ........ 175
TATHMINI YA UTENDAJI WA TAASISI ZA MAFUNZO, UTAFITI NA ELIMU YA JUU ........ 176
SURA YA KUMI NA NANE ........ 187
UFANISI WA MAMLAKA ZA UDHIBITI KATIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAO ... 188
SURA KUMI NA TISA ........ 202
UTENDAJI WA MASHIRIKA YA UMMA KATIKA SEKTA YA AFYA ........ 203
SURA YA ISHIRINI ........ 211
UFANISI KATIKA SEKTA YA MADINI, GESI NA MAFUTA ........ 212

# ORODHA YA MAJEDWALI


Jedwali Na. 1: Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa idadi kipindi cha miaka mitano mfululizo ..... 7
Jedwali Na. 2: Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi miaka iliyopita kwa mashirika ya umma 9
Jedwali Na. 3: Utekelezaji wa maagizo ya kamati ya kudumu ya bunge ............................10
Jedwali Na. 4: Mashirika yenye maagizo ya muda mrefu kutoka kwa kamati.......................10
Jedwali Na. 5: Mwenendo wa Hasara kwa mashirika ya umma kwa Kipindi cha Mwaka Mmoja hadi Mitatu.....................................................................................13
Jedwali Na. 6: Mwenendo wa mashirika yanayoendeshwa kwa kutegemea mikopo ...............22
Jedwali Na. 7: Mashirika ya umma yaliyoshindwa kutuma mchango wa asilimia 15 kwa miaka miwili mfululizo.......................................................................24
Jedwali Na. 8: Maelezo ya mabadiliko yaliyoidhinishwa...............................................28
Jedwali Na. 9: Tathmini ya Utendaji duni wa usafirishaji mizigo....................................31
Jedwali Na. 10: Gharama za kukodisha ndege kwa miaka sita mfululizo ............................35
Jedwali Na. 11: Miradi iliyochelewa kutekelezwa .....................................................36
Jedwali Na. 12: Kuchelewesha malipo ya fidia kwa waathirika wa mradi ...........................39
Jedwali Na. 13: Taarifa za nguzo zilizobaki zenye urefu wa mita 8 .................................40
Jedwali Na. 14: Mashirika ya umma ambayo yalikusanywa mapato nje mfumo wa GEPG .........49
Jedwali Na. 15: Mashirika yenye matumizi yasiyokuwa na tija mwaka 2023/24 ....................57
Jedwali Na. 16: Mashirika yenye matumizi yasiyostahili mwaka 2023/24 ............................59
Jedwali Na. 17: Mashirika yenye masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu kwa mwaka 2023/24 ...............................................................................61
Jedwali Na. 18: Mashirika ya umma yaliyofanya matumizi zaidi ya kiwango cha bajeti ...........71
Jedwali Na. 19: Mashirika ya umma yaliyokuwa na bakaa zisizotumika ndani ya muda uliowekwa .......................................................................................73
Jedwali Na. 20: Mashirika ya umma yenye ushiriki usioridhisha katika maandalizi ya bajeti .....75
Jedwali Na. 21: Mashirika ya umma yenye mapungufu katika matumizi ya mfumo wa bajeti wa Serikali ..................................................................................77
Jedwali Na. 22: Orodha ya mashirika ya umma yanayomiliki ardhi bila hatimiliki..................79
Jedwali Na. 23: Orodha ya mali zilizotelekezwa, zisizotumika, na zilizoharibika...................80
Jedwali Na. 24: Mali ambazo hazijakabidhiwa kwa Kampuni ya ndege ..............................83
Jedwali Na. 25: Orodha ya mashirika ya umma yaliyocheleweshewa bidhaa na huduma..........87
Jedwali Na. 26: Mashirika yaliyo na mikataba ya ununuzi yenye dhamana za utendaji zilizofikia ukomo wa muda...........................................................................91
Jedwali Na. 27: Orodha ya mashirika ya umma yaliyochelewesha Malipo ...........................94
Jedwali Na. 28: Mashirika yaliyofanya ununuzi nje ya mfumo.........................................95
Jedwali Na. 29: Orodha ya mashirika yaliyotumia mbinu za ununuzi zisizothibitishwa ...........97
Jedwali Na. 30: Mashirika yaliyonunua zaidi ya bajeti..................................................99
Jedwali Na. 31: Orodha ya mashirika yaliyogawanya ununuzi ....................................... 101
Jedwali Na. 32: Bakaa ya mikopo iliyotolewa kwa wafanyakazi walioacha kazi.................. 118
Jedwali Na. 33: Madai ya Wafanyakazi.............................................................. 119
Jedwali Na. 34: Makato ya kisheria ya wafanyakazi ambayo hayakuwasilishwa shilingi bilioni 11.89.............................................................................. 121
Jedwali Na. 35: Mashirika yaliyoajiri au Kuteua Wafanyakazi katika Nafasi za Kaimu Bila kupata idhini ya Katibu Mkuu- Utumishi............................................................. 123
Jedwali Na. 36: Maafisa waliokaimu katika nafasi zao kwa zaidi ya miezi sita ................... 124
Jedwali Na. 37: Maafisa katika nafasi ya kaimu au walioajiriwa bila sifa ......................... 126
Jedwali Na. 38: Upungufu wa watumishi 7,479 katika mashirika ya umma 20.................... 126
Jedwali Na. 39: Mashirika ya umma yaliotoa ajira za muda mfupi bila kuwa na muongozo ..... 127
Jedwali Na. 40: Mashirika ya Umma ambayo hayakutumia mfumo wa PEPMIS.................... 129
Jedwali Na. 41: Ucheleweshaji wa kulipwa kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ............. 131
Jedwali Na. 42: Malipo bila risiti za kodi za kielektroniki.......................................... 134
Jedwali Na. 43: Maelezo ya utendaji wa Benki ya Biashara dhidi ya kiwango cha udhibiti cha Benki.................................................................................... 140
Jedwali Na. 44: Mwenendo wa hasara wa TIB Rasilimali kwa kipindi cha miaka mitano ......... 144
Jedwali Na. 45: Orodha ya wadaiwa ambao michango yao haijawasilishwa ....................... 147
Jedwali Na. 46: Orodha ya vitega uchumi visivyozalisha mapato .................................. 151

Jedwali Na. 47: Maelezo ya shughuli zilizopangwa dhidi ya utendaji halisi ........................ 152
Jedwali Na. 48: Maelezo ya bajeti iliyoidhinishwa dhidi ya kilichotolewa na Serikali ............ 157
Jedwali Na. 49: Miradi iliyochelewa ................................................................. 157
Jedwali Na. 50: Maelezo ya maonesho yaliyopangwa kufanyika na yaliyofanyika ................. 159
Jedwali Na. 51: Miradi ya Maji Iliyocheleweshwa katika mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira Mwanza na Songea ........................................................................ 166
Jedwali Na. 52: Kucheleweshwa kwa Kutatuliwa kwa Malalamiko.................................. 168
Jedwali Na. 53: Ucheleweshaji wa Uunganishaji katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira ........................................................................................................ 169
Jedwali Na. 54: Ushauri na kozi fupi Halisi dhidi ya Lengo la Kila Mwaka .......................... 177
Jedwali Na. 55: Upungufu wa udahili wa wanafunzi .................................................. 181
Jedwali Na. 56:Taasisi zilizositishwa na kushushwa hadhi ........................................... 183
Jedwali Na. 57: Mwenendo wa uzalishaji mbolea nchini dhidi ya uagizaji kutoka nje ya nchi 2020/21 -2023/24.............................................................................................. 200
Jedwali Na. 58: Mwenendo wa ununuaji mbolea kutoka nje kwa Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja kwa miaka minne ............................................................................................ 201
Jedwali Na. 59: Madai ya bima ya afya yaliyokataliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima wa Afya ... 205
Jedwali Na. 60:Oda za Hospitali zilizoshindwa Kutekelezwa na Bohari Kuu ya Dawa............ 207
Jedwali Na. 61: Miradi ambayo upembuzi yakinifu haukufanyika.................................... 216
Jedwali Na. 62: Utendaji Duni wa Mkandarasi wa Uchimbaji Madini ................................ 219
Jedwali Na. 63: Asilimia ya Wafanyakazi wa Kitanzania dhidi ya Wageni katika Malipo ya Mishahara ........................................................................................................ 220
Jedwali Na. 64: Maelezo ya Tofauti Zilizozidi Kiwango Kinachokubalika cha asilimia 1.......... 226
Jedwali Na. 65: Asilimia ya Kuongezeka kwa Matumizi kutoka Kiwango rejea au msingi ........ 227

## ORODHA YA VIAMBATISHO


Kiambatisho Na. I: Hati za ukaguzi na mahitimisho ya uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake na sheria ya bajeti na kanuni zake kwa mwaka wa fedha 2023/24 229
Kiambatisho Na. II: Mashirika ya Umma yasiyo na Ukwasi wa kulipa madeni ya Muda Mfupi 237
Kiambatisho Na. III: Mashirika yaliyopata Nakisi mwaka mmoja hadi miaka mitatu 239
Kiambatisho Na. IV: Miradi ya Ubia iliyosimama 240
Kiambatisho Na. V:Mshirika ya Umma yenye madai ya muda mrefu Sh. trilioni 3.58 243
Kiambatisho Na. VI: Mashirika ya umma yenye madeni yanayodaiwa kwa muda wa zaidi ya miezi 12 kwa mwaka 2023/24 245
Kiambatisho Na. VII: Fedha za bajeti zilizotolewa kulinganisha na fedha zilizoidhinishwa 247
Kiambatisho Na. VIII: Makusanyo pungufu yatokanayo na vyanzo vya ndani 249
Kiambatisho Na. IX:Orodha ya mashirika yenye mali na bidhaa zilizokaa muda mrefu bila kuuzwa 251
Kiambatisho Na. X: Taasisi za umma zisikuwa na Bodi za Wakurugenzi 252
Kiambatisho Na. XI: Mapungufu katika uendeshaji wa Shughuli za Bodi ya Wakurugenzi 253
Kiambatisho Na. XII: Kushindwa kutumia mifumo ya Tehama ya kielektroniki kwa ufasaha 254
Kiambatisho Na. XIII: Mashirika Yaliyokuwa Na Nyenzo Duni Za Kusimamia Shughuli Za Uendeshaji 256
Kiambatisho Na. XIV: Mashirka ya umma yanayoendeshwa bila kuwa na miongozo iliyoidhinishwa na katibu mkuu Ofisi ya Rais-Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora 257
Kiambatisho Na. XV: -Mashirika ya Umma ambayo hayakutekeleza mfumo wa HCMIS 258
Kiambatisho Na. XVI: Kodi ambazo Hazijawasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania Shilingi bilioni 9.65 259
Kiambatisho Na. XVII: Upungufu wa huduma za majisafi (Mita za ujazo kwa siku) 260
Kiambatisho Na. XVIII: Upotevu wa maji 261
Kiambatisho Na. XIX: Mwenendo wa madai katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira 261
Kiambatisho Na. XX: Uwiano hafifu kati ya walimu na wanafunzi 262
Kiambatisho Na. XXI: Kutoa programu ambazo hazijaidhinishwa na kuchelewesha utekelezaji wa programu zilizoidhinishwa 263
Kiambatisho Na. XXII: Malengo na Uzalishaji Halisi wa Kiwanda cha Madawa Keko 266



# SALAMU KUTOKA KWA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Ninayo furaha kuwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni 2024 ambayo inajumuisha mashirika ya umma 217.

Ninaipongeza Serikali, inayoongozwa na **Mh.Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika kuendeleza uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma. Pia, nashukuru ushirikiano wa menejimenti za mashirika ya umma katika kutoa taarifa na ufafanuzi muhimu kwa ajili ya kuandaa ripoti hii ya ukaguzi.

Matokeo ya ukaguzi katika ripoti hii yanalenga kuimarisha uwajibikaji, utawala bora, na uwazi katika usimamizi wa rasilimali za umma. Ofisi yangu imefanya ukaguzi katika mashirika ya umma 217, ikitathmini utendaji, uzingatiaji wa kanuni, na ufanisi kwa ujumla. Hati zinazoridhisha zilikuwa asilimia 98 ya hati zote sawa na mwaka jana.

Aidha, mashirika ya umma bado yanakabiliwa na changamoto kama vile Hasara zinazojirudia, ukata wa fedha, upungufu katika utawala bora, na ucheleweshaji katika utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi. Nawasihi maafisa masuuli, bodi za wakurugenzi, na mamlaka za usimamizi kuchukua hatua madhubuti za kurekebisha hali hiyo. Pia, natoa wito kwa Bunge na wadau wengine kutumia ripoti hii kuimarisha utawala bora, kudumisha usimamizi na uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma.

Ofisi ya yangu imejidhatiti kutekeleza jukumu lake la usimamizi kwa weledi mkubwa, katika kuhakikisha rasilimali za umma zinasimamiwa kwa ufanisi na tija kwa manufaa ya wananchi wote.

Mwisho, ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa weledi na jitihada zao katika kuhakikisha ninatekeleza jukumu langu la kikatiba.

Charles E. Kichere
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Ripoti hii inaonesha ukaguzi wa mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2024. Inajumuisha utendaji wa kifedha na uendeshaji wa mashirika ya umma 217, kubainisha changamoto na kutoa mapendekezo ya kuimarisha utawala na uwajibikaji:

## Hati za Ukaguzi

Kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024, nilikamilisha kaguzi 217 za mashirika ya umma na kutoa hati za ukaguzi. Kati ya hati 217 nilizotoa, 213 zilikuwa ni hati zinazoridhisha na nne zilikuwa ni hati zenye shaka. Asilimia ya hati zinazoridhisha imendelea kuwa asilimia 98 sawa na mwaka jana.

## Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi Zilizopita na Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali

Tathimini yangu ya mapendekezo ya kaguzi zilizopita na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali inaangazia uhitaji wa kuimarisha juhudi za utekelezaji.

Kati ya mapendekezo 6,749 yaliyotolewa kwa mashirika ya umma 217 katika miaka iliyopita, 2,589 (Asilimia 38) yalitekelezwa kikamilifu, huku 2,916 (Asilimia 43) yakiwa katika hatua ya utekelezaji. Aidha, 1012 (Asilimia 15) hayakutekelezwa, na 232 (Asilimia 3) yalipitwa na wakati kwa muktadha wa mabadiliko ya matukio.

Vilevile, kati ya maagizo 209 ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali yaliyotolewa kwa mashirika ya umma 53 katika mwaka wa 2023/24, Maagizo 100 (Asilimia 48) yalitekelezwa kikamilifu, maagizo 99 (Asilimia 47) yakiwa katika hatua ya utekelezaji, na maagizo 10 (Asilimia 5) bado hayajatekelezwa.

Kuharakisha utekelezaji wa mapendekezo na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ni muhimu katika kushughulikia changamoto zilizopo.

## Utendaji wa Kifedha wa Mashirika ya Umma

Nilikagua utendaji wa kifedha wa mashirika ya umma **217** kwa mwaka wa fedha wa 2023/24, nikilinganisha na mwaka wa fedha uliopita 2022/23 na kubaini mashirika ya umma 12 yalipata hasara ya kifedha kwa miaka mitatu mfululizo, mashirika matano yalipata hasara kwa miaka miwili mfululizo, wakati mashirika mawili yalipata hasara kwa mwaka wa 2023/24.

Pia, nilibaini mashirika ya umma **64** yalikabiliwa na ukata, yakiwa na madeni ya muda mfupi kuliko mali za muda mfupi kwa zaidi ya mwaka mmoja. Miongoni mwao, mashirika ya umma ya biashara yalikuwa **14** , wakati mashirika ya umma yasiyo ya kibiashara yakiwa **50.** Uwiano wa mashirika haya ulianzia 0.00 hadi 0.96 ikionesha upungufu wa kifedha na ukosefu wa ufanisi katika kusimamia fedha za muda mfupi.

Zaidi ya hayo, nilibaini mashirika ya umma yasiyo ya kibiashara 28 yameendelea kupata nakisi kwa zaidi ya mwaka mmoja kutokana na ukusanyaji mdogo wa mapato ya vyanzo vya ndani na utegemezi mkubwa wa ruzuku ya serikali, na kuibua shaka kuhusu uendelevu wao wa kifedha.

Pia, niliabini mashirika ya umma 11 yameshindwa kuchangia asilimia 15 ya mapato ghafi kwenda serikalini kama inavyotakiwa, kwa miaka miwili mfululizo, huku shirika moja likilimbikiza michango ambayo haijalipwa kwa zaidi ya miaka minne.

### Ufanisi wa Mashirika ya Umma Katika Kuimarisha Biashara

Katika tathmini yangu ya ufanisi wa uendeshaji wa mashirika ya umma ya biashara na ya kimkakati, nilibaini Shirika la Reli Tanzania limeshindwa kufikia asilimia 61 ya mkakati wake wa usafirishaji wa shehena kwa wafanyabiashara wakubwa watano. Pia Shirika la Reli Tanzania limeshindwa kutoa huduma za usafiri kwa abiria katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa asilimia 72 kutokana na upungufu wa treni za kisasa zinazoendana na huduma hiyo.

Katika Kampuni ya ndege Tanzania, nilibaini tozo za ukodishaji wa ndege na akiba ya matengenezo kwa miaka sita mfululizo yenye jumla ya shilingi bilioni 369.13 ambazo hazijalipwa, na matengenezo yasiyo na tija kiasi cha shilingi bilioni 20.63 ya Ndege-5H-MWF (Q300) ambayo ilikuwa haifanyi kazi, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024. Hii imesababisha kampuni ya ndege Tanzania kupata hasara kubwa ya kifedha na kupunguza utendaji wake. Hatimaye, Kampuni ya Ndege Tanzania ilipata hasara ya shilingi bilioni 91.80 na kupunguza uwezo wa utendaji.

Zaidi ya hayo, katika Kampuni ya huduma za meli Tanzania nilibaini miradi minne mikubwa, ambayo inahusisha ukarabati wa meli, ujenzi wa maeneo ya meli, na ujenzi wa gati katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria, ulikuwa haujaanza. Miradi hii ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 8.89 na dola za Marekani milioni 251.07.

## Usimamizi wa Mapato Katika Mashirika ya Umma

Katika ukaguzi wangu nilibaini mashirika ya umma saba yalipata hasara ya shilingi milioni 966.42 itokanayo na mapato yasiyotozwa kwa kiwango sahihi. Vilevile nilibaini upotevu wa mapato ya shilingi bilioni 6.97 kutokana na hali mbaya ya barabara ya Rongai na ukiukwaji wa mkataba wa ukodishaji katika Hifadhi za Taifa Tanzania . Sambamba na hayo, nilibaini utendaji duni wa Shirika la Madini la Taifa katika huduma ya uchimbaji, uliopelekea hasara ya mapato yaliyotarajiwa ya dola za Marekani milioni 15.52 sawa na shilingi bilioni 40.77.

Kwenye ukusanyaji wa mapato nilibaini mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo wa GePG shilingi bilioni 89.73 katika mashirika ya umma kumi (asilimia 4) kati ya mashirika ya umma 217 niliyoyapitia mwaka 2023/24. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 68.27 (sawa na asilimia 318) kutoka shilingi bilioni 21.46 zilizoripotiwa kwa mwaka uliopita.

Pamoja na hayo nilibaini mashirika ya umma 106 yanamadai makubwa ya zaidi ya mwaka mmoja yanayofikia shilingi trilioni 3.58, yanayohusiana na huduma zilizotolewa kwa wateja.

## Usimamizi wa Matumizi Katika Mashirika ya Umma

Nilibaini kuwa mashirika ya umma 12 yalifanya matumizi yasiyokuwa na tija ya jumla ya shilingi bilioni 371.42, hii ni ongezeko la asilimia 413 ikilinganishwa na shilingi bilioni 72.36 katika mashirika ya umma 17 mwaka uliopita. Vilevile, nilibaini kuwa mashirika 10 yalifanya matumizi yasiyostahili ya jumla ya shilingi bilioni 6.75, ikiwa ni ongezeko la asilimia 45 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4.64 katika mashirika ya umma 11 mwaka uliopita.

Vilevile, ukaguzi wangu ulibaini kuwa mashirika 66 ya umma yalikuwa na madeni ya jumla ya shilingi trilioni 3.70, ambayo yalikuwa hayajalipwa kwa zaidi ya miezi 12.

## Usimamizi wa Bajeti Katika Mashirika ya Umma

Nilibaini Serikali haikutoa shilingi bilioni 485.91 kwa mashirika ya Umma 66 kama ilivyopangwa katika mwaka wa fedha 2023/24. Aidha, kwa kipindi cha mwaka wa 2022/23, Serikali haikutoa shilingi trilioni 1.01 kwa mashirika 50.

Vilevile, nilibaini mashirika ya umma 80 hayakukusanya fedha kiasi cha shilingi trilioni 2.07 kutoka katika bajeti ya vyanzo vya ndani katika mwaka wa fedha 2023/24. Aidha, kwa kipindi cha mwaka wa 2022/23, mashirika ya umma 66 hayakukusanya fedha kiasi cha shilingi bilioni 284.71 kutoka katika bajeti ya vyanzo vya ndani.

Pia, nilibaini mashirika ya umma 12 yalitumia zaidi ya bajeti kwa kiasi cha shilingi bilioni 7.65 bila idhini ya afisa masuuli au Bodi ya Wakurugenzi, Aidha, kwa mwaka wa fedha 2022/23, niliripoti mashirika ya umma nane kati ya mashirika 215 yalitumia zaidi ya bajeti kwa kiasi cha shilingi bilioni 21.14 bila idhini ya Afisa Masuuli au Bodi ya Wakurugenzi.

### Usimamizi wa Mali Katika Mashirika ya Umma

Katika uhakiki wangu nilibaini mashirika 18 yanamiliki viwanja 259 vyenye thamani ya shilingi bilioni 201.67 bila ya kuwa na hati miliki. Vilevile, mashirika ya umma 24 hayakuandaa na kutekeleza ipasavyo mipango ya matengenezo ya mali.

Aidha, nilibaini ucheleweshaji katika uhamishaji wa mali zenye thamani ya shilingi bilioni 3.59 kwenda Kampuni ya Sisalana Tanzania. Pia, Kampuni ya Ndege Tanzania haikukabidhiwa mali zilizokuwa chini ya lililokuwa Shirika la kusimamia Mali za Shirika la Ndege la Zamani (Air Tanzania Holding Corporation).

Pia, nilibaini kuwepo kwa ucheleweshaji wa muda mrefu wa uhamishaji wa mali za Mgodi wa Tulawaka zenye thamani ya shilingi bilioni 22.42 kutoka Kampuni ya Pangea Minerals kwenda Kampuni ya STAMIGOLD, kutokana na kukosekana na hati ya kulipa kodi.

### Usimamizi wa Mikataba na Ununuzi

Mapitio yangu katika mashirika ya umma saba yalibaini wasambazaji na watoa huduma walichelewesha utoaji wa bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi bilioni 8.68 na dola za Marekani milioni 16.25 hadi kufikia siku 330.

Vilevile, nilibaini mashirika ya umma 12 yalichelewesha malipo ya madai ya wakandarasi na wazabuni wa bidhaa yenye thamani ya shilingi bilioni 54.84, Euro 194,000 na dola za Marekani milioni 354.45 kwa muda wa siku 7 hadi siku 365.

Aidha, nilibaini mashirika ya umma saba yalibadili njia za ununuzi kwa mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 11.31. Hii inakiuka Kanuni za Ununuzi wa Umma kwa kupunguza ushindani pasipo idhini ya bodi ya zabuni.

### Tathmini ya Utawala na Usimamizi na Vihatarishi

Nilibaini mashirika ya umma 36 yaliendeshwa bila kuwa na Bodi ya Wakurugenzi; mashirika matatu yalikuwa na Bodi ya Wakurugenzi lakini yalikosa Mwenyekiti wa Bodi; mashirika saba yalikuwa na

Mwenyekiti wa Bodi lakini hayakuwa na wajumbe wa Bodi; na mashirika 12 yalikosa kamati za Bodi, katiba ya Bodi, au makubaliano ya mkataba wa utendaji, vyote vinapunguza ufanisi wa utawala na kazi za uangalizi ndani ya mashirika ya umma.

Pia, nilibaini mashirika ya umma saba yalishindwa kuandaa au kuhuisha mpango mkakati na mpango wa biashara. Jumla ya mashirika ya umma 38 hayakuwa na nyenzo sahihi zilizowezesha mashirika hayo kufanya kazi zao kwa ufanisi. Aidha mashirika ya umma 30 yalikuwa na mapungufu katika utumiaji wa mifumo ya kiuendeshaji ya kielektroniki.

### Usimamizi wa Rasilimali Watu

Nilibaini ukusanyaji hafifu wa madeni ya Mikopo kwa wafanyakazi wa mashirika ya umma shilingi bilioni 1.28. Vilevile, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, jumla ya mashirika ya umma 10 yalikuwa na deni la shilingi bilioni 12.64, ambalo kimsingi lilitokana na madai ya wafanyakazi na madai yasiyolipwa, wakati jumla ya mashirika ya umma tisa hayakuwa yamewasilisha makato ya kisheria ya wafanyakazi wake yenye jumla ya shilingi bilioni 11.89, kwa kipindi cha kuanzia siku 30 hadi siku 1095.

Aidha, ukaguzi wangu ulibaini kuwapo kwa mashirika ya umma 29 ambayo yanaendelea kutumia miongozo ya Rasilimali watu isiyoidhinishwa. Hii inajumuisha, kuwa na miongozo na sera zilizopitwa na wakati, kutokuwa na mpango bora wa kurithisha madaraka, mpango wa kubakiza watumishi, pamoja na kuwa na ikama.

Vilevile, nilibaini mashirika ya umma matano yaliajiri au kukaimisha madaraka bila idhini ya Katibu Mkuu Utumishi Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha nilibaini kuwapo kwa maafisa 136 waliokaimu nafasi mbalimbali kwa zaidi ya miezi sita katika mashirika ya umma 19 ambapo kipindi cha zaidi ya miezi sita kilikuwa kati ya mwezi mmoja hadi miezi 57. Nilibaini uwepo wa wafanyakazi 31 wanaofanya kazi au walioteuliwa kukaimu nafasi mbalimbali katika mashirika ya umma sita bila kuwa na sifa zinazohitajika.

### Usimamizi wa Kodi katika Mashirika ya Umma

Tathmini yangu ya ufuataji wa Sheria za kodi kwenye mashirika ya umma ilibaini mashirika ya umma 17 hayakuwasilisha kodi kiasi cha shilingi bilioni 9.65 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hali hii inaonesha kuimarika kwa kiasi kinachowasilishwa ikilinganishwa na

mwaka 2022/23 ambapo mashirika 16 hayakuwasilisha kodi za jumla ya shilingi bilioni 33.45 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, Malipo yaliyofanyika bila risiti za kielektroniki yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 2.17 (kwa mashirika tisa) mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 4.14 (kwa mashirika 12) mwaka 2023/24.

### Utendaji wa Benki za Serikali na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

Nilibaini Benki ya Biashara Tanzania, Benki ya TIB Maendeleo na Benki ya Azania hazikusimamia ipasavyo mikopo iliyotolewa ya shilingi bilioni 558.53. Mikopo hiyo ilijumuisha shilingi bilioni 104.84 kutoka Benki ya Biashara Tanzania wakati shilingi bilioni 277.07 ni kutoka benki ya Azania na shilingi bilioni 176.62 ilikuwa ni ya Benki ya TIB Maendeleo. Dhamana zilizoahidiwa za mikopo hiyo ama hazikuwa zimekatiwa bima, au zilikuwa bandia au hazikuwepo. Mapungufu katika usimamizi wa dhamana husababisha hatari ya mikopo kwa benki na wakopajiwanaweza kutorejesha mikopo hiyo.

Pia, nilibaini Benki ya Biashara Tanzania haikuweza kuendana na kiwango cha awali kilichowekwa na Benki Kuu ambapo ilikuwa na uwiano wa mtaji wa asilimia 13.41 ambao ni chini ya uwiano unaohitajika wa asilimia 14.5. Wakati huohuo, Benki ilikuwa na akaunti za amana za makampuni ya simu yanayotoa huduma za fedha zenye jumla ya shilingi bilioni 129.18 sawa na uwiano wa asilimia 97 ya mtaji mkuu dhidi ya uwiano unaohitajika wa asilimia 50. Vilevile, uwiano wa gharama kwa mapato ulikuwa asilimia 76 dhidi ya mahitaji ya uwiano wa asilima 55. Kutofuatiana kwa uwiano uliotajwa hapo juu kunaweza pia kuathiri ufanisi wa uendeshaji wa Benki.

Katika ukaguzi nilibaini Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ina salio la mikopo isiyolipwa kwa muda mrefu inayofikia shilingi trilioni 3.57, ambapo shilingi trilioni 2.28 ni ya iliyokuwa PSPF zamani na inatarajiwa kulipwa na Serikali na shilingi trilioni 1.29 ni mkopo uliotolewa kwa Serikali kwa kipindi kinachotofautiana kati ya mwaka 1 hadi miaka 17. Mikopo hii isiyolipwa na Serikali imezuia uwezo wa mifuko ya pensheni kufanya uwekezaji zaidi, wakati Serikali hailipi riba ya mikopo na mifuko imesitisha kutoza riba.

Aidha, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi ulishindwa kukusanya kodi ya pango linayofikia shilingi bilioni 19.52 kutoka kwa wapangaji wake. Kiasi hiki kingetumika kwa uwekezaji zaidi. Pia, katika mwaka wa fedha 2023/24, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi zilishindwa

kukusanya michango inayodaiwa kufikia shilingi trilioni 1.18 kutoka kwa wanufaika wanaostahiki, jambo ambalo linaathiri ukwasi wa fedha, kwani linaweza kuathiri ulipaji wa madeni wakati yanapofika muda wa kulipwa.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ulikuwa na uwekezaji katika maeneo nane unaofikia shilingi bilioni 161.53 ambao mfuko haukupata faida yoyote. Kuwekeza kwenye miradi ambayo haizalishi faida yoyote inamaanisha kuwa hakuna thamani ya fedha katika uwekezaji huo.

## Tathmini ya Sekta ya Utalii Nchini Tanzania

Juhudi za Serikali katika kuboresha sekta ya utalii, hasa baada ya kuathiriwa sana na Uviko 19, ziko wazi na zinaonesha matokeo chanya. Hata hivyo, nilibaini masuala ambayo bado ni thabiti kwa sekta yakiwemo; ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya kutangaza utalii na kushiriki kwenye maonesho; kuenea kwa kasi kwa mimea vamizi inayotishia mifumo ya ikolojia ya hifadhi; pia, niliona usimamizi duni wa miundombinu ikiwa ni pamoja na utunzaji duni wa taka ngumu na usimamizi wa barabara.

Vilevile, nilibaini kutotangazwa kwa maeneo ya urithi wa kale kama vile Engaruka na Mumba, na Mapango ya Amboni yaliyopo mkoa wa Tanga. Pia, nilibaini usimamizi duni wa mtandao wa intaneti katika uendeshaji shughuli za kitalii ndani ya Hifadhi za Taifa.

## Utendaji wa Mamlaka za Maji

Nilibaini ucheleweshaji wa hadi siku 622 katika kukamilisha miradi ya maji katika Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira, kutokana na changamoto za fedha na usimamizi wa mikataba, zikihusisha miradi 13 yenye thamani ya shilingi bilioni 34.27.

Pia, nilibaini uhaba mkubwa wa maji ulioathiri Mamlaka 26 kati ya 34 za Maji, na upungufu ulio kati ya 30% hadi 77% ya mahitaji, hasa kutokana na kukosekana kwa fedha na ucheleweshaji wa miradi hiyo.

Aidha, hasara ya mapato iliyotokana na upotevu wa maji ilifikia shilingi bilioni 182.21 (2022/23: shilingi bilioni 162.25), iliyosababishwa na uchakavu wa miundombinu inayosababisha uvujaji wa maji. Madeni ya Mamlaka za Maji yaliongezeka hadi shilingi bilioni 149.71, kutoka shilingi bilioni 138.64 (2022/23), kutokana na malimbikizo ya tozo za maji na usafi wa mazingira.

## Tathimini ya Utendaji wa Taasisi za Mafunzo, Utafiti na Elimu ya Juu

Katika uhakiki wangu nilibaini mapungufu katika usimamizi wa utafiti na ushauri, pamoja na udahili duni wa wanafunzi katika taasisi saba za elimu ya juu.

Pia, nilibaini ukosefu wa vifaa vya mafunzo, kama vile uhaba wa madarasa katika Chuo cha Usafirishaji cha Taifa, uhaba wa zana na vifaa vya mafunzo katika Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Zaidi ya hayo, nilibaini usimamizi usiofaa wa shughuli za mafunzo, ikijumuisha kutokuzingatia uwiano wa wanafunzi na wahadhiri katika Chuo cha Usafirishaji cha Taifa, Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini na Chuo Kikuu cha Dodoma, utoaji wa programu zisizoidhinishwa, ucheleweshaji wa utekelezaji wa programu zilizoidhinishwa, na uendeshaji wa taasisi bila mitaala iliyoidhinishwa.

Aidha, nilibaini ongezeko la utegemezi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa ruzuku ya Serikali. Utegemezi huo, umekua kwa asilimia 84 ndani ya miaka mitano, kutoka shilingi bilioni 255.62 mwaka 2019/20 hadi shilingi bilioni 469.67 mwaka 2023/24. Kwa upande mwingine, marejesho ya mikopo yalipungua kwa asilimia 7, kutoka shilingi bilioni 190.72 mwaka 2019/20 hadi shilingi bilioni 176.61 mwaka 2023/24. Hali hii ilitokana na kutokuwa na mbinu za kutosheleza za kukusanya mikopo na kuwekeza fedha.

Zaidi ya hayo, nilibaini mafunzo yasiyotosheleza kwa Mtaala wa Mafunzo ya Elimu yenye Msingi wa Umahiri katika taasisi 51 na pia, taasisi 12 za ufundi zilidahili wanafunzi wapya licha ya kuzuiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

## Ufanisi wa Mamlaka za Udhibiti katika Kutekeleza Majukumu Yao

Katika ukaguzi wa Mamlaka za udhibiti katika kutekeleza majukumu yao, nilibaini kasoro mbalimbali kama vile udhaifu katika kusimamia hatua za kiudhibiti, Kushindwa kutumia teknolojia kikamilifu kuboresha na kuongeza ufanisi wa kutekeleza majukumu ya kiudhibiti, na kukosa ufanisi katika utoaji na usimamizi wa leseni.

Pia nilibaini mapungufu ya Bodi za Mazao katika usimamizi wa mazao ya biashara kama vile; Uwezekano wa kukwama kwa upanuzi wa maeneo mapya ya kilimo cha kahawa kutokana na vikwazo vilivyowekwa katika Mkataba wa Ulaya wa kuzuia uharibifu wa misitu, na kutotekelezwa kwa mkakati wa kuimarisha bei ya kahawa.

Vilevile, nilibaini uratibu duni kati ya bodi za mazao na halmashauri za wilaya na wadau wengine; uwezo mdogo wa uzalishaji wa mbolea nchini hali inayopelekea utegemezi mkubwa wa uagizaji wa mbolea kutoka nje ya nchi; na haja ya kutathmini upya utekelezekaji wa ununuzi wa mbolea kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja.

### Ufanisi wa Mashirika ya Umma Katika Sekta ya Afya

Katika ukaguzi wangu wa utendaji wa mashirika ya umma katika sekta ya afya nilibaini gharama za matibabu ya msamaha kiasi cha shilingi bilioni 17.84 katika hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila ambazo hazikurejeshwa kwenye hospitali hizo.

Pia, nilibaini uwepo wa dawa zilizokwisha muda wake katika Bohari Kuu ya Dawa, Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Taifa Muhimbili -Mloganzila zenye thamani ya shilingi bilioni 4.44. Kwa upande wa Bohari Kuu ya Dawa, dawa zilizokwisha muda wake zilipungua kutoka shilingi bilioni 11.74 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 4.18 mwaka 2023/24. Aidha, nilibaini kulikuwa na dawa zilizobakiza mwezi mmoja hadi miezi sita kabla ya muda wake wa matumizi kwisha zikiwa zimehifadhiwa katika Bohari Kuu ya Dawa zenye thamani ya shilingi bilioni 4.86 ambazo aidha hazikugawiwa bure au kwa bei pungufu ili kuepuka kuharibikia bohari.

Pia, nilibaini Mfuko wa Bima ya Afya ulikataa madai ya mashirika ya umma mawili yenye jumla ya shilingi bilioni 11.23 kwa mwaka 2023/24, ambapo madai ya aina hiyo yamepungua kutoka shilingi bilioni 11.83 yaliyokataliwa mwaka 2022/23 kwa mashirika manne. Aidha Mfuko wa Bima wa Afya ulichelewa kufanyia kazi madai ya watoa huduma ya afya kiasi cha shilingi bilioni 416.08, huku baadhi ya madai yakifikia siku 122.

### Utendaji Katika Sekta ya Uziduaji

Nilibaini ucheleweshaji wa miradi inayotekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Taifa ikiwewo Mradi wa Engaruka Soda Ash na Ucheleweshaji wa Uanzishwaji wa Mradi wa Liganga wa Chuma na Chuma cha Pua. Vilevile nilibaini ucheleweshaji wa Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya mradi wa ngozi wa megawati 30 unaotekelezwa na Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania. Mradi ulikuwa ukamilike kufikia mwaka 2023 hata hivyo wakati wa ukaguzi wangu kufikia tarehe 20 Machi 2024 mradi ulikuwa umechelewa kwa miezi 27 nyuma ya muda, mradi ulikuwa hatua za awali za uchimbaji wa visima vidogo vya uchunguzi ili kuthibitisha uwepo wa rasilimali za jotoardhi.

Vilevile, katika kampuni ya STAMIGOLD nilibaini Kiwango Kikubwa cha sumu katika mabaki ya kiwanda cha uchakataji zaidi ya 50 ppm, nilibaini kuwa viwango vya cyanide vilikuwa juu kwa mwaka mzima,

vikivuka mara kwa mara kikomo salama cha 50 ppm, huku kiwango cha wastani kikiwa 87.5 ppm. Sambamba na hayo nilibaini utendaji duni wa mkandarasi wa uendeshaji wa migodi katika Kampuni (STAMIGOLD), Utendaji wa uchimbaji madini haukufikia malengo yaliyopangwa, ambapo, uzalishaji wa madini ulikuwa chini kwa asilimia 44, uhamishaji wa mabaki ya mgodi ulikuwa chini kwa asilimia 22, na jumla ya uhamishaji wa malighafi ulikuwa chini kwa asilimia 24.

Zaidi ya hayo, kuhusiana na Kampuni ya Gesi Tanzania kudumisha miundombinu ya gesi asilia, nilibaini takriban mita 80 za bomba la gesi asilia (mabomba ya Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania na SONGAS) kuwa wazi kutokana na mmomonyoko wa udongo kando ya bomba la gesi asilia. Hii ni kinyume na Kanuni ya 58 ya Petroli (Gesi Asilia) (Shughuli za Usafirishaji na Usambazaji), ya mwaka 2018.

Aidha nilibaini kasi duni na upungufu katika uwekezaji wa vituo vya kujaza Gesi asilia ya CNG. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa ni vituo vitatu tu vilivyofanikiwa kuanzishwa, wakati kampuni nyingine 32 zilikutana na changamoto kama vile ucheleweshaji katika kupata vibali vya kisheria kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

# Utangulizi



# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Ripoti hii inaelezea kwa muhtasari hoja za ukaguzi na mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mashirika ya umma 217 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Ukaguzi huu ulifanyika kwa mujibu wa Ibara ya 143 (2) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, pamoja na Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418. Ripoti hii ina sura 20, zinazoelezea hoja za ukaguzi na mapendekezo ya ukaguzi yanayolenga kuboresha ufanisi wa kiutendaji, uwazi, uwajibikaji, na utawala bora katika mashirika ya umma.

## 1.1 Malengo ya Ukaguzi

Ukaguzi ulilenga kukusanya vielelezo na ushahidi wa kikaguzi wa kutosha na wenye mashiko katika kutoa hati za ukaguzi juu ya taarifa za fedha, kutathmini ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya shirika husika, na kuangalia uzingatiaji wa sheria, taratibu na kanuni, hususani sheria za bajeti, ununuzi, na kodi.

## 1.2 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi wa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024 ulijumuisha ukaguzi wa taarifa za fedha na uzingatiaji wa sheria za bajeti na ununuzi katika mashirika ya umma. Pia, ulijumuisha tathmini ya ufanisi wa kiutendaji kazi wa mifumo ya udhibiti wa ndani, usimamizi wa shirika na udhibiti wa vihatarishi, ukusanyaji wa mapato, na usimamizi wa matumizi na rasilimali watu. Vilevile, ukaguzi huu ulihusisha tathmini ya utendaji wa sekta za afya, utalii, na maji, pamoja na taasisi za elimu ya juu, mamlaka za udhibiti, benki za Serikali, na sekta ya uziduaji.

## 1.3 Mbinu na Njia za Ukaguzi

Ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Ukaguzi (ISSAI) vilivyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI).

Mbinu za Ukaguzi zilizotumika zilijumuisha kupitia na kuchambua taarifa na nyaraka, kufanya mahojiano, na kutembelea maeneo yaliyobainishwa.

Ukaguzi ulilenga katika kubainisha na kutathmini viashiria vya hatari zinazoweza kuathiri malengo ya shirika, taarifa zake za fedha na uzingatiaji wa sheria na kanuni. Mbinu hii huongeza ufanisi wa ukaguzi kwa kushughulikia viashiria vya hatari vyenye athari kubwa na maeneo

yaliyo katika hatari kubwa ya kuwa na makosa kwenye taarifa za fedha.

# Hati za Ukaguzi



# SURA YA PILI

# HATI ZA UKAGUZI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea kwa muhtasari hati za ukaguzi zilizotolewa kwa mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2023/24 na kuchambua mwenendo wa hati hizo kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2019/20 hadi 2023/24. Hati hizi zinatokana na tathmini ya vielelezo na ushahidi wa kikaguzi uliokusanywa wakati wa ukaguzi, ikihusisha mapitio na uchambuzi wa taarifa za fedha ili kubaini kama taarifa hizo ziliandaliwa kwa kuzingatia misingi na miongozo ya uandaaji wa taarifa za fedha, kama vile Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha (IFRSs), Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Sekta ya Umma (IPSASs), na Kiwango cha Uandaaji wa Taarifa za Kifedha Tanzania Na. 1 (TFRS1) kwa ujumla wake. Tathmini hii ilifanyika kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi wa Umma (ISSAI).

## 2.1 Aina za Hati za Ukaguzi

Kuna aina nne za hati za ukaguzi: hati inayoridhisha, hati yenye shaka, hati mbaya, na kushindwa kutoa maoni.

**Hati inayoridhisha:** Hii hutolewa wakati mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi kwa kuzingatia viwango, misingi na miongozo inayokubalika ya uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za fedha.

**Hati yenye shaka:** Hii hutolewa pale taarifa za fedha zinapoonekana zimeandaliwa kwa usahihi isipokuwa kwa baadhi ya maeneo ambayo baada ya kupata vielelezo na ushahidi wa kikaguzi wa kutosha na wenye mashiko, mkaguzi anahitimisha kuwa makosa kwenye maeneo hayo likiwa moja au yakiwekwa pamoja yana athari, lakini hayaathiri maeneo yote katika taarifa za fedha.

Pia, hati yenye shaka hutolewa pale mkaguzi anaposhindwa kupata vielelezo na ushahidi wa kikaguzi wa kutosha na wenye mashiko kumwezesha kuhitimisha ukaguzi lakini athari zinazotokana na kukosa uthibitisho huo kwa ujumla wake haziathiri maeneo yote ya taarifa za fedha.

**Hati mbaya:** Hii hutolewa pale mkaguzi anapokuwa amepata vielelezo na ushahidi wa kikaguzi wa kutosha na wenye mashiko kudhihirisha kuwa kuna makosa kwenye taarifa za fedha, na, kuwa, makosa hayo ama kwa kuyaangalia mojamoja au kwa ujumla wake

ni makubwa na yenye athari kwa taarifa zote za fedha; hivyo, kuhitimisha kuwa taarifa hizo hazikufuata viwango, misingi na miongozo inayokubalika ya uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za fedha.

**Kushindwa kutoa maoni:** Hii hutokea pale mkaguzi anaposhindwa kupata vielelezo vya kutosha na ushahidi wenye mashiko kuhusu taarifa za fedha ili kumuwezesha kutoa hati ya ukaguzi; hivyo, mkaguzi kuhitimisha kuwa athari za makosa yanayoweza kuwa kwenye hesabu ambayo hayakubainika yanaweza kuwa makubwa na yenye athari kwa maeneo yote ya taarifa hiyo.

Pia, ikiwa kuna mazingira yenye mashaka, Mkaguzi anaweza kushindwa kutoa maoni, licha ya kuwa amepata vielelezo na uthibitisho wa kikaguzi wa kutosha kuhusu kila shaka. Hii inatokana na kuwapo kwa uhusiano wa moja kwa moja na wenye athari kwenye maeneo yote ya taarifa za fedha, hivyo kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi.

## 2.2 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa Mwaka Huu

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, nimekamilisha kaguzi 217 za mashirika ya umma na kutoa hati za ukaguzi. Kati ya hati za ukaguzi 217 nilizotoa, 213 (98%) zinaridhisha, na nne (2%) ni zenye shaka, kama ilivyooneshwa katika **Kiambatisho Na. I.**

Ukilinganisha na mwaka wa fedha 2022/23, idadi ya mashirika yaliyoripotiwa imeongezeka kutoka 215 hadi 217 katika mwaka wa fedha 2023/24. Hii inatokana na kujumuishwa kwa mashirika matano yaliyokaguliwa kwa mara ya kwanza, ambayo ni: Kampuni ya Uwekezaji ya TANAPA, Kampuni ya Msamvu Properties Company Limited, Kampuni ya Sisalana Tanzania, Kampuni ya Ushauri Elekezi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, na Kampuni ya Uzalishaji ya KMTC. Kwa upande mwingine, mashirika matatu yamefutwa kufuatia kuhamishiwa kwa majukumu ya mashirika haya kwenye mashirika mengine, ambayo ni Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Korogwe, Mfuko wa Wakfu wa Kuendeleza Zao la Korosho, na Kitengo cha Uzalishaji na Ushauri Elekezi cha Chuo cha Ufundi Arusha.

## 2.3 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi

**Jedwali Na. 1** linaonesha mwenendo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa mashirika ya umma kwa miaka mitano mfululizo tangu mwaka wa fedha 2019/20 hadi 2023/24.

Mwelekeo wa hati za ukaguzi unaonesha mabadiliko katika asilimia ya hati za ukaguzi zinazoridhisha zilizotolewa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Mwaka 2019/20, asilimia hiyo ilikuwa 98, lakini ilipungua hadi 95 mwaka 2020/21. Hii ilifuatiwa na ongezeko la taratibu kwa miaka miwili iliyofuata, ikifikia 97 mwaka 2021/22 na 98 mwaka 2022/23 na 2023/24.

Kwa ujumla, asilimia ya hati za ukaguzi zinazoridhisha imekuwa kati ya 95 na 98 katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, jambo linaloashiria uzingatiaji mzuri wa viwango vya kimataifa vya uandaaji wa taarifa za fedha (IPSAS na IFRS).

**Jedwali Na. 1: Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa idadi kipindi cha miaka mitano mfululizo**

| Aina ya hati ya ukaguzi | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|---|---|---|
| Inayoridhisha | 162 | 185 | 196 | 211 | 213 |
| Yenye shaka | 3 | 8 | 5 | 4 | 4 |
| Kushidwa kutoa maoni | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 |
| Mbaya | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Jumla | 165 | 195 | 203 | 215 | 217 |
| Asilimia ya hati zinazoridhisha | 98% | 95% | 97% | 98% | 98% |

**Chanzo:** *Uchambuzi wa taarifa za kifedha zilizokaguliwa*

# Muhtasari wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Miaka Iliyopita



# SURA YA TATU

# MUHTASARI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA MIAKA ILIYOPITA

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi na maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC). Pia inaelezea hatua zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli katika kutekeleza mapendekezo yangu na maagizo hayo, ambayo yalitolewa kwa menejimenti pamoja na Bodi za wakurugenzi zilizopewa dhamana ya usimamizi wa mashirika husika.

Wakati wa ukaguzi na uhakiki wa maagizo hayo, nilibaini maboresho, na ninatambua juhudi zilizofanywa na maafisa masuuli katika kutekeleza mapendekezo na kufanyia kazi maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kwa mashirika ya umma katika kutekeleza majukumu yao ya uangalizi na usimamizi.

## 3.1 Tathmini ya hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo kwa Kipindi Kilichopita katika Mashirika ya Umma

Tathmini ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, hadi mwaka wa fedha 2022/23, kwa mashirika ya umma 217 (2021/22: 215), imeonesha kuwa utekelezaji kwa jumla ni wa kuridhisha kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 2**

**Jedwali Na. 2: Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi miaka iliyopita kwa mashirika ya umma**

| Mwaka wa fedha | Yame tekelezwa | Yanayo tekelezwa | Haya kutekelezwa | Yamepit wa na wakati | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **2022/23** | 2,589(38%) | 2916(43%) | 1,012(15%) | 232(4%) | 6,749 |
| **2021/22** | 2,413(39%) | 2,776(45%) | 720 (12%) | 242(4%) | 6,151 |
| **2020/21** | 2,195(36%) | 2,611(43%) | 1,064 (17%) | 276(4%) | 6,146 |

**Chanzo**: *Taarifa za Ukaguzi*

## 3.2 Tathmini ya hali ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali

Kifungu cha 38(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sura ya 418 kinahitaji maafisa masuuli wa mashirika ya umma kuzingatia maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali juu ya masuala ya kifedha.

Tathmini ya hali ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa miaka mitatu mfululizo, hadi kufikia mwaka wa fedha 2023/24 kwa mashirika ya umma 53 (2022/23: 37), ilionesha kuwa kiwango cha utekelezaji kinaridhisha. **Jedwali Na. 3**.

**Jedwali Na. 3: Utekelezaji wa maagizo ya kamati ya kudumu ya bunge**

| Mwaka wa fedha | Yame tekelezwa | Yanayo tekelezwa | Haya kutekelezwa | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 2023/24 | 100(48%) | 99(47%) | 10(5%) | 209 |
| 2022/23 | 45(33%) | 89(65%) | 2(2%) | 136 |
| 2021/22 | 70(43%) | 92(56%) | 1(1%) | 163 |

***Chanzo***: *Taarifa za ukaguzi*

Pia, mashirika ya umma sita yalikuwa na maagizo 15 ambayo hayakutekelezwa kikamilifu kwa kipindi kinachoanzia miaka saba hadi 13, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 4**

**Jedwali Na. 4: Mashirika yenye maagizo ya muda mrefu kutoka kwa kamati**

| Na. | Jina la shirika | Yanayote kelezwa | Mwaka wa Maagizo | Idadi ya miaka ya utekelezaji wa maagizo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi | 3 | 2010/11 | 13 |
| 2 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga | 2 | 2010/11 | 13 |
| 3 | Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania | 2 | 2011/12 | 12 |
| 4 | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 1 | 2015/16 | 8 |
| 5 | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 5 | 2017/18 | 7 |
| 6 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza | 2 | 2017/18 | 7 |
| | **Jumla** | **15** | | |

**Chanzo**: *Taarifa za Ukaguzi*

Mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira (**Lindi, Shinyanga, na Mwanza**) zina maagizo ya muda mrefu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, ambayo yalizitaka mamlaka hizo kupunguza gharama za uendeshaji ili kuendana na ukusanyaji wa mapato; kulinda mazingira yaliyo karibu na vyanzo vya maji ili kuzuia upungufu wa maji, kuharakisha uunganishaji wa maji; na kuhakikisha ukusanyaji wa madeni unafanyika kwa wakati. Hata hivyo, utekelezaji umekwamishwa na ukosefu wa fedha.

Viwango vya sasa vya tozo za maji zinazolipwa na watumiaji wa maji havikidhi gharama za uendeshaji, hivyo kusababisha mamlaka kutegemea msaada na ruzuku za Serikali. Aidha, madeni yaliyosalia, kwa kiasi kikubwa ni kutoka katika mashirika ya Serikali kwa huduma za maji zinazotolewa kwa mashirika hayo.

Kwa upande wa mashirika ya umma mingine, yalikuwa na mapendekezo kama vile; Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania iliagizwa kulipa madeni ya muda mrefu;Mamlaka ya Elimu

na Mafunzo ya Ufundi Stadi iliagizwa kulipa masurufu ya muda mrefu na mikopo ya wafanyakazi; na Hospitali ya Taifa Muhimbili iliagizwa kuhakikisha uwasilishaji wa malipo ya kodi ya mapato yatokanayo na ajira kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa wakati, pia ishughulikie madeni ya muda mrefu.

# Utendaji wa Kifedha wa Mashirika ya Umma



# SURA YA NNE

# UTENDAJI WA KIFEDHA WA MASHIRIKA YA UMMA

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inatathmini utendaji wa kifedha wa mashirika ya umma (mashirika ya kibiashara na  yasiyo ya kibiashara) kwa kuangalia faida, usimamizi wa madai, na ukwasi. Mashirika ya umma ya kibiashara ni yale yaliyoanzishwa kwa lengo la kupata faida na hayategemei ruzuku ya Serikali kwa kiasi kikubwa katika kujiendesha. Kwa upande mwingine, mashirika ya umma yasiyo ya kibiashara ni yale yanayotoa huduma kwa umma bila kulenga kupata faida, na hutegemea ruzuku ya Serikali, ada, na michango mbalimbali ya wadau ili kuendesha shughuli zake.

Tathmini hii imetokana na uchambuzi wa taarifa za fedha za mashirika husika kwa mwaka wa fedha 2023/24, kwa kulinganisha na taarifa za fedha za miaka iliyopita. Sura hii haijajumuisha benki zinazomilikiwa na Serikali, mifuko ya hifadhi ya jamii, na mashirika yanayohusika na usimamizi na udhibiti wa masoko ya mitaji na dhamana, kwa kuwa utendaji wake umeelezewa katika sura ya 14.

## 4.1 Mwenendo wa Hasara wa Mashirika ya Umma ya kibiashara kwa Kipindi cha Mwaka Mmoja na Zaidi ya Mwaka Mmoja

Katika ukaguzi wa  taarifa za fedha za mashirika ya umma ya kibiashara 52 nilibaini kuwa mashirika 12 yalipata hasara kwa miaka mitatu mfululizo, wakati mashirika matano yalipata hasara kwa miaka miwili mfululizo, huku mashirika mawili yalipata hasara kwa mwaka mmoja wa fedha 2023/24.Hasara hizi zinasababishwa na utendaji duni wa uwekezaji na shughuli za biashara, usimamizi usio mzuri wa matumizi ya fedha, pamoja na ukusanyaji mdogo wa mapato kutokana na mikakati isiyofaa ya kibiashara.

Hali hii inaweza kusababisha kupungua kwa uwezo wa kugharamia shughuli muhimu na uwekezaji, na kutegemea kwa kiasi kikubwa ruzuku za Serikali ili kufidia upungufu wa kifedha. **Jedwali Na. 5** linaonesha orodha ya mashirika ya kibiashara yaliyopata hasara kwa mwaka mmoja, miaka miwili au mitatu mfululizo.

**Jedwali Na. 5: Mwenendo wa Hasara kwa mashirika ya umma kwa Kipindi cha Mwaka Mmoja hadi Mitatu**

| Na. | Jina la Shirika | 2023/24 Sh. '000 | 2022/23 Sh. '000 | 2021/22 Sh. '000 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Reli Tanzania | 224,591,063 | 101,663,607 | 190,013,510 |
| 2 | Kampuni ya Ndege Tanzania | 91,797,855 | 56,640,694 | 35,238,360 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Shirika la Mawasiliano Tanzania | 27,781,000 | 4,317,000 | 19,229,000 |
| 4 | Shirika la Posta Tanzania | 23,637,758 | 1,343,784 | - |
| 5 | Kampuni ya Mkulazi | 19,042,650 | 17,808,601 | 29,279,055 |
| 6 | Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro | 5,051,268 | 4,690,924 | 4,931,143 |
| 7 | Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibiolojia Tanzania | 4,263,332 | 6,118,670 | 3,855,713 |
| 8 | Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania | 3,505,286 | 407,688) | - |
| 9 | Kampuni ya Sisalana Tanzania | 2,442,979 | 1,502,609 | 1,769,938 |
| 10 | Kiwanda cha Madawa Keko | 1,841,907 | 1,892,319 | 1,350,649 |
| 11 | Shirika la Masoko ya Kariakoo | 1,420,705 | 41,569,864 | 519,284 |
| 12 | Kampuni ya TTCL Pesa | 1,394,661 | 352,737 | - |
| 13 | Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania | 1,341,053 | 1,239,191 | 791,675 |
| 14 | Kampuni ya Gesi Tanzania | 1,325,000 | 4,588,000 | - |
| 15 | Kituo cha Uwekezaji APC | 1,246,500 | 1,200,302 | 1,946,024 |
| 16 | Kampuni ya uzalishaji KMTC | 612,914 | - | - |
| 17 | Soko la Bidhaa Tanzania | 561,926 | 793,743 | 509,243 |
| 18 | Kampuni ya Uwekezaji TANAPA | 445,396 | - | - |
| 19 | Kampuni ya Uchapishaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | 13,005 | 7,387 | - |

**Chanzo***: Uchambuzi wa taarifa za fedha zilizokaguliwa mwaka 2023/24*

Muhtasari wa maelezo ya utendaji kwa mashirika ya kibiashara ambayo yamepata hasara kwa miaka mitatu mfululizo ni kama ifuatavyo:

(i) **Shirika la Reli Tanzania** lilirekodi ongezeko la hasara kwa asilimia 120, ikiongezeka kutoka shilingi bilioni 102 mwaka 2022/23 hadi kufikia shilingi bilioni 224 mwaka 2023/24. Ongezeko hili kubwa lilichangiwa hasa na kupungua kwa mapato na kupanda kwa gharama za uendeshaji, licha ya kupokea ruzuku ya Serikali ya jumla ya shilingi bilioni 29.01 kwa ajili ya uendeshaji na maendeleo ya shirika.

Pia, mapato ya uendeshaji yalipungua kutokana na huduma za usafirishaji mizigo na abiria kuathiriwa na upungufu wa vichwa vya treni na idadi isiyotosheleza ya mabehewa.

Kupungua kwa mapato ya uendeshaji kulisababishwa na changamoto nyingi. Miongoni mwao ilikuwa uhaba wa vichwa vya treni pamoja na idadi ndogo ya mabehewa, ambayo ilipunguza uwezo wa Shirika kukidhi mahitaji ya usafiri. Zaidi ya hayo, vikwazo vya mwendo kasi kati ya makutano ya Ruvu hadi makutano ya Mruazi vya chini ya kilomita 20 kwa saa, mzunguko mdogo wa mabehewa na kufungwa kwa njia kwa takribani miezi minne kutokana na mvua kubwa iliyonyesha kuanzia Novemba 2023 hadi Machi 2024 viliathiri utendaji wa biashara ya usafirishaji wa mizigo kutoka shilingi bilioni 45.56 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 39.33 mwaka 2023/24.

Aidha, jumla ya gharama za mwaka 2023/24 ziliongezeka hadi shilingi bilioni 296.96 kutoka shilingi bilioni 225.96 za mwaka wa fedha 2022/23. Gharama za mwaka huu pia zinajumuisha hasara ya jumla ya shilingi bilioni 35.05 iliyotokana na ubadilishaji wa fedha za kigeni kwa ajili ya shughuli za SGR kabla ya kuanza kazi rasmi mwezi Julai 2024.

**Ninapendekeza Shirika la Reli Tanzania lijikite katika kuboresha ufanisi wa utendaji kazi wake ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na kutekeleza hatua madhubuti za kupunguza gharama, na (b) kuandaa mpango wa kina wa kupata injini za treni na mabehewa ili kukidhi mahitaji ya usafiri ipasavyo.**

(ii) **Kampuni ya Ndege Tanzania** imeendelea kurekodi hasara za kifedha kwa miaka sita mfululizo, licha ya kupokea ruzuku kutoka serikalini. Mwaka 2023/24, Kampuni ya Ndege Tanzania ilipokea shilingi bilioni 70 kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi na gharama zingine za wafanyakazi, pamoja na shilingi bilioni 57 kama ruzuku ya maendeleo kwa miradi ya uwekezaji. Hata hivyo, licha ya msaada huu wa kifedha, hasara halisi ya Kampuni ya Ndege Tanzania iliongezeka kwa asilimia 62, ikipanda kutoka shilingi bilioni 56.6 mwaka 2022/23 hadi kufikia shilingi bilioni 91.8 mwaka 2023/24, huku jumla ya hasara zikifikia shilingi bilioni 534.

Hali mbaya ya kifedha ilichangiwa hasa na gharama kubwa za kodi na matengenezo ya ndege mpya zilizonunuliwa, ambazo ziliongeza gharama kwa Kampuni.

Zaidi ya hayo, kuharibika kwa ndege za Airbus A220-300 kutokana na kutu na hitilafu za injini zinazohusiana na mtengenezaji, ilisababisha usumbufu mkubwa wa safari, upotevu wa mapato, na gharama zisizorejeshwa za bima, matengenezo, na gharama za wafanyakazi. Pia, ucheleweshaji wa shughuli za ndege za mizigo kutokana na

ruhusa za kuruka na kutua ambazo hazikupatikana, ulizidisha vikwazo katika upatikanaji wa mapato.

Changamoto hizi zinaendelea kuonesha haja ya dharura ya hatua za kudhibiti gharama, kuboresha uhakika wa ndege, na mikakati ya kuongeza mapato ili kuhakikisha uendelevu wa kifedha wa Kampuni ya Ndege Tanzania kwa muda mrefu.

**Ninapendekeza Kampuni ya Ndege Tanzania ishirikiane na Serikali kufanya utafiti kuhusu njia nzuri zaidi ya uendeshaji wa ndege, kwa kuzingatia masuala ya kifedha, kisiasa na kiuchumi ili kuongeza ufanisi wa uendeshaji.**

(iii) **Shirika la Mawasiliano la Tanzania** lilipata hasara ya shilingi bilioni 27.78 mwaka 2023/24, ikiwa ni ongezeko la asilimia 543 kutoka shilingi bilioni 4.32 mwaka 2022/23. Hii inatokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji, ambazo ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 104.23 hadi kufikia shilingi bilioni 140.73. Ongezeko hili la gharama lilisababishwa na kuhamishwa kwa Mkongo wa Taifa na Kituo cha Taifa cha Data ya Mtandao uliongeza jumla ya mali za Shirika la Mawasiliano la Tanzania, na kusababisha kupanda kwa gharama za uchakavu kwa shilingi bilioni 13.6.

Hata hivyo, mapato yote yaliyokusanywa kutoka Mkongo wa Taifa kwa mwaka 2023/24, ambayo ni takribani shilingi bilioni 24, yalielekezwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ili kulipa deni la Serikali lililotokana kwa kupata mkongo huo, hivyo kulifanya Shirika la Mawasailiano Tanzania kukosa mapato kwa ajili ya uwekezaji na gharama za uendeshaji. Kutopata mapato ya mkongo, pamoja na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji, kumeathiri sana uendelevu wa kifedha wa shirika la mawasiliano Tanzania, na kusababisha hasara kubwa.

**Ninapendekeza Shirika la mawasiliano Tanzania (a) liboreshe ufanisi katika utendaji ili kuongeza ukusanyaji wa mapato, na (b) kuwasiliana na Serikali ili mapato yatokanayo na Mkongo wa Taifa yabaki katika shirika hilo ili kuliwezesha kushindana ipasavyo sokoni na kujiendesha kwa ufanisi.**

(iv) **Shirika la Posta Tanzania** lilipata hasara kwa miaka miwili mfululizo ya fedha. Katika mwaka 2023/24, shirika lilipata hasara ya shilingi bilioni 23.63, ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 22.29 (asilimia 1,659) ikilinganishwa na hasara ya shilingi bilioni 1.34 iliyoripotiwa mwaka uliopita, 2022/23. Hasara katika mwaka huu wa fedha, 2023/24, ilichangiwa zaidi na kupungua kwa mapato kwa asilimia 20, kutoka shilingi bilioni 37.11 mwaka wa fedha 2022/23 hadi shilingi bilioni 30.89 mwaka wa fedha 2023/24, wakati jumla ya gharama

pia iliongezeka kwa asilimia 46 ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita 2022/23. Pamoja na kupokea shilingi bilioni 2 kutoka serikalini kama ruzuku kwa shughuli za maendeleo, shirika bado lilishindwa kufikia malengo yake ya mapato na kuendelea kupata hasara.

**Ninapendekeza Shirika la Posta la Tanzania lijikite katika kuboresha ufanisi wa utendaji kazi ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na kutekeleza hatua madhubuti za kupunguza gharama.**

(v) **Kampuni ya Mkulazi** ilipata hasara kwa miaka mitatu mfululizo. Mwenendo huu wa hasara ulichangiwa na kuchelewa kuanza kwa uzalishaji wa sukari, kwani mpango wa awali wa uzalishaji wa sukari ulipaswa kuanza Septemba 2018, hata hivyo hadi kufikia mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2024 Kiwanda kilikuwa katika hatua za majaribio.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/24, ongezeko la hasara lilichangiwa na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji kwa kiwango cha juu kutoka shilingi bilioni 26.02 hadi shilingi bilioni 34.50, pamoja na kupungua kwa mapato kutoka shilingi bilioni 4.64 hadi shilingi bilioni 4.23.

**Ninapendekeza kampuni ya Mkulazi ijikite katika kuboresha ufanisi wa kazi ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na kutekeleza hatua madhubuti za kupunguza gharama.**

(vi) **Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibiolojia Tanzania**, utendaji wake ulikuwa duni katika mwaka wa fedha 2023/24 ambapo ulichangiwa na kushuka kwa mapato kwa asilimia 25, licha ya kupungua kwa asilimia nane kwa gharama za uendeshaji, na kupungua kwa asilimia 60 kwa gharama za uzalishaji. Bila Serikali kuchangia shilingi milioni 280.98, hasara ingeweza kufikia shilingi bilioni 4.39 katika mwaka wa fedha 2023/24.

**Ninapendekeza Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibiolojia Tanzania kiboreshe ufanisi wa utendaji kazi ili kuongeza ukusanyaji wa mapato.**

(vii) **Kiwanda cha Dawa Keko** kimeendelea kupata hasara kwa miaka sita mfululizo. Mnamo mwaka 2024, kiwanda kiliripoti hasara ya shilingi bilioni 1.84, ambapo hasara imepungua kwa asilimia tatu ikilinganishwa na hasara ya shilingi bilioni 1.89 iliyorekodiwa mwaka 2023. Kushuka huku kunatokana na kupungua kwa mauzo kwa asilimia 52, sambamba na kupungua kwa gharama za mauzo kwa asilimia 41. Sababu ya kuendelea kupata hasara katika Kiwanda cha Dawa Keko kutokana na uzalishaji mdogo, ambao haukidhi gharama

za uendeshaji, pamoja na utegemezi mkubwa kwa mteja mmoja tu, ambaye ni Bohari kuu ya Dawa. Utegemezi huu unazuia kampuni kuweza kutafuta masoko mapya nje ya Bohari kuu ya Dawa.

**Ninapendekeza Wizara ya Fedha iipatie Kiwanda cha Dawa Keko fedha kwa ajili ya kuongeza mtaji wa kiwanda ili kuwezesha ununuzi wa malighafi na vifaa vya kisasa vya uzalishaji na kuhakikisha ufanisi wa uzalishaji kulingana na viwango vya sasa vya utengenezaji dawa.**

(viii) **Shirika la Masoko ya Kariakoo** liliboresha kwa kiasi kikubwa utendaji wake wa kifedha mwaka 2023/24, na kupunguza hasara yake hadi kufikia shilingi bilioni 1.45 kutoka shilingi bilioni 41.57 mwaka 2022/23. Hasara ya mwaka uliopita ilichangiwa zaidi na uharibuifu wa jengo kwa shilingi bilioni 31.03 kufuatia janga la moto. Wakati hasara ya mwaka huu ilichangiwa na mapato kidogo ikilinganishwa na gharama, jumla ya mapato na gharama ilikuwa shilingi bilioni 1.53 na shilingi bilioni 3.72 mtawalia.

Ingawa kuungua kwa jengo hakukuwa sababu tena, Shirika la Masoko ya Kariakoo bado lilitegemea ruzuku ya Serikali ya shilingi bilioni 1.36 kwa mishahara ya wafanyakazi na malipo mengine katika mwaka wa fedha 2023/24 ikilinganishwa na ruzuku ya shilingi bilioni 1.18 mwaka 2022/23. Bila msaada huu, hasara halisi katika mwaka wa fedha 2023/24 ingekuwa shilingi bilioni 2.81 (shilingi bilioni 1.45 + shilingi bilioni 1.36).

Hasara inayoendelea katika Shirika la Masoko la Kariakoo inaleta wasiwasi. Pia, nilibaini kuwa soko jipya lililojengwa baada ya soko la zamani la Shirika la Masoko ya Kariakoo kuungua bado halijaanza kutumika. Ili kufikia uthabiti wa kifedha wa muda mrefu, shirika la masoko kariakoo linapaswa litanue wigo wa ukusanyaji wa mapato, litekeleze udhibiti wa gharama, na lipange upya usimamizi wa fedha ili kutumia kikamilifu rasilimali zake za kimkakati.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Masoko ya Kariakoo liharakishe kuanza kutumika kwa soko jipya na kuimarisha upatikanaji wa mapato, kutekeleza udhibiti wa gharama, na kurekebisha usimamizi wa fedha ili kutumia kikamilifu rasilimali zake za kimkakati.**

(ix) **Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania**, ambayo ni kampuni tanzu ya Shirika la Umeme Tanzania, ilipata ongezeko la hasara kutoka shilingi milioni 791.68 mwaka 2021/22 hadi shilingi bilioni 1.34 mwaka 2023/24, ikipelekea kampuni kuwa na changamoto kubwa ya kifedha.

Sababu kuu za kupata hasara ni gharama kubwa za uendeshaji hasa katika utekelezaji wa miradi na upungufu wa uwekezaji wa mtaji kutoka kwa kampuni mama ambayo ni Shirika la Umeme Tanzania. Kukosekana kwa uwekezaji wa mtaji wa kutosha kutoka kwa kampuni mama, kumepunguza uwezo wa kampuni kuongeza na kuendesha shughuli zake kwa ufanisi pamoja na kugharamia matumizi muhimu. Hivyo, kupata msaada wa ziada wa kifedha na kutekeleza hatua za kudhibiti gharama itasaidia Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania kuboresha utendaji wake wa kifedha.

**Ninapendekeza Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania iombe nyongeza ya mtaji kutoka Shirika la Umeme Tanzania au itafute vyanzo mbadala vya fedha ili kupunguza ukata wa fedha. Aidha, inapaswa kuchukua hatua za kupunguza matumizi ya uendeshaji ili kuimarisha hali ya kifedha.**

(x) **Katika kituo cha uwekezaji cha APC**, hasara imeongezeka katika mwaka wa fedha 2023/24 ikilinganishwa na mwaka 2022/23. Kupanda kwa hasara kulichangiwa na ongezeko la jumla ya gharama kwa shilingi milioni 968 kutoka shilingi bilioni 5.76 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 6.73. Ongezeko hilo la gharama lilichangiwa na ongezeko la gharama za mauzo kwa asilimia 32 kutoka shilingi milioni 717.48 hadi shilingi milioni 945.76 na gharama za utawala kwa asilimia 40 kutoka shilingi bilioni 1.21 hadi shilingi bilioni 1.70.

Wakati mapato yameongezeka kwa shilingi milioni 937 kutoka shilingi bilioni 4.39 hadi shilingi bilioni 5.32 sawa na ongezeko la asilimia 21. Gharama imeongezeka kwa kiwango cha juu zaidi kuliko ongezeko la mapato katika mwaka fedha 2023/24, na kusababisha hasara kubwa ikilinganishwa na mwaka uliopita. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa kulikuwa na upungufu wa asilimia 86 wa matumizi ya kumbi za mikutano, ambayo ni miongoni mwa biashara kuu ya APC, katika mwaka wa 2023/24.

**Ninapendekeza kuwa Kituo cha Uwekezaji cha APC kijikite katika kuboresha ufanisi wake wa utendaji kazi ili kuongeza ukusanyaji wa mapato kutokana na biashara kuu na kutekeleza hatua madhubuti za kupunguza gharama.**

(xi) Katika mwaka wa fedha 2023/24, **Soko la Bidhaa Tanzania** liliripoti hasara ya shilingi milioni 561.92, ikilinganishwa na shilingi milioni 793.76 mwaka wa 2022/23 na shilingi milioni 323.27 mwaka wa 2021/22. Hasara hii ilichangiwa nakuendelea kufanya kazi kwa misingi ya mnada, hivyo kutoza ada ndogo ya miamala au kutotoza

kabisa ada kwa baadhi ya bidhaa, jambo ambalo halilingani na gharama za uendeshaji.

Pia, ongezeko la gharama za uendeshaji kwa asilimia 17 (kutoka shilingi bilioni 2.00 hadi shilingi bilioni 2.33) lilichangia katika hasara ya mwaka wa fedha 2023/24. Licha ya kupokea ruzuku kutoka serikalini ya shilingi bilioni 1.33 na kuongezeka kwa mapato kwa asilimia 163, Soko la Bidhaa Tanzania iliendelea kufanya kazi kwa hasara.

**Ninapendekeza Soko la Bidhaa Tanzania lijikite katika kuboresha ufanisi wa utendaji kazi na kuangalia upya mtindo wa uendeshaji ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na kutekeleza hatua madhubuti za kupunguza gharama.**

## 4.2 Mashirika ya Umma Yasiyo na Ukwasi wa Kulipa Madeni ya Muda Mfupi

Wakati wa ukaguzi wa taarifa za fedha katika mashirika ya umma **217** kwa kipindi cha hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, nilibaini kuwa mashirika ya umma **64** yalikuwa na kiwango kikubwa cha madeni ya muda mfupi kuliko kiwango cha mali za muda mfupi kati ya mwaka mmoja hadi miaka mitatu. Kati ya hayo, mashirika **14** yalikuwa ya kibiashara na mashirika **50** ni yasiyo ya kibiashara.

Aidha, nilibaini kuwa uwiano kati ya mali na madeni ya muda mfupi (Jumla ya mali za muda mfupi/Jumla ya madeni ya muda mfupi) wa mashirika haya ulikuwa kati ya 0.00 hadi 0.96, wakati kiwango kinachokubalika ni uwiano wa 1:1 ambacho kinaashiria kuwa shirika lina mali za kutosha za muda mfupi kulipia madeni yake ya muda mfupi. **Kiambatisho Na. II** kinaonesha orodha ya mashirika ya umma yenye changamoto za ukwasi kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi miaka mitatu.

Hii ina maana kuwa mashirika **64** yana changamoto za ukwasi na uwiano unaoashilia usimamizi duni wa mtiririko wa fedha, au utegemezi mkubwa wa ukopaji wa muda mfupi. Kushindwa kulipa madeni kwa wakati kunaweza kusababisha shirika kutoaminiwa na wadau wake. Pia, kunaweza kupunguza uwezo wake wa kufanya kazi kwa ufanisi. Hali hii inaweza kukwamisha uwezo wa shirika kutoa huduma muhimu na kutimiza wajibu wake.

**Ninarudia pendekezo langu kuwa, mashirika husika ya umma yafanye mapitio ya kina ya bajeti zao ili kubaini maeneo yenye matumizi ya ziada au yasiyo na ufanisi, na kurekebisha mgao wa**

**bajeti kwa kuweka kipaumbele kwenye matumizi muhimu na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima.**

## 4.3 Mashirika ya Umma Yanayojiendesha kwa Kutegemea Mikopo kwa Kipindi cha Mwaka Mmoja hadi Miaka Mitatu

Mikopo ni mbinu ya kawaida katika uendeshaji wa mashirika ya umma.Hata hivyo, huongeza hatari za kifedha. Uwiano wa kukopa na mtaji, ni kipimo kinachoonesha ni kwa kiwango gani shughuli za shirika zinaendeshwa kwa mtaji wa shirika na mikopo. Uwiano huu ukiwa ni zaidi ya asilimia 100, unamaanisha kuwa shughuli za shirika kwa kiwango kikubwa zinaendeshwa kwa mikopo kuliko mtaji. Kwa maana nyingine ni kuwa shirika haliwezi kuendesha shughuli zake bila mikopo. Hali hii huliweka shirika katika hatari kubwa ya changamoto za kifedha hasa wakati wa kushuka kwa uchumi au mabadiliko ya mazingira ya biashara.

Ili kuhakikisha uwiano mzuri wa mikopo na mitaji ni muhimu sana kuweka juhudi za kuliepusha shirika kutoka katika hatari za kifedha. Pia, ni muhimu katika kuhakikisha uhimilivu na uendelevu wa shirika wa muda mrefu.

Katika ukaguzi wa mashirika ya umma ya kibiashara **52** kwa mwaka wa fedha wa 2023/24, nilibaini kuwa mashirika **15 (asilimia 29)** yalikuwa na uwiano wa mikopo usiofaa (Jumla ya mikopo kwa Jumla ya mtaji) unaozidi asilimia 100. Kati ya mashirika **15**, mashirika sita yalikuwa na uwiano hasi. Hii inaonesha utegemezi mkubwa wa mikopo katika uendeshaji wa shirika, na kuyaweka mashirika haya katika hatari zaidi ya kifedha zinazotokana na gharama kubwa za mikopo.

Hii ilisababishwa hasa na mikopo ya ziada, na gharama kubwa za kukopa kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya mikopo na riba. Hali hii inaathiri jitihada za kupata faida. Pia, inaathiri mtiririko wa fedha, ambapo sehemu kubwa ya mapato inaweza kuelekezwa kwenye kulipa madeni kuliko uendeshaji wa shughuli za shirika na ukuaji wake au uwekezaji wa mtaji.

Mashirika yenye uwiano wa mikopo, wa zaidi ya asilimia 100 kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi miaka mitatu yameorodheshwa kwenye **Jedwali Na. 6.**

**Jedwali Na. 6: Mwenendo wa mashirika yanayoendeshwa kwa kutegemea mikopo**

| Na. | Jina la Shirika | 2023/24 (Asilimia) | 2022/23 (Asilimia) | 2021/22 (Asilimia ) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kampuni ya Ushauri Elekezi wa Mazingira Jengekwa ya Chuo Kikuu Ardhi | 1137 | 1214 | - |
| 2 | Soko la Bidhaa Tanzania | 379 | - | - |
| 3 | Kituo cha Uwekezaji APC | 266 | 257 | - |
| 4 | Mamlaka ya Bandari Tanzania | 248 | 156 | 138 |
| 5 | Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania | 208 | 172 | - |
| 6 | Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme | 201 | 245 | 162 |
| 7 | Kampuni ya Uwekezaji ya TANOIL | 197 | 169 | - |
| 8 | Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania | 139 | 175 | - |
| 9 | Kampuni ya Ndege Tanzania | (344) | (247) | (310) |
| 10 | Kiwanda cha Dawa Keko | (368) | (697) | (581 026) |
| 11 | Kampuni ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam | (408) | (522) | (4140) |
| 12 | Kituo cha Kompyuta Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | (458) | (258) | (810) |
| 13 | Kampuni ya Gesi Tanzania | (725) | (783) | - |
| 14 | Kampuni ya STAMIGOLD | (3137) | (1997) | - |
| 15 | Shirika la Reli Tanzania | (84918) | 5493 | 2355 |

**Chanzo:** *Uchambuzi wa wakaguzi kutoka katika taarifa za fedha zilizotolewa 2023/24*

**Ninarudia mapendekezo yangu kwa mashirika ya umma husika; (a) yadhibiti utendaji wa kifedha na yatathmini athari inayoweza kutokea kutokana na mabadiliko yoyote kwenye soko au uchumi kwenye uwezo wa kutimiza majukumu yao; (b) yatathmini muundo wa mtaji na ulipaji wa deni ili kuzuia ukuaji wa riba unaotokana na kuchelewa kulipa deni, na (c) Serikali itathmini uwepo wa haya mashirika na kuangalia kama Serikali inahitaji kuendelea nayo au la.**

## 4.4 Mashirika ya Umma Yasiyo ya Kibiashara Yaliyopata Nakisi kwa Zaidi ya Mwaka Mmoja

Katika ukaguzi wa mashirika ya umma **157** yasiyo ya kibiashara kwa mwaka wa fedha 2023/24, nilibaini mashirika **28** yamekuwa yakifanya kazi kwa nakisi kwa zaidi ya mwaka mmoja. Hii ilichangiwa na ukusanyaji mdogo wa mapato ya vyanzo binafsi na utegemezi uliokithiri wa ruzuku ya Serikali.

Katika ripoti yangu ya mwaka wa fedha 2022/23, nilibaini mashirika ya umma **23** yasiyo ya kibiashara yaliyopata nakisi. Hata hivyo, katika mwaka huu wa 2023/24, idadi ya mashirika ya umma yaliyoripoti nakisi imeongezeka hadi kufikia 28, jambo linaloakisi ongezeko la mashirika ya umma matano ikilinganishwa na mwaka uliopita. Orodha ya mashirika ya umma yasiyo ya kibiashara yaliyopata nakisi kwa zaidi ya mwaka mmoja nimeyaainisha katika **Kiambatisho Na. III.**

**Ninarudia mapendekezo yangu kuwa: (a) Mashirika ya umma husika yajikite katika kuboresha ufanisi wa kiutendaji ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na kutekeleza hatua madhubuti za kupunguza gharama; na (b) Serikali iimarishe usimamizi wa mashirika haya kwa kuteua wajumbe wa bodi wenye utaalamu na ujuzi wa huduma husika zinazotolewa na mashirika hayo.**

## 4.5 Upungufu Uliobainika katika Uchangiaji wa Asilimia 15 ya Mapato Ghafi Kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali kwa miaka Miwilii Mfululizo

Nilibaini upungufu katika malipo ya asilimia 15 ya mapato ghafi kama mchango kwenye Akaunti ya Mfuko Mkuu wa Serikali kutoka mashirika ya umma kwa miaka miwili mfululizo kinyume na Kifungu cha 12 (3) cha Sheria ya Fedha za Umma sura ya 348 ambacho kinataka wakala wa Serikali, au shirika la umma ambalo linatoza na kukusanya ada kwa hudumu iliyotoa, kuchangia asilimia 15 ya mapato ghafi kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

Kati ya mashirika 18 ambayo yalitakiwa kulipa mchango wa asilimia 15, mashirika 11 yalichangia kiasi pungufu au kutokuchangia kabisa. Kutokana na hali hiyo, katika mwaka 2023/24, shilingi bilioni 103.98 hazikuchangwa na mashirika hayo kama inavyotakiwa kutoka katika mapato ghafi bila kuhusisha ruzuku ya Serikali. **Jedwali Na. 7** linaonesha mashirika ambayo yalitoa mchango kwa Serikali kwa kiasi au la.

Kushindwa kupeleka michango hii kunaikosesha Serikali mapato muhimu, hivyo kukwamisha uwezo wake wa kutoa ruzuku na huduma muhimu za umma.

**Jedwali Na. 7: Mashirika ya umma yaliyoshindwa kutuma mchango wa asilimia 15 kwa miaka miwili mfululizo**

| Na. | Jina la Shirika | 2023/24 Sh.000 | | | 2022/23 Sh.'000 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mchango Unaohitajika Asilimia 15 | Mchango Uliolipwa | mchango Usiolipwa | Mchango Unaohitajika Asilimia 15 | Mchango Uliolipwa | mchango Usiolipwa |
| 1 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | 21,023,630 | 150,000 | 32,300,042 | 20,292,000 | 500,000 | 19,792,000 |
| 2 | Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania | 13,489,467 | 12,757,402 | 732,065 | 11,921,819 | 11,099,972 | 821,847 |
| 3 | Shirika la Viwango Tanzania | 13,085,941 | 7,718,341 | 4,744,951 | 12,660,010 | 6,660,360 | 5,999,650 |
| 4 | Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania | 3,667,913 | 3,458,481 | 209,432 | 3,558,606 | 3,558,606 | 0 |
| 5 | Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania | 3,415,172 | 1,513,440 | -237,735 | 2,157,833 | 0 | 2,157,833 |
| 6 | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira | 2,852,077 | 1,008,516 | 1,843,561 | 2,038,141 | 300,000 | 1,738,141 |
| 7 | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 2,417,060 | 500,000 | 1,417,060 | 2,134,581 | 200,000 | 1,934,581 |
| 8 | Bodi ya Sukari Tanzania | 1,970,072 | 385,108 | 187,233 | 1,081,883 | 920,197 | 161,686 |
| 9 | Kituo cha Uwekezaji Tanzania | 1,355,364 | 0 | 1,355,364 | 810,546 | 0 | 810,546 |
| 10 | Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana | 768,024 | 345,697 | 422,327 | 548,180 | 51,379 | 496,801 |
| 11 | Mamlaka ya Bandari Tanzania | 216,474,939 | 155,702,971 | 60,771,968 | 195,037,494 | 418,457,674 | 0 |
| | **JUMLA** | **280,519,659** | **183,539,956** | **103,746,268** | **252,241,093** | **441,748,188** | **33,913,085** |

**Chanzo:** *Uchambuzi wa wakaguzi uliotokana na taarifa za fedha za mwaka 2023/24 na 2022/23*

Aidha, ukaguzi wangu ulibaini kuwa Mamlaka ya Bandari Tanzania inadaiwa michango ya muda mrefu yenye jumla ya shilingi bilioni 134.77 ikiwa ni malipo ambayo hayakuwasilishwa kwa mwaka 2019/20.

**Ninapendekeza Serikali iimarishe mifumo ya ufuatiliaji na utekelezaji ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria, ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu kwa mashirika ya umma kutofuata sheria. Pia, Msajili wa Hazina anapaswa kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha**

mashirika hayo yanatoa michango kwa wakati kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Fedha za Umma Sura ya 348

# Ufanisi wa Mashirika ya Umma Katika Kuimarisha Mazingira ya Kibiashara




# SURA YA TANO

# UFANISI WA MASHIRIKA YA UMMA KATIKA KUIMARISHA MAZINGIRA YA KIBIASHARA

## 5.0 Utangulizi

Ufanisi wa uendeshaji una jukumu kubwa katika kuboresha mazingira ya biashara kwa kuhakikisha kuwa mashirika yanaongeza uzalishaji, kuboresha utoaji wa huduma na kupunguza gharama za uendeshaji.

Sura hii inatathmini ufanisi wa mashirika ya umma katika kuwezesha ukuaji wa biashara kupitia majukumu, mikakati na sera zao. Inatathmini mipango muhimu inayolenga kuboresha hali ya biashara na kuendeleza ukuaji endelevu wa uchumi huku ikibainisha changamoto za kiutendaji ndani ya mashirika haya.

### 5.1 Shirika la Nyumba la Taifa

#### a) Utekelezaji Hafifu wa Mradi wa 711 Kawe Ulisababisha Madeni ya shilingi bilioni 49.09

Shirika la Nyumba la Taifa na Kampuni ya Ujenzi waliingia mkataba tarehe 4 Aprili 2014 kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa mradi wa Kawe 711 katika kiwanja Na. 711/1 wenye thamani ya shilingi bilioni 105.11, ikiwa ni pamoja na kodi ya ongezeko la thamani.

Kwa mujibu wa mkataba na taarifa ya utekelezaji wa mradi kwa mwaka wa fedha 2023/24 iliyopitiwa wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa kazi za ujenzi wa mradi huo zilianza tarehe 7 Novemba 2014. Hata hivyo, tarehe 1 Aprili 2018, kazi zilisitishwa kutokana na Shirika la Nyumba la Taifa kushindwa kutimiza wajibu wa malipo ndani ya muda uliowekwa kwenye mkataba. Hadi tarehe ya kusitishwa kwa kazi, mradi ulifikia asilimia 25 na mnamo Agosti 2022, Shirika la Nyumba la Taifa lilimlipa Mkandarasi malipo yake yaliyothibitishwa ambayo yalikuwa bado hayajalipwa.

Hata hivyo, baada ya muda, mkandarasi alikokotoa na kuwasilisha madai ya gharama za ziada ikiwemo mabadiliko ya mradi, kusitishwa kwa mradi, riba, na ongezeko la bei, ambapo jumla ya ongezeko lilifikia shilingi bilioni 49.09. Tarehe 13 Disemba 2023, Bodi ya Shirika la Nyumba la Taifa iliidhinisha ongezeko hilo la shilingi bilioni 49.09 ambalo ni sawa na asilimia 47 ya mkataba wa awali na kuathiri mwenendo wa gharama za mradi. Kwa maelezo zaidi kuhusu madai yaliyoidhinishwa, tafadhali rejea **Jedwali Na. 8.**

**Jedwali Na. 8: Maelezo ya mabadiliko yaliyoidhinishwa**

| Aina ya madai | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|
| Madai ya Mabadiliko ya mradi | 16,981,771 |
| Madai ya Kusimamishwa kwa Kazi | 647,330 |
| Madai ya gharama za huduma za kifedha (Riba) | 2,894,687 |
| Madai ya ongezeko la bei | 28,574,906 |
| **Jumla** | **49,098,695** |

***Chanzo:*** *Taarifa ya vikao vya bodi ya shirika la Nyumba la Taifa 2023/24*

Hali hii ilichangiwa na usimamizi duni wakati wa utekelezaji wa mradi bila kuhakikisha upatikanaji wa fedha. Kwa mtazamo wangu mabadiliko katika bei ya mkataba wa ujenzi yatakuwa na athari kubwa kwa gharama ya jumla ya mradi, na kufanya mradi kuwa ghali zaidi na pengine kuathiri bei za nyumba zinazojengwa.

**Ninapendekeza Shirika la Nyumba la Taifa: (a) lihakikishe kuwa fedha za kumalizia mradi zinatengwa ili kuepuka tena kusitishwa kwa mradi na kwa siku zijazo, kuhakikisha kuwa hakuna mradi utakaoanzishwa bila ya kuwa na uhakika juu ya upatikanaji wa fedha ili kufanya malipo ya madai ya wakandarasi kwa wakati; na (b) kufanya uchambuzi wa kifedha wa kina ili kuweka bei za mauzo ya nyumba ambazo zitawawezesha kufikia malengo ya mauzo kama ilivyopangwa awali.**

### b) Miradi ya Ubia Ambayo Haijakamilika kwa Kipindi cha Zaidi ya Miaka 11 mpaka 27

Kifungu 4.1.4 cha Sera ya Ubia ya Shirika la Nyumba la Taifa ya mwaka 2022 kinaeleza kuwa, malengo ya ubia ni pamoja na kuendeleza viwanja muhimu, ambapo majengo yaliyopo kwenye viwanja hivyo yanaonekana kukosa ubora kutokana na udhaifu wa muundo wa jengo. Pia, Shirika linalenga kuzingatia kanuni za mipango miji zinazohitajika.

Kupitia mapitio ya utekelezaji wa miradi ya ubia, nilibaini kuwa miradi 24 ya ubia ilikuwa haijakamilika kwa kipindi kilichokuwa kinatofautiana kwa miaka 11 hadi 27 tangu kusainiwa kwa mikataba, ingawa ujenzi wake ulipangwa kukamilika ndani ya miaka miwili hadi mitatu kuanzia tarehe ya mkataba, kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. IV.** Hata hivyo, licha ya uwepo wa miradi hii ambayo haijakamilika kwa muda mrefu katika mwaka wa fedha 2023/24, Shirika la Nyumba la Taifa limesaini mikataba mipya ipatayo 20 ya ubia.

Hali hii ilitokana na udhibiti duni wa usimamizi katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi. Ninaamini kuanzishwa kwa miradi mipya ya

ubia huku mingine ikiwa imesitishwa uendelezaji wake kwa kipindi cha kuanzia miaka 11 hadi 27 kunahatarisha ukuaji wa Shirika kwa ujumla wake na matumizi ya rasilimali zake, kwani kunasababisha kufunga rasilimali zake kwenye miradi ambayo haitazalisha faida.

**Ninapendekeza Shirika la Nyumba la Taifa liandae mikakati ya utekelezaji ili kuhakikisha miradi yote iliyokwama inakamilika, ama kwa Shirika kuchukua usimamizi wake moja kwa moja au kwa kuhakikisha mshirika anakuwa na wajibu wa kukamilisha mradi na akishindwa kukamilisha atalipa adhabu na fidia kwa hasara ya mapato iliyopatikana kwa Shirika.**

## 5.2 Kituo Cha Uwekezaji Tanzania

### a) Kucheleweshwa kwa Uchakataji na Uidhinishaji wa Vyeti vya Motisha kwa Wawekezaji

Wakati wa ukaguzi, nilibaini ucheleweshaji katika uidhinishaji wa vyeti vya motisha kwa wawekezaji, ambapo muda wa uidhinishaji mara kwa mara ulizidi kikomo cha siku saba za kazi kama ilivyobainishwa na Kifungu cha 18 (4) cha Sheria ya Uwekezaji ya Tanzania ya mwaka 2022. Kwa mfano, nilibaini kuwa maombi 178 sawa na asilimia 25 ya vyeti vya motisha 705, yaliidhinishwa kwa kuchelewa kati ya siku saba hadi siku 417. Vilevile, nilibaini ucheleweshaji wa hadi siku 336 katika uchapishaji wa vyeti vya motisha, jambo ambalo ni kinyume na Kifungu cha 18 (4) cha Sheria ya Uwekezaji ya Tanzania ya mwaka 2022.

Hali hii ilichangiwa na kutokuwepo kwa mifumo ya udhibiti na ufuatiliaji pamoja na vigezo vya utendaji vya kufuatilia maendeleo ya idhini ya maombi tangu tarehe ya kuwasilishwa. Ucheleweshaji kama huu unaweza kuzuia uwezo wa waombaji kutumia fursa zilizopo, hivyo kuathiri matokeo ya maendeleo ya kiuchumi au ya kibiashara.

**Ninapendekeza Kituo cha Uwekezaji Tanzania kiwe na utaratibu wa ufuatiliaji wa mara kwa mara wa maombi ya wawekezaji kwa kuandaa ripoti itakayoelezea sababu za ucheleweshaji wa idhini kwa kila ombi na hii itasaidia uboreshaji wa mchakato wa maombi na dosari kutatuliwa kwa wakati.**

### b) Kituo cha uwekezaji Tanzania Hakina Programu ya Uhamasishaji Katika Uwekezaji

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa Kituo cha uwekezaji Tanzania hakina programu ya kukuza uwekezaji ili kusaidia kutambua fursa za kimkakati na wawekezaji watarajiwa. Pia nilibaini hitaji la programu la kukuza uwekezaji halijawasilishwa kwenye Bodi ya wakurugenzi, kwani haijawahi kujadiliwa kama ajenda hadi tarehe 30 Juni 2024. Hii inakuwa ni kinyume na Kanuni ya 27(1-3) ya Kanuni za Uwekezaji Tanzania za mwaka 2023, ambayo inakitaka Kituo cha Uwekezaji Tanzania kuandaa na kuwasilisha programu ya kukuza uwekezaji kwenye Bodi ili kuidhinishwa.

Kwa maoni yangu, hii inaweza kusababisha kukosa fursa za kimkakati na kukatisha tamaa wawekezaji.

**Ninapendekeza Kituo cha uwekezaji Tanzania kihakikishe kuwa programu ya kukuza uwekezaji inatayarishwa na kuwasilishwa kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa ajili ya kuidhinishwa na baadaye kutekelezwa.**

## 5.3 Shirika la Reli Tanzania

### a) Shirika la Reli Tanzania Lilishindwa kwa Asilimia 67 Kutekeleza Masharti ya Makubaliano ya Kibiashara Katika Usafirishaji wa Mizigo

Aya ya 3.4 ya Muundo wa Shirika la Shirika la Reli Tanzania, iliyoidhinishwa Mei 2018, ilianzisha Kurugenzi ya Maendeleo ya Biashara yenye jukumu la kutoa utaalamu katika maendeleo ya biashara, masoko, utafiti, na kutafuta fursa za biashara za ndani na nje ya nchi. Ili kufikia malengo haya, Shirika la Reli Tanzania liliingia katika makubaliano na makampuni makubwa kwa ajili ya kuwasafirishia mizigo yao.

Katika mapitio yangu ya mikataba na makubaliano na wasambazaji wakuu wanne wa mizigo, nilibaini kuwa Shirika la Reli Tanzania lilishindwa kutekeleza kwa asilimia 67 masharti ya makubaliano. Hadi tarehe 30 Juni 2024, Shirika la Reli Tanzania lilikuwa limesafirisha tani 115,400 pekee (sawa na asilimia 33) kati ya tani 351,038 zilizotakiwa kusafirishwa. Hii inamaanisha kuwa Shirika la Reli Tanzania halikuweza kusafirisha tani 235,638 (asilimia 67). Hali hii, ilichangiwa na treni zisizo na ufanisi. Maelezo zaidi angalia **Jedwali Na. 9.**

**Jedwali Na. 9: Tathmini ya Utendaji duni wa usafirishaji mizigo**

| Na. | Jina la Kampuni | Tani zilizokubaliwa kusafirishwa (A) | Tani halisi zilizosafirishwa (B) | Tofauti ya tani (A-B) | Asilimia ya utendaji duni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kampuni ya 1 | 252,000 | 70,920 | 181,080 | 72 |
| 2 | Kampuni ya 2 | 70,238 | 33,160 | 37,078 | 53 |
| 3 | Kampuni ya 3 | 9,600 | 4,920 | 4,680 | 49 |
| 4 | Kampuni ya 4 | 19,200 | 6,400 | 12,800 | 67 |
| **JUMLA** | | **351,038** | **115,400** | **235,638** | **67** |

**Chanzo:** *Taarifa ya utekelezaji ya mwaka wa fedha 2023/24*

Hali hiyo inaweza kusababisha kuchelewesha kufikia malengo yaliyokusudiwa na Shirika la Reli Tanzania. Ili kutatua suala hilo, Shirika la Reli Tanzania linakusudia kununua injini mpya kumi za treni hadi mwisho wa Juni 2025. Injini nyingine nane za ziada zinatarajiwa kununuliwa ifikapo robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2024/25.

**Ninapendekeza Shirika la Reli Tanzania kuharakisha mchakato wa ununuzi wa injini mpya za treni na kuhakikisha uwazi na uzingatiaji wa sheria za ununuzi na kuweka mfumo wa ufuatiliaji unaoeleweka ili kufuatilia maendeleo na kupunguza ucheleweshaji wowote unaoweza kutokea.**

### b) Kutokufanikiwa kwa Lengo Mkakati la Utoaji Huduma za Usafiri wa Treni za Abiria katika Mkoa wa Dar es Salaam kwa Asilimia 72

Mpango Mkakati wa Shirika la Reli Tanzania wa mwaka 2019/20 hadi 2023/24 pamoja na ripoti ya utekelezaji wake kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024 inaonesha kuwa Shirika lilianzisha huduma za treni za abiria za Pugu na Ubungo ili kuongeza mapato na kupunguza msongamano wa watu ndani ya Jiji la Dar es Salaam. Lengo la uwezo wa kusafirisha abiria lililowekwa lilikuwa abiria 4,231,513 kwa mwaka wa fedha 2018/19 na kuongezeka hadi abiria 10,696,977 kufikia mwaka 2023/24, kama ilivyoainishwa katika Mpango Mkakati wa mwaka 2019/20 hadi 2023/24.

Hata hivyo, mapitio yangu ya utendaji wa Shirika yalibaini kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, Shirika lilikuwa limesafirisha abiria wapatao 3,053,428 sawa na asilimia 28, huku lengo likiwa halijafikiwa kwa abiria wapatao 7,643,549 sawa na asilimia 72. Kutofikia lengo kulitokana na ushindani ambao Shirika linakabiliana nao, ikiwa ni pamoja na ruti mpya za mabasi na uhamisho wa kituo cha mabasi cha abiria kwenda Kamata, Kariakoo. Pia, kuna ukosefu

wa treni za kisasa na zenye uwezo wa kutoa huduma bora za abiria zinazoweza kushindana kwa ufanisi.

Kwa maoni yangu, hii inaweza kusababisha Shirika kutofikia malengo yake ya mapato iliyoyakusudia. Zaidi, Shirika halitofikia lengo la kupunguza msongamano wa watu katika Jiji la Dar es Salaam.

Shirika la Reli Tanzania lilieleza kuwa liko katika mchakato wa kununua treni nne ambazo zitatoa huduma inayofaa kwa abiria.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Reli Tanzania liongeze kasi ya mchakato wa kupata treni mpya au kufanyia matengenezo treni zilizopo ili kuwezesha mzunguko wa haraka na wa ufanisi kwa abiria.**

## 5.4 Shirika la Mawasiliano Tanzania

### Kushindwa Kufikia Malengo ya Huduma za Maunganisho ya Faiba Mlangoni kwa Wateja Asilimia 93

Katika ukaguzi wangu nilibaini tofauti kubwa kati ya lengo la utendaji na mafanikio halisi ya maunganisho ya faiba mlangoni kwa mwaka wa fedha 2023/24. Idadi halisi ya maunganisho hadi mwishoni mwa mwaka wa fedha 2023/24 ilikuwa nyumba 10,781, ambayo ni sawa na asilimia 7 ya lengo lililopangwa la nyumba 150,000 kwa kipindi hicho. Aidha, nilibaini Shirika halikufikia lengo kwa nyumba 139,219 (sawa na asilimia 93), ambazo hazikuunganishwa kama ilivyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Shirika wa mwaka 2022/23 hadi 2026/27.

Hali hii ilisababishwa na ukosefu wa rasilimali fedha kwa ajili ya miundombinu na vifaa vya kutosha kuhakikisha kuwa nyumba zinaunganishwa kwenye huduma ya faiba mlangoni. Hii inaweza kusababisha kupotea kwa fursa za mapato, kuzuia utendaji wa kifedha wa shirika na uwezo wake wa kutoa huduma ya faiba kwa umma, na hivyo kuathiri ukuaji wa biashara na uchumi.

**Ninapendekeza Shirika la Mawasiliano Tanzania litafute vyanzo mbadala vya ufadhili kama vile mikopo ya benki ili kuhakikisha kuwa lengo lililopangwa la maunganisho ya huduma za faiba mlangoni linatimizwa kama ilivyopangwa.**

## 5.5 Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania

### Kutoanzishwa kwa Studio ya Uzalishaji wa Maudhui ya Kidijitali

Katika mapitio ya Mpango Mkakati wa utekelezaji wa mwaka 2022/23 hadi 2026/27, nilibaini kuwa Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania ilikuwa imelenga kuanzisha studio kamili ya uzalishaji wa maudhui ya kidijitali ifikapo Disemba 2023. Uzalishaji kamili wa maudhui ya kidijitali ungeweza kusaidia kampuni kupanua mawanda yake, kukidhi ufanisi wa juu kulingana na gharama, kunyumbulika, na kuwa na uwezo wa kushirikisha watazamaji.

Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi mwezi Januari 2025, studio ya uzalishaji wa maudhui ya kidijitali haikuwa imeanzishwa.Tatizo hili lilichangiwa na ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi, jambo ambalo linadhoofisha uwezo wa Kampuni ya magazeti ya Serikali Tanzania kushindana katika sekta ya habari za kidijitali. Pia, linapunguza wigo mpana wa maudhui ya habari.

**Ninapendekeza Serikali kupitia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuipatia fedha za bajeti Kampuni ya Magazeti ya Serikali ili kusaidia utekelezaji wa uanzishwaji wa studio kwa ajili ya uzalishaji wa Maudhui ya Kidijitali ili kuiwezesha kampuni kufikika katika wigo mpana na kuwa na uwezo wa kushirikisha watazamaji wengi.**

## 5.6 Kampuni ya Ndege Tanzania

### a) Ndege Zisizotumika kwa Muda Mrefu za Kampuni ya Ndege Tanzania

Aya ya 1.4.6.2 ya Mwongozo wa Taratibu za Matengenezo wa mwaka 2024 kinaeleza kuwa mojawapo ya majukumu ya Afisa Mkuu wa Matengenezo ni kutekeleza matengenezo ya ndege yaliyoratibiwa na yasiyoratibiwa kwenye uwanja na kuhakikisha kuwa matengenezo yanafanyika kwa wakati uliopangwa.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa ndege nne aina ya Airbus A220 zilikaa bila kutumika kwa muda wa siku 279 hadi 721 hadi kufikia mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2024. Kampuni ya Ndege Tanzania iliripoti kuwa ndege hizo zimekaa bila kutumika kwa muda mrefu kutokana na utendaji duni wa ndege hizi aina ya Airbus A220. Hii ni kwa sababu ndege hizi zilitengenezwa zikiwa na huduma duni za ukarabati baada ya uuzaji, kama vile upatikanaji wa vipuri vya injini na vipuri vingine.

Ukaguzi zaidi ulibaini kuwa, Kampuni ya Ndege Tanzania ilitumia gharama zisizobadilika shilingi bilioni 9.16 kwa ndege hizo aina ya Airbus A220 ambazo zilikaa bila kutumika katika mwaka 2023/24 huku Kampuni ikipata shilingi bilioni 5.49 kama motisha ya kukodisha kutoka kwa Wakala wa Ndege za Serikali. Kiasi hiki kilifidia asilimia 60 pekee ya jumla ya gharama zisizobadilika zilizotumika kwa ndege za Airbus ambazo hazikuwa zimetumika kwa muda mrefu.

Hii ilitokana na upembuzi yakinifu usiotosheleza kabla ya kununua ndege na kutozingatia masharti ya mkataba wa ununuzi wa ndege kuhusu kudai fidia za matengenezo ya injini pindi zinapo haribika katika kipindi cha waranti. Matokeo yake, kampuni inaingia gharama zisizo za lazima ambazo zingeweza kufidiwa kupitia waranti.

**Ninapendekeza kuwa Kampuni ya Ndege Tanzania (a) ishirikiane na Serikali kutathmini changamoto za kiufundi zinazohusiana na ndege za Airbus A220 ili kubaini kama inawezekana kuendelea kufanya kazi kwa mtindo huu, (b) Ifanye utafiti kuhusu aina za ndege zinazofaa zaidi kwa ajili ya kufanya kazi kwa ufanisi, kwa kuzingatia vigezo vya kiuchumi na hali ya kijiografia, na (c) ishirikiane na Wakala wa Ndege za Serikali kufanya mapitio ya kina ya mikataba ya ununuzi wa ndege na matengenezo ili kutambua na kudai fidia ya ndege kutofanya kazi wakati zikiwa kwenye matengenezo chini ya muuzaji.**

### b) Matengenezo na Ukarabati usio na Tija kwa Ndege DASH 8 Q300 (5H-MWF) Uliogharimu shilingi bilioni 20.63

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa jumla ya shilingi bilioni 20.63 zilitumika kwa ajili ya matengenezo na bima ya ndege aina ya DASH 8 Q300 (5H-MWF) tangu ilipopelekwa Malta kwa ajili ya matengenezo Novemba 2020. Ndege hiyo ilikuwa haijatumika kwa zaidi ya miaka saba, ikiwa ni pamoja na takribani miaka minne ya matengenezo ambayo hayakufanikiwa wakati huo. Licha ya gharama iliyotumika na mapato yaliyokosekana kutokana na kutotumika kwa ndege hiyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024.

Sababu kuu zilizoainishwa ni pamoja na kupitwa na wakati kwa muundo wa ndege na kusababisha changamoto katika upatikanaji wa vipuri huku kampuni ya Ndege Tanzania ikishindwa kutathmini uwezekano wa kiuchumi wa kufanya ukarabati wa ndege kabla ya kuingia gharama hizo. Kutokana na hali hiyo, kampuni ya Ndege

Tanzania imepata hasara kubwa ya kifedha na kupungua kwa uwezo wa kufanya kazi.

**Ninapendekeza kuwa Kampuni ya Ndege Tanzania ifanye tathmini kulingana na hali ya sasa ya sekta ya ndege na mahitaji ya soko ili kuboresha utendaji kazi wa ndege ya DASH 8 Q-300**(5H-MWF)**, kwa kuzingatia hali yake na upatikanaji wa vipuri.**

### c) Kodi na Tozo za Akiba ya Matengenezo ya Ndege ambazo Hazijalipwa kwa Miaka Sita Mfululizo shilingi bilioni 369.13

Kifungu cha 4.1 cha Mikataba ya Ukodishaji wa Ndege kati ya Wakala wa Ndege wa Serikali na Kampuni ya Ndege Tanzania kinamtaka Mkodishwaji (Kampuni ya Ndege Tanzania) kulipa ada ya kudumu ya kukodisha ndege ya kila mwezi kwa Mkodishaji (Wakala wa Ndege za Serikali).

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa katika kipindi cha miaka sita mfululizo, tozo za ukodishaji zisizolipwa na Kampuni ya Ndege Tanzania ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 27.89, zilizoripotiwa tarehe 30 Juni 2018, hadi kufikia shilingi bilioni 369.13 tarehe 30 Juni 2024, kama ilivyofafanuliwa katika **Jedwali Na 10**. Malipo yaliyolimbikizwa katika mwaka wa fedha wa 2023/24 (shilingi bilioni 369.13 ) ni sawa na asilimia 63 ya jumla ya madeni yote ya sasa iliyoripotiwa kwenye hesabu za Shirika (shilingi bilioni 595) hadi tarehe 30 Juni 2024.

**Jedwali Na. 10: Gharama za kukodisha ndege kwa miaka sita mfululizo**

| Na. | Mwaka | Maelezo | Kiasi -Sh '000 |
|---|---|---|---|
| 1 | 2018/19 | Gharama za kukodisha ndege | 27,890,014 |
| 2 | 2019/20 | Gharama za kukodisha ndege | 43,050,837 |
| 3 | 2020/21 | Gharama za kukodisha ndege | 54,779,766 |
| 4 | 2021/22 | Gharama za kukodisha ndege | 47,761,687 |
| 5 | 2022/23 | Gharama za kukodisha ndege | 86,709,861 |
| 6 | 2023/24 | Gharama za kukodisha ndege | 108,939,560 |
| | | | 369,131,725 |

**Chanzo:** *Taarifa za fedha za kampuni ya ndege 2018/19-2023/24*

Hii ilichangiwa na gharama kubwa ya uendeshaji na matengenezo ya Ndege yaliyofanywa na Kampuni ya Ndege Tanzania, kupata hasara ya kifedha katika miaka sita mfululizo.

**Ninapendekeza Kampuni ya Ndege Tanzania na Wakala wa Ndege wa Serikali wa Tanzania wajadiliane na kuweka mpango wa**

**malipo wa kodi na tozo za ukodishaji ndege. Mpango huu ujumuishe pamoja na urekebishaji wa deni, kuongeza muda wa malipo, na kupunguza tozo za kila mwezi ili kampuni ya Ndege Tanzania iweze kumudu kuzilipa.**

## 5.7 Kampuni ya Huduma ya Meli

### a) Kuchelewa Kuanza kwa Miradi Minne Mikubwa yenye Thamani ya shilingi bilioni 8.89 na dola za Marekani milioni 251.07

Nilibaini kuwa hadi kufikia tarehe 20 Disemba 2024, Kampuni ya huduma za Meli ilikuwa haijaanza utekelezaji wa miradi mikubwa minne, ambayo inahusisha ukarabati wa meli, ujenzi wa eneo la meli na ujenzi wa kivuko kipya cha gati. Miradi hii ilipangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2023/24 na mikataba ilikuwa tayari imesainiwa na wakandarasi. Ucheleweshaji huo ulitokana na Kampuni ya Huduma za Meli kushindwa kutimiza masharti ya malipo ya awali yaliyotakiwa na wakandarasi, ambayo ni shilingi bilioni 1.33 na dola za Marekani 36,401, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 11**.

Hii inaweza kukwamisha Kampuni kufikia malengo yake ya muda mrefu na kukosa faida zilizotarajiwa za miradi hii kwa umma.

**Jedwali Na. 11: Miradi iliyochelewa kutekelezwa**

| Na. | Namba ya Mkataba. | Maelezo | Tarehe ya kusainiwa mkataba | Kiasi cha mkataba Sh. '000 | Malipo ya awali Sh. '000 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PA/115/2022-2023/HQ/W/06 | Ukarabati wa MT Nyangumi katika Ziwa Viktoria | 17/11/2023 | 8,892,804 | 1,333,920 |
| **Jumla** | | | | **8,892,804** | **1,333,920** |
| **Na.** | **Namba ya mkataba.** | **Maelezo** | **Tarehe ya kusainiwa mkataba** | **Kiasi cha mkataba Dola za Marekani. '000** | **Malipo ya awali Dola za Marekani. '000** |
| 2 | PA/115/2022-2023/HQ/W/05 | Ujenzi wa uwanja wa meli katika Ziwa Tanganyika | 11/10/2023 | 129,436 | 18,995 |
| 3 | PA/115/2022-2023/HQ/W/04 | Ujenzi wa kivuko kimoja kipya cha RoRo & Wagon chenye uwezo wa kubeba tani 3,500 | 11/10/2023 | 63,467 | 9,100 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | katika Ziwa Tanganyika 11/10/2023 | | | |
| 4 | PA/115/2022-2023/HQ/W/03 | Ujenzi wa kivuko kimoja kipya cha RoRo & Wagon chenye uwezo wa kubeba tani 3,500 katika Ziwa Tanganyika 11/10/2023 | 11/10/2023 | 58,171 | 8,305 |
| **Jumla** | | | | **251,075** | **36,401** |

**Chanzo***: Mafaili ya mikataba kwa mwaka wa fedha 2023/24*

**Ninapendekeza Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi, itoe fedha kwa Kampuni ya Huduma za Meli kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kulingana na makadirio ya bajeti ili kuwezesha utekelezaji wa miradi kwa wakati.**

## 5.8 Mamlaka ya Bandari Tanzania

### a) Kutorejeshwa kwa Mzani wa Kupimia Mizigo Ulioharibika Katika Bandari ya Kibirizi- Kigoma

Katika ukaguzi wa usimamizi wa Bandari ya Ziwa Tanganyika, iliyopo mkoa wa Kigoma, nilibaini kuwa tarehe 30 Machi 2024, mzani wa kupimia mizigo katika Bandari ya Kibirizi uliharibika kutokana na kufurika kwa Ziwa Tanganyika na kufunika eneo la mzani. Hata hivyo, hadi kufikia wakati wa ukaguzi, Januari 2025, mzani ulikuwa haujatengenezwa tena, licha ya kuwa ni muhimu sana kwa shughuli za kila siku za bandari. Kupitia mahojiano niliyofanya na wasimamizi nilibaini kuwa, kutokana na kukosekana kwa mzani, uzito wa mizigo ulikuwa unakadiriwa kulingana na uzoefu wa awali na mazoea kwa aina ya bidhaa zinazoshughulikiwa.

Ukaguzi zaidi ulibaini kuwa, mnamo tarehe 1 Novemba 2024, Mamlaka ya Bandari Tanzania, kupitia barua yenye Kumb Na. TA.317/639/01/12 iliomba Wakala wa Vipimo kuhakiki mzani kwa ajili ya matengenezo. Wakala wa vipimo alikamilisha uhakiki wake tarehe 16 Januari 2025 na kutoa mwongozo kwa Mamlaka ya Bandari kuhusu mahitaji ya matengenezo ya mizani. Hata hivyo, Mzani katika Bandari ya Kibirizi bado ulikuwa haujakarabatiwa hadi kufikia mwishoni mwa ukaguzi wangu tarehe 30 Januari 2025, ikiwa ni sawa na kipindi cha miezi 10 kuanzia tarehe ya kuharibika kwa mzani tarehe 30 Machi 2024.

Ucheleweshaji huu ulitokea kwa sababu Mamlaka ya Bandari ilichelewa kukabidhi mizani kwa Wakala wa Vipimo kwa ajili ya kurekebishwa. Kwa maoni yangu, kukosekana kwa mizani inayofanya kazi kunaweza kusababisha makadirio ya uzito wa mizigo yasiyo sahihi, na kusababisha ankara zisizo sahihi

**Ninapendekeza Mamlaka ya Bandari Tanzania ifikirie suluhisho la muda, kama vile kutumia mizani inayohamishika, ili kuhakikisha usahihi wa upimaji wa mizigo wakati mchakato wa ununuzi au matengenezo ya mzani wa kudumu yakiendelea.**

## 5.9 Shirika la Umeme Tanzania

### a) Ucheleweshaji wa Malipo ya Fidia kwa Waathirika wa Miradi ya Umeme shilingi bilioni 17.94

Ukaguzi wa nyaraka za miradi na taarifa za maendeleo zinazohusiana na njia za usafirishaji wa umeme kutoka Pugu hadi Dundani na kutoka Tunuru hadi Masasi zinaonesha kuwa mikataba miwili ilisainiwa kabla ya maridhiano ya masuala ya ardhi kuhusu fidia, ambapo Shirika la Umeme Tanzania lilitakiwa kulipa shilingi bilioni 17.94 ikiwa ni fidia kwa waathirika wa mradi. Hata hivyo, hadi kufikia wakati wa ukaguzi tarehe 31 Agosti 2024, waathirika wa mradi walikuwa hawajalipwa fidia. Hii ni kinyume na Kifungu cha 11(1) cha Sheria ya Utwaaji Ardhi Sura ya 118 **(Rejea Jedwali Na. 12).**

Mapitio zaidi yalibaini kuwa, licha ya kumbusho lililotumwa kupitia barua zenye kumbukumbu Na.DMSPRI/DP/MPID/PC/PM/SGR-5/2024029 na MD/MESG/SURVEY/21 za tarehe 28 Agosti 2024 kutoka Shirika la Umeme Tanzania kwenda Wizara ya Uchukuzi kwa ajili ya kuomba kupelekwa fedha za fidia ya ardhi kwa ajili ya Njia ya Kusafirisha Umeme ya SGR kutoka Pugu hadi Dundani. Hata hivyo, hakuna malipo yoyote yaliyokuwa yametolewa hadi ukaguzi unakamilika.

Ucheleweshaji huu wa utekelezaji wa mradi unaweza kusababisha hatari ya kuongezeka kwa gharama za mradi.

**Jedwali Na. 12: Kuchelewesha malipo ya fidia kwa waathirika wa mradi**

| Na. | Namba ya Mkataba | Maelezo ya mkataba | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|---|---|
| 1 | PA/001/2022-23/HQ/W/66B | Usanifu wa Uhandisi, Ugavi, Ufungaji, Upimaji na kukabidhi wa 220/33kV, Laini ya Usafirishaji kutoka Pugu hadi Dundani. | 4,142,670 |
| 2 | PA/001/2022-23/HQ/W/67 - Sehemu ya Pili | Upimaji na Utumaji wa njia ya Kusambaza umeme ya 220KV kutoka Tunduru hadi Masasi, Kuanzishwa kwa kituo kidogo cha 220/33KV 2x60MVA huko Masasi na Upanuzi wa 220KV katika Kituo Kidogo cha Tunduru - Sehemu ya Pili | 13,800,000 |
| | | | **17,942,670** |

**Chanzo:** *Ripoti za maendeleo ya mradi na hati za mkataba*

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania (a) liwasiliane na Wizara ya Uchukuzi na mamlaka nyingine zinazohusika, zikiwemo Wizara ya Fedha na Shirika la Reli Tanzania, kushughulikia kero zote zinazohusu fedha za fidia, kuhakikisha malipo ya haraka kwa wahusika na kuepuka ucheleweshaji wa miradi; na (b) lihakikishe kuwa, katika siku zijazo, mikataba ya kandarasi zinazohitaji fidia inaingiwa mara tu baada ya masuala ya ardhi kukamilika.**

### b) Ongezeko la Madai katika Miradi ya GRID IMARA Iliyofikia shilingi bilioni 440

Shirika la Umeme Tanzania linatekeleza Miradi ya Uimarishaji wa Gridi ya Taifa yenye gharama inayokadiriwa kufikia Dola za Marekani milioni 1,945.49 (sawa na shilingi trilioni 4.9). Miradi hiyo inahusisha ujenzi wa njia za kusafirisha na kusambaza umeme, uanzishaji wa vituo vidogo na vituo vya kubadilishia umeme, uboreshaji wa vituo vidogo vilivyopo, ununuzi wa vifaa mbalimbali vinavyotumika kusambaza umeme kwa wateja, na uimarishaji wa gridi ya taifa unaofadhiliwa na Serikali.

Ukaguzi wangu wa utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa GRID IMARA umebaini kuwa kuna miradi 27 inayoendelea katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Hata hivyo, nilibaini changamoto zinazohusiana na ulipaji wa madai ya miradi kwa wakati, ikijumuisha malipo ya awali, fidia na tathmini kwa waathirika wa mradi, na malipo ya wakandarasi. Hali hii imekuwa mbaya zaidi, kwani madai ambayo hayajalipwa yameongezeka kutoka shilingi bilioni 240.27

mwishoni mwa mwaka wa fedha 2022/23 hadi shilingi bilioni 440 katika mwaka wa fedha 2023/24.

Hii ilitokana na Wizara ya Fedha kuchelewa kutolewa kwa fedha. Nina maoni kuwa, kwa kuwa baadhi ya madai yalianzia tarehe 15 Machi 2023, na zaidi ya miezi 15 imepita bila kutatuliwa, mradi huo uko katika hatari kubwa ya kupata riba na adhabu, ambayo itaongeza gharama ya mradi.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania lianzishe majadiliano na Mkandarasi kuhusu ratiba za malipo ili kupunguza hatari ya adhabu ya riba. Aidha, kabla ya kuanza kwa awamu nyingine, Shirika la Umeme Tanzania linapaswa lihakikishe kuwa fedha zinapatikana kabla ya utekelezaji wa miradi hiyo.**

### c) Kuwepo kwa Nguzo Ambazo ni Kinyume na Maelekezo ya Kampuni shilingi bilioni 1.41

Aya ya 1.26.5 ya Mwongozo wa Maelekezo ya Uhandisi wa Usambazaji ndani ya Shirika la Umeme Tanzania (Toleo la 9) inasema kuwa, nguzo zinazopaswa kutumika zinapaswa ziwe na urefu wa mita 11 na 12 kwa nguzo za kati au ngumu (kulingana na muundo na ukubwa wake). Matumizi ya nguzo imara yenye urefu wa mita 13 yanachukuliwa kuwa ni muundo wa zaidi ya mahitaji ya urefu unaotakiwa na hauapaswi kutumika, isipokuwa kwa maeneo maalumu tu kama vile sehemu za kuvuka mabonde marefu.

Katika ukaguzi wa hesabu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024, nilibaini kuwa wazabuni waliwasilisha jumla ya nguzo 36,818, kila moja ikiwa na urefu wa mita 8. Kati ya hizo nguzo 8,876 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.41, zilibakia hadi kufikia mwisho wa mwaka 30 Juni 2024. Hii inamaanisha kuwa nguzo 27,942 tayari zimeshatumika.

Hii ni kinyume na matakwa ya mwongozo wa maelekezo ya uhandisi, ambayo yanataka urefu wa nguzo uwe wa mita 11 hadi 13. Maelezo zaidi yametolewa katika **Jedwali Na. 13.**

**Jedwali Na. 13: Taarifa za nguzo zilizobaki zenye urefu wa mita 8**

| Stoo | Kiasi cha nguzo | Bei ya kila nguzo | Kiasi cha fedha Sh. '000 |
|---|---|---|---|
| Arusha | 200 | 167,321.71 | 33,464 |
| Pwani | 13 | 166,475.40 | 2,164 |
| Ilala | 75 | 167,659.32 | 12,574 |
| Iringa | 913 | 144,331.87 | 131,775 |
| Kinondoni | 1,980 | 166,121.18 | 328,919 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kinondoni Kusini | 1,824 | 167,659.58 | 305,811 |
| Kilwa | 40 | 179,633.98 | 7,185 |
| Mbeya | 2,517 | 152,422.24 | 383,646 |
| Morogoro | 2 | 167,659.58 | 335 |
| Mtwara | 4 | 182,000.00 | 728 |
| Musoma | 15 | 167,659.50 | 2,514 |
| Songea | 28 | 159,872.45 | 4,476 |
| Tunduru | 1,153 | 159,872.45 | 184,332 |
| Sumbawanga | 111 | 170,121.18 | 18,883 |
| Tabora | 1 | 167,475.00 | 167 |
| **Jumla** | **8,876** | | **1,416,979** |

**Chanzo:** *Leja ya stoo ya mwaka 2023/24*

Hii inasababishwa na uandaaji wa vipimo ambavyo ni kinyume na mwongozo wa maagizo ya uhandisi. Hii inaweza kusababisha usumbufu wa mara kwa mara, kuongeza gharama za matengenezo na kusababisha mapungufu katika mfumo wa usambazaji umeme kwa sababu ya uharibifu unaoweza kutokea kwenye nguzo.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Umeme Tanzania lihakikishe nguzo zote za umeme zilizonunuliwa ambazo hazikidhi viwango vinavyotakiwa hazijumuishwi katika miradi ya baadaye au ziambatanishwe na ripoti za kihandisi zilizoidhinishwa ili kuthibitisha kufaa kwake kwa matumizi katika miradi mingine.**

### d) Tathmini na Usimamizi wa Madeni kati ya TANESCO na Kampuni ya Kufua Umeme ya IPTL

Mapitio yangu ya taarifa za madeni katika Shirika la Umeme Tanzania kwa mwaka wa fedha 2023/24 yalibainisha uwepo wa deni lililotokana na ucheleweshaji wa malipo kwa muda mrefu kwa Kampuni ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL). Sehemu ya deni hilo inahusisha kiasi cha shilingi bilioni 111.48 ambacho kimeafikiwa na kukubalika na pande zote mbili kinachohusiana na ankara za madai zilizohakikiwa zilizotolewa kati ya mwaka 2009 na 2017. Kufuatia ucheleweshwaji wa malipo ya deni hilo kwa muda mrefu, kiasi cha riba katika deni hilo kimeongezeka kwa kiwango kikubwa hadi kufikia shilingi bilioni 127.22, ikiwa ni asilimia 114 ya deni halisi. Hivyo, hadi tarehe 30 Juni 2024 jumla ya deni halisi pamoja na riba imefikia shilingi bilioni 238.71. Ucheleweshwaji huu unasababishwa na changamoto za kibajeti ambazo zimekuwa zikijirudia kwa muda mrefu, na hivyo kuongeza gharama kwa serikali kwa kiwango kikubwa.

Vilevile, tathmini yangu ilibaini uwepo wa mgogoro unaoendelea kati ya Shirika la Umeme Tanzania na Kampuni ya IPTL, ambayo kwa

kiasi kikubwa unatokana na uamuzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji wa kutokuhuisha leseni ya uzalishaji umeme kwa Kampuni ya IPTL kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2017 hadi 2022. Hali hii ilisababisha Kampuni ya IPTL kuwasilisha madai ya gharama za uzalishaji, fidia ya kusitisha mkataba, na ada za huduma za kisheria, huku ikiendelea kukumbushia juu ya riba katika madai hayo. Shirika la Umeme Tanzania linadai kuwa mgogoro huo ulitatuliwa katika kesi ya madai Na. 200 ya mwaka 2015. Hata hivyo, kutokana na kutokuwepo kwa makubaliano ya pande mbili katika mgogoro huu, kunazidisha kwa kiwango kikubwa hatari za kifedha, sintofahamu na kuyumbisha sekta ya nishati nchini Tanzania.

Aidha, Kampuni ya IPTL haijatekeleza wajibu wake wa kurejesha malipo kwa Serikali ya Tanzania kama ilivyoainishwa katika Mkataba wa Makubaliano wa tarehe 1 Machi 2021 licha ya kipindi cha urejeshaji wake wa miezi 12 ambacho kilikuwa kinaisha tarehe 28 Februari 2022 kupita. Malipo hayo ya dola za Marekani milioni 148.4 (sawa na shilingi bilioni 389.83) yalitokana na matumizi mabaya ya fedha zilizohusiana na Akaunti ya Tegeta Escrow, ambayo awali ilianzishwa kwa ajili ya kuwezesha malipo ya gharama za umeme.

Hali hii inaendelea kuongeza madeni kwa Serikali kwa kiwango kikubwa, jambo linaloweza kuathiri hali ya uchumi na kupunguza imani ya umma katika mifumo ya usimamizi wa rasilimali za umma.

**Ninapendekeza kuwa Serikali ifanye tathmini kamili ya madai yote na madeni yanayohusiana na Kampuni ya IPTL ili kubaini uhalali wake, usahihi wake, na utekelezaji wa makubaliano ya kisheria. Vilevile, Serikali inapaswa kutekeleza wajibu wa urejeshaji wa fedha inazoidai Kampuni ya IPTL kiasi cha dola za Marekani milioni 148.4 kwa kuzingatia Mkataba wa Makubaliano wa mwaka 2021 kwa kuchukua hatua za kisheria na kifedha ili kuhakikisha urejeshaji wa haraka wa kiasi kilichobaki pamoja na riba.**

## 5.10 Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania (TCPM)

### a) Kutokuwa na Uwezo wa Kutekeleza Jukumu lake la Msingi katika Uzalishaji wa Nguzo za Zege

Kifungu cha 3 (b) cha Hati ya Makubaliano Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za zege Tanzania (TCPM) ya tarehe 06 Agosti 2014 inaeleza kuwa malengo ya uanzishwaji wa TCPM kama kampuni tanzu ya TANESCO yalikuwa ni kutekeleza jukumu la utengenezaji wa nguzo

za umeme za zege, kufanya na kutekeleza aina zote za upimaji wa mitambo, ubora wa mitambo na miundo.

Katika ukaguzi wangu, niligundua kuwa Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za zege Tanzania ilipokea shilingi bilioni 6 kutoka kwa kampuni mama TANESCO. Katika mwaka 2023/24 kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 4 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha nguzo za zege na maabara kwa ajili ya kupima ubora wa nguzo za zege, huku Shilingi bilioni 2 zilikusudiwa kwa ajili ya gharama za uendeshaji.

Hata hivyo, sehemu kubwa ya fedha hizi zilielekezwa kulipia gharama za uendeshaji na kulipa wazabuni wanaotengeneza nguzo nje ya kampuni ya kutengeneza nguzo za zege Tanzania.

Kwa zaidi ya miaka 10, kampuni ya kutengeneza nguzo za zege Tanzania imejitahidi kuwekeza katika utengenezaji wa nguzo za zege kwa kutumia mtaji wa hisa za TANESCO na kulipia gharama za uendeshaji. Kwa matokeo hayo, kampuni inabaki kuwa tegemezi kwa kutumia maabara kutoka nje ya Kampuni kwa majaribio, na hivyo kushindwa kutekeleza lengo lake la awali la kuwa mtengenezaji na mtathmini wa ubora wa nguzo za zege.

**Kwa kuwa Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania kwa sasa haiwezi kutekeleza jukumu lake la msingi ipasavyo; ninapendekeza ifanywe kuwa sehemu ya idara maalum ndani ya TANESCO, au iboreshwe na kuwa kampuni huru, ikiwa na vifaa kamili na fedha za kutosha.**

# Usimamizi wa Mapato na Fedha Katika Mashirika ya Umma



# SURA YA SITA

# USIMAMIZI WA MAPATO NA FEDHA KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

## 6.0 Utangulizi

Usimamizi mzuri wa mapato unahakikisha uhimilivu wa kifedha, uwajibikaji, na utoaji mzuri wa huduma katika mashirika ya umma. Sura hii inaeleza maeneo muhimu yanayohitaji kuboreshwa, yakiwemo upotevu wa mapato, kutozingatiwa kwa mifumo ya udhibiti wa ndani kunakosababisha usimamizi duni wa mapato, pamoja na kutokuzingatia mifumo ya kisheria inayosimamia fedha za umma.

### 6.1 Mapungufu katika usimamizi wa mapato

Usimamizi wa mapato unahusisha uzingatiaji wa taratibu zilizowekwa za udhibiti, mbinu za ukusanyaji, na kubuni au kutafuta vyanzo vipya vya mapato. Ukaguzi wangu ulibaini mapungufu yafuatayo katika usimamizi wa mapato:

#### 6.1.1 Hasara Itokanayo na Mapato Yasiyotozwa kwa Viwango Sahihi shilingi milioni 966.42

Ukaguzi wangu umebaini Hasara itokanayo na mapato yasiyotozwa kwa kiwango sahihi na mashirika saba ya umma kiasi cha **shilingi milioni 966.42** Uchambuzi wa kina umeelezwa hapo chini

(i) Nilibaini **Shirika la Bima la Taifa,** lilitoza ada za bima chini ya viwango vilivyowekwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kwa aina tano za bima zisizohusisha magari, jambo lililosababisha upotevu wa mapato ya **shilingi milioni 607.52**. Hii ilitokana na uhakiki duni wa uthibitishaji wa ada katika mchakato wa kutoa bima.

**Ninapendekeza Shirika la Bima la Taifa liongeze uhakiki wa ada za bima ili kuhakikisha uzingatiaji wa viwango vya bei elekezi vilivyoidhinishwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima.**

(ii) Katika, **Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania,** nilibaini mteja mmoja ambaye shirika lilitumia kiwango maalumu kwa kumuuzia gesi bila kuangalia matumizi ya mteja huyo kwa sababu ya ukosefu wa kromatografia ya gesi inayotumika kunasa maelezo ya kipengele cha ubadilishaji. Hii ni tofauti na wateja wengine ambao hawakuwa na kiwango maalumu, ambapo walitozwa kulingana na matumizi yao ya gesi. Hii ilisababisha utozaji pungufu wa dola za Marekani 14,786 (**shilingi milioni 38.8**). Upotevu huu wa mapato unaweza kuongezeka ikiwa matumizi ya mteja huyo yataongezeka.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania lihakikishe linatoa ankara kulingana na matumizi halisi ya gesi ya wateja.**

(iii) Katika, **Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote,** nilibaini kuwa Mfuko uliwatoza wamiliki wa leseni za mawasiliano 44 kiasi cha shilingi milioni 292.68 badala ya shilingi milioni 365.85, hivyo kusababisha utozaji pungufu wa **shilingi milioni 73.17.** Hii ilitokana na matumizi ya kiwango cha asilimia moja badala ya asilimia 1.25 katika miezi mitatu kuanzia Julai hadi Septemba 2023. Udhaifu katika usimamizi wa bili ulisababisha utozaji pungufu wa ada ya kila mwezi.

**Ninapendekeza Mfuko wa Huduma za Mawasiliano kwa Wote uhakikishe utozaji sahihi wa ada ya kila mwezi, na uhakikishe ada zote zilizotozwa chini ya kiwango kinachostahili zinawasilishwa .**

(iv) Katika**, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma,** nilibaini kuwa Mamlaka ilipaswa kukusanya shilingi milioni 104.58 kwa kutumia ada iliyoidhinishwa ya shilingi 30,000 kwa manunuzi madogo yafikayo 3,486 yaliofanywa na mashirika ya umma. Hata hivyo, Mamlaka ilikusanya shilingi milioni 34.26 kwa kutumia ada isiyo sahihi ya shilingi 10,000 na shilingi 2,000. Hali hii ilisababisha upungufu wa makusanyo ya **shilingi milioni 70.32.** Hii ilitokana na udhibiti dhaifu wa mfumo wa ada, hali iliyosababisha hasara kwa shirika.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma inaboresha udhibiti wa mfumo wa ada, ikiwa ni pamoja na mapitio ya mara kwa mara ili kuhakikisha ada stahiki zilizoidhinishwa zinaingizwa kwenye mfumo hali itakayohakikisha uzingatiaji wa kanuni za ununuzi wa umma.**

(v) Katika ukaguzi wa **Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi,** nilibaini kuwa wanafunzi 36,978 walilipa ada chini ya kiwango kinachotakiwa. Hali hii ilisababisha hasara ya **shilingi milioni 94.87** katika malipo ya kutunukiwa cheti kwa ajili ya kujiendeleza kielimu. Hali hii ilisababishwa na kutokuwepo kwa uhakiki madhubuti na kusababisha upotevu wa mapato.

**Ninapendekeza Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi liweka mifumo ya uhakiki, kubaini malipo yasiyokamilika, na lifanye upatanisho wa mara kwa mara wa malipo.**

(vi) Katika, **Shirika la Umeme Tanzania** nilibaini ucheleweshaji wa kuwabadilisha wateja 7,056 viwango vya matumizi kutoka kiwango cha D1 licha ya matumizi yao kuzidi kilowati (kWh) 75 kwa miezi mitatu mfululizo. Hii ilitokana na udhibiti dhaifu na ukosefu wa mifumo ya ufuatiliaji wa matumizi na ilisababisha upotevu wa mapato wa shilingi milioni 50.76.
**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania liboreshe mifumo yake ili kuhamisha wateja kwa wakati na kuhakikisha wanatozwa ankara stahiki ili kuzuia upotevu wa mapato.**

(vii) Katika **Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania** nilibaini kuwa mamlaka ilitumia viwango vya ada vilivyo chini ya

viwango vilivyoidhinishwa kwa upangaji wa maeneo wakati wa Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam. Hali hii ilisababisha upotevu wa mapato ya **shilingi milioni 30.98.**

**Ninapendekeza Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania ihakikishe inatumia viwango sahihi vya ada na kuhakikisha mabadiliko yoyote ya viwango vya ada za maonesho yanapata idhini ya Bodi ya Wakurugenzi.**

### 6.1.2 Mapato ambayo Hayakupatikana Kutokana na Hali Mbaya ya Barabara ya Rongai na Ukiukwaji wa Mkataba wa Ukodishaji katika Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa Tanzania shilingi bilioni 6.97

Ukaguzi wangu katika Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA) ulibaini kushuka kwa kiwango kikubwa cha mapato katika lango la Rongai. Kushuka huko kulitokana na hali mbaya ya barabara ya Rongai yenye urefu wa kilomita 6, ambayo iliharibika na kutopitika. Kutokana na hali hii, KINAPA ililazimika kufunga lango hilo kuanzia mwezi Novemba 2023 hadi Juni 2024. Hivyo, kushindwa kukusanya mapato, licha ya kuwa ilikusanya shilingi bilioni 1.28 katika miezi minne ya mwanzo (Julai hadi Oktoba 2023). Uharibifu wa barabara hiyo ulisababishwa na matumizi ya malori mazito ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kwa shughuli za misitu. Hatahivyo, nilibaini KINAPA ndiyo imebeba mzigo wote wa matengenezo bila mchango wowote kutoka kwa wakala kwa kuwa hakuna makubaliano rasmi kati ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania na Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro kuhusu majukumu ya matengenezo ya barabara. Wakati huohuo, Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania imekuwa ikiwatoza watalii wa KINAPA ada ya kuingia ya dola za Marekani 10 kwa kila mtalii. Kufungwa kwa barabara ya Rongai kumepunguza fursa kwa wageni kutembelea hifadhi na kufurahia rasilimali za asili na za kitamaduni, hivyo kusababisha kupoteza fursa ya kukusanya mapato. Nimaoni kuwa wakala wa Misitu achangie katika utengenezaji wa barabara.

Aidha, nilibaini kuwa moja ya kampuni ambayo ni muwekezaji ilishindwa kuanza ujenzi wa nyumba za wageni za mazingira rafiki (eco-lodges) katika hifadhi za KINAPA, ANAPA na SENAPA ndani ya muda uliokubaliwa, hali iliyosababisha TANAPA kufuta leseni yao mnamo tarehe 20 Desemba 2023. Kutokana na uvunjaji wa mkataba huo, kampuni hiyo inadaiwa kodi ya msingi ya ardhi inayofikia **kiasi cha shilingi milioni 367.87** (dola za Marekani 140,000). Kifungu cha 50 cha Viwango vya TANAPA kwa mwaka wa 2023/24 kinawataka wawekezaji wa utalii kulipa kodi ya kila mwaka ya ardhi ya dola za Marekani 40,000 kwa KINAPA na ANAPA, na dola za Marekani 60,000 kwa SENAPA. Malimbikizo haya ya malipo yameendelea kwa kipindi cha miaka miwili, ambapo KINAPA na ANAPA zinadai kila moja dola za Marekani 40,000, na SENAPA dola za Marekani 60,000, na kufanya jumla ya dola za Marekani 140,000.

Pia, nilibaini kushindwa kukusanywa kwa ada za kulala ndani ya hifadhi (concession fees) zinazofikia **Shilingi bilioni 6.61** (dola za Marekani 2,518,000). Kifungu cha 50(c) cha Viwango vya TANAPA (Julai 2023 – Juni 2024) kinawataka wawekezaji kulipa asilimia 50 ya ada kamili ya uwezo wa vitanda iwapo ujenzi utakawia, na iwapo kazi haitaanza ndani ya miaka mitatu, leseni inatakiwa kufutwa. Ada hizi zinatofautiana kati ya hifadhi, ambapo ni dola za Marekani 40 kwa mtu kwa usiku mmoja kwa KINAPA na ANAPA, na dola za Marekani 60 kwa SENAPA.

Hivyo TANAPA jumla ya mapato ambayo hayakupatikana yalifikia **shilingi bilion 6.97**.

**Ninapendekeza (a) Kuwepo na ushirikiano baina ya KINAPA na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ili kugharamia matengenezo ya barabara na kuhakikisha barabara inapitika mwaka mzima. Huku majadiliano ya ushiriakiano yakiendelea, KINAPA inapaswa kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Rongai na kufungua tena Lango la Rongai ili kuongeza ukusanyaji wa mapato, na (b) Kuimarisha utekelezaji wa mikataba na ukusanyaji wa ada kwa wakati ili kuhakikisha malipo yote yanayodaiwa kutoka kwa Mpangaji yanarejeshwa kwa hifadhi.**

### 6.1.3 Utendaji Duni wa Shirika la Madini la Taifa Umesababisha Upotevu wa Fursa ya Mapato shilingi bilioni 40.77

Kifungu cha 6(c) cha sheria ya kuanzisha Shirika la Madini la Taifa ya mwaka 2015, kinalitaka Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kutoa huduma za ushauri, kazi za kandarasi, tafiti za upembuzi yakinifu, na tafiti za mazingira kwa mujibu wa sheria husika. Pia, kinalilazimu Shirika kushughulikia usanifu, maendeleo, na usimamizi wa migodi kama ilivyoainishwa katika maelekezo hayo. Kwa sasa, Shirika la Madini la Taifa linahusika na huduma za ushauri za uchimbaji katika mgodi wa Geita Gold Mine (GGM), Shanta Gold Mine, na Buckreef Gold Mine kwa kutumia mbinu za uchimbaji wa mzunguko wa nyuma (Reverse Circulation (RC)) na mbinu ya uchimbaji wa madini inayotumia biti yenye almasi (Diamond Drilling (DD)).

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa shirika lilishindwa kutoa huduma za ushauri wa uchimbaji kwa wateja kwa asilimia 62.9 kwa mbinu zote za Mzunguko wa Nyuma **(RC)** na mbinu ya kutumia almasi (DD). Kwa mujibu wa mpango wa awali, STAMICO ilitakiwa kuchimba mita 63,120. Hata hivyo, ni mita 26,009.4 tu ndizo zilifanikwa kuchimbwa kwa njia ya uchimbaji wa Mzunguko wa Nyuma (RC), sawa na asilimia 41.2 ya lengo. Vilevile, kwa mbinu ya uchimbaji wa kutumia almasi (DD), STAMICO ilifanikiwa kuchimba mita 30,007 tu kati ya mita 91,040, ikiwa ni asilimia 33 ya lengo. Udhaifu huu wa utendaji uliathiri wateja wakubwa katika uchimbaji, wakiwemo Geita Gold Mine, Shanta Gold Mine, na Buckreef Gold Mine.

Pia, nilibaini kuwa STAMICO inatoza wastani wa dola za Marekani 101 kwa kila mita ya RC. Vivyo hivyo, shirika linatoza wastani wa dola za Marekani 193 kwa kila mita ya DD. Uchambuzi zaidi ulibaini kuwa malengo ya uchimbaji yasiyotimizwa ya mita 98,143.60 (mita 37,110.60 kwa RC na mita 61,033.00 kwa DD) yangeweza kuzalisha mapato ya dola za Marekani milioni 15.52 ( sawa na shilingi bilioni 40.77).

Upotevu huu wa mapato ulisababishwa na hitilafu za vifaa na ucheleweshaji wa matengenezo, hali iliyosababisha kuvurugika kwa ratiba za uchimbaji.

**Ninapendekeza Shirika la Madini la Taifa liweke na kudumisha akiba ya vipuri muhimu vya mashine za uchimbaji ili kupunguza muda wa kusimama kwa vifaa, kuhakikisha matengenezo yanafanyika kwa wakati, na kuboresha ufanisi wa kiutendaji ili kuongeza mapato.**

### 6.1.4 Ukusanyaji wa Mapato Nje ya Mfumo wa GePG shilingi bilioni 89.73

Waraka wa Hazina Na. 3 wa mwaka 2017 pamoja na taratibu za Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali (GePG) toleo la 1.1 la Novemba 2019, lililotolewa na Wizara ya Fedha, zinataka fedha zote za umma kukusanywa kupitia mfumo wa GePG. Hata hivyo, mapitio yangu yalibaini kuwa mashirika kumi ya umma yaliyoorodheshwa katika **Jedwali Na. 14** yalikusanya mapato ya shilingi bilioni 89.73 nje ya mfumo wa GePG kinyume na Waraka wa Hazina Na. 3 wa mwaka 2017. Hili ni ongezeko la shilingi bilioni 68.27 (sawa na asilimia 318) kutoka shilingi bilioni 21.46 zilizoripotiwa kwa mashirika saba mwaka uliopita. Hii inachangiwa na kutokutekelezwa ipasavyo kwa Waraka wa Hazina.

**Jedwali Na. 14: Mashirika ya umma ambayo yalikusanywa mapato nje mfumo wa GEPG**

| Na. | Mashirika ya Umma | Kiasi Kilichokusanywa (Sh. '000 |
|---|---|---|
| 1. | Kampuni ya Mbolea Tanzania | 45,702,895 |
| 2. | Kampuni ya Sisalana Tanzania | 22,191,847 |
| 3. | Shirika la Mawasiliano Tanzania | 8,400,518 |
| 4. | Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba | 7,222,467 |
| 5. | Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini | 3,991,558 |
| 6. | Kampuni ya Mkulazi | 1,406,303 |
| 7. | Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania | 556,397 |
| 8. | Bodi ya Pamba Tanzania | 141,659 |
| 9. | Soko la Ubadilishanaji Bidhaa Tanzania | 109,503 |
| 10. | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania | 9,655 |
| | **Jumla Kuu** | **89,732,802** |

**Chanzo**: *Taarifa za makusanyo ya fedha pamoja na ripoti za GePG*

Kushindwa kukusanya mapato kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali kuna madhara makubwa yakiwamo, upotevu wa mapato na ukosefu wa uwazi.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yazingatie Waraka Na. 3 wa 2017 wa Hazina, ili kuhakikisha mapato yote yanakusanywa kupitia mfumo wa GePG ili kuimarisha uwajibikaji na uwazi.**

### 6.1.5 Hatari ya Kupoteza Mapato kutoka kwa Watoa Huduma wa Mawasiliano shilingi bilioni 1.37 katika Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote

Kanuni Na. 5 ya Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ya mwaka 2009, kama zilivyorekebishwa katika Tangazo la Serikali Na. 210 la Aprili 2023, inawataka wamiliki wote wa leseni za mawasiliano kulipa kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ada ya huduma ya asilimia 1.25 (kwa mwaka 2023/24 na 2024/25) ya mapato ghafi ya mwaka ya uendeshaji, ikilipwa kila mwezi kwa malimbikizo. Kanuni hii inaeleza zaidi kuwa ada yoyote ya huduma ya mawasiliano inayocheleweshwa kwa zaidi ya siku thelathini itatozwa riba kwa kiwango rasmi cha benki.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa wamiliki 50 sawa na asilimia 50 kati ya 99 wa leseni za mawasiliano hawakuwasilisha ripoti zao za mapato ya kila mwezi na walitozwa shilingi bilioni 1.37 kwa msingi wa makadirio bila ushahidi wa viwango vilivyoidhinishwa na Bodi. Hali hii inaleta uwezekano wa kutoza ada pungufu kwa watoahuduma kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote.

**Ninapendekeza kuwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote uhakikishe utozaji wa ada kila mwezi unafanyika kwa mujibu wa Kanuni zake za mwaka 2009. Mfumo unapaswa kuanzishwa ili kupata rekodi sahihi za mapato, kwa mfano kutoka TRA, na kutekeleza adhabu kwa kutofuata kanuni. Aidha, ada zote zilizotozwa chini ya kiwango zinapaswa kurejeshwa kikamilifu kutoka kwa watoahuduma.**

### 6.1.6 Mapungufu katika Usimamizi wa Mapato ya Kodi ya Pango katika Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro

Katika ukaguzi wa mikataba ya mapato ya upangaji na biashara ya ukodishaji katika Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro, niligundua kuwa kuna mikataba ya muda mrefu bila marekebisho ya viwango vya kodi ya pango.Ukaguzi wangu uilibaini kuwa mkataba wa miaka 22 wa mpangaji uliomalizika tarehe 1 Januari 2024. Mkataba uliendelea kuwa na kiwango cha malipo ya dola za Marekani 2,978.8 (dola za Marekani 1 kwa kila mita ya mraba 2978.8) kwa mwaka  hivyo kufikia jumla ya dola za Marekani 65,533.6 kwa kipindi chote cha miaka 22 bila mapitio yeyote. Aidha, mkataba huo uliongezwa kutoka tarehe 2 Mei 2024 hadi 1 Desemba 2024 kwa masharti yale yale ya awali. Vilevile, Kampuni ilisaini mkataba wa upangaji wa miaka 15 tarehe 2 Novemba 2022 na Mpangaji Mwingine lakini mkataba huo haukuwa na kipengele cha mapitio ya kodi ya pango mara kwa mara, hali inayozua shaka kuhusu uboreshaji wa mapato kwa muda mrefu.

Hali hii imetokana na mapungufu katika kupitia upya masharti ya mikataba ili kuhakikisha upangaji una manufaa. Kutokufanya mapitio ya mikataba mara kwa mara kunasababisha hasara za kifedha, hatari za kisheria, na changamoto za kiutendaji.

**Ninapendekeza kuwa Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro ihakikishe kuwa mikataba inakaguliwa mara kwa mara na kuhakikisha kuwa marekebisho ya kodi ya pango yanafanyika kwa vipindi maalumu.**

## 6.2 Usimamizi wa Madai ya Kibiashara

Usimamizi wa madai unajumuisha kufuata udhibiti wa msingi na taratibu za ukusanyaji na makubaliano na wadaiwa husika. Ukaguzi wangu ulibaini mapungufu yafuatayo kuhusu usimamizi wa madai katika mashirika ya umma.

### 6.2.1 Kutokuwepo kwa Uhakika wa Ukusanyaji wa Malimbikizo ya Deni la Mgodi wa Buzwagi shilingi bilioni 4.15

Ukaguzi wangu ulibaini kutokuwepo kwa uhakika wa kurejeshwa kiasi cha shilingi bilioni 4.15 kutoka kwenye kampuni ya madini ya Pangea iliyokuwa inasimamia mgodi wa Buzwagi ambapo sehemu ya kipengele cha mkataba kililenga kuboresha Ubora wa Huduma ambapo kipengele hicho kilitaka kampuni hiyo kuchangia gharama za huduma ikishirikiana na Shirika la Umeme Tanzania.

Licha ya wajibu wa kimkataba unaoitaka kampuni hiyo kuilipa Shirika la Umeme Tanzania baada ya miezi minne ya huduma mfululizo, nilibaini kuwa jumla ya ankara zenye thamani ya shilingi bilioni 11.15 zilitolewa kwa kipindi cha miaka kumi (2010/11 hadi 2019/20), hata hivyo ni shilingi bilioni 6.99 tu zilizolipwa mwaka 2022, na hivyo kiasi cha shilingi bilioni 4.15 kimebaki hakijalipwa tangu mwaka 2022.

Aidha, nilibaini kuwa mgodi wa Buzwagi ulisitisha shughuli zake mnamo Julai 2021 na kufungwa rasmi mnamo Julai 2022. Kutokana na kufungwa kwa mgodi huo, nina shaka kuhusu uhakika wa ulipwaji wa kiasi kilichobaki.

Kuna uwezekano wa kupoteza fedha kutokana na ucheleweshaji wa upatanisho wa malipo kama inavyotakiwa na mkataba, hasa ikizingatiwa kuwa mteja amefunga shughuli zake.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania liweke mikakati madhubuti ya urejeshaji wa deni na kuhakikisha kiasi chote kilichosalia kinakusanywa bila kucheleweshwa zaidi.**

### 6.2.2 Kuwepo Madai ya Muda Mrefu Ambayo bado Hayajalipwa shilingi trilioni 3.58

Nilifanya mapitio ya madai ya biashara kwa mwaka uliomalizika tarehe 30 Juni 2024 katika mashirika ya umma 217. Nilibaini kuwa mashirika ya umma **106** yana madai makubwa ya zaidi ya miezi 12 yanayofikia shilingi trilioni 3.58. Madeni hayo yanahusiana na huduma zilizotolewa kwa wateja (Rejea **Kiambatisho Na. V)**. Niliripoti suala kama hilo katika ripoti yangu ya mwaka 2022/23, ambapo mashirika 66 ya umma yalikuwa na ukusanyaji hafifu wa madeni ya biashara yenye thamani ya shilingi trilioni 2.92. Madai ya biashara yaliendelea kuathiri mtiririko wa fedha wa mashirika na uwezo wao wa kutekeleza shughuli zilizopangwa. Maelezo zaidi kuhusu baadhi ya mashirika yaliyokutwa na upungufu huu ni kama ifuatavyo: -

a) **Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya**: Nilibaini kuwa Mfuko wa Bima ulikuwa ukidai kiasi cha shilingi bilioni 180 kama mikopo kwa mashirika manne ya Serikali, huku shilingi bilioni 28 za riba zikiwa zimekwishatolewa kama hasara katika mwaka uliopita. Hakukuwa na marejesho yoyote katika mwaka husika, kinyume na mikataba ya mkopo, hii inatokana na ucheleweshaji wa Serikali katika kusimamia na kulipa madeni yake ya ndani. Hali hii inahatarisha uwezo wa mfuko kuendelea kuwa na mtiririko wa fedha wa kutosha.

b) **Bohari ya Dawa** : Hadi mwisho wa mwaka wa fedha nilibaini kuwa Bohari ya Dawa ilikuwa na madai ya shilingi bilioni 267.79 kutoka kwa Serikali, pungufu kidogo ya shilingi bilioni 13.13 (sawa na asilimia 5) kutoka mwaka uliopita uliokuwa na deni la shilingi bilioni 280.93. Deni hili linahusiana na gharama za Bohari ya Dawa katika upokeaji, uhifadhi, na usambazaji wa dawa na vifaa vya matibabu vilivyotolewa kama msaada. Madai haya makubwa yanaathiri mtaji wa kazi wa Bohari ya Dawa, uwezo wake wa kuwa na kiwango sahihi cha bidhaa, na shughuli zake kuu, hivyo Serikali inapaswa kulipa deni hili ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa bajeti na kupunguza changamoto za kifedha.

c) **Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu**: Nilibaini kuwa deni linalohusu urejeshaji wa mikopo kutoka kwa wanufaika limeongezeka kwa shilingi bilioni 123.04 hadi kufikia shilingi bilioni 931.14, ongezeko la asilimia 15 kutoka mwaka uliopita uliokuwa na deni la shilingi bilioni 808.11. Ucheleweshaji wa marejesho haya unatokana na ukosefu wa ufuatiliaji wa kutosha wa wadaiwa.

d) **Shirika la Nyumba la Taifa**: Ukaguzi wangu ulibaini kuwa wapangaji 3,440 waliokuwa na madeni ya shilingi bilioni 19.09 kwenye mfumo wa

bili kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, walihama bila kulipa madeni yao. Uongozi wa Shirika ulieleza kuwa wadaiwa hawa bado wanafuatiliwa na wakusanya madeni. Tatizo hili linatokana na udhibiti hafifu wa mfumo wa ankara na ukusanyaji wa mapato, hali inayohatarisha hasara ya kifedha kwani kuna uwezekano mkubwa wa madeni haya kutolipwa kabisa.

e) **Hospitali ya Taifa Muhimbili :** Kwa mujibu wa Sera ya Mkopo ya mwaka 2014, hospitali haipaswi kutoa huduma kwa mkopo kwa taasisi zenye historia ya kutolipa madeni yao. Aidha, Aya ya 9.1(iii) yaa sera hiyo kinataka huduma kusitishwa kwa wateja wenye madeni yaliyozidi siku 60 tangu kutolewa kwa ankara. Hata hivyo, Hospitali ya Taifa Muhimbili ilikiuka sera hii kwa kutoa huduma za shilingi bilioni 4.28 kwa taasisi zilizo na madeni ya shilingi bilioni 6.71 na shilingi bilioni 16.6 kwa wagonjwa binafsi. Aidha, madeni ya shilingi bilioni 3.08 yaliyopitiliza muda hayakuwasilishwa kwa wakusanya madeni kama inavyotakiwa na sera. Haya yote yanatokana na udhaifu katika ukusanyaji wa madeni, utekelezaji hafifu wa sera, na changamoto za mfumo wa usimamizi wa madeni, hali inayosababisha matatizo ya kifedha na kuathiri utoaji wa huduma bora za afya.

f) **Madai yasiyo hai Shilingi bilioni 35.21**: Nilibaini kuwa mashirika ya umma umma ikiwemo Bohari ya Dawa, Shirika la Mawasiliano Tanzania, na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili zinakabiliwa na changamoto kubwa za usimamizi wa madai, huku madai ya muda mrefu yakiendelea kutokusanywa kwa miaka kadhaa. Bohari ya Dawa ina akaunti za wateja wasio hai na madeni yasiyolipwa ya shilingi bilioni 7.93, wakati, Shirika la Mawasiliano Tanzania lina wateja wa muda mrefu wasiofanya biashara na shirika wenye madeni ya shilingi bilioni 27.19. Pia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kimekabiliwa na changamoto ya madeni yasiyo hai ambayo hayajakusanywa kwa muda mrefu yenye thamani ya shilingi milioni 90.67. Changamoto hizi zinasababishwa na ukosefu wa maridhiano ya hesabu, udhaifu wa hatua za utekelezaji wa ulipaji, na kumbukumbu za wateja zisizo sahihi, jambo linaloathiri mtiririko wa fedha na uendelevu wa shirika husika.

g) **Mfuko wa Mafunzo ya Usafiri wa Anga**: Nilibaini kuwa wadau wa huduma za usafiri wa anga wapatao 109 pamoja na Mamlaka ya Usafiri wa Anga hawakulipa michango ya lazima ya mafunzo yenye jumla ya shilingi bilioni 2.10 kwa mwaka wa fedha 2023/24, kinyume na Kanuni ya 7 ya Kanuni za Usafiri wa Anga (Mchango na Usimamizi wa Mfuko wa Mafunzo) za mwaka 2013, na kuongeza madeni hadi shilingi bilioni 17.96 kufikia Juni 2024. Wadau hao wanadai kuwa Mfuko wa Mafunzo

na Ushuru wa Maendeleo ya Ujuzi (SDL) unahudumia madhumuni sawa na tozo za Mfuko wa Mafunzo ya Usafiri wa Anga, jambo linalopelekea kutokufuata sheria. Tangu mwaka 2013, mfuko huu umewafundisha marubani 13 tu na wahandisi wa matengenezo ya ndege 11, ikiwa ni chini sana ya lengo la marubani 130 na wahandisi 442. Hali hii inahatarisha ustahimilivu wa mfuko katika kutimiza majukumu na manufaa yake. Pia, hadi tarehe 30 Juni 2024, marejesho ya mikopo kwa Mfuko kutoka kwa wanufaika wanne yalifikia shilingi milioni 57.63, kiasi ambacho ni chini sana ya matarajio. Mapato haya hayakufikia malengo ya shilingi milioni 251, hivyo kuwa na upungufu wa shilingi milioni 193.37. Marejesho ya mikopo yalianza 2018/19 na 2019/20, lakini yameshindwa kufikia kiwango kilichotarajiwa, jambo linaloonyesha udhaifu katika juhudi za urejeshaji wa mikopo.

**Ninarejea mapendekezo yangu kuwa mashirika husika ya umma yaboreshe mifumo ya udhibiti wa ndani katika ukusanyaji wa madeni, ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wadaiwa wote ili kuhakikisha kuwa wanamaliza madeni yao.**

# Usimamizi wa Matumizi Katika Mashirika ya Umma



## SURA YA SABA

# USIMAMIZI WA MATUMIZI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

## 7.0 Utangulizi

Usimamizi bora wa matumizi unawezesha mgawanyo sahihi wa rasilimali za umma na kuhakikisha zinatumika kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo ya uthibiti wa fedha, hali inayowezesha ufanisi wa utendaji wa mashirika katika kutoa huduma zinazokusudiwa.

Sura hii inaeleza mapungufu niliyobaini, kama vile: matumizi yasiyo na tija kutokana na ucheleweshaji wa kutekeleza majukumu ya kimkataba na kisheria; kutolipa kwa wakati madeni ya muda mrefu yanayozidi miezi 12 kutokana na kukosekana kwa fedha; usimamizi duni wa madeni ya riba; na kufanya malipo kinyume cha sheria na kanuni za fedha.

## 7.1 Matumizi Yasiyo na Tija ya shilingi bilioni 371.42

Matumizi yasiyokuwa na tija hutokana na kulipwa kwa malipo ambayo shirika husika halikupata manufaa sawia ya thamani ya fedha iliyolipwa. Matumizi ya aina hii ni yale yanayoepukika na yasiyo ya lazima, kama vile tozo za adhabu na riba zinazotokana na kutokuzingatia matakwa ya kisheria na kimkataba.

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024, nilibaini mashirika ya umma 12 kati ya mashirika 217 yaliyofanya matumizi yasiyokuwa na tija ya jumla ya shilingi bilioni 371.42, ikiwa ni ongezeko la asilimia 413 ya matumizi yasiyokuwa na tija ikilinganishwa na mwaka jana ambapo kulikuwa na mashirika 17 yenye jumla ya shilingi bilioni 72.36.

Matumizi yasiyokuwa na tija, kwa sehemu kubwa yanatokana na tozo za adhabu na riba kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya wazabuni na wakandarasi; kuchelewa kupeleka ritani za kodi na kuchelewa kutuma makato ya kisheria ya watumishi kwa mamlaka husika; na kufanya malipo zaidi ya kazi halisi iliyofanyika. Hii inasababisha upotevu wa fedha za umma na kuzuia ufanisi wa matumizi sahihi ya rasilimali fedha zilizokabidhiwa kwa mashirika husika.

**Jedwali Na. 15** linaonesha orodha ya mashirika ya umma yenye matumizi ya fedha yasiyokuwa na tija katika mwaka wa fedha 2023/24.

**Jedwali Na. 15: Mashirika yenye matumizi yasiyokuwa na tija mwaka 2023/24**

| Na | Jina la Shirika | Maelezo | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Umeme Tanzania | Riba iliyotokana na barua za udhamini wa malipo (Letter of Credit) zilizobadilishwa kuwa mikopo yenye riba kutokana na kukosa fedha za kulipa muda wa malipo ulipofika, riba kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya ununuzi wa gesi, riba kutokana na ucheleweshwaji wa malipo ya wakandarasi wa mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere, na Kampuni ya kufua umeme ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL), pamoja na gharama zilizolipwa kwa kazi ya usanifu wa jengo, ambayo utumizi wake ulisitishwa kufuatia kubadilishwa kwa eneo la ujenzi wa ofisi za Shirika la Umeme Tanzania mkoa wa Kilimanjaro | 295,729,095 |
| 2 | Shirika la Nyumba la Taifa | Gharama za ziada zilizotokana na mabadiliko ya kazi, kusitishwa kwa mradi, riba, na kupanda kwa bei wakati wa kuanza upya kwa mradi wa Kawe 711 mwezi Agosti 2022, baada ya kusitishwa mwezi Aprili 2018 kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya madai ya mkandarasi; pamoja na adhabu za ucheleweshaji (liquidated damages) zilizotozwa na Wakala wa Huduma za Ununuzi serikalini kutokana na kuchelewa kukamilika kwa majengo ya ofisi za Wakala huo. | 49,430,360 |
| 3 | Kampuni ya Huduma za Meli | Malipo ya faini kwa kuchelewesha kulipa madai ya mkandarasi kwa ajili ya kusanifu na kujenga meli mpya (MV Mwanza) | 5,836,472 |
| 4 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | Riba kutokana na ucheleweshwaji wa malipo ya madai ya mkandarasi wa mradi wa ujenzi wa jengo la Maji House | 2,472,515 |
| 5 | Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro | Riba iliyotozwa kutokana na ucheleweshaji wa malipo ya madai ya mkandarasi, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya changalawe kutoka Endulen mpaka Ndutu pamoja na gharama za kuhifadhi mizigo bandarini na kwenye ghala la dhamana zilizosababishwa na ucheleweshaji wa utoaji wa magari mawili ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. | 72,944 |
| 6 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma | Riba iliyotokana na ucheleweshaji wa malipo kwa mkandarasi | 35,023 |
| 7 | Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania | Malipo ya riba na faini yaliyotokana na ukadiriaji wa chini wa kodi ya mapato ya kampuni na ucheleweshaji wa kuwasilisha marejesho ya kodi. | 17,353,240 |

| Na | Jina la Shirika | Maelezo | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|---|---|
| 8 | Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji | Faini kwa ucheleweshaji wa kuwasilisha tozo ya ujuzi na maendeleo kwa kipindi cha kati ya miezi 2 hadi 11 | 24,087 |
| 9 | Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania | Malipo ya faini kutokana na ucheleweshaji wa kulipa michango ya pesheni ya watumishi saba kwenda kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Sekta ya Umma. | 53,181 |
| 10 | Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili | Faini zilizotozwa kutokana na ucheleweshaji wa kuwasilisha michango ya pensheni kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Sekta ya Umma. | 31,893 |
| 11 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya | Faini na riba zilizotokana na ucheleweshaji wa kutuma makato ya kisheria kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Sekta ya Umma, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, na Mamlaka ya Mapato Tanzania. | 10,917 |
| 12 | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko | Ucheleweshaji wa kukamilisha mashauri ya kinidhamu kwa kipindi cha miezi 7 hadi 12 zaidi ya miezi mitatu iliyoainishwa kisheria bila kibali cha Katibu Mkuu Utumishi kwa mujibu wa Kanuni ya 37 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, hali iliyopelekea ulipaji wa mishahara kwa watumishi saba waliosimamishwa kazi kwa muda mrefu. | 370,627 |
| | **Jumla** | | **371,420,354** |

**Chanzo:** *Nyaraka na taarifa za mashirika husika za matumizi na malipo*

**Ninapendekeza mashirika ya umma yaliyoripotiwa: (a) yaboreshe na kuimarisha udhibiti na mikakati ya usimamizi wa matumizi, ikiwemo kuandaa na kutekeleza mikakati yenye kuendana na uhalisia katika usimamizi wa mtiririko wa fedha ili kuhakikisha madeni yanalipwa kwa wakati; na (b) kuongeza udhibiti wa malipo ili kuepuka matumizi yasiyokuwa na tija.**

## 7.2 Matumizi Yasiyostahili ya shilingi bilioni 6.75

Matumizi yasiyostahili yanatokana na malipo ambayo hayakidhi vigezo na matakwa ya kisheria na udhibiti, makubaliano ya kimkataba, na viwango vya uhasibu.

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024, nilibaini mashirika ya umma 10 yaliyokuwa na matumizi yasiyostahili yenye jumla ya shilingi bilioni 6.75 ikiwa ni ongezeko la asilimia 45 kulinganisha na matumizi ya shilingi bilioni 4.64 katika mashirika 11 kwa mwaka jana.

Matumizi mengi yasiyostahili yalihusisha malipo kwa mkandarasi zaidi ya kazi halisi iliyofanyika, malipo ya posho yaliyozidi viwango vilivyoidhinishwa, pamoja na malipo kwa wapokeaji wasiostahiki, wakiwemo watumishi waliokwisha ondoka kazini na wale waliokuwa wakikaimu bila idhini ya Katibu Mkuu Utumishi.

Upungufu huu unaonesha uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za umma, na kuongeza wasiwasi wa kuwepo kwa udanganyifu na kuhatarisha ufanisi na usimamizi wa matumizi ya rasilimali fedha katika mashirika tajwa. **Jedwali Na. 16** linaonesha mashirika ya umma yenye matumizi yasiyostahili mwaka 2023/24.

**Jedwali Na. 16: Mashirika yenye matumizi yasiyostahili mwaka 2023/24**

| Na | Jina la Shirika | Maelezo | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|---|---|
| 1. | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko | Malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa mkataba walioajiriwa nje ya Mpango wa Utumishi wa Bodi na bila idhini ya Katibu Mkuu Utumishi | 2,055,146 |
| 2. | Shirika la Umeme Tanzania | Mishahara iliyolipwa kwa watumishi waliokwisha ondoka kazini, pamoja na posho za kukaimu zilizolipwa kwa watumishi waliokaimu bila idhini ya Katibu Mkuu Utumishi. | 2,041,861 |
| 3. | Kampuni ya Ndege Tanzania | Malipo ya posho za usafiri na nyumba yaliyozidi viwango vilivyoidhinishwa | 1,315,830 |
| 4. | Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania | Posho za kukaimu zilizolipwa kwa watumishi waliokaimu bila idhini ya Katibu Mkuu Utumishi | 561,675 |
| 5. | Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro | Malipo yaliyofanywa kwa mkandarasi zaidi ya kazi halisi iliyofanywa. | 536,712 |
| 6. | Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme | Posho ya madaraka iliyolipwa, ingawa haipo kwenye | 77,600 |

| Na | Jina la Shirika | Maelezo | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|---|---|
| | | mpango wa motisha wa kampuni ulioidhinishwa. | |
| 7. | Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania | Malipo ya posho ya nyumba zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa. | 71,695 |
| 8. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe | Malipo ya posho za nyumba, simu na umeme kwa watumishi nane waliokaimu, ambao uteuzi wao haukuidhinishwa na Katibu Mkuu Utumishi. | 55,996 |
| 9. | Hospitali ya Taifa Muhimbili | Malipo ya mshahara kwa watumishi waliokuwa kwenye likizo ya bila malipo. | 19,920 |
| 10. | Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi | Malipo ya mshahara kwa watumishi walioondoka kazini. | 17,860 |
| | **Jumla** | | **6,754,295** |

**Chanzo:** *Nyaraka na taarifa za mashirika husika za matumizi na malipo*

Aidha, kufuatia ukaguzi wangu, Hospitali ya Taifa Muhimbili imechukua hatua ya kuwaondoa watumishi husika kwenye orodha ya malipo ya mishahara. Vilevile, uongozi wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro umeahidi kurejesha fedha zilizolipwa kupita kiasi kwa kukata kwenye malipo yatakayofuata ya mkandarasi. Fedha hizi zingepotea kama mapungufu haya yasingebainika katika ukaguzi wangu.

**Ninapendekeza mashirika ya umma yaliyoripotiwa: (a) yaimarishe udhibiti kuhakikisha kuwa malipo ya posho za kukaimu na mafao mengine yanatolewa tu kwa watumishi wa kukaimu walioidhinishwa na Katibu Mkuu (Utumishi); (b) yahakikishe kuwa malipo yanatolewa tu kwa kazi iliyothibitishwa ipasavyo ambayo inaonesha kazi halisi iliyofanywa; na (c) yachukue hatua za mara moja kurejesha fedha zilizolipwa kwa matumizi yasiyostahili.**

## 7.3 Masurufu ambayo Hayajarejeshwa kwa Muda Mrefu ya shilingi bilioni 5.34

Kuanzia kanuni ya 96 hadi 103 ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 zinatoa mwongozo juu ya usimamizi wa masurufu, ambao pia

umeakisiwa katika kanuni za fedha za mashirika ya umma. Kanuni hizo zinataka masurufu kurejeshwa ndani ya siku saba hadi 14 baada ya kukamilika kwa shughuli husika; na kutotoa masurufu mengine kwa mtumishi kabla ya kuwasilisha vielelezo vya uthibitisho wa matumizi ya masurufu ya awali; na ikitokea mtumishi kashindwa kuwasilisha vielelezo vya uthibitisho wa matumizi anapaswa kukatwa moja kwa moja kwenye malipo yake ya mshahara.

Ukaguzi ulibaini mashirika ya umma nane yaliyokuwa na masurufu ya jumla ya shilingi bilioni 5.34 ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu kwa kipindi cha kuanzia siku 10 hadi siku 1,140 baada ya kukamilika kwa kazi husika. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 29 ikilinganishwa na mwaka jana ambapo mashirika ya umma 16 yaliyokuwa na jumla ya masurufu ya shilingi bilioni 4.12 ambayo hayakuwa yamerejeshwa. **Jedwali Na. 17** linaonesha mashirika ya umma yenye masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Kuwapo kwa masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu kunatoa mianya ambayo inaweza kutumika kufanya udanganyifu na matumizi mabaya ya fedha za umma. Pia, kunaweza kusababisha kupotosha taarifa za kifedha, kwa kuwa masurufu huwekwa kama sehemu ya madai kutoka kwa wafanyakazi lakini katika hali halisi matumizi yake huwa yamekwisha kamilika; hivyo kupaswa kuwa sehemu ya matumizi na siyo madai.

**Jedwali Na. 17: Mashirika yenye masurufu ambayo hayajarejeshwa kwa muda mrefu kwa mwaka 2023/24**

| Na | Jina la Shirika | Uchelewaji (Siku) | Kiasi (Sh. '000) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania | 14 hadi 90 | 2,164,329 |
| 2. | Chuo cha Uhasibu Arusha | 90 hadi 1,140 | 1,410,847 |
| 3. | Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania | 14 hadi 1,080 | 558,611 |
| 4. | Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili | 14 hadi 1,095 | 428,273 |
| 5. | Shirika la Posta Tanzania | Zaidi ya siku 14 | 347,815 |
| 6. | Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu | 10 hadi 332 | 275,206 |
| 7. | Chuo Kikuu cha Dodoma | 271 hadi 312 | 140,255 |
| 8. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya | 10 hadi 201 | 18,333 |
| | **Jumla** | | **5,343,669** |

**Chanzo:** *Uchambuzi wa taarifa na nyaraka za masurufu za mashirika husika*

**Ninapendekeza mashirika husika yasimamie na kuhakikisha masurufu yanarejeshwa kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuwakata mishahara watumishi ambao hawajafanya marejesho ya masurufu**

**ama kwa kutowasilisha vielelezo vya ushahidi wa matumizi ya masurufu.**

## 7.4 Malipo ya Awali Yanayoweza Kupelekea Hasara ya shilingi bilioni 7.51

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa mwezi Julai 2017, Shirika la Umeme Tanzania liliingia mkataba Na. PA/001/2016/HQ/G/01 wa miaka mitatu na mzabuni kwa ajili ya ugavi wa vifaa vya usambazaji wa huduma za umeme kwa mradi wa wateja 250,000 wenye thamani ya shilingi bilioni 33.68 ikiwa ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani. Kwa mujibu wa masharti ya mkataba, Shirika lilifanya malipo ya awali ya shilingi bilioni 6.73. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi mwezi Oktoba 2024, ikiwa ni miaka saba baadaye, mzabuni bado hajatekeleza majukumu yake ya kimkataba, na hivyo kufanya urejeshwaji wa malipo yaliyofanyika kuwa na shaka. Hali hii inaweza kusababisha hasara ya shilingi bilioni 6.73 kwa Shirika endapo fedha hizo hazitarejeshwa.

Vilevile, nilibaini kuwa hadi tarehe 30 Juni 2024, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kilifanya malipo ya awali ya shilingi milioni 783.25 kwa ajili ya ununuzi wa mali na vifaa vya matumizi ya ofisi, ambapo wazabuni hawakuwa wamewasilisha mali na bidhaa hivyo kwa zaidi ya miezi 12.

Malipo ya awali yaliyokaa kwa muda mrefu kutokana na ucheleweshaji wa uwasilishaji wa bidhaa na huduma yanapelekea mashirika husika kushindwa au kuchelewesha kutoa huduma kwa wakati na hivyo kukwamisha upatikanaji wa manufaa yanayotarajiwa kwa umma.

**Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma yaliyoripotiwa: (a) yashirikiane na wazabuni husika ili kuhakikisha mali, vifaa na bidhaa ambazo hazijawasilishwa ziwasilishwe kwa wakati; (b) yachukue hatua za kisheria, ikiwemo kutoza adhabu na riba, ili kudai fidia kwa faida na manufaa yaliyopotea; na (c) yaimarishe udhibiti wa ndani kwa kufanya mapitio ya mara kwa mara na kufuatilia malipo yaliyofanywa kwa wazabuni ili kuhakikisha utoaji wa bidhaa na huduma zinazokusudiwa kwa wakati. Katika hali ya ucheleweshaji wa muda mrefu, hatua za kurejesha fedha zichukuliwe mara moja.**

## 7.5 Madeni ya Muda Mrefu ya Jumla ya shilingi trilioni 3.70

Madeni ni madai halali ambayo bado hayajalipwa kwa bidhaa, kazi ama huduma zilizotolewa kwa mashirika ya umma. Kushindwa kuwalipa wadai kwa wakati kunaweza kusababisha adhabu, riba, na

kuzorota kwa mahusiano na wadai hao pamoja na wadau wengine muhimu.

Wakati wa ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2024, nilibaini kuwa mashirika ya umma 66 yalikuwa na madeni ya jumla ya shilingi trilioni 3.70 ambayo hayajalipwa kwa kipindi cha zaidi ya miezi 12. Taarifa za kina za madeni kwa kila shirika zimeoneshwa katika **Kiambatisho Na. VI.**

Pia, uchambuzi zaidi katika mashirika ya umma yaliyo na madeni ya zaidi ya shilingi bilioni 50 ulibainisha yafuatayo:

**Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA):** Deni lililoripotiwa la shilingi trilioni 1.02 linajumuisha shilingi bilioni 721.47 sawa na asilimia 70 zinazohusiana na mchango wa Serikali wa asilimia 70, shilingi bilioni 134.77 sawa na asilimia 13 zinazohusiana na mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali, shilingi bilioni 126.22 sawa na asilimia 12 zinazohusiana na wazabuni wa bidhaa na huduma, na shilingi bilioni 46.46 sawa na asilimia 5 zilizowekwa kama dhamana ya mikataba ya uhandisi. Ucheleweshwaji wa malipo unatokana na mapato ya vyanzo vya ndani yasiyotosheleza kulipa madai ya wazabuni na mchango wa asilimia 15 ya mapato ghafi. Kwa upande mwingine, Uongozi umeomba kusamehewa kwa deni linalotokana na mchango wa asilimia 70 kutoka kwa Msajili wa Hazina, ombi hilo bado halijakubaliwa.

**Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO):** Deni lililoripotiwa la shilingi trilioni 1.00 linajumuisha shilingi bilioni 668.54 sawa na asilimia 66 zinazohusiana na taasisi za Serikali, na shilingi bilioni 337.47 sawa na asilimia 34 zinazodaiwa na sekta binafsi. Ucheleweshwaji wa malipo haya unatokana na changamoto za mtiririko wa fedha zilizotokana na mapato yasiyotosheleza kutoka vyanzo vya ndani.

**Shirika la Reli Tanzania (TRC):** Deni lililoripotiwa la shilingi bilioni 661.32 linajumuisha shilingi bilioni 416.34 sawa na asilimia 63 zinazohusiana na kodi, ushuru, na riba linazodaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA); wakati kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 244.98 sawa na asilimia 37 kinahusiana na miradi ya reli, ikijumuisha shilingi bilioni 228.68 sawa na asilimia 93 zinazohusiana na mradi wa Reli ya Kisasa (SGR).

**Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL):** Deni lililoripotiwa la shilingi bilioni 434.34 linajumuisha shilingi bilioni 354.21 (82%) zinazohusiana na taasisi za Serikali, na shilingi bilioni 80.13 (18%)

zinazodaiwa na sekta binafsi. Uchambuzi zaidi ulibainisha kuwa kati ya deni la Serikali la shilingi bilioni 354.21, shilingi bilioni 260.19 (73%) zinahusiana na malipo ya ukodishaji ndege kwa masharti nafuu kwa Wakala wa Ndege za Serikali ya Tanzania (TGFA). Kucheleweshwa kwa ulipaji wa madeni haya kunatokana na mapato yasiyotosheleza kutoka vyanzo vya ndani, pamoja na changamoto katika usimamizi na utekelezaji wa mkataba wa ukodishaji ndege na TGFA.

**Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL):** Deni lililoripotiwa la shilingi bilioni 132.80 linajumuisha shilingi bilioni 60.94 sawa na asilimia 46 zinazohusiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa ada za masafa ya mawasiliano, namba maalumu za huduma, na mirabaha; shilingi bilioni 43.87 sawa na asilimia 33 zinazodaiwa na Kampuni ya Helios Towers Tanzania kwa huduma za kupangisha miundombinu ya mawasiliano kwenye minara; na shilingi bilioni 27.99 sawa na asilimia 21 zinazohusiana na wazabuni wengine. Hali hii inatokana na ukata wa fedha wa Shirika la Mawasiliano Tanzania.

**Bohari Kuu ya Dawa (MSD):** Deni lililoripotiwa la shilingi bilioni 93.70 linajumuisha shilingi bilioni 61.59 sawa na asilimia 66 zinazodaiwa na wazabuni wa dawa na vifaa tiba, na shilingi bilioni 31.75 sawa na asilimia 34 zinazodaiwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA). Ucheleweshwaji wa kulipa madeni haya unatokana na watoahuduma za afya wa umma kutolipa madeni yao kwa wakati, hali inayosababisha changamoto ya mtiririko wa fedha katika Bohari Kuu ya Dawa.

**Shirika la Posta Tanzania (TPC):** Deni lililoripotiwa la shilingi bilioni 68.83 linajumuisha shilingi bilioni 54.7 sawa na asilimia 79 zinazodaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), shilingi bilioni 8.8 sawa na asilimia 13 zinazodaiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Sekta ya Umma (PSSSF), na kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 5.33 sawa na asilimia 8 kinahusiana na wadai wengine. Ucheleweshwaji wa kulipa madeni haya unasababishwa na changamoto za ukwasi zinazolikabili Shirika.

**Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA):** Deni lililoripotiwa la shilingi bilioni 64.04 linajumuisha shilingi bilioni 32.02 sawa na asilimia 50 zinazohusiana na miradi ya maji ikihusisha wakandarasi na wazabuni wa vifaa, shilingi bilioni 22.56 sawa na asilimia 35 zinazohusiana na bili za umeme, shilingi bilioni 4.81 sawa na asilimia 8 zinazohusiana na huduma za bonde la Mto Wami, shilingi bilioni 1.31 zinazohusiana na malipo ya huduma ya ulinzi, na

shilingi bilioni 3.3 sawa na asilimia 5 zinazohusiana na wazabuni na watoa huduma wengine, ikiwa ni pamoja na huduma za utangazaji na bima. Kucheleweshwa kwa ulipaji wa madeni haya kunatokana na kuchelewa kwa utoaji wa fedha za miradi ya maji kutoka Wizarani na mapato yasiyojitosheleza kutoka vyanzo vya ndani.

**Kampuni ya STAMIGOLD:** Deni lililoripotiwa la shilingi bilioni 52.04 linajumuisha shilingi bilioni 16.18 sawa na asilimia 31 zinazodaiwa na wazabuni wa mafuta; wakati kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 35.86 sawa na asilimia 69 kinadaiwa na wakandarasi wa huduma uchimbaji na wazabuni wa huduma nyinginezo. Ucheleweshaji wa kulipa madeni haya unachangiwa na changamoto za mtiririko wa fedha kwenye Kampuni.

Kwa ujumla madeni katika mashirika ya umma yalitokana na changamoto za mtiririko wa fedha zilizochangiwa na ucheleweshwaji na kukosekana kwa fedha kutoka serikalini, kutokufanya vizuri kwa biashara za mashirika ya kibiashara, na mikakati duni ya usimamizi wa mtiririko wa fedha ili kuhakikisha madeni yanalipwa kwa wakati.

Kulimbikiza madeni, yaliyo tayari kulipwa, kwa muda mrefu kunashusha hadhi na kuharibu taswira ya mashirika ya umma na Serikali. Pia, wazabuni wanaweza kukataa kutoa huduma au kutoa huduma kwa masharti magumu kwa mashirika husika hivyo kuathiri utendaji wa shughuli za kila siku za mashirika hayo. Aidha, ucheleweshaji wa malipo kwa muda mrefu husababisha riba na adhabu ambazo zinakuwa gharama za ziada na zisizokuwa na tija.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika: (a) yaweke na kutekeleza mikakati madhubuti ya usimamizi wa mtiririko wa fedha pamoja na mipango bora ya utekelezaji ili kuhakikisha kuwa malimbikizo ya madeni yaliyoripotiwa yanalipwa bila kuchelewa zaidi, na kwa siku zijazo, madai ya wazabuni yalipwe kwa wakati; na (b) kwa madai yanayohitaji ufadhili wa Serikali, Serikali ihakikishe fedha zinatolewa kwa wakati kwa mashirika husika.**

## 7.6 Ununuzi wa Umeme kwa Kutegemea Taarifa za Mzalishaji pasipo Kuthibitishwa na Shirika la Umeme Tanzania shilingi bilioni 2.91

Kifungu cha 4.8 cha Jedwali la Tatu la Kanuni za Umeme (Maendeleo ya Miradi Midogo ya Umeme) za Mwaka 2020 kinataka kuwa mita kuu isomwe kwa pamoja na muuzaji na mnunuzi kila tarehe 1 ya mwezi (au tarehe nyingine itakayokubaliwa na pande zote) ili kubaini kiasi halisi cha umeme kilichosafirishwa kwenye mfumo wa mnunuzi tangu usomaji wa awali wa mita kuu.

Ukaguzi wa ankara za kila mwezi na fomu za usomaji wa mita kuu ya umeme ulionunuliwa na Shirika la Umeme Tanzania kutoka kwa mzalishaji wa umeme wenye thamani ya dola za Marekani milioni 1.12 (sawa na shilingi bilioni 2.91), ulibaini kuwa ukokotoaji wa kiasi cha umeme kilichonunuliwa ulifanyika kwa kutumia taarifa za usomaji wa mita kuu ya muuzaji pekee, bila uthibitisho huru wa Shirika kupitia mita ya uhakiki.

Aidha, hakukuwa na ushahidi unaoonesha kuwa Shirika lilishuhudia usomaji wa mita hiyo ili kuthibitisha ankara zilizotolewa, bali usomaji ulifanywa na muuzaji pekee, ambaye baada ya usomaji hutuma nakala ya taarifa kwa Shirika. Hali hii inatoa mianya ya udanganyifu na inaweza kusababisha malipo kupita kiasi kwa kuwa hakuna uhakika kuwa kiasi cha umeme kilichotozwa kinalingana na matumizi halisi.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Umeme Tanzania lihakikishe linafanya uhakiki wa taarifa za ununuzi wa umeme ili kuthibitisha taarifa za usomaji wa mita kuu, na pia lihakikishe kuwa usomaji wa mita kuu unafanywa kwa pamoja.**

# Usimamizi wa Bajeti Katika Mashirika ya Umma




## SURA YA NANE

# USIMAMIZI WA BAJETI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

## 8.0 Utangulizi

Usimamizi thabiti wa bajeti unawezesha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa mujibu wa malengo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 na mipango ya kimkakati ya mashirika ya umma. Aidha, mchakato huu unasimamiwa na Sheria ya Bajeti, Sura ya 439, kanuni na miongozo yake.

Nilikagua mchakato wa uandaaji na utekelezaji wa bajeti ya mashirika ya umma 217 na kubaini kuwa mashirika 173 yalifuata sheria za bajeti, ingawa kulikuwepo na mapungufu machache yanayohitaji maboresho.

Sura hii inaangazia masuala muhimu, yakiwemo utoaji hafifu wa fedha za bajeti kutoka Serikali kuu, ukusanyaji pungufu wa mapato kutoka vyanzo vya ndani, matumizi ya fedha zaidi ya bajeti, upungufu uliobainika katika fedha za bakaa, ushirikishwaji usioridhisha wa wadau katika kuandaa na kutekeleza bajeti, pamoja na upungufu katika matumizi ya mifumo ya usimamizi na udhibiti wa bajeti.

## 8.1 Muendelezo wa Utoaji wa Fedha za Bajeti Pungufu kutoka Serikalini wa shilingi bilioni 485.91

Kwa miaka iliyopita, nimekuwa nikiripoti mara kwa mara kuhusu Serikali kutotoa kikamilifu fedha zilizoidhinishwa kwa mashirika ya umma. Katika mwaka wa fedha 2023/24, tathmini yangu ya utekelezaji wa bajeti ilionesha kuwa mashirika ya umma 66 kati ya 188 (Bila kujumuisha mashirika ya umma ya kibiashara) hayakupokea zaidi ya asilimia 10 ya fedha zilizopangwa kwenye bajeti kwa mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2024.

Mashirika haya yalitarajia kupokea shilingi trilioni 1,074.31 bilioni kutoka serikalini katika mwaka wa fedha 2023/24, lakini Serikali ilitoa shilingi bilioni 588.40, sawa na asilimia 55 ya bajeti iliyoidhinishwa, hali iliyosababisha upungufu wa shilingi bilioni 485.91, sawa na asilimia 45 **(**Rejea **Kiambatisho Na. VII).**

Hii inaonesha kuwa hatua stahiki hazikuchukuliwa kushughulikia changamoto hii, kama inavyoonekana katika mwenendo wa miaka iliyopita ambapo, katika mwaka wa fedha 2022/23, shilingi trilioni 1.01 (sawa na asilimia 48 ya bajeti yote) hazikutolewa, mwaka wa 2021/22 shilingi bilioni 161.88 (sawa na asilimia 30 ya bajeti yote) hazikutolewa na mwaka wa 2020/21 shilingi trilioni 1.13 (sawa na asilimia 29 ya bajeti yote) hazikutolewa. Mwenendo huu umeoneshwa kwenye **Kielelezo Na.1.**

**Kielelezo Na. I: mwenendo wa utoaji hafifu wa fedha za bajeti kutoka Serikalini**




**Chanzo**: *Uchambuzi wa Mkaguzi kutoka katika taarifa za ukaguzi*

Utoaji pungufu wa fedha za bajeti kutoka serikalini unaathiri kwa kiasi kikubwa mashirika ya umma katika kutekeleza shughuli zao kwa ufanisi, na kusababisha kushuka kwa ubora na wingi wa huduma zinazotolewa kwa umma.

**Narudia mapendekezo yangu kuwa Serikali ihakikishe uhalisia wa makadirio ya bajeti yanayowasilishwa na mashirika ya umma, na baada ya kuidhinishwa, itoe kikamilifu fedha zilizoidhinishwa ili kuimarisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na mashirika husika na kufikia malengo yao.**

## 8.2 Ukusanyaji Pungufu wa Mapato Yatokanayo na Vyanzo vya Ndani wa shilingi trilioni 2.07

Mashirika ya umma hukusanya mapato kutoka vyanzo mbalimbali kama ada, mauzo, mapato ya uwekezaji, na vyanzo vingine, ambavyo hutumiwa kwa matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Mapato haya huainishwa kama mapato yao ya ndani.

Nilibaini mashirika ya umma 80 kati ya 217 yalikusanya shilingi trilioni 2.57, sawa na asilimia 55 ya fedha zote za bajeti ya mapato ya vyanzo vyao vya ndani ambayo ni shilingi trilioni 4.64. Hivyo, jumla ya shilingi trilioni 2.07, sawa na asilimia 45 ya fedha za bajeti ya mapato ya nyanzo vyao vya ndani, hazikukusanywa **(**Rejea **Kiambatisho Na. VIII).**

Hii inaonesha kuwa hatua stahiki hazikuchukuliwa katika kushughulikia upungufu wa ukusanyaji wa mapato, kama inavyoonekana katika ripoti zangu za miaka iliyopita ambapo upungufu wa ukusanyaji ulikuwa shilingi bilioni 284.71 (asilimia 36 ya bajeti yote) katika mwaka wa 2022/23, shilingi trilioni 1.61 (asilimia 63 ya bajeti yote) katika mwaka wa 2021/22, na shilingi bilioni 174.63 (asilimia 32 ya bajeti yote) katika mwaka wa 2020/21.

Uchambuzi wangu ulibaini kuwa mashirika ya umma sita yalikuwa na mwenendo usioridhisha katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa miaka mitatu mfululizo, ikiwemo: Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini, na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro, kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na II**.

**Kielelezo Na. II: Ongezeko la upungufu wa ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa mashirika ya umma**




**Chanzo**: *Uchambuzi wa mkaguzi katika taarifa za ukaguzi*

Aidha, sababu za upungufu katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani zilikuwa kama ifuatavyo; Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira zinakabiliwa na changamoto za kukusanya madeni kutoka kwa mashirika ya Serikali na upotevu wa maji wakati wa usambazaji unaopelekea kupoteza mapato.

Katika taasisi za elimu ya juu, udahili wa wanafunzi umepungua na kuwa chini ya matarajio kutokana na makadirio ya bajeti ya udahili yasiyo na uhalisia, umuhimu wa programu zinazotolewa na chuo kwa wanafunzi na upatikanaji mdogo wa mikopo ya wanafunzi kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Vilevile, mamlaka za udhibiti zinakutana na changamoto katika ukusanyaji wa ada za kila mwaka kutoka kwa wadau wao kutokana na mifumo duni ya ukusanyaji.

Mapato yasiyokusanywa husababisha upungufu wa fedha, kuathiri shughuli zilizopangwa na kuzuia kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika (a) yafanye tathmini kamili katika mifumo yao ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, ikiwemo kutambua maeneo dhaifu na kutengeneza mikakati ya kuboresha ukusanyaji wa mapato, na (b) yaandae makadirio ya bajeti ya mapato ya ndani katika uhalisia.**

## 8.3 Matumizi ya Fedha Zaidi ya Bajeti bila Kuidhinishwa shilingi bilioni 7.65

Nilibaini mashirika ya umma 12 yalikuwa na bajeti iliyoidhinishwa ya shilingi bilioni 22.50 lakini yalifanya matumizi ya shilingi bilioni 30.15. Hali hiyo ilisababisha kuwa na matumizi ya shilingi bilioni 7.65 ambayo hayakuwa katika bajeti au yalitumia zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa kwenye bajeti. Matumizi haya ya zaidi ya kiasi cha bajeti hayakupata idhini ya afisa masuuli wala Bodi ya wakurugenzi kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 18.**

**Jedwali Na. 18: Mashirika ya umma yaliyofanya matumizi zaidi ya kiwango cha bajeti**

| Na. | Mashirika ya umma | Bajeti iliyoidhinishwa | Matumizi halisi | Nakisi ya bajeti |
|---|---|---|---|---|
| | | Sh. '000 | | |
| 1 | Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania | 6,012,840 | 8,862,010 | (2,849,170) |
| 2 | Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila | 8,013,415 | 8,993,279 | (979,864) |
| 3 | Chuo cha Usimamizi wa Fedha | 1,962,763 | 2,853,693 | (890,930) |
| 4 | Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania | 2,281,915 | 2,790,209 | (508,294) |
| 5 | Kampuni ya Mkulazi | 770,394 | 1,253,704 | (483,310) |
| 6 | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania | 241,824 | 627,173 | (385,349) |
| 7 | Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari | 354,998 | 732,264 | (377,266) |
| 8 | Kampuni ya Majengo ya Biashara ya Jiji la Mwanza | 92,358 | 400,942 | (308,584) |
| 9 | Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania | 1,454,503 | 1,745,286 | (290,783) |
| 10 | Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania | 0 | 281,674 | (281,674) |
| 11 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same Mwanga | 337,877 | 508,947 | (171,070) |
| 12 | Kampuni ya TTCL Pesa | 985,884 | 1,109,101 | (123,217) |
| | **Jumla** | **22,508,771** | **30,158,282** | **(7,649,511)** |

**Chanzo**: *Taarifa za utekelezaji wa bajeti*

Hii inaonesha kuwa hatua stahiki hazijachukuliwa katika kuhakikisha mashirika ya umma yanafuata bajeti zao, kwani nilibaini kasoro hii katika miaka iliyopita. Katika mwaka wa fedha 2022/23, mashirika

nane yalitumia jumla ya shilingi bilioni 21.14 zaidi ya bajeti bila idhini, huku mwaka wa fedha 2021/22 mashirika saba yalitumia zaidi ya bajeti kwa shilingi bilioni 118.04 bila idhini.

Aidha, kati ya mashirika yalioainishwa katika ripoti za miaka iliyopita, Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila ilitumia zaidi ya kiasi cha bajeti bila kufuata utaratibu kwa miaka miwili mfululizo, ambapo matumizi yalikuwa shilingi milioni 979.86 katika mwaka wa 2023/24 na shilingi bilioni 1.26 katika mwaka wa 2022/23.

Hii inatokana na kutokuwa na Mfumo madhubuti unaosimamia na kudhibiti matumizi ya fedha zilizopangwa na kutofanya marejeo ya bajeti. Kwa mfano, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila, hali hii ilitokana na ukosefu wa ufuatiliaji na udhibiti thabiti wa bajeti ndani ya mfumo wa malipo. Wakati huo, katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same Mwanga, matumizi zaidi ya bajeti yalitokana na ukosefu wa mfumo wa udhibiti wa bajeti.

Aidha, Nilibaini sababu nyingine za matumizi zaidi ya bajeti, zikiwemo:

- **Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania** ilipokea maelekezo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutekeleza shughuli ambazo hazikupangwa kwenye bajeti katika maadhimisho ya Nanenane.

- **Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania** ilitumia zaidi ya bajeti kutokana na muunganiko wa **Taasisi ya Utafiti ya Viuatilifu Tanzania** na **Sekta ya Afya ya Mimea** kuunda Mamlaka hiyo.Hivyo,Mamlaka hiyo (ambapo awali ilikuwa Taasisi ya Utafiti ya Viuatilifu Tanzania ) iliagizwa na Wizara ya Kilimo kutekeleza shughuli za **Sekta ya Afya ya Mimea** bila kujumuisha bajeti yake. Pia, Mamlaka hiyo ililipa mchango kwenye mfuko mkuu wa Serikali zaidi ya kiasi kilichotengwa kwenye bajeti kutokana na makusanyo ya mapato ya ndani kuzidi kiwango kilichopangwa.

- Vilevile, **Chuo cha Usimamizi wa Fedha** kililipa mchango kwenye mfuko mkuu wa Serikali zaidi ya kiasi kilichotengwa kwenye bajeti kutokana na maelekezo ya Msajili wa Hazina.
- **Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania** ilitumia zaidi ya bajeti yake katika maandalizi ya muungano wa Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini na Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo.

Matumizi ambayo hayakuwa kwenye bajeti au zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa kwenye bajeti yanakwamisha utekelezaji kamili wa shughuli zilizopangwa kufanyika kwa mwaka husika, hatimaye huathiri malengo ya shirika na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

**Ninarudia mapendekezo yangu kuwa mashirika ya umma yahakikishe: (a) Yanafanya makadirio sahihi ya bajeti na kufanya marejeo ya bajeti katikati ya mwaka ili kuzingatia mabadiliko yanayotarajiwa; (b) Yanapata idhini kutoka kwa mamlaka husika katika kufanya matumizi ambayo hayakuwa katika bajeti; na (c) Yanatumia mfumo wa udhibiti wa bajeti na kuzingatia sheria za bajeti na kanuni zake.**

## 8.4 Upungufu Uliobainika katika Fedha za Bakaa

### (i) Uwepo wa Fedha za Bakaa Zisizotumika Ndani ya Muda Uliowekwa shilingi bilioni 1.19

Kanuni ya 21 ya Kanuni za Bajeti za mwaka 2015 inamtaka afisa masuuli kuwasilisha ombi la kuhama na bakaa kwenda mwaka wa fedha unaofuata, kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali, akitoa maelezo ya sababu za kutotumia fedha hizo kwa mwaka wa fedha husika. Aidha, Kanuni ya 21(3) ya Kanuni hizo inabainisha kuwa fedha(bakaa) ambazo hazikutumika mpaka mwisho wa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha unaofuata, zirudishwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Nilibaini kuwa mashirika ya Umma manne hayakurudisha bakaa zenye jumla ya shilingi bilioni 1.19 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali baada ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha uliofuata (2023/24). Aidha, hadi tarehe 30 Juni 2024, fedha hizo bado zilikuwa hazijarejeshwa, isipokuwa Chuo cha Uhasibu Arusha, ambacho kilirejesha bakaa ya chuo hicho mnamo Juni 2024, ikiwa ni miezi tisa baada ya muda uliowekwa kupita. Taarifa ya mashirka hayo imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 19.**

**Jedwali Na. 19: Mashirika ya umma yaliyokuwa na bakaa zisizotumika ndani ya muda uliowekwa**

| Na. | Mashirika ya umma | Bakaa iliyo vuka mwaka | Bakaa iliyotumika | Bakaa iliyobaki |
|---|---|---|---|---|
| | | | Sh. '000 | |
| 1 | Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro | 1,899,732 | 1,320,243 | 579,489 |
| 2 | Chuo cha Uhasibu Arusha | 2,114,387 | 1,897,613 | 216,774 |
| 3 | Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini | 410,991 | 175,101 | 235,890 |
| 4 | Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania | 664,159 | 507,905 | 156,254 |
| | **Jumla** | 5,089,269 | 3,900,862 | 1,188,407 |

**Chanzo**: *Taarifa za bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24*

Hii inasababishwa na utekelezaji usioridhisha wa shughuli zilizokusudiwa. Hali ya menejimenti kushindwa kurejesha fedha ambazo hazikutumika kwa wakati unaotakiwa kunaweza pelekea fedha kutumika katika matumizi ambayo hayakupangwa.

**Ninapendekeza mashirika ya Umma yahakikishe: (a) Shughuli zilizokusudiwa zinatekelezwa kwa muda husika ili kuhakikisha bakaa zinatumika ndani ya muda uliowekwa; na (b) Kurudisha fedha zote ambazo hazikutumika kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Bajeti.**

### (ii) Kutofuatilia Matumizi ya Bakaa katika Shirika la Bima la Taifa shilingi bilioni 22.42

Shirika la Bima la Taifa lilikuwa na bakaa ya shilingi bilioni 22.42, iliyokusudiwa kutumiwa katika robo ya kwanza ya mwaka uliofuata, kwa mujibu wa Kanuni ya 21(2) ya Kanuni za Bajeti za mwaka 2015.

Hata hivyo, sikuweza kuthibitisha iwapo fedha hizo zilitumika ndani ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24, kwani Shirika halikufuatilia matumizi ya fedha hizo.

Ufuatiliaji usioridhisha unaweza kusababisha fedha hizo kutumika kwa shughuli ambazo hazikukusudiwa.

**Ninapendekeza Shirika la Bima la Taifa liboreshe ufuatiliaji wa bakaa kupitia mifumo ya bajeti na kuandaa ripoti za utekelezaji kuhusu matumizi ya fedha hizo.**

### (iii) Matumizi ya Bakaa shilingi bilioni 7.02 bila Idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Nilibaini kuwa Bodi ya Mkonge Tanzania na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam walitumia bakaa zenye jumla ya shilingi bilioni 1.12 na shilingi bilioni 5.9, mtawalia, bila idhini kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali, kinyume na Kanuni ya 21 (1) ya Kanuni za Bajeti za mwaka 2015.

Hii ilitokana na kutokuomba idhini kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa wakati au ufuatiliaji usioridhisha baada ya kuomba idhini, hali ambayo inaweza kusababisha matumizi mabaya ya bakaa.

**Ninapendekeza Bodi ya Mkonge Tanzania na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam waombe idhini ya matumizi ya bakaa kwa wakati na wafuatilie mrejesho kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali**

## 8.5 Kutoshirikisha Wadau Pamoja na Kutozingatia Mpango Mkakati katika Maandalizi ya Bajeti ya Mashirika ya Umma

Mashirika ya umma yanatakiwa kuandaa mipango na makadirio ya bajeti kwa njia ya kushirikisha na kupata idhini kutoka kwa Mamlaka zao za Kisheria hususani Baraza la Wafanyakazi na Kamati ya Bajeti, Aidha, makadirio hayo yanatakiwa kuzingatia Mpango mkakati wa mashirika ya umma.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kasoro mbalimbali zinazohusiana na uandaaji wa bajeti katika mashirika ya umma. Kasoro hizo zimeelezwa katika aya zifuatazo:

### (i) Kutoshirikisha Wadau Ipasvyo katika Maandalizi ya Bajeti ya Mashirika ya Umma

Nilibaini kuwa mashirika ya umma saba hayakushirikisha ipasavyo wadau wao katika uandaaji wa bajeti kama nilivyoainisha katika **Jedwali Na.20**. Hata hivyo, jitihada zimefanyika ikilinganishwa na ripoti yangu ya awali, ambayo nilibaini mashirika ya umma 16 yenye tatizo hilo.

Nilibaini kuwa kasoro hii imejirudia katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko, kama nilivyoripoti kwenye ripoti yangu ya mwaka 2022/23.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi bado haina Kamati ya Bajeti, huku Kamati ya Bajeti ya Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ikiwa haifanyi kazi ipasavyo.

**Jedwali Na. 20: Mashirika ya umma yenye ushiriki usioridhisha katika maandalizi ya bajeti**

| Na. | Mashirika ya umma | Madhaifu yaliobainika |
|---|---|---|
| 1 | Kampuni ya Ndege Tanzania | Kamati ya bajeti haijaundwa |
| 2 | Chuo Kikuu Cha Mzumbe | Kamati ya bajeti haijaundwa |
| 3 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela Kasumulu | Kamati ya bajeti haijaundwa |
| 4 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi | Kamati ya bajeti haijaundwa |
| 5 | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko | Barala la Wafanyakazi halijaundwa na hakuna Ushahidi kuonesha Kamati ya bajeti ilitelekeza majukumu yake ipasavyo |
| 6 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita | Hakuna Ushahidi kuonesha Kamati ya bajeti ilitelekeza majukumu yake ipasavyo |
| 7 | Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania | Hakuna Ushahidi kuonesha Kamati ya bajeti ilitelekeza majukumu yake ipasavyo |

**Chanzo:** *Taarifa za bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24*

Mashirika hayo hayakuzingatia umuhimu wa kushirikisha wadau wote katika mchakato wa maandalizi ya bajeti. Hali hii inaonesha kutokuwa na uwazi katika mchakato wa bajeti, hivyo kuibua shaka kuhusu uwajibikaji na usimamizi wa kifedha.

**Ninapendekeza mashirika ya umma kutambua umuhimu wa ushiriki wa wadau wote katika maandalizi ya bajeti kwa ajili ya uwazi.**

### (ii) Mashirika ya Umma Yaliyoandaa Bajeti bila Kuzingatia Mpango Mkakati

Nilibaini kuwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko na Bodi ya Chai Tanzania zilikuwa na makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24 ya shilingi bilioni 134.86 na shilingi bilioni 3.04, mtawalia, ambayo yalitokana na Mpango Mkakati uliopitwa na wakati wa 2018/19-2022/23 na 2014/15-2018/19, mtawalia. Hii inamaanisha kuwa fedha zinaweza kutengwa katika shughuli ambazo hazikuwa kipaumbele, jambo linaloweza kusababisha ukosefu wa fedha kwa malengo yaliyokusudiwa.

Aidha, nilibaini kuwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi lilikuwa na shughuli zenye bajeti ya shilingi milioni 393.49 ambazo hazikuwa kwenye Mpango Mkakati. Hii ilitokana na ukosefu wa mifumo madhubuti ya kufuatilia shughuli za bajeti dhidi ya malengo ya kimkakati, hali inayoweza kusababisha kutengwa kwa fedha kwenye shughuli zisizo za kimkakati, hivyo kusababisha upotevu wa rasilimali bila thamani halisi ya fedha.

**Ninapendekeza mashirika ya umma (a) yahakikishe wadau wa bajeti wanashiriki katika kuandaa bajeti na mpango mkakati, na (b) yazingatie Mpango Mkakati katika maandalizi ya Bajeti na kuweka mifumo ya ufuatiliaji na utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia mpango mkakati.**

## 8.6 Mapungufu katika Matumizi ya Mfumo wa Bajeti wa Serikali katika Mashirika ya Umma

Aya ya 1.2(113)(ii) ya Miongozo ya Utayarishaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali 2023/24 inawataka maafisa masuuli kutumia mfumo wa bajeti wa Serikali katika mchakato mzima wa bajeti.

Nilibaini mashirika ya umma matano hayakutumia mfumo wa bajeti wa Serikali, na mashirika ya umma sita yalikuwa na changamoto katika kutumia mfumo huo **(Rejea Jedwali Na. 21).** Hii inaonesha mapungufu katika jitihada zilizofanyika ikilinganishwa na mwaka 2021/22 ambapo nilibaini mashirika 13 yalikuwa na tatizo kama hilo. Hata hivyo, kwa mashirika ya umma niliyoripoti kwa mwaka 2021/22 ambapo Kampuni ya Ndege Tanzania ilikuwa mojawapo, nilibaini kampuni hiyo bado inakabiliwa na changamoto katika matumizi ya mfumo wa bajeti wa Serikali .

Mapungufu hayo yanatokana na kukosekana kwa utengamanishi kati ya mfumo wa bajeti wa Serikali na mifumo ya uhasibu ya mashirika ya umma.

**Jedwali Na. 21: Mashirika ya umma yenye mapungufu katika matumizi ya mfumo wa bajeti wa Serikali**

| Na. | Mashirika ya umma | Mapungufu yaliyobainika |
|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako | Hawatumii |
| 2 | Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila | Hawatumii |
| 3 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same Mwanga | Hawatumii |
| 4 | Kampuni ya Sisalana | Hawatumii |
| 5 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Ngara | Hawatumii |
| 6 | Shirika la Bima la Taifa | Haijitoshelezi(Hakuna utengamanishi kati ya mfumo wa bajeti wa Serikali na Mfumo wa uhasibu) |
| 7 | Shirika la Reli Tanzania | Haijitoshelezi(Hakuna utengamanishi kati ya mfumo wa bajeti wa Serikali na Mfumo wa uhasibu) |
| 8 | Kampuni ya Ndege Tanzania | Haijitoshelezi(Hakuna utengamanishi kati ya mfumo wa bajeti wa Serikali na Mfumo wa uhasibu) |
| 9 | Bohari Kuu ya Dawa | Haijitoshelezi (Mageresho ya bajeti yaliyopo kwenye mfumo wa bajeti wa Serikali hayafanani na mageresho ambayo yapo kwenye mfumo wa uhasibu |
| 10 | Chuo kikuu cha Ardhi | Haijitoshelezi(Mageresho ya bajeti yaliyopo kwenye mfumo wa bajeti wa Serikali hayafanani na mageresho ambayo yapo kwenye mfumo wa uhasibu |
| 11 | Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania | Haijitoshelezi(Moduli ya utekelezaji wa bajeti ilikuwa haifanyi kazi katika mfumo wa bajeti wa Serikali |

**Chanzo***: Taarifa za bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/24*

Kutokuwepo au matumizi yasiyoridhisha ya mfumo wa bajeti wa Serikali yanadhoofisha uwezo wa Serikali kufuatilia na kudhibiti kwa ufanisi utekelezaji wa bajeti za mashirika ya umma. Hii inaweza kuwa na athari kubwa katika ugawaji wa rasilimali kwa ufanisi.

**Ninapendekeza kwa mashirika ya umma yawasiliane na Wizara ya Fedha kuhakikisha utatuzi wa changamoto za mfumo, hususani utengamanishi thabiti kati ya mfumo wa bajeti wa Serikali na mifumo ya uhasibu ya mashirika ya umma ili kufanya tathmini na usimamizi wa bajeti.**

# Usimamizi wa Mali



# SURA YA TISA

# USIMAMIZI WA MALI

## 9.0 Utangulizi

Usimamizi wa mali unahusisha kuendeleza, kutumia, kutengeneza, na kuboresha mali kwa gharama nafuu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, sheria na miongozo ya usimamizi wa mali za umma. Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa mwaka 2019 uliotolewa na Wizara ya Fedha, pamoja na Kanuni za Fedha za Umma (Usimamizi wa Mali za Umma), za mwaka 2024 ndizo zinazotumika katika usimamizi wa mali za umma.

Sura hii inaonesha mapungufu katika usimamizi wa mali uliobainishwa wakati wa ukaguzi wa mwaka wa fedha 2023/24 na mapendekezo ya kuboresha.

## 9.1 Mashirika ya Umma kumiliki Ardhi bila kuwa na Hatimiliki yenye Thamani ya shilingi bilioni 201.67

Kwa mujibu wa agizo lililotolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi mwezi Septemba 2014 (Rej. CAB.39/156/01/52), Wizara, Idara, na Wakala wote wa Serikali wanapaswa kupata hatimiliki za ardhi na majengo ya umma yaliyo chini ya usimamizi wao.

Katika ukaguzi wa taarifa za mali zisizohamishika nilibaini kuwa viwanja vya ardhi 259, vyenye thamani ya shilingi bilioni 201.67, vinamilikiwa na mashirika ya umma 18 bila mashirika hayo kuwa na hati ya umiliki wa viwanja hivyo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 22.** Hali hii inatokana na mashirika ya umma kuchelewa kuomba na kufuatilia hati miliki kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, pamoja na kuwepo kwa migogoro ya kisheria hasa kwa ardhi zilizovamiwa. Kukosekana kwa hatimiliki kunaweza kusababisha uvamizi holela na kukosa haki ya kisheria kuhusu uhali wa umiliki, hasa wakati wa migogoro ya kisheria.

**Jedwali Na. 22: Orodha ya mashirika ya umma yanayomiliki ardhi bila hatimiliki**

| Na. | Jina la Shirika | Idadi ya viwanja | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|---|---|
| 1. | Shirika la Nyumba la Taifa | 139 | 172,748,240 |
| 2. | Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro | 1 | 8,000,000 |
| 3. | Mamlaka ya Bandari Tanzania | 15 | 7,617,361 |
| 4. | Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania | 7 | 2,513,200 |
| 5. | Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi | 1 | 2,237,000 |
| 6. | Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo | 15 | 2,123,350 |
| 7. | Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania | 2 | 1,859,712 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **8.** | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza | 29 | 1,698,145 |
| **9.** | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko | 1 | 770,000 |
| **10.** | Kampuni ya Sisalana Tanzania | 15 | 728,393 |
| **11.** | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama - Shinyanga | 10 | 583,456 |
| **12.** | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita | 1 | 324,370 |
| **13.** | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu | 12 | 231,581 |
| **14.** | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tabora | 6 | 134,984 |
| **15.** | Chuo Kikuu Mzumbe | 1 | 70,000 |
| **16.** | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea | 2 | 24,300 |
| **17.** | Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania | 1 | 6,000 |
| **18.** | Bohari Kuu ya Dawa | 1 | 4,500 |
| | **JUMLA** | **259** | **201,674,592** |

**Chanzo:** *Rejista ya mali zilizonunuliwa 2023/24*

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika (a) yahakikishe yanawasilisha maombi ya hati miliki kwa wakati mara baada ya kununua ardhi na kufuatilia kwa karibu kwa mamlaka inayotoa hati ili kupata hatimiliki; na (b) yahakikishe ardhi zote zinalindwa dhidi ya uvamizi ili kuzuia migogoro ya kisheria.**

## 9.2 Kuwepo kwa Mali Zilizotelekezwa, Zisizotumika na Zilizoharibika zenye Thamani ya shilingi bilioni 37.07 katika Mashirika ya Umma

Kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Fedha za Umma (Usimamizi wa Mali za Umma) za mwaka 2024 inamtaka afisa masuuli kuhakikisha kuwa mali za umma zinatumika kwa ufanisi na kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Katika hali ambapo mali ya umma haitumiki, haifanyi kazi, au inatumiwa chini ya kiwango kwa muda wa miezi sita au zaidi, afisa masuuli anapaswa kutoa taarifa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha kwa hatua na maelekezo zaidi

Uhakiki wangu ulibaini majengo yaliyotelekezwa, yasiyotumika, na yaliyoharibika pamoja na mashine zisizotumika za thamani ya shilingi bilioni 37.07.

**Jedwali Na. 23: Orodha ya mali zilizotelekezwa, zisizotumika, na zilizoharibika**

| Na | Mashirika ya Umma | Maelezo | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|---|---|
| 1. | Kampuni ya Nyumba na Pensioni | Jengo la IPS linalomilikiwa na Kampuni ya Nyumba na Pensheni liko katika hali duni, na sehemu | 23,790,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | nyingi zimeendelea kuwa katika hali mbaya kwa zaidi ya miaka mitatu | |
| **2.** | Bohari Kuu ya Dawa | Mitambo imebaki kutotumika kwa zaidi ya miaka mitatu tangu iliponunuliwa mwaka wa 2020/21 | 6,339,814 |
| **3.** | Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania | Jengo la Biashara lililopo Ismani, Upanga Dar es Salaam, limeachwa bila kutumika kwa zaidi ya mwaka mmoja bila uwekezaji, ingawa liko katika eneo la kimkakati kwa uwekezaji | 3,963,000 |
| **4.** | Hifadhi za Taifa Tanzania | Majengo sita ya utalii yaliyokamilika katika hifadhi za Tarangire, Burigi Chato na Katavi ambayo yamekamilika lakini hayatumiki kwa zaidi ya mwaka mmoja. | 1,769,805 |
| **5.** | Tume ya Ushindani | Tume ya Ushindani inamiliki ghorofa ya saba ya Jengo la Azikiwe, lililopo kwenye kiwanja namba 2386/12-2389/12 katika Mtaa wa Azikiwe, Dar es Salaam. Hata hivyo, nafasi ya ofisi imebaki tupu/haitumiki tangu mwaka 2021. | 319,757 |
| **6.** | Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro | Mradi uliotelekezwa wa kituo cha walinzi cha Garlus katika hifadhi ya Pololeti. Ujenzi ulisimama tangu Novemba 2023 na kazi hazikuwahi kuendelea hadi wakati wa ukaguzi huu tarehe 25 Septemba 2025 | 297,810 |
| | | Hosteli ya Makoromba ilitelekezwa kwa miaka saba | 208,109 |
| **7.** | Mamlaka ya Elimu Tanzania | Bweni katika Shule ya Sekondari ya Mbomai lililokamilika lakini halitumiki kutokana na ukosefu wa samani | 141,934 |
| **8.** | Baraza la Taifa la Ujenzi | Sehemu kubwa ya jengo lake la mita za mraba 488 katika Samora Tower halitumika kufuatia kuhamia Dodoma mwaka 2021, pia eneo la mita za mraba 54 katika Jengo la OAS-Azikiwe Avenue limebaki bila matumizi kwa muda mrefu | 136,404 |
| **9.** | Shirika la Nyumba la Taifa | Tawi la Tanga lilijenga nyumba za makazi tano za vyumba vitatu kila kimoja na nyingine tano za nyumba viwili kila moja, na ujenzi huo ulikamilika lakini havitumiki | 100,000 |
| **10.** | Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili | Mfumo wa Usimamizi wa Magari/Mali zisizohamishika ulitengenezwa mwaka 2020 lakini haujaanza kutumika | 9,000 |
| | **Jumla** | | **37,075,633** |

**Chanzo**: *Rejesta ya Mali za Kudumu*

Mali hazijatumiwa hasa kutokana na ukosefu wa fedha za ununuzi, ukarabati au kumalizia, michakato ya ununuzi inayoendelea kwa muda mrefu, na ukosefu wa mkakati ulio bayana kuhusu matumizi ya mali zisizotumika. Kuendelea kwa hali ya kutotumika na hali duni ya majengo na mali nyingine kunachagiza kuharibika na kupoteza thamani, jambo ambalo linaweza kusababisha gharama za matengenezo zisizo za lazima.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika kuchukue hatua za haraka kuweka na kufunga vifaa muhimu na samani, kukarabati majengo ili kuendelea kuwa katika nafasi ya ushindani na kuhifadhi na kupata mapato ya kodi kutoka kwa wapangaji. Pia, kutenga fedha kwa ajili ya kuharakisha ufungaji wa mitambo na kumalizia kazi zingine ambazo hazijakamilika.**

## 9.3 Kuwepo kwa Mali Zilizokaa Muda Mrefu na Zisizotumika Bila Matengenezo au Kuuzwa katika Mashirika ya Umma shilingi bilioni 6.42

Ukaguzi ulibaini kuwa mashirika ya umma 14 yalikuwa na jumla ya mali zilizokaa muda mrefu na zisizotumika 5,068, ikiwa ni pamoja na magari, pikipiki, vifaa, samani za ofisi, na vifaa vingine zenye thamani ya shilingi bilioni 2.92 kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na.IX**. Mali hizi hazijatumika kwa muda mrefu kati ya miezi 6 hadi miaka 27 bila kufanyiwa matengenezo au kuuzwa.

Pia, nilibaini kuwa mashirika ya umma matano yalikuwa na bidhaa 20,095 zilizopitwa na wakati kwa muda wa miezi 6 hadi miaka 7 bila kuondolewa zenye thamani ya shilingi bilioni 3.50. Hii inatokana na mipango duni ya kuondoa mali zilizokaa muda mrefu na zisizotumika. Kutofanya matengenezo ya magari yaliyokaa muda mrefu na kuuzwa kwa mali zisizoweza kutumika kunaweza kusababisha kushuka kwa thamani kutokana na kuendelea kuharibika. Pia, bidhaa zilizokwisha muda zilichukua nafasi isiyo ya lazima na kusababisha gharama nyingine za utunzaji.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yaweke mpango wa matengenezo au kuuza mali** zilizokaa **muda mrefu na kuutekeleza kwa ufanisi.**

## 9.4 Kuwepo kwa Mali ambazo Hazijakabidhiwa kwa Kampuni ya Ndege Tanzania kutoka kwa Kampuni Hodhi ya Shirika la Ndege na Ucheleweshaji wa Uhamisho wa Umiliki wa Mali kwa Kampuni ya Sisalana Tanzania shilingi bilioni 3.59

Katika ukaguzi wa **Kampuni ya Ndege Tanzania**, nilibaini kuwa wakati wa kurekebishwa kwa kampuni ya Ndege Tanzania ya zamani, shirika lililoundwa ili kusimamia mali na madeni ya Kampuni hiyo (Air Tanzania Holding Corporation) lilichukua udhibiti wa mali tisa.

Hata hivyo, ushahidi upo kwa uhamishaji wa mali mbili pekee kutoka shirika hilo simamizi kwenda kwa Wizara ya Mambo ya Nje, wakati kwa mali saba zilizobaki, hakuna nyaraka zinazoonesha uondoaji wake au uhamisho kwa msimamizi aliyeteuliwa au kwa kampuni mpya iliyoundwa yaani Kampuni ya Ndege Tanzania.

Pia, nilibaini kuwa kati ya mali saba, mali tatu hazijakabidhiwa kwa Kampuni ya Ndege Tanzania hadi tarehe ya kukamilisha ukaguzi mwezi Disemba 2024 licha ya Shirika la Ndege kuikumbusha Wizara ya Mambo ya Nje mara kadhaa kuhusu kukamilisha mchakato wa kukabidhi mali ambazo zilikuwa chini ya usimamizi wa Wizara kufuatia kusitishwa kwa shirika la usimamizi wa mali na madeni ya iliyokuwa Kampuni ya Ndege Tanzania zamani (Air Tanzania Holding Corporation (ATHCO)), wakati mali nne zilizobaki hazikuwa na ushahidi wa ama kuuzwa au kuhamishwa kwenda shehemu nyingine (Rejea **Jedwali Na. 24**).

Hii inatokana na mapungufu katika kurekebishwa upya kwa kampuni ya ndege ya zamani, ambapo inazuia upatikanaji na uhamisho wa mali kwa urahisi. Aidha, kumekuwa na ufuatiliaji usio wa kutosha kwa Msajili wa Hazina na Wizara ya Mambo ya Nje ili kuhakikisha kuwa Kampuni ya Ndege inapata nyaraka zote muhimu zinazothibitisha kuwa umiliki wa mali hizo umewekwa kwa kampuni. Ukosefu wa kupanga marekebisho ipasavyo unaleta mashaka kuhusu umiliki, usajili, au uhamisho wa mali hizi, hivyo kukwamisha zaidi ushirikishwaji wake katika rekodi za kampuni mpya.

**Jedwali Na. 24: Mali ambazo hazijakabidhiwa kwa Kampuni ya ndege**

| Na | Namba ya Kiwanja | Jina la Mali | Cheti cha umiliki Na | Eneo | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 3209 | Haki ya kukodisha katika viwanja | 139851 | Kisingu Hill, Kampala-Uganda | Hakuna ushahidi wa uondoaji au uhamisho. |
| 2 | 662 | Haki ya kumiliki makazi | 684 | Barabara ya Tanu-Mtwara Tanzania | Hakuna ushahidi wa uondoaji au uhamisho. |
| 3 | 1-48. | Haki ya kukodisha katika viwanja | 11720 | KIA-Tanzania | Hakuna ushahidi wa uondoaji au uhamisho. |
| 4 | 4/3, 4/4, 4/5, 4/6 | Haki ya kukodisha katika viwanja | N/A | Oysterbay, DSM-Tanzania | Hakuna ushahidi wa uondoaji au uhamisho. |
| 5 | 3821 | Haki ya kumiliki makazi | 17760 | Manda Hill, Lusaka-Zambia | Chini ya usimamizi wa Wizara hakijakabidhiwa. |
| 6 | 2/472 | Haki ya kukodisha katika viwanja | 2/472 | Oledume, Nairobi-Kenya | Chini ya usimamizi wa Wizara hakijakabidhiwa. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **7** | 7/31. | Haki ya kumiliki makazi | T49305 /1995 | Johan-nesburg-South Africa | Chini ya usimamizi wa Wizara hakijakabidhiwa. |
| **8** | 340 | Haki ya kumiliki makazi | 21374 | Chelstone, Lusaka-Zambia | Imeondolewa kwenda Wizara ya Mambo ya Nje |
| **9** | 289 | Haki ya kumiliki makazi | 5205/98 | Mji wa Malborough, Harare Zimbabwe | Imeondolewa kwenda Wizara ya Mambo ya Nje |

**Chanzo***: Jedwali la Tatu la Sheria ya ATC (Upangaji upya na uwekaji wa mali na madeni) ya mwaka 2002*

- Kwa **Kampuni ya Sisalana Tanzania,** nilibaini kucheleweshwa kwa uhamisho wa umiliki wa mali za jumla ya shilingi bilioni 3.59. Mali hizi zilinunuliwa kutoka kampuni ya Katani Tanzania, ambayo ilifutwa baada ya kushindwa kulipa mkopo uliotolewa na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi.
  Hii inahusishwa na kucheleweshwa kwa kukamilisha uhamisho wa kisheria wa mali kutoka kampuni ya Katani Tanzania kwenda kampuni ya Sisalana Tanzania. Mali hizo ziliwekwa kama dhamana ya mkopo ambao Kampuni ya Katani Tanzania ilishindwa kulipa. Kuchelewa kukamilishwa kwa uhamisho wa kisheria kunaikosesha Kampuni ya Sisalana umiliki halali, kukitokea migogoro kuhusu mali hizo.

**Ninapendekeza (a) mashirika ya umma yafanye mapitio ya kina ili kutambua na kuthibitisha mali zote zinazomilikiwa na kampuni katika maeneo mbalimbali; na (b) yafuatilie kwa karibu katika Mamlaka husika kuhusu umiliki wa kisheria wa mali, na kuhakikisha kuwepo na nyaraka sahihi za umiliki na uhamisho na kuhusisha washauri wa kisheria na kifedha ili kushughulikia masuala yoyote yenye utata yanayohusiana na umiliki wa mali.**

## 9.5 Kucheleweshwa kwa Uhamisho wa Mali kutoka Kampuni ya Madini Pangea kwenda Kampuni ya STAMIGOLD zenye Thamani ya shilingi bilioni 22.42

Mnamo tarehe 15 Novemba 2013, Kampuni ya Madini ya Pangea na ABG waliingia katika makubaliano na Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ya kuhamisha Mgodi wa Tulawaka wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 11.63 kutoka Kampuni ya Madini ya Pangea kwenda Kampuni ya STAMIGOLD.

Kabla ya kusainiwa kwa mkataba huo tarehe 28 Oktoba 2013, nilibaini kuwa Shirika la Madini la Taifa liliunda kampuni tanzu, (Kampuni ya STAMIGOLD), kwa madhumuni ya kuendesha mgodi wa Tulawaka. Hata hivyo, hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha tarehe 30 Juni 2024, mali zenye thamani ya shilingi bilioni 22.42

bado hazikuwa zimehamishiwa kwenye Kampuni ya STAMIGOLD na zilikuwa bado zimesajiliwa chini ya Kampuni ya Madini ya Pangea.

Zaidi ya hayo, kufikia mwisho wa mwaka wa fedha tarehe 30 Juni 2024, Kampuni ya Madini ya Pangea haikupata hati ya kuthibitisha kutokuwa na deni la kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania kutokana na masuala ya kodi ambayo bado hayajatatuliwa. Hali hii ilisababisha hati miliki za mali zote kubaki katika jina la Kampuni ya Madini ya Pangea badala ya Kampuni ya STAMIGOLD.

Kwa maoni yangu, ucheleweshaji huu unaweza kuhatarisha usimamizi wa mali hizo, jambo ambalo linaweza kuathiri ufanisi wa uendeshaji wa kampuni.

**Ninapendekeza Shirika la Madini la Taifa liharakishe uhamisho wa mali za Mgodi wa Tulawaka kutoka Kampuni ya Madini ya Pangea kwenda Kampuni ya STAMIGOLD na lifatilie kwa karibu mchakato wa upatikanaji wa hati ya kuthibitisha kutokuwa na deni la kodi kati ya Kampuni ya Madini Pangea na Mamlaka ya Mapato Tanzania.**

# Usimamizi wa Mikataba na Ununuzi

National e-Procurement System of Tanzania

# SURA YA KUMI

# USIMAMIZI WA MIKATABA NA UNUNUZI

## 10.0 Utangulizi

Kifungu cha 48 (3) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, [Sura 410],kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutathmini kama shirika nunuzi la Serikali limezingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake. Katika sura hii, nimetathmini uzingatiaji wa sheria ya ununuzi wa umma na kanuni zake kwa mashirika ya umma 217, ambapo nilibaini kuwa mashirika ya umma 128 yalizingatia sheria ya ununuzi wa umma na kanuni zake, wakati mashirika ya umma 89 yalibainika kutozingatia sheria kikamilifu na yanahitaji kufanya maboresho.

## 10.1 Usimamizi Duni na Kuchelewa Kukamilisha Utekelezaji wa Mikataba ya Bidhaa, Huduma na Ujenzi yenye Thamani ya shilingi bilioni 8.68 na dola za Marekani milioni 16.25

Kanuni ya 114 ya Kanuni za Ununuzi za Umma, za mwaka 2013, zinahitaji usimamizi madhubuti wa ununuzi wa bidhaa, huduma na ujenzi.

Wakati wa ukaguzi wa mikataba ya ununuzi katika mashirika ya umma nane nilibaini kuwa wazabuni na watoa huduma walicheleweshа utoaji wa bidhaa, huduma na ujenzi wenye thamani ya shilingi bilioni 8.68 na dola za Marekani milioni 16.25, kwa muda wa kuanzia siku 1 hadi siku 330, kama ilivyoorodheshwa kwenye **Jedwali Na. 25**. Katika ripoti yangu ya mwaka 2021/22, niliripoti ucheleweshaji kwa mashirika 12. Katika mwaka 2022/23 nilibaini mashirika 22 pia yalicheleweshewa bidhaa na wazabuni. Hata hivyo, kwa mwaka huu, idadi ya mashirika ya umma yaliyocheleweshewa bidhaa, huduma na ujenzi imepungua hadi kufikia nane.

**Jedwali Na. 25: Orodha ya mashirika ya umma yaliyocheleweshewa bidhaa na huduma**

| Na. | Jina la Shirika | Kiasi cha Mkataba Sh. '000 | Muda uliochelewa (Siku) |
|---|---|---|---|
| 1. | Chuo cha Uhasibu Arusha | 4,799,103 | 42 hadi 229 |
| 2. | Bohari Kuu ya Dawa | 2,136,396 | 1 hadi 172 |
| 3. | Shirika la Mawasiliano Tanzania | 996,221 | 235 hadi 330 |
| 4. | Chuo Kikuu cha Dodoma | 311,071 | 7 hadi 90 |
| 5. | Kampuni ya Gesi Tanzania | 255,000 | 140 |
| 6. | Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini | 130,096 | 27 hadi122 |
| 7. | Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania | 59,348 | 12 hadi 15 |
| | Jumla | 8,687,235 | |
| **Na** | Jina la Taasisi | **Kiasi (USD '000)** | Muda uliochelewa (Siku) |
| 8 | Kampuni ya Mbolea Tanzania | 16,250 | 60 |

**Chanzo:** *Mafaili ya Ununuzi ya mashirika ya mwaka 2023/24*

Ucheleweshwaji huo ulisababishwa na makadirio pungufu ya mawanda ya kazi, ucheleweshaji wa ununuzi wa vifaa na mahitaji ya mradi, mifumo ya udhibiti wa ndani kushindwa kufanya kazi, ukosefu wa fedha, na mabadiliko ya hali ya hewa na mabadiliko ya kazi za mradi.

Ucheleweshaji wa utekelezaji wa shughuli una athari mbaya katika kufikia malengo ya mashirika ya umma na unakwamisha ukuaji wa uchumi wa nchi.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika kuchukua hatua madhubuti ili kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati na bidhaa au huduma zilizonunuliwa zinawasilishwa bila kuchelewa.**

## 10.2 Kushindwa Kufanya Ununuzi wa Moja kwa Moja kutoka kwa Wazalishaji wa Vifaa vya Ujenzi vyenye Thamani ya shilingi bilioni 6.29

Nilibaini Chuo cha Uhasibu Arusha kilinunua tani 8,392 za saruji na nondo zenye thamani ya shilingi bilioni 6.29 ambazo zilihitajika kwa ajili ya miradi mbalimbali inayotekelezwa kwa njia ya ujenzi wa kutumia rasilimali za ndani. vifaa vilinunuliwa kupitia mfumo wa makubaliano ya ununuzi ya muda mrefu na wazabuni, badala ya kununua moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji kinyume na Aya ya 13.1 ya Mwongozo wa ujenzi kwa kutumia rasilimali za ndani wa Mei 2020. Hali hii imeongeza gharama za miradi inayotekelezwa kupitia rasilimali za ndani, ambayo inaweza kusababisha changamoto za kifedha na kuchelewa kukamilika kwa mradi.

**Ninapendekeza Chuo cha Uhasibu Arusha kifuate Mwongozo wa ujenzi kwa kutumia rasilimali za ndani ili kuhakikisha ufanisi wa gharama na thamani ya fedha.**

## 10.3 Kufanya Mabadiliko ya Mikataba kinyume na Taratibu za Udhibiti wa Ununuzi wa umma, yenye Thamani ya shilingi bilioni 2.58

Chuo cha Uhasibu Arusha kiliingia mikataba miwili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi kwa ajili ya Kampasi Kuu ya Arusha na Kampasi ya Babati yenye thamani ya shilingi bilioni 4.94, ikijumuisha saruji na nondo zenye thamani ya shilingi bilioni 2.76. Hata hivyo, chuo kilifanya ununuzi wa ziada wa saruji na nondo, ambao ulifikia thamani ya shilingi bilioni 5.34, hivyo kuzidi kiasi kilichoidhinishwa kwa shilingi bilioni 2.58.

Ununuzi wa ziada haukuanzishwa na idara tumiaji, haikuidhinishwa na bodi ya zabuni. Licha ya kuvuka ukomo wa mabadiliko ya mkataba ya asilimia 15, mabadiliko hayo hayakuidhinishwa na mamlaka za

uidhinishaji wa bajeti. Aidha, nyongeza iliyosainiwa haikufafanua idadi ya vifaa vya ziada vilivyohitajika.

Kushindwa kwa bodi ya zabuni kutathmini, kufuatilia, na kudhibiti ununuzi chini ya makubaliano maalumu, kwa kupitia maazimio yaliyofanyika bila ya wajumbe kukutana "circular resolutions", pamoja na kutokupata idhini za bajeti. Hii ilisababisha ongezeko la gharama zisizotarajiwa, na hatimaye kuathiri thamani ya fedha katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

**Ninapendekeza Chuo cha Uhasibu Arusha kiimarishe udhibiti wake wa ununuzi ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria za ununuzi na kuzuia mabadiliko ya mikataba yasiyoidhinishwa.**

## 10.4 Udhaifu katika Usimamizi na Udhibiti wa Malipo ya Awali kwa Wazabuni

### (a) Malipo ya Awali kwa Wazabuni na Wakandarasi Yaliyokiuka Taratibu shilingi bilioni 3.66

Katika ukaguzi wa usimamizi wa mikataba katika mashirika ya umma sita nilibaini mapungufu katika malipo ya awali yenye jumla ya shilingi bilioni 3.66. Malipo haya ya awali yalihusisha shilingi milioni 827 katika Chuo cha Uhasibu Arusha, shilingi milioni 150 kwa Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini, na shilingi milioni 12 kwa kampuni ya Sisalana Tanzania ambayo yalifanyika bila kupata dhamana kutoka kwa wazabuni.

Aidha, nilibaini malipo ya awali ya shilingi milioni 71 yalifanyika katika **Hospitali ya Taifa Muhimbili** na shilingi milioni 324 katika **Chuo cha Uhasibu Arusha**. Katika Hospitali ya Muhimbili, ujenzi ulisitishwa kabla malipo ya awali hayajarejeshwa, wakati katika **Chuo cha Uhasibu Arusha** gari moja halikuwasilishwa. Dhamana zilizotolewa zilikuwa zimekwishamaliza muda wake, jambo ambalo limesababisha hasara ya kifedha kwa mashirika hayo.

Katika **Kampuni ya STAMIGOLD**, wasambazaji walipokea malipo ya awali ya shilingi milioni 148 kati ya Julai 2023 na Machi 2024 kwa bidhaa ambazo hazikuwa zimewasilishwa kufikia tarehe ya ukaguzi ya 13 Septemba 2024. Zaidi ya hayo, wasambazaji watatu walikataa kuwasilisha bidhaa baada ya kupokea malipo ya awali ya shilingi milioni 74, kwa sababu walikuwa wanaidai Kampuni madai mengine ya muda mrefu.

Katika **Shirika la Umeme Tanzania**, mkandarasi alikuwa na mkataba wa kusambaza, kufunga, kujaribu na kukabidhi kituo cha umeme cha kilovoti 220/132/33, megavoti-Ampia2x120 katika eneo la Ununio, na alikuwa ametoa dhamana ya malipo ya awali. Hata hivyo, kabla malipo ya awali hayajarejeshwa kikamilifu, dhamana hiyo ilifika ukomo wa muda wake. Dhamana hiyo ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 2.13 na mkandarasi alishindwa kuihuisha kutokana na matatizo ya kifedha.

Ukosefu wa dhamana za malipo ya awali na kushindwa kurejesha malipo kunayaweka mashirika katika hatari ya kupoteza fedha za umma ikiwa wasambazaji au wakandarasi watashindwa kutimiza majukumu yao. Mapungufu haya yametokana na ukomo wa muda wa dhamana kabla ya urejeshaji wa malipo ya awali na kushindwa kuongeza muda wa dhamana na kufanya malipo kwa wasambazaji kabla ya kuwasilisha bidhaa.

### (b) Shirika la Umeme Tanzania Limeshindwa Kulipa Malipo ya Awali Kinyume na Mikataba Shilingi bilioni 88.09 na dola za Marekani milioni 43.18

Shirika la Umeme Tanzania linatekeleza miradi ya usanifu wa kihandisi, ugavi, ufungaji, upimaji na kuwezesha njia ya kusafirisha umeme ya kilovolti 220/33 kutoka Pugu hadi Dundani. Na Mradi mwingine wa kusanifu, usambazaji, ufungaji, upimaji na kuwezesha mradi wa njia ya kusambaza umeme wa msongo wa kilovolti 220 kwa ajili ya kusambaza umeme katika mradi wa Reli ya Kisasa(SGR) kutoka Isaka hadi Mwanza yenye mkataba wa shilingi bilioni 88.09 na dola za Marekani milioni 43.18 kuanzia tarehe 01 Novemba 2023 hadi 20 Julai 2025.

Miradi ilikuwa ikiendelea na wakandarasi walikuwa wamewasilisha ankara za malipo ya awali kama ilivyoainishwa kwenye mkataba na mahitaji ya utekelezaji. Hata hivyo, malipo haya hayakuwa yamechakatwa kufikia tarehe ya ukaguzi ya tarehe 28 Januari 2025. Hii ilisababisha ucheleweshaji wa malipo hadi kufikia siku 367, ambayo ilikuwa ni kinyume na masharti ya mkataba. Ucheleweshaji huo ulisababishwa na ukosefu wa fedha za kutosha kusaidia utekelezaji wa mradi.

Hali hii inaonesha kuwa mradi unaweza kukabiliwa na changamoto katika kufanya malipo ya haraka ya ankara za mradi na uwezekano wa kusababisha adhabu kwa kuchelewa kwa malipo. Pia huweka hatari ya kuongezeka kwa gharama kutokana na marekebisho ya bei.

**Ninapendekeza (a) Mashirika ya Umma husika yahakikishe dhamana za malipo ya awali zinawasilishwa na kufanya juhudi za kina kurejesha malipo ya awali ambayo hayajarejeshwa, ili kupunguza hatari ya kupoteza fedha za umma iwapo wasambazaji au wakandarasi watashindwa kutekeleza majukumu yao; na (b) Shirika la Umeme Tanzania liimarishe mtiririko wa fedha na kuhakikisha kuwa fedha za kutosha zinapatikana kwa ajili ya malipo ya awali na utekelezaji wa mradi mzima.**

## 10.5 Mikataba Iliyotekelezwa Bila Dhamana ya Utendaji yenye Thamani ya shilingi bilioni 66.83 na dola za Marekani 700,870

Nilibaini mapungufu katika dhamana za utendaji katika mikataba ya mashirika ya umma 10 yenye thamani ya shilingi bilioni 66.83 na dola za Marekani 700,870 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 26 na malezo yafuatayo:**

Nilibaini mashirika ya umma **mawili** yalitekeleza mikataba miwili yenye thamani ya shilingi bilioni 1.74 bila kuwa na dhamana za utendaji, jambo ambalo linakiuka Kanuni ya 29 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013. Hata hivyo, kumekuwa na maboresho ikilinganishwa na ripoti ya mwaka 2022/23, ambapo nilibaini mapungufu kama haya katika mashirika ya umma 14.

Pia, nilibaini mashirika ya umma **matatu** yalisaini mikataba mitatu yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 4.90 kabla ya kuwasilishwa dhamana za utendaji zinazohitajika, hivyo kukiuka aya ya 11.2 ya Mwongozo ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kuhusu dhamana wa mwezi Februari 2022.

Aidha, mashirika ya umma **matano** yalikuwa na dhamana za utendaji zilizokwisha muda wake kwa mikataba tisa inayoendelea yenye thamani ya shiingi bilioni 41.18 na dola za Marekani 700,870. Hii inakiuka Kanuni ya 29(6) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 inayohitaji dhamana za utendaji ziwepo hadi kukamilika kwa mkataba. Tatizo hili lilitokana na nyongeza za muda wa mikataba bila nyongeza zinazoambatana za muda wa dhamana ya utendaji.

Aidha, nilibaini **Shirika la Nyumba la Taifa** liliingia kwenye mikataba sita yenye thamani ya shilingi bilioni 19, hata hivyo dhamana zilizowasilishwa hazikuhakikiwa ili kuthibitishwa kabla ya kusaini mikataba hiyo.

**Jedwali Na. 26: Mashirika yaliyo na mikataba ya ununuzi yenye dhamana za utendaji zilizofikia ukomo wa muda**

| Jina la Shirika | Idadi ya Mikataba | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|---|
| Chuo cha Uhasibu Arusha | Bila dhamana | 864,000 |
| Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari | Bila dhamana | 877,000 |
| **Jumla ndogo** | | **1,741,000** |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | Kusaini kabla dhamana | 3,999,212 |
| Chuo cha Uhasibu Arusha | Kusaini kabla dhamana | 863,760 |
| Hifadhi za Taifa Tanzania | Kusaini kabla dhamana | 42,754 |
| **Jumla ndogo** | | **4,905,727** |

| | | |
|---|---|---|
| Kampuni ya STAMIGOLD | Dhamana kuisha muda | 23,554,710 |
| Hifadhi za Taifa Tanzania | Dhamana kuisha muda | 12,555,688 |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro | Dhamana kuisha muda | 3,186,847 |
| Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea | Dhamana kuisha muda | 1,168,863 |
| Mamlaka ya Bandari Tanzania | Dhamana kuisha muda | 718,032 |
| **Jumla ndogo** | | **41,184,140** |
| Shirika la Nyumba la Taifa | Dhamana hazikuhakikiwa | 19,002,393 |
| **Jumla Kuu** | | **66,833,260** |
| **Jina la Shirika** | **Idadi ya Mikataba** | **Kiasi (Dola za Marekani)** |
| **Mamlaka ya Bandari Tanzania** | 1 | 700,870 |

**Chanzo:** *Mafaili ya Ununuzi ya mashirika ya umma, 2023/24*

Kwa maoni yangu, ukosefu au kumalizika kwa muda wa dhamana za utendaji yanaweka mashirika ya umma katika hatari ya kupoteza fedha za umma endapo msambazaji au mkandarasi atashindwa kutimiza masharti ya mkataba..

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika kuhakikisha mikataba yote inakuwa na dhamana ipasavyo ili kulinda maslahi yao na kuepuka hasara za kifedha zinazoweza kutokea. Pia, mchakato wa nyongeza za mikataba uimarishwe ili kuhakikisha kuwa mikataba na dhamana za utendaji zinaongezwa ipasavyo na kuhakiki dhamana kabla ya kusaini mikataba.**

## 10.6 Kusimamishwa kwa Mradi wa Ujenzi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili Kutokana na Kukosekana kwa Fedha shilingi bilioni 1.36

Mradi wa ujenzi wa awamu ya pili wa Mradi wa Wodi za Watu Mashuhuri na Wodi za Watu Binafsi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili wenye thamani ya shilingi bilioni 1.36, ulisitishwa tarehe 17 Desemba 2023 kutokana na changamoto za kifedha. Kazi hiyo ilikuwa imepangwa kukamilika kwa muda wa miezi sita, kuanzia tarehe 24 Desemba 2021. Kutokana na hali hiyo, Hospitali ya Taifa Muhimbili ilisimamisha rasmi kazi ya mkandarasi tarehe 17 Februari 2024, na tarehe 4 Juni 2024, pande zote mbili zilikubali kufunga mkataba huo.

Katika ukaguzi, nilibaini kuwa Wizara ya Afya iliipa idhini Hospitali ya Muhimbili kutafuta wawekezaji kwa ajili ya kazi iliyobaki. Kuanzisha mradi bila uhakika wa fedha kunakiuka Kanuni ya 75(1)(3)

ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013, ambayo inahitaji kuhakikisha kuwepo kwa fedha kabla ya kuanza mradi.

Kuna hatari ya kupoteza shilingi milioni 71.51, zilizolipwa kama malipo ya awali, kwani hazijarejeshwa kikamilifu na dhamana ya malipo ya awali imekwisha muda wake. Pia, mradi ukianza tena, gharama za ziada zinaweza kutokea kutokana na mfumuko wa bei na mabadiliko ya gharama za vifaa na wafanyakazi. Kusimamishwa kwa mradi kunaweza kuchelewesha huduma muhimu kwa wagonjwa, hasa wale wanaohitaji huduma maalumu au za binafsi.

**Ninapendekeza Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ihahikishe uwepo wa fedha za kutosha kabla ya kuanza miradi ili kuzuia ucheleweshaji na ongezeko la bei. Pia, ihakikishe marejesho ya malipo ya awali yanafanyika na kuwa na mifumo ya udhibiti wa ndani madhubuti juu ya mwelekeo wa mradi, muda wa utekelezaji, na muundo wa kifedha, hasa ikiwa wawekezaji wa nje watapatikana.**

## 10.7 Kutokamilisha Uainishaji wa Kiufundi katika Ununuzi wa Vifaa na Utekelezaji wa Miradi wenye Thamani ya shilingi bilioni 6.34 katika Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza

Nilibaini kuwa mikataba mitano katika Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mwanza ambayo ununuzi wa vifaa na utekelezaji wa ujenzi katika Mkoa wa Mwanza yenye thamani ya shilingi bilioni 6.34, haikuwa na malezoo kamilifu na bayana ya kiufundi katika mikataba. Mikataba haikujumuisha maelezo ya kina ya vifaa, ubora wa kazi, viwango, na mahitaji ya ubora. Tatizo hili lilitokana na mapungufu ya watumishi katika maandalizi ya nyaraka za zabuni.

Uainishaji wa kiufundi ni muhimu kwa kuhakikisha uelewa ulio bayana wa viwango vya mradi. Bila uainishaji huo, mapungufu ya ubora na utekelezaji yanaweza kutokea, na kusababisha matokeo duni na zabuni za gharama kubwa kutoka kwa wakandarasi kutokana na kutokuelewana kuhusu wigo wa mradi.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza ihakikishe kuwa na uainishaji wa kiufundi ulio kamili kwa ajili ya ununuzi na utekelezaji wa miradi, na ishughulikie uainishaji wowote unaokosekana katika miradi inayoendelea ili kufikia viwango vya ubora vinavyohitajika.**

## 10.8 Kuchelewa kulipwa kwa Madeni ya Wakandarasi na Wazabuni ya shilingi bilioni 54.84; yuro 194,000 na dola za Marekani milioni 354.45

Nilibaini kuwa mashirika ya umma 13 yalichelewesha malipo ya madai ya wakandarasi na wazabuni yenye thamani ya shilingi bilioni 54.84, Yuro 194,000 na dola za Marekani milioni 354.45. Malipo

yalicheleweshwa kwa siku kati ya siku **7** hadi **579**. Hii ilitokana na kuchelewa kwa utoaji wa fedha kutoka serikalini, pamoja na changamoto za kifedha ndani ya mashirika hayo. Hii ilikiuka vifungu vya mikataba vinavyotaka malipo yafanywe ndani ya siku 28. Orodha ya mashirika hayo yameainishwa katika **Jedwali Na. 27**.

**Jedwali Na. 27: Orodha ya mashirika ya umma yaliyochelewesha Malipo**

| Na. | Jina la Shirika | Idadi ya mika taba | Kiasi Sh. '000 | Muda uliochelewa (Siku) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha | 1 | 16,418,000 | 270 hadi 365 |
| 2. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara | 3 | 8,955,121 | 25 hadi 349 |
| 3. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | 1 | 8,833,532 | 180 hadi 450 |
| 4. | Bohari Kuu ya Dawa | 46 | 8,376,466 | 176 hadi 488 |
| 5. | Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro | 1 | 4,719,872 | 49 hadi 140 |
| 6. | Mamlaka ya Bandari Tanzania | 1 | 2,916,551 | 185 |
| 7. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe | 5 | 2,660,177 | 273 hadi 579 |
| 8. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga | 2 | 819,770 | 60 |
| 9. | Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini | 1 | 573,052 | 114 |
| 10. | Kampuni ya Ranchi za Taifa | 1 | 245,340 | 197 |
| 11. | Chuo cha Ufundi Arusha | 3 | 192,448 | 44 hadi 63 |
| 12. | Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam | 1 | 131,933 | 365 |
| | Jumla | | 54,842,262 | |
| **Na.** | Jina la Shirika | **Idadi ya Mika taba** | **Kiasi (Yuro)** | Muda uliochelewa (Siku) |
| | Mamlaka ya Bandari Tanzania | 1 | 194,000 | 311 |
| **Na.** | Jina la Shirika | **Idadi ya Mika taba** | **Kiasi ( Dola za Marekani)** | Muda uliochelewa (Siku) |
| 13 | Reli ya Kisasa | 5 | 354,459,151 | 7 hadi 310 |

**Chanzo:** *Mafaili ya ununuzi ya mashirika ya umma ya mwaka wa fedha 2023/24*

Kushindwa kuwalipa wakandarasi na wazabuni kwa wakati, husababisha riba inayoongeza gharama za miradi, hivyo kuchelewesha kukamilika kwa mikataba. Kwa mfano, Shirika la Umeme Tanzania limetozwa riba ya shilingi bilioni 147.12, wakati Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam limelimbikiza riba ya shilingi bilioni 2.74. Hali hii inadhoofisha uaminifu na sifa ya shirika la umma husika na Serikali.

**Ninapendekeza (a) Mashirika ya umma yahakikishe malipo yanafanyika kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya mkataba ili kuepuka gharama za ziada, na (b) Kwa madai yanayohitaji ufadhili**

**wa Serikali, fedha zitolewe kwa haraka kwa mashirika ya umma husika.**

## 10.9 Ununuzi Uliofanywa Nje ya Mfumo wa NeST wenye Thamani ya shilingi bilioni 7.66

Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ilianzisha Mfumo wa Kitaifa wa Ununuzi wa Kielektroniki wa Tanzania (NeST) kwa ajili ya mchakato wa ununuzi. Serikali kupitia Waraka Na. PST/GEN/2023/01/67 wa tarehe 01 Oktoba 2023, uliotolewa na Katibu Mkuu - Hazina, iliagiza mashirika yote ya ununuzi nchini (Tanzania Bara) kuanza kutumia mfumo wa NeST kwa ununuzi, kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1)(k) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410.

Mapitio yangu yalionesha kuwa mashirika ya umma 18 kati ya 217 yalifanya ununuzi wenye thamani ya shilingi bilioni 7.66 nje ya mfumo wa NeST, kama ilivyooneshwa katika **Jedwali Na. 28**.

**Jedwali Na. 28: Mashirika yaliyofanya ununuzi nje ya mfumo**

| Na. | Jina la Shirika | Idadi ya Mikataba | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|---|---|
| 1. | Kiwanda cha Dawa Keko | 6 | 1,800,059 |
| 2. | Chuo cha Uhasibu Arusha | 1 | 863,760 |
| 3. | Bodi ya Korosho Tanzania | 18 | 838,048 |
| 4. | Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari | 1 | 626,402 |
| 5. | Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania | 10 | 602,405 |
| 6. | Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania | 27 | 528,417 |
| 7. | Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 1 | 499,051 |
| 8. | Kituo cha Uwekezaji Tanzania | 1 | 434,272 |
| 9. | Taasisi ya Mifupa Muhimbili | 1 | 395,000 |
| 10. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida | 1 | 226,731 |
| 11. | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira | 7 | 174,985 |
| 12. | Taasisi ya Taifa ya Utafiti Wa Dawa | 1 | 153,018 |
| 13. | Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila | 4 | 149,699 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **14.** | Kampuni ya Sisalana Tanzania | 10 | 96,991 |
| **15.** | Tasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania | 37 | 87,105 |
| **16.** | Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania | 9 | 74,773 |
| **17.** | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi | 1 | 71,685 |
| **18.** | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanga | 1 | 39,505 |
| | Jumla | | 7,661,906 |

**Chanzo:** *Mafaili ya ununuzi ya mashirika ya umma, 2023/24*

Aidha, katika Taasisi ya Mipango ya Maendeleo ya Vijijini, Chuo cha Ufundi Arusha, Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Arusha, Shirika la Umeme Tanzania na Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro. Mashirika haya yalipata changamoto kama vile: Mkuu wa Usimamizi wa Ununuzi kushindwa kuwakabidhi ripoti ya tathmini kwa wasaidizi, upekuzi wa mikataba kufanywa nje ya mfumo, kushindwa kupata dhamana za utendaji zaidi ya kupata tamko; Pia, moduli nyingine, kama vile mchakato wa majadiliano, idhini za bodi ya zabuni, na uhariri wa mikataba kutofanya kazi. Ununuzi huu uliofanyika nje ya mfumo wa NeST unazuia uwazi na udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali.

**Ninapendekeza (a) Mashirika ya umma yahakikishe yanafuata kikamilifu matakwa ya kutumia NeST kama ilivyoainishwa na sheria; (b) Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ifanye ufuatiliaji ili kuimarisha uzingatiaji wa sheria; na (c) Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ipitie mfumo huo, na kurekebisha mapungufu yake.**

## 10.10 Ununuzi Uliofanywa kwa Njia za Ununuzi Zisizothibitishwa wenye Thamani ya shilingi bilioni 11.31

Nilibaini mashirika ya umma saba yaliyobadilisha njia za ununuzi kwa mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 10.28, ambayo hayakufuata mpango wa ununuzi wa mwaka. Hii inakiuka Kanuni za Ununuzi wa Umma na kupunguza ushindani, kwani njia kama vile ununuzi kwa kutumia mzabuni mmoja, njia zenye vikwazo, na ununuzi wa kitaifa zilitumika. Mbinu hizi zinakosa ushindani na huongeza hatari ya bei kupanda na kupunguza thamani ya fedha.

Pia, hakukuwa na uthibitisho uliotolewa kwa mabadiliko haya ya njia za ununuzi, na hivyo kuzuia uwezekano wa kuthibitisha mantiki ya kubadili. Aidha, mabadiliko haya hayakuidhinishwa, kwani yalikwepa udhibiti wa bodi ya zabuni. **Jedwali Na. 29** linatoa orodha ya

mashirika yaliyobadilisha mbinu za ununuzi bila sababu za uthibitisho.

**Jedwali Na. 29: Orodha ya mashirika yaliyotumia mbinu za ununuzi zisizothibitishwa**

| Na. | Jina la Taasisi | Idadi ya Mikataba | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|---|---|
| 1. | Shirika la Nyumba la Taifa | 4 | 6,501,941 |
| 2. | Chuo cha Uhasibu Arusha | 3 | 2,612,520 |
| 3. | Kituo cha Uwekezaji Tanzania | 1 | 499,724 |
| 4. | Shirika la Umeme Tanzania | 1 | 297,747 |
| 5. | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 2 | 183,420 |
| 6. | Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila | 1 | 151,342 |
| 7. | Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania | 1 | 31,860 |
| | Jumla | 13 | 10,278,554 |

**Chanzo:** *Mafaili ya ununuzi ya mashirika ya umma, 2023/24*

Aidha, katika Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko nilibaini shughuli za ununuzi zinazohusiana na bidhaa, ushauri na ujenzi zenye thamani ya shilingi bilioni 1.04 zilifanyika bila idhini kutoka kwa bodi ya zabuni. Hali hii ilisababishwa na kutokuwepo kwa bodi ya zabuni katika shirika hilo, jambo ambalo linahatarisha uwazi katika ununuzi.

**Ninapendekeza mashirika ya umma yahakikishe ununuzi unafanyika kwa njia ya ushindani ili kufikia thamani ya fedha. Ikiwa mabadiliko ya mbinu za ununuzi yanahitajika, sababu za kuchagua mbinu fulani lazima zielezwe wazi na ziidhinishwe na Bodi ya Zabuni kabla ya utekelezaji.**

## 10.11 Zabubi Walizopewa Wabia bila Kufanyiwa Tathmini ya Kutosha shilingi bilioni 14.83

Mapitio ya mchakato wa ununuzi katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa yalionesha kuwa, mnamo tarehe 16 Mei 2024, Chuo kilitoa mkataba wa kazi za ujenzi kwa ubia kwa ajili ya ujenzi wa majengo manne katika maeneo mawili, yenye thamani ya shilingi bilioni 14.83. Baada ya kupitia ripoti ya tathmini, nilibaini kuwa tathmini hiyo ilifanywa kwa kulinganisha ubia huo na wazabuni wengine watano. Hata hivyo, ripoti hiyo haikutoa maelezo yoyote

kuhusu uwezo wa wanachama wa ubia, na hakukuwa na tathmini ya kipekee ya uwezo wa kila mwanachama wa ubia.

Hii inaleta wasiwasi kuhusu sifa na uzoefu wa ubia huo, kwani hakuna tathmini za kila mwanachama wa ubia iliyofanywa kabla ya kukamilisha utoaji wa mkataba. Hii inakiuka Kanuni ya 9(10)(11) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, 2013, ambayo inataka wanachama wa ubia na ubia kwa ujumla kutathminiwa kila mmoja kwa mujibu wa uzoefu wao na utendaji waliokwisha fanya zamani. Ukosefu huu wa tathmini ya kina unazuia uwazi, haki katika ushindani, na unaweza kusababisha changamoto wakati wa utekelezaji.

**Ninapendekeza kuwa katika siku zijazo, tathmini za baada ya kufuzu zifanyike ili kuthibitisha uzoefu wa mkandarasi, uwezo wa kifedha wa kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mikataba, na uangalizi wa karibu utolewe wakati wote wa utekelezaji wa mradi.**

## 10.12 Kutoanzishwa kwa Kanzidata ya Viwango vya Bei ili Kudhibiti Bei katika Ununuzi wa Umma

Mamlaka za Udhibiti mara nyingi huweka viwango vya bei ili kuhakikisha kuna bei za haki katika sekta mbalimbali. Kanzidata za viwango vya bei zinawawezesha mamlaka za udhibiti kufuatilia na kutekeleza viwango hivi, kusaidia kupunguza tabia za kuhodhi soko au bei na kuwalinda watumiaji dhidi ya bei zilizopandishwa. Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ina jukumu la kuanzisha, kudumisha, na kusimamia kuhifadhi kazidata za viwango vya bei kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu cha 9 (1)(o) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410. Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma haijaanzisha kanzidata ya kuweka viwango vya bei kwa ajili ya matumizi ya mashirika ya umma wakati wa ununuzi wa huduma za ujenzi, bidhaa, na huduma zingine, kama inavyotakiwa. Kwa mujibu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, sababu kuu zinazokwamisha kuanzishwa kwa kanzidata hii ni ukosefu wa rasilimali fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya utafiti wa bei za soko, jambo hili lina hatarisha kupanda kwa bei pale ambapo nguvu za soko pekee zinapotumika kuamua bei.

**Ninapendekeza (a) Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma itoe kipaumbele kuanzishwa kwa kanzidata ya bei kwa kutenga bajeti ya kutosha ili kukidhi mahitaji haya; na (b) Serikali iingilie kati katika mchakato huu ili kuhakikisha kuwa kanzidata ya kuweka viwango vya bei inaanzishwa kwa wakati.**

## 10.13 Ugawaji wa Vifaa vya Ujenzi Bila Utaratibu Sahihi Katika Eneo la Ujenzi vyenye Thamani ya shilingi bilioni 2.16 katika Chuo cha Uhasibu Arusha

Katika Chuo cha Uhasibu Arusha, nilibaini vifaa vyenye thamani ya shilingi bilioni 2.16 vilitolewa bila utaratibu kwa ajili ya ujenzi. Nyaraka za utoaji hazikuwa na maelezo muhimu, ikiwa ni pamoja na majina na saini za wafanyakazi wanaoomba na kupokea vifaa kwenye eneo la ujenzi. Ingawa saini ya mtunza stoo ilikuwepo, ikionesha kuwa vifaa vimetolewa, hapakuwa na nyaraka zinazothibitisha kupokelewa au kufafanua vifaa vilipelekwa wapi. Zaidi ya hayo, nyaraka hazikujumuisha maelezo muhimu, kama vile tarehe, eneo, au sehemu mahususi ya jengo ambapo vifaa vilitumika. Tatizo hili lilitokana na ukosefu wa ufuatiliaji na usimamizi wa taratibu za kudhibiti hatua na matumizi ya vifaa vya ujenzi, kama ilivyoainishwa na Kifungu cha 33.5 cha Mwongozo wa ujenzi kwa kutumia rasilimali za ndani wa mwaka 2020.

Ukosefu wa nyaraka za kuthibitisha utoaji wa vifaa unaibua wasiwasi kuhusu usahihi wa udhibiti na kuna hatari ya udanganyifu.

**Ninapendekeza Chuo cha Uhasibu Arusha kihakikishe (a) vifaa vyote vinaandikwa kwa mujibu wa taratibu za utoaji wa vifaa, na (b) kichunguze matumizi ya vifaa ili kufuatilia vifaa vilivyotolewa na kutumika kwenye eneo la ujenzi, na kuboresha uwajibikaji.**

## 10.14 Manunuzi zaidi ya Bajeti bila kuidhinishwa shilingi bilioni 6.33

Katika tathmini yangu ya ununuzi katika mashirika ya umma manne, nilibaini kuwa thamani ya mikataba ilizidi kiasi kilichoidhinishwa katika Mpango wa Mwaka wa Ununuzi kwa shilingi bilioni 6.33. Kinyume na Kanuni ya 69 (3)(7) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013, ambayo inataka makadirio sahihi ya mahitaji ya bidhaa, huduma na ujenzi. Mchakato wa bajeti na makadirio haukuzingatia mabadiliko ya bei za soko na mabadiliko ya viwango vya kubadilisha dola ya Marekani. Zaidi ya hayo, kulikuwa na kutokufuata udhibiti wa bajeti, kwani ununuzi haukuidhinishwa na Bodi. Maelezo yanapatikana katika **Jedwali Na. 30.**

**Jedwali Na. 30: Mashirika yaliyonunua zaidi ya bajeti**

| S/N | Jina la Shirika | Idadi ya Mikataba | Gharama za Bajeti (Sh.'000) | Gharama za Mkataba (Sh.'000) | Gharama Zilizozidi (Sh. '000) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kampuni ya STAMIGOLD | 2 | 7,969,946 | 14,086,774 | 6,116,828 |
| 2 | Shirika la Umeme Tanzania | 1 | 100,000 | 297,747 | 197,747 |
| 3 | Bodi ya Tumbaku Tanzania | 1 | 145,450 | 159,214 | 13,764 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 1 | 88,845 | 100,268, | 11,423 |
| | Jumla | 5 | | | 6,339,762 |

**Chanzo:** *Mafaili ya ununuzi ya mashirika ya umma, 2023/24*

Kuzidi kwa bajeti ya ununuzi kunaweza kuibua shaka kuhusu ufanisi wa michakato ya bajeti, mipango, na ufuatiliaji, hivyo kuleta maswali ya uwajibikaji na uwazi. Pia, rasilimali zinaweza kuhamishwa kutoka kwenye shughuli zingine zilizopangwa, na kusababisha ucheleweshaji au kufutwa kwa vipaumbele vingine.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika, kuhakikisha ununuzi wote unazingatia Mpango wa Mwaka wa Ununuzi uliothibitishwa, ukiakisi bei halisi. Hii itasaidia kuepuka matumizi yasiyopangwa na kuongeza ufanisi wa kufikia malengo ya ununuzi.**

### 10.15 Udhaifu katika Maandalizi na Usimamizi wa Mkataba wa Mradi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere Uliosababisha Madai Kutokana na Marekebisho ya Bei shilingi trilioni 1.14

Katika mwaka 2023/24, nilibaini Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere ulikuwa na maombi ya malipo Na. 59 kwa kazi iliyofanywa hadi tarehe 30 Juni 2024, ambapo mkandarasi alidai marekebisho ya bei kuhusiana na gharama za wafanyakazi na vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya shilingi trilioni 1.14. Mapitio yangu ya utekelezaji wa mkataba kwa kuzingatia namna ya kushughulikia marekebisho ya bei kwa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere yalionesha kuwa masharti yanayohusika na marekebisho ya bei hayakuwa yamejumuishwa kwenye mkataba. Kutokana na hilo, wakati wa mgogoro wa marekebisho ya bei, Bodi ya Utatuzi wa Migogoro ilitoa uamuzi unaomuunga mkono mkandarasi. Hivyo, Bodi iliruhusu marekebisho ya bei kutokana na ukosefu wa masharti maalumu katika mkataba yanayohusu marekebisho ya bei katika tarehe ya kukamilika kwa mradi ilipozidi tarehe ya awali ya kukamilika.

Aidha, nilibaini Shirika la Umeme Tanzania lilitoa nyongeza ya muda kwa misingi ya huruma (ex-gratia) bila kuzingatia athari za marekebisho ya bei. Mkataba ulianza tarehe 15 Desemba 2018, na mradi ulitarajiwa kukamilika tarehe 14 Juni 2022, na mkandarasi hakuwa na haki ya kupewa nyongeza ya muda kulingana na masharti ya mkataba. Hata hivyo, kama hatua ya kuokoa mradi na kuepuka kuchelewa kukamilika, Shirika la Umeme Tanzania lilitoa nyongeza mara mbili ya muda kwa misingi ya huruma (ex-gratia) ya miezi 12. Hata hivyo, Shirika la Umeme Tanzania halikuzingatia ipasavyo athari za kifedha za marekebisho ya bei kwa mradi, na kusababisha Shirika la Umeme Tanzania kubeba gharama za ziada kufidia kushindwa kwa mkandarasi kufikia muda wa mwisho wa kimkataba.

Hii imetokana na maandalizi duni ya zabuni na nyaraka za mkataba, ambayo yalisababisha kushindwa kujumuisha masharti yanayohusika

na marekebisho ya bei, na hivyo kusababisha ongezeko kubwa la gharama za mradi ambazo zimeongezeka kwa Shirika la Umeme Tanzania na Serikali kwa ujumla.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania lihakikishe maandalizi ya kina na mapitio ya zabuni na nyaraka za mkataba, liimarishe majadiliano kwenye maeneo yenye hatari kubwa katika miradi changamano, na lishirikishe washauri wa nje wenye uzoefu wakati wa hatua muhimu au migogoro kwa usimamizi bora wa mkataba.**

## 10.16 Kugawanya Viwango vya Ununuzi ili kukwepa njia Sahihi ya Ununuzi wenye Thamani ya shilingi bilioni 1.61

Sheria za Ununuzi wa Umma zinakataza kugawanya ununuzi kwa madhumuni ya kukwepa kutumia njia sahihi za ununuzi, isipokuwa kugawanya huko kukiwa kunafanyika kwa lengo la kukuza ushiriki mpana wa washauri wa ndani, wasambazaji, au wakandarasi, kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 49 (1) (c) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410. Hata hivyo, nilibaini kuwa mashirika ya umma matano yalikuwa yamegawanya ununuzi wao, wenye jumla ya shilingi bilioni 1.61 katika sehemu ndogo ndogo ili kuepuka taratibu sahihi za ununuzi.

Hii inapunguza ushindani, haki na uwazi, na kusababisha kutokuwa na ufanisi na kushindwa kupata thamani bora ya fedha kutokana na ununuzi uliogawanywa, ambao unaweza kusababisha gharama za juu. Maelezo ya mashirika husika yanapatikana katika **Jedwali Na. 31.**

**Jedwali Na. 31: Orodha ya mashirika yaliyogawanya ununuzi**

| Na. | Jina la Shirika | Idadi ya Mikataba | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Bandari Tanzania | 19 | 949,830 |
| 2. | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima | 2 | 340,000 |
| 3. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida | 34 | 226,730 |
| 4. | Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari | 11 | 60,526 |
| 5. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | 9 | 42,621 |
| | Jumla | 75 | 1,619,707 |

**Chanzo:** *Mafaili ya ununuzi ya mashirika ya umma, 2023/24*

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yahakikishe uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na kanuni zake kwa kufanya ununuzi kwa mujibu wa viwango vya fedha na njia zinazofaa, na kuepuka kugawanya ununuzi isipokuwa kama ni kwa ajili ya kukuza ushiriki mpana wa wasambazaji, wakandarasi, au washauri wa ndani.**

## 10.17 Kubadilisha Mawanda ya Mkataba Baada ya Kusainiwa kwa Mikataba na kusababisha Gharama ya Ziada ya shilingi bilioni 1.79

Nilibaini Shirika la Umeme Tanzania lilikuwa na mkataba wa usambazaji, ufungaji, upimaji na kukabidhi kituo cha umeme cha kilovoti 220/132/33, 2x120MVA huko Ununio- Sehemu ya 1, wenye thamani ya dola za Marekani milioni 3.92 na shilingi bilioni 5.09 (ikijumuisha VAT) sawa na jumla ya shilingi bilioni 14.30, ulibadilishwa kufuatia mabadiliko ya mawanda. Mnamo tarehe 9 Oktoba 2023, idara ya mtumiaji iliomba mabadiliko ya mawanda na muundo katika mkataba. Ombi hili lilitokea miezi nane baada ya utekelezaji wa mradi. Wigo wa awali, ambao ulijumuisha mzunguko mmoja wa 220kv kutoka Kunduchi hadi Ununio (4.3km), ulibadilishwa kuwa mizunguko miwili ya kilovoti 220. Mzunguko mmoja utaingiza kituo cha Ununio kutoka Ubungo, na mzunguko mwingine utaingiza kilovoti 132kuelekea Rasi-Kilomoni kutoka kituo cha Kunduchi. Hii ilisababisha Marekebisho Na. 2, ambayo yalibadilisha bei ya mkataba kuwa dola za Marekani milioni 4.79 na shilingi bilioni 4.85, na kufanya jumla ya gharama kuwa shilingi bilioni 16.09. Hii ni sawa na gharama za ziada za shilingi bilioni 1.79 ikilinganishwa na bei ya awali ya shilingi bilioni 14.30.

Mabadiliko haya yalitokana na kushindwa kwa idara ya mtumiaji kufanya tathmini ya mahitaji kabla ya kuanzisha mchakato wa ununuzi, na ukosefu wa ushindani ulileta hatari ya kutofikiwa kwa thamani bora ya fedha.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Umeme Tanzania lihakikishe kuwa tathmini ya kina na utafiti wa upembuzi yakinifu unafanywa na idara ya mtumiaji kabla ya kuanzisha zabuni zijazo. Hii itasaidia kuhakikisha ushindani na kusaidia kufikia thamani ya fedha.**

## 10.18 Mkataba Uliosainiwa Bila Kuzingatia Ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Afisa Sheria wa Shirika Kuhusu Kufanya Uhakiki wa Kina Kiasi cha Dola za Marekani milioni 1.23, Yuro milioni 4.20 na shilingi bilioni 58.03

Katika ukaguzi na kutathmini ya uzingatiaji wa taratibu za uhakiki wa mikataba, nilibaini Shirika la Umeme Tanzania lilikuwa na mikataba minne yenye thamani ya shilingi bilioni 56.99 na dola za Marekani milioni 1.23, wakati Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ilikuwa na mkataba wenye thamani ya Yuro milioni 4.20.

Katika mashirika yote mawili, Mwanasheria Mkuu aliombwa ushauri wa kisheria. Mwanasheria Mkuu alishauri Shirika la Umeme Tanzania kufanya tathmini za kufuzu baada ya mchakato wa ununuzi ili kutathmini umahiri na uwezo wao wa kukamilisha mkataba kwa wakati na kwa ufanisi. Hata hivyo, nilibaini kuwa uongozi haukufanya uhakiki wa kina, ukitaja vikwazo vya bajeti na kutegemea tu utendaji wa zamani wa wasambazaji. Katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, ushauri wa Mwanasheria Mkuu ulikuwa ni kutathmini kama shirika hilo lilikuwa katika hali nzuri, kwa mujibu wa fedha, kisheria, kiutendaji, na hatari za kiutendaji na sifa zinazohusiana na mkataba wa ushauri. Hata hivyo, ushauri huu haukuzingatiwa. Ninaamini kutegemea tu utendaji wa zamani wa wazabuni haitoshi, kwani uwezo na umahiri wa kampuni unaweza kubadilika, hasa ukizingatia zabuni za miaka miwili iliyopita, ambazo zinaweza zisidhihirishe uwezo wao wa sasa.

Aidha, nilibaini Shirika la Reli Tanzania lilikuwa na mikataba miwili yenye thamani ya shilingi milioni 257. Tarehe 06 Juni 2024 rasimu za mikataba hiyo zilitumwa kwa ajili ya kupata ushauri wa kisheria. Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria alishauri kubadilishwa kwa tarehe ya uwasilishaji wa bidhaa iliyopendekezwa ya tarehe 1 Julai 2024, haikuwa na uhalisia na ilihitaji kurekebishwa. Licha ya ushauri huu, mikataba ilisainiwa bila kujumuisha maoni ya kisheria. Hata hivyo, nilibaini uwasilishwaji wa bidhaa ulifanyika tarehe 20 Septemba 2024, pia uwasilishaji mwingine wa Mashine ya Thermo Printer na Mashine ya Kukusanya Mapato ulifanyika tarehe 30 Septemba 2024. Hivyo, uwasilishaji ulichelewa kinyume na muda uliopangwa.

Katika Shirika la Nyumba la Taifa, mkoa wa Dodoma, mikataba yenye thamani ya shilingi milioni 788 ilisainiwa bila uhakiki wa kutosha, kinyume na kanuni. Hii inatokana na udhaifu wa udhibiti wa ndani katika mchakato wa zabuni. Hata hivyo, idadi ya mashirika ya umma yanayoshindwa kufanya uhakiki imepungua: mwaka 2021/22 mashirika nane hayakufanya uhakiki, mwaka 2022/23 yalikuwa mashirika manne, na mwaka 2023/24 ni shirika moja tu.

Kusaini mikataba bila kutathmini uwezo wa wasambazaji au wakandarasi kunaweza kuathiri utekelezaji wa mradi na uwasilishaji wa vifaa. Pia, kushindwa kufanya uhakiki na Mwanasheria Mkuu au maafisa wa kisheria wa mashirika kunaweza kusababisha masharti yasiyofaa, na kuweka mashirika katika hatari za kisheria.

**Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma husika yazingatie mahitaji ya kisheria na ushauri wa kitaalamu kwa kuhakikisha uzingatiaji wa michakato ya uhakiki wa kina. Hii itapunguza hatari na kuboresha utekelezaji wa mikataba kwa mafanikio.**

## 10.19 Tathmini ya Zabuni iliyo Kinyume na Sheria Iliyopendekezwa na Bodi ya Zabuni dola za Marekani milioni 13.02 na shilingi bilioni 3.68

Katika ukaguzi wangu wa mchakato wa ununuzi katika Shirika la Umeme Tanzania kwa zabuni ya usambazaji, ufungaji, upimaji, na kukabidhi kituo cha umeme cha kilovoti 220/132/33, na megavoti-Ampia 2x120 huko Ununio – Sehemu ya II, nilibaini matatizo katika tathmini ya zabuni. Tathmini ilifanyika mara tatu na timu mbili tofauti, na ukiukaji wa taratibu za ununuzi ulijitokeza. Mzabuni aliyeshindwa kutoa mwitikio alileta nyaraka nje ya TANePS mnamo tarehe 23 Mei 2023, baada ya tarehe ya mwisho, na alijumuisha dola za Marekani 568,144.11, jambo ambalo lilikiuka Kifungu cha 8 na 9 cha tangazo la mwaliko wa zabuni. Vifungu hivi vinataka zabuni ambazo hazikupokelewa kupitia TANePS zisikubaliwe kwa tathmini, bila kujali hali yoyote.

Bodi ya zabuni iliathiri mapendekezo ya kamati ya tathmini kwa kuelekeza kuteuliwa kwa kamati maalumu wakati wa kikao chake mnamo tarehe 29 Mei 2023, kinyume na Kifungu cha 40(2) cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2022, ambacho kinataka mapendekezo ya Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi yazingatiwe.

Mkataba ulitolewa kwa mkandarasi licha ya upungufu wa kiufundi ulioonekana katika tathmini. Zabuni ya mkandarasi ya tarehe 22 Novemba 2022 ilionesha bei ya dola za Marekani milioni 12.45 na shilingi bilioni 2.51, bila gharama za transfoma na digitali. Hata hivyo, ripoti ya tathmini ya tarehe 04 Agosti 2023 ilipendekeza tuzo kwa mkandarasi chini ya masharti ya majadiliano, ingawa upungufu wa kiufundi ulizingatiwa kuwa mdogo na mkandarasi alionekana kuwa na mwitikio, kinyume na kifungu cha 28.2 cha nyaraka za zabuni, kinachotaka zabuni inayopita kikamilifu iwe inakubaliana na masharti, vigezo, na vipimo vyote vya nyaraka za zabuni, bila kupotoka kwa viwango, kuacha au kuweka masharti. Uposhi wa viwango ni ule ambao, ukirekebishwa, unaweza kuathiri kwa njia isiyo ya haki nafasi ya ushindani ya wazabuni wengine wanaowasilisha zabuni.

Ukaguzi wangu katika Benki ya Biashara ya Tanzania ulibaini kuwa zabuni nne zenye thamani ya shilingi bilioni 1.17 hazikutimiza vigezo vya kifedha, kiufundi na kibiashara. Hata hivyo, timu ya tathmini ilipendekeza 'kukubalika'. Hii inaweza kusababisha kutokuwajibika au upendeleo, na kukatisha tamaa wazabuni wenye sifa nzuri kushiriki zabuni zijazo.

Hatua zisizo za kisheria zilifanyika kwa sababu zabuni ilitathminiwa kwa msingi wa bei ya chini pekee, badala ya mwitikio kwa vigezo vya tathmini. Hii inaweza kusababisha mizozo ya mikataba na wazabuni wengine ambao walitendewa isivyo haki, na pia kuongeza

hatari ya udanganyifu, jambo linaloweza kusababisha hasara za kifedha kwa mashirika.

**Ninapendekeza (a) Shirika la Umeme Tanzania lifanye tathmini ya uadilifu, umahiri na muundo wa Bodi ya Zabuni ili kuimarisha udhibiti; na (b) Kwa mashirika ya umma husika, yaepuke ukiukwaji wa sheria na kanuni za ununuzi wakati wa mchakato wa tathmini ya zabuni kwa kuhakikisha masharti yaliyoainishwa yanazingatiwa ili kusaidia katika uchunguzi, tathmini, na kulinganisha zabuni.**

# Tathmini ya Utawala na Usimamizi wa Vihatarishi




# SURA YA KUMI NA MOJA

# TATHMINI YA UTAWALA NA USIMAMIZI WA VIHATARISHI

## 11.0 Utangulizi

Ili kuhakikisha mashirika ya umma yanafanya kazi kwa maslahi ya umma, Serikali imeanzisha muundo wa utawala na usimamizi unaosimamia shughuli za mashirika hayo na kuhakiksha yanatekeleza majukumu yake kuendana na malengo ya Serikali. Hii ni pamoja na kuanzisha vyombo vya usimamizi kama vile Bodi za Wakurugenzi pamoja na kuweka sheria, kanuni, na sera zenye lengo la kuchochea utawala bora, uwajibikaji, na kuweka mifumo madhubuti ya usimamizi wa vihatarishi.

Sura hii imeangazia changamoto zinazotokana na kutokuwa na utawala bora kwenye usimamizi wa vihatarishi ikiwemo kutokuwepo kwa Bodi za Wakurugenzi, kuwa na nyenzo duni za utendaji na kutofuata maelekezo ya Serikali yanayohusiana na utawala na usimamizi thabiti. Changamoto hizo zimefafanuliwa kwa kina kama ifuatavyo:-

## 11.1 Mashirika ya Umma Yasiyokuwa na Bodi ya Wakurugenzi

Nilibaini Serikali ilichukua hatua na kuteua Bodi ya Wakurugenzi katika mashirika ya umma saba kati ya mashirika nane ambayo hayakuwa na Bodi ya Wakurugenzi kama ilivyoripotiwa katika ripoti yangu ya mwaka 2022/23 ambapo Serikali haikufanya uteuzi katika Bodi ya Pareto Tanzania. Aidha, niligundua idadi ya mashirika ambayo hayakuwa na bodi ya wakurugenzi hadi kufikia mwezi wa Februari 2025 iliongezeka na kufika 36 ambapo mashirika hayo yamekuwa bila Bodi kwa kipindi cha mwezi mmoja hadi miezi 24. Maelezo zaidi yameoneshwa katika **Kielelezo Na III** na **Kiambatisho Na. X.**

**Kielelezo Na. III: Mwelekeo wa mashirika ya umma Yasiyo na Bodi ya Wakurugenzi**




**Chanzo:** *Taarifa za utumishi za mashirika husika kwa mwaka wa fedha 2023/24*

Idadi ya mashirika ya umma ambayo hayakuwa na Bodi za Wakurugenzi ilipungua kwa asilimia 38 kutoka mashirika 13 mwaka 2021/22 hadi mashirika 8 mwaka 2022/23, hali iliyoonesha kuimarika kwa mchakato wa teuzi za bodi za wakurugenzi. Hata hivyo, katika mwaka 2023/24, idadi ya mashirika yasiyokuwa na bodi za wakurugenzi iliongezeka kwa asilimia 350 hadi kufikia mashirika 36, ikionesha kuzorota kwa juhudi za awali za michakato ya teuzi za bodi za wakurugenzi kama ilivyooneshwa katika Kielelezo **Na.III**.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yashirikiane na Serikali kuhakikisha Bodi za Wakurugenzi zinateuliwa kwa wakati. Aidha, Serikali, kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina, iweke mfumo wa kufuatilia tarehe za kumalizika kwa uanachama wa bodi zote ili kuruhusu michakato ya teuzi mpya kufanyika miezi sita kabla ya tarehe ya kumalizika kwa uanachama wa wajumbe ya bodi hizo.**

## 11.2 Bodi za Wakurugenzi Kuendelea Kukabiliwa na Mapungufu Katika Kusimamia Utendaji wa Mashirika ya Umma

Katika mwaka 2022/23, nilibaini Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini pekee ndiyo kilichokuwa na wajumbe wa bodi bila mwenyekiti. Hata hivyo, katika kipindi cha mwaka 2023/24 idadi hiyo iliongezeka na kufikia mashirika matatu (Rejea **Kiambatisho Na. XI**). Aidha nilibaini mashirika ya umma saba yaliripotiwa kuwa na Mwenyekiti bila kuwa na Wajumbe wa Bodi, ambapo idadi hiyo

inawakilisha ongezeko la asilimia 133 ikilinganishwa na mashirika matatu yaliyoripotiwa mwaka 2023/24 (Rejea **Kiambatisho Na. XI**).

Wakati huohuo, nilibaini bodi za mashirika mawili yakiwemo Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania, na Shirika la Reli Tanzania hayakuwa na idadi sahihi ya Wajumbe wa Bodi wanaohitajika kwa mujibu wa muundo wa bodi uliyoidhinishwa ambapo kulikuwa na upungufu wa wajumbe wa bodi kuanzia mmoja hadi watatu.

Nilibaini hali hii ilisababishwa na wajumbe wa Bodi waliopo madarakani kuteuliwa ama kupangiwa majukumu mengine ya kiserikali, na kukosekana kwa utaratibu wa kuhakikisha wajumbe wa Bodi wapya wanateuliwa kwa wakati au kuteuliwa tena mara baada ya muda wa kuwa wajumbe wa bodi unapomalizika. Bila kuwa na Bodi ya Wakurugenzi inayofanya kazi kwa ufanisi, utendaji wa mashirika ya umma unaathiriwa na kusababisha hatari za kutokuwa na ustawi wa kifedha, na kupoteza imani kwa wadau.

**Ninapendekeza Mashirika ya umma kufanya kazi kwa karibu na Serikali ili kuhakikisha teuzi za wajumbe wa bodi zinafanyika kwa wakati mara tu mjumbe wa bodi atakapopangiwa majukumu mapya katika Serikali. Aidha Ofisi ya Msajili wa Hazina iweke mfumo wa kufuatilia muda wa uanachama wa wajumbe wa bodi na ichukue hatua za kuanza mchakato wa teuzi miezi sita kabla ya muda wa uanachama wa wajumbe wa bodi kumalizika.**

Aidha, nilibaini mashirika ya umma 12 yalipata changamoto katika kutekeleza majukumu yake, kama vile kukosekana kwa kamati za Bodi, Mkataba wa Bodi, pamoja na makubaliano ya mikataba ya utendaji katika Bodi hizo za Wakurugenzi na kusababisha changamoto kubwa katika uwajibikaji katika Mashirika ya umma (Rejea **Kiambatisho Na. XI).** Tatizo hili lilitokana na ukosefu wa ufahamu katika mashirika ya umma kuhusu hitaji la kusaini mikataba ya utendaji baina yake na Ofisi ya Msajili wa Hazina, kuundwa kwa Kamati ya Bodi pamoja kuwa na Mikataba ya Bodi.

Kukosekana kwa miongozo ya Serikali, kunaathiri ufanisi wa mashirika, Serikali kushindwa kutimiza malengo yake, kuongezeka kwa vihatarishi, kuzorota kwa ukwasi, na kupoteza imani ya wadau.

**Ninapendekeza Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma kuhakikisha nyenzo na miongozo ya Serikali zipo, kama vile**

**Mikataba ya Bodi, kuunda kamati za Bodi na pia kuhakikisha kuwa mikataba ya utendaji na uwajibikaji imesainiwa kwa wakati.**

## 11.3 Mashirika ya Umma Kushindwa Kutekeleza Miundo ya Mashirika Iliyoidhinishwa

Nilibaini Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania haikuwa imeanzisha idara pamoja na mfumo wa kusimamia bima ya afya kwa wote, kinyume na kifungu cha 7 cha Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Na.13 ya mwaka 2023. Pia nilibaini Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita haikuwa imeanzisha Kitengo cha huduma za kisheria, Kitengo cha TEHAMA pamoja na Kitengo cha Takwimu ambavyo vilitakiwa kuwepo kulingana na muundo wa mashirika.

Hali hiyo ilisababishwa na kasi ndogo katika utekelezaji wa maazimio ya kuanzisha kurugenzi pamoja na mfumo wa kusimamia Bima ya Afya kwa Wote. Vilevile nilibaini kuwepo kwa ucheleweshaji wa kutoa ajira katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita hali inayoleta changamoto katika kutekeleza muundo. Kushindwa kutekeleza kwa ukamilifu miundo, na mifumo iliyoidhinishwa kunadhoofisha usimamizi wa udhibiti, kuchelewesha utoaji wa huduma, na inaweza kusababisha kupungua kwa ufanisi.

**Ninapendekeza mashirika ya umma yahakikishe miundo na mifumo ya mashirika iliyoidhinishwa na mamlaka husika inatekelezwa kikamilifu; na mashirika yote yahakikishe yanaajiri watumishi wenye sifa ili kujaza idara na vitengo vyote vilivyo wazi.**

Pia, katika Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini, nilibaini uwepo wa idara tano ambazo hazikujumuishwa katika muundo ulioidhinishwa wa mwaka 2022, ambazo ni: Idara ya Maendeleo ya Vijijini na Upangaji wa Mikoa, Mafunzo ya Idadi ya Watu na Upangaji wa Mazingira, Mkuu wa Kampasi, Mkuu wa Masuala ya Kitaaluma na Mkuu wa Masuala ya Utawala – katika kituo cha kanda ya ziwa. Vile vile nilibaini Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ilianzisha kanda mpya za kiofisi ambapo kanda hizo hazikuwepo kwenye muundo ulioidhinishwa. Ofisi hizo mpya za kikanda zilizoanzishwa ni pamoja na Kanda ya Ziwa Tanganyika, Kanda ya Unguja, Kanda ya Pemba, Kanda ya Kusini, na Kanda ya Magharibi.

Hali hii ilisababishwa na mabadiliko katika mpangilio wa mashirika unaotaka kuongeza mawanda ya mashirika ambapo uliongeza umuhimu wa kuanzishwa kwa idara au kanda mpya kabla ya

kuboresha miundo ya shirika. Kushindwa kuingiza mabadiliko haya katika muundo kunaweza kusababisha uharibifu wa rasilimali, mkanganyiko katika utendaji, na upungufu wa ufanisi kutokana na kukosekana kwa njia za wazi za mawasiliano ndani ya shirika.

**Ninapendekeza kuwa menejimenti ishirikiane na Katibu Mkuu - Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuboresha na kupata kibali cha muundo wa mashirika uliorekebishwa, na ihakikisha mashirika yanakuwa na mpangilio sahihi wa muundo ili kuongeza ufanisi katika utendaji.**

## 11.4 Mashirika ya Umma Kutokuaandaa au Kutohuisha Mpango Mkakati na Mpango wa Biashara

Ili kuongeza utendaji, ufanisi na tija, Kifungu cha 113(i) cha Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24 kilielekeza maafisa masuuli kuhuisha Mpango Mkakati ya Shirika kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26). Ni muhimu kufuatilia utekelezaji wa mipango mkakati pamoja na mipango ya biashara katika kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

Nilibaini mashirika ya umma matatu ambayo ni Kampuni ya Ushauri Elekezi ya Uzalishaji Chuo cha Ufundi Arusha, Kampuni ya Gesi Tanzania, na Kiwanda cha Kuzalisha Mashine na Vipuli Kilimanjaro hayakuandaa mipango mkakati wa kuendesha mashirika hayo kwani yanategemea mpango mkakati wa shirika mama.

Wakati huohuo nilibaini Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela – Kasumulu, haikuwa imeandaa mwongozo wa kimkakati wa mpango wa biashara. Aidha, nilibaini Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Hifadhi za Taifa umepitwa na wakati, na Mpango Mkakati wa Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania (2013/14 – 2017/18) umepitwa na wakati kwa takribani miaka sita. Vilevile, Mpango Mkakati wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko uliisha muda wake mwaka 2022/23, na kusababisha bodi hiyo kufanya kazi kwa mwaka mzima wa 2023/24 bila muongozo wa kimkakati.

Kutokuwa na Mpango Mkakati au Mpango wa Biashara kulitokana na ukosefu wa fedha, kuchelewa kuwashirikisha wakandarasi washauri ambao wangefanya zoezi hilo, pamoja na uwepo wa usimamizi dhaifu hasa katika Kampuni ya Gesi Tanzania na Kiwanda cha Kuzalisha Mashine na Vipuli Kilimanjaro, ambapo mashirika haya

yalitegemea zaidi kampuni mama badala ya kujitegemea na kutengeneza Mipango Mkakati yao binafsi.

Kukosekana kwa mpango mkakati na mpango wa biashara kunasababisha mashirika kukosa maono na uratibu wa rasilimali, kudhoofisha ufuatiliaji na tathmini, na hatimaye kuzuia kufikia malengo yaliyokusudiwa ya shirika.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yaendelea kuandaa mpango mkakati wa mashirika na kuwasilisha mipango ya kimkakati na biashara kwa mamlaka husika ili iidhinishwe. Vilevile ninapendekeza yaongeze au yaanzishe utaratibu wa ufuatiliaji ili kuhakikisha mipango hii inatumika kama zana bora na mwongozo wa kuchochea fursa ya ukuaji ndani ya mashirika husika.**

## 11.5 Mashirika ya Umma Kushindwa Kutumia Mifumo ya TEHAMA ya Kielektroniki kwa Ufasaha

Kifungu cha 28 cha Sheria ya Serikali Mtandao, 2019 kinatoa mamlaka kwa mashirika ya umma kutumia teknolojia ya TEHAMA katika utoaji wa huduma, kutengamanisha mifumo ya utendaji ili kuongeza ufanisi, kupanga upya na kuboresha mtiririko wa shughuli za mashirika katika kutoa huduma, kuweka mifumo na utaratibu wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato huku mifumo hiyo ikitengamanishwa na mifumo ya malipo ya Serikali, iliyoidhinishwa. Kuongeza mifumo ya udhibiti wa ndani, hupunguza hatari za ubadhilifu, inaboresha ufanisi, kupunguza gharama, kuhakikisha uthabiti au ubora wa taarifa inayoingizwa kwenye mfumo, na kuimarisha misingi ya maamuzi na kukuza ushirikiano ambao huimarisha na kuboresha usimamizi na utoaji wa huduma bora kwa umma.

Nilibaini mashirika ya umma manne ambayo hayana mifumo ya TEHAMA ambayo ingewewezesha mashirika hayo kutekeleza majukumu ya msingi kwa ufanisi. Pia nilibaini mashirika ya umma 26 hayatumii mifumo ya TEHAMA kikamilifu na hayajatengamanisha mifumo yao na mifumo ya kiundeshaji ya kiserikali kama vile Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi (ERMS), Mfumo wa Malipo Serikalini (MUSE), Mfumo wa Bajeti wa Serikali (Planrep), Mfumo wa Kielektroniki wa Manunuzi wa Serikali (NeST) na Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (GePG). Mashirika haya yamekuwa na changamoto ya kutumia mifumo ya TEHAMA kutokana na sababu mbalimbali

ikiwemo ukosefu wa fedha, kutokuwa na wataalamu wa TEHAMA wa kutosha, mashirika kukosa mchanganuo mzuri wa taratibu zake za kiutendaji, pamoja na kukosekana kwa mkakati madhubuti wa matumizi ya TEHAMA (Rejea **Kiambatisho Na. XII**).

Kutokana na matumizi hafifu ya TEHAMA na kutotumia mifumo ya kielektroniki, utekelezaji wa majukumu ya shirika unatumia muda mrefu zaidi, ugumu na mzigo wa kazi unaongezeka, na kuleta hatari ya kutofautiana taarifa kati ya mifumo wa uendeshaji na mifumo wa uhasibu. Pia, kushindwa kwa mashirika kutumia wa Mfumo GePG kunapunguza uwazi katika ukusanyaji wa mapato, na kupunguza uwezo wa Serikali kupata taarifa halisi za makusanyo ya mapato yanayoripotiwa na mashirika husika.

**Ninapendekeza mashirika ya umma yaongeze kasi ya kuwekeza na kutumia mifumo ya kielektroniki ili kuwezesha na kuongeza uwazi, uwajibikaji, ufanisi, kupunguza gharama, na kufuata viwango vya kiteknolojia vya Serikali Mtandao .**

## 11.6 Mashirika ya Umma Yanayotumia Miongozo ya Utendaji Kazi Isiyojitosheleza

Nilibaini mashirika ya umma 39 kati ya 217 hayakuwa na miongozo ya utendaji kazi inayojitosheleza kuwezesha mashirika hayo kufanya kazi zao kwa ufanisi. Mashirika hayo yalikosa miongozo ya utendaji kazi ikiwemo mipango kazi ya kila mwaka, mifumo ya kisheria ya uanzishwaji na uendeshaji wa mashirika, miongozo ya uhasibu iliyohuishwa na inayoendana na wakati, sera, kanuni za kifedha na sera za usimamizi wa vihatarishi **(** Rejea **Kiambatisho Na. XIII).**

Hii ilisababishwa na mapitio na tathmini ya muda mrefu inayofanywa na menejimenti na mamlaka za kuidhinisha. Vivyo hivyo, ilibainika kuwepo kwa utegemezi ulipolitiliza wa kimiongozo wa kampuni tanzu kutoka kwa kampuni mama.

Kutokuwepo kwa miongozo ya utendaji kazi katika uendeshaji wa mashirika kunasababisha changamoto kubwa na kuathiri uwezo wa mashirika katika kufanya kazi kwa ufanisi, kwa uwiano na kwa mujibu wa viwango na kanuni zilizowekwa. Kwa mfano, tulibaini kuwa Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha hakikuwa na mkakati rasmi wa kimaandishi wa masoko. Hali inayoashiria kutokuwepo kwa mpango kamili wa kuongeza juhudi za kutangaza shughuli za kituo hicho ili kuwafikia walengwa au kutenga rasilimali

pesa kwa lengo la kuhakikisha shughuli za utangazaji zinafanyika, hali ambayo inaathiri ufanisi.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yahakikishe miongozo ya utendaji kazi inatayarishwa, kusahihishwa na kuidhinishwa na mamlaka husika ili kuboresha na kuongeza ufanisi wa shughuli zao.**

## 11.7 Utata katika Uendeshaji na Usimamizi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro

Nilibaini kuwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) kwa sasa unafanya kazi chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) badala ya kufanya kazi chini ya Kampuni ya Uendeshaji na Uendelezaji Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KADCO). Hii ni baada ya mkataba wa upangaji wa uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro chini ya Kampuni ya Uendeshaji na Uendelezaji Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KADCO) kuisha muda wake mnamo tarehe 09 Novemba 2023.

Mnamo tarehe 06 Novemba 2023, ikiwa ni siku tatu kabla ya muda wa mkataba kuisha, Wizara ya Uchukuzi iliandika barua ikielekeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kuchukua majukumu kamili ya kiutawala na kusimamia uendeshaji kwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro baada ya mkataba wa kukodisha uliosainiwa baina ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro na Kampuni ya Uendeshaji na Uendelezaji Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro kumalizika tarehe 09 Novemba 2023. Hata hivyo, tarehe 29 Desemba 2023, Wizara husika iliandika barua nyingine iliyofuta maelekezo ya awali, na kumuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Uendeshaji na Uendelezaji Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro kuendelea kutekeleza shughuli zake chini ya makubaliano yaliyopo (concession agreement) hadi pale itakapotolewa taarifa nyingine kutoka serikalini, ikibatilisha hatua ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania kuchukua madaraka.

Utata huu unatokana na mawasiliano duni baina ya mashirika haya, kutokuwepo kwa mpango wa mpito wa wazi, pamoja na mfumo wa kisheria usio wazi. Hali hii inaleta changamoto katika uwajibikaji, hatari za udhibiti, changamoto za kimkataba kutoka kwa wadau na hatari za kisheria kutokana na mkanganyiko wa masharti ya uendeshaji yasiyofafanuliwa vizuri.

**Ninapendekeza Wizara ya Uchukuzi ichanganue kwa ufasaha majukumu ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na Kampuni ya Uendeshaji na Uendelezaji Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KADCO) ili kupata suluhisho la kudumu.**

## 11.8 Kutokuwepo kwa Kanuni za Kusimamia Hifadhi za Bahari, Chakula na Lishe

Nilibaini kuwa Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari (MPRU) pamoja na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC) hazikuwa na kanuni muhimu zinazowezesha mashirika hayo kufanya usimamizi madhubuti katika sekta zao.

Kifungu cha 4(4)(b) cha Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu [Sura ya 146] kinatoa mamlaka kwa Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari (MPRU), kuandaa na kutekeleza kanuni za kusimamia na kulinda Hifadhi za Bahari.

Licha ya kuwepo kwa maeneo 18 ya hifadhi za majini yaliyohifadhiwa na kuwepo kwa mpango madhubuti wa kuanzisha maeneo mapya sita yaliyohitaji kuhifadhiwa katika maziwa makuu, hakuna mfumo na kanuni za udhibiti zilizoanzishwa ili kutekeleza jambo hilo. Vilevile nilibaini kuwa sheria ya hifadhi ya bahari na maeneo tengefu imepitwa na wakati, hivyo kutokushughulikia maeneo yanayohitaji usimamizi wa Mamlaka hiyo. Kushindwa kusimamia hili, kunazorotesha juhudi za uhifadhi na kusababisha hali ya kutokuwa na uhakika kuhusu athari za muda mrefu za kiikolojia.

Kwa mfano, katika Hifadhi ya Bahari ya mkoani Mtwara, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania limejenga bomba la mafuta ndani ya eneo lililohifadhiwa. Nilibaini kuwa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari kwa kuainisha madhara au kupinga shughuli zinazokinzana na maslahi ya maeneo ya hifadhi. Hii ilisababishwa na kutokuwa na kanuni za uendeshaji au mfumo wa kutoa taarifa kwa wadau husika juu ya masuala ya hifadhi za bahari na maeneo tengefu.

Vilevile , nilibaini kuwa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), iliyoanzishwa chini ya Sheria Na. 24 ya mwaka 1973, baadaye kurekebishwa na Sheria Na. 3 ya mwaka 1995, haijawahi kuwa na kanuni za uendeshaji ambazo zingesaidia taasisi hiyo katika utekelezaji wa majukumu yake. Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania inawajibika katika kuandaa sera, uratibu wa mpango wa lishe,

utafiti, na ufuatiliaji wa chakula na lishe kwa ujumla, ambapo majukumu haya yangefanywa kwa ufanisi kama kungekuwapo na kanuni. Pia nimebaini taasisi hii haikuwa na miongozo ya kusimamia na kudhibiti wahamasishaji wanaoshughulika na virutubisho na lishe kwa viwango bora na maelezo sahihi .

Pia, kutokuwepo kwa bodi ya wakurugenzi inayosimamia na kuratibu shughuli zote za Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania kumesababisha ongezeko la wahamasishaji wa tiba lishe na lishe ambao hawakuidhinishwa na mamlaka na kuanza kutoa miongozo ya lishe ya chakula jambo ambalo si jukumu lao bali ni jukumu la Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania. Watu hawa wanaweza kutoa taarifa ambazo siyo sahihi na kuathiri ubora wa lishe na chakula nchini.

Mapungufu haya ya udhibiti yanahusishwa na kuchelewa kuchukua hatua stahiki kutoka kwa wadau wakuu ikiwemo Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania, Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari na Wizara zinazohusika, pamoja na ukosefu wa Bodi ya Wakurugenzi ambao wangesaidia kusimamia jambo hili. Kutokuwepo kwa sheria na kanuni sahihi zilizoidhinishwa kunapunguza usimamizi, kudhoofisha mamlaka ya taasisi, na kuongeza hatari ya utoaji wa huduma usio na ufanisi.

**Ninapendekeza kuwa Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari na Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania kushirikiana na wizara zao ili kupitia na kurekebisha sheria zao na kuandaa kanuni za kusaidia utekelezaji wa majukumu yao, na bodi za wakurugenzi kwa mashirika yote mawili ziteuliwe ili kusaidia kutekeleza majukumu yao kikamilifu ya kiusimamizi na kuimarisha utekelezaji wa majukumu yao.**

# Usimamizi wa Rasilimali Watu



# SURA YA KUMI NA MBILI

# USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU

## 12.0 Utangulizi

Ufanisi katika usimamizi wa rasilimali watu ni muhimu kwa mashirika ya umma ili kuongeza tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya tasisi sambamba na kupunguza gharama za uendeshaji. Kazi muhimu za usimamizi wa rasilimali watu zinajumuisha kuajiri, kufanya uteuzi, kufanya tathimini ya utendaji wa watumishi, usimamizi na kuendeleza taaluma za watumishi, mpango wa kurithishana madaraka, kulipa fidia mbalimbali, na mahusiano baina ya wafanyakazi.

Katika ukaguzi nilibaini dosari katika usimamizi wa rasilimali watu, kama vile kukaimu nafasi za uteuzi kwa muda mrefu, dosari katika michakato ya kuajiri; kutotekelezwa kwa mifumo ya serikali ya kieletroniki katika usimamizi wa rasilimali watu ya Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Rasilimali Watu na Mfumo wa Taarifa za Utendaji wa Watumishi wa Umma; na kushindwa kuwasilisha michango na makato ya kisheria ya wafanyakazi kwenye mashirika husika. Sura hii inaelezea kasoro, dosari na changamoto za usimamizi wa rasilimali watu, sababu zake na mapendekezo ya kuboresha.

## 12.1 Ukusanyaji Hafifu wa Madeni ya Mikopo kwa Wafanyakazi wa Mashirika ya Umma shilingi bilioni 1.29

Katika ukaguzi nilibaini kuwa jumla ya shilingi milioni 105, zilizokopeshwa kwa watumishi walioacha kazi katika mashirika ya Umma matano, hazijarejeshwa, baada ya watumishi hao kuondoka katika mashirika hayo.

Vilevile, nilibaini urejeshwaji usioridhisha kwenye mikopo wa jumla ya shilingi bilioni 1.18 kwa wafanyakazi walioacha kazi katika mashirika ya umma manne ambapo urejeshwaji wa mikopo hiyo haukuzingatia mpango wa malipo uliokubalika hapo awali (Rejea **Jedwali Na. 32**)

### Jedwali Na. 32: Bakaa ya mikopo iliyotolewa kwa wafanyakazi walioacha kazi

| Na. | Jina la Shirika | Kiasi (Sh. '000) |
|---|---|---|
| Mashirika yenye mikopo isiyorejeshwa na wafanyakazi walioacha kazi. | | |
| 1. | Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania | 51,313 |
| 2 | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji | 18,116 |
| 3 | Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi | 15,997 |
| 4 | Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha | 11,307 |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila | 8,600 |
| **Jumla ndogo** | | **105,333** |
| **Urejeshwaji wa mikopo na wafanyakazi bila kuzingatia mpango wa malipo uliokubalika** | | |
| 6. | Shirika la Nyumba la Taifa | 841,818 |
| 7. | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi | 304,208 |
| 8. | Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila | 21,854 |
| 9. | Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania | 13,595 |
| **Jumla ndogo** | | **1,181,475** |
| **Jumla Kuu** | | **1,286,808** |

**Chanzo:** *Orodha ya mikopo ya wafanyakazi wa Mashirika ya umma 2023/24*

Mapungufu katika usimamizi wa mikopo iliyotolewa kwa wafanyakazi yalitokana na ukosefu wa dhamana ya kulinda mikopo, ukosefu wa ufuatiliaji wa ratiba ya marejesho ya malipo, na baadhi ya mikopo kutokuwa na ratiba rasmi ya kufanya malipo au marejesho. Hali hii inaweza kusababisha mikopo hii kutorejeshwa na wafanyakazi hao walioacha kazi na kusababisha hasara kwa mashirika ya umma.

**Ninapendekeza mashirika ya umma yachukue hatua stahiki za utekelezaji ikiwa ni pamoja na kuwa na mikataba mipya ya kutekeleza urejeshaji, na kuwa na ratiba rasmi ya malipo ili kurejesha mikopo hiyo kwa usahihi.**

## 12.2 Kutolipwa kwa Madeni na Malimbikizo ya Wafanyakazi yenye Jumla ya shilingi bilioni 12.64

Nilibaini hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, jumla ya mashirika ya umma 12 yalikuwa na jumla ya deni la shilingi bilioni 12.64 linalojumuisha malimbikizo ya madai ya wafanyakazi ambayo hayakulipwa. Aidha madai hayo hayakulipwa kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi miaka 11. Madai hayo yalikuwa ni stahiki za wafanyakazi hao ambapo zilikuwa kama sehemu ya malipo yao baada ya kutekeleza majukumu yao (Rejea **Jedwali Na. 33).**

**Jedwali Na. 33: Madai ya Wafanyakazi**

| Na. | Jina la Shirika | Kiasi (Sh. '000) |
|---|---|---|
| 1. | Chuo Kikuu Cha Kilimo Sokoine | 9,804,967 |
| 2. | Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania | 570,766 |
| 3. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | 521,077 |
| 4. | Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania | 533,342 |
| 5. | Shirika la Masoko ya Kariakoo | 402,939 |
| 6. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha | 201,786 |
| 7. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela-Kasumulu | 172,799 |
| 8. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega | 101,566 |
| 9. | Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka | 120,147 |
| 10. | Chuo cha Uhasibu Arusha | 173,582 |
| 11. | Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam | 31,641 |

| | | |
|---|---|---|
| 12. | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 7,340 |
| | **JUMLA** | **12,641,900** |

**Chanzo***: Orodha ya madai na madeni ya Mashirika ya umma ya mwaka 2023/24*

Malimbikizo na madai ya wafanyakazi yalisababishwa na ukosefu wa fedha katika mashirika hayo pamoja na kushindwa kuwa na mpango madhubuti wa malipo unaolenga kutoa kipaumbele kwa malipo ya madai na madeni hali inayoleta changamoto katika kulipa madai yanapofika wakati wake. Changamoto hii inaweza kushusha morali ya wafanyakazi, kuathiri hamasa yao na kuzorotesha utendaji wa wafanyakazi hao.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yahakikishe yanatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kulipa malimbikizo na madeni yote ya wafanyakazi kwa wakati.**

## 12.3 Usimamizi Usioridhisha wa Makato ya kisheria ya shilingi bilioni 11.89 katika Mashirika ya Umma

Kifungu cha 19(2) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma ya mwaka 2018 na Kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi Sura ya 50 kinataka michango ya wanachama kuwasilishwa kwa mfuko husika ndani ya mwezi mmoja baada ya kumalizika kwa mwezi ambao michango inapaswa kulipwa.

Hata hivyo, nilibaini mashirika ya umma 10 hayakuwa yamewasilisha makato ya kisheria ya wafanyakazi wake yenye jumla ya shilingi bilioni 11.89 hadi kufikia mwezi Juni 2024. Makato hayo yalicheleweshwa kwa kipindi kuaniza siku 30 hadi 1095 **(**Rejea **Jedwali Na. 34).**

Hii ilitokana na changamoto ya kifedha iliyoyakumba mashirika hayo pamoja na ukosefu wa mipango ya malipo inayotoa kipaumbele kwa malipo ya makato ya kisheria. Hali hii inaweza kuhatarisha upatikanaji wa mafao ya wafanyakazi pindi wanapo staafu. Vilevile, mashirika haya yanaweza kutozwa riba na adhabu kwa kutotekeleza masharti ya mifuko ya hifadhi ya jamii.

**Jedwali Na. 34: Makato ya kisheria ya wafanyakazi ambayo hayakuwasilishwa shilingi bilioni 11.89**

| Na. | jina la Shirika | Kiasi (Sh. '000) |
|---|---|---|
| **Mashirika ambayo hayakupeleka makato ya kisheria kwa wakati** | | |
| 1 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | 8,325,258 |
| 2 | Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibiolojia Tanzania | 1,313,697 |
| 3 | Shirika la Masoko ya Kariakoo | 867,071 |
| 4 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi | 470,077 |
| 5 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara | 292,797 |
| 6 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu | 114,056 |
| 7 | Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro | 168,205 |
| 8 | Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu | 194,924 |
| 9 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela - Kasumulu | 48,998 |
| 10 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega | 24,807 |
| | Jumla | 11,886,284 |

**Chanzo:** *Orodha ya madai na madeni ya Mashirika ya umma ya mwaka 2023/24*

Pia, nilibaini kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi kavu ilikuwa na wafanyakazi 72 amabao walikuwa wanafanya kazi kwa mikataba; hata hivyo, nilibaini michango ya kisheria ya shilingi milioni 194.92 haikukatwa kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi wala haikuwasilishwa na mwajiri kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Utumishi wa Umma. Tatizo hili lilitokana na ukosefu wa vifungu katika mikataba ya ajira vinavyohusu ulazima wa kuwasilisha michango hiyo ya kisheria kwa Mifuko wa Hifadhi ya Jamii.

**Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma husika yahakikishe (a) yanatenga fedha za kutosha ili kuwa na uhakika kuwa michango ya kisheria inapelekwa kwenye mamlaka husika kwa wakati, (b) mikataba ya ajira inawekwa vipengele vinavyoonesha ulazima wa michango hiyo ya kisheria kupelekwa kwenye mamlaka husika.**

## 12.4 Mashirika ya Umma Yanayoendeshwa Bila kuwa na Miongozo Iliyoidhinishwa na Katibu Mkuu- Utumishi

Kanuni za serikali zinahitaji mashirika ya umma kuwa na miongozo ya rasilimali watu iliyoidhinishwa na Katibu Mkuu (Utumishi) -Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikiwa ni pamoja na kanuni za wafanyakazi, mipango ya motisha, miundo ya shirika, na mipango wa kurithishana madaraka.

Ukaguzi wangu wa mwaka ulioishia 2022/23 ulibaini uwepo wa mashirika ya umma nane ambayo yalikuwa yanajiendesha bila kutumia miongozo ya Rasilimali watu iliyoidhinishwa na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Katika ukaguzi wangu wa mwaka huu nilibaini mashirika hayo yameongezeka na kufikia jumla ya mashirika 29. Mashirika hayo hayakuwa na miongozo inayojitosheleza ya uendeshaji rasilimali watu ikiwemo kuwa na miongozo na sera zilizopitwa na wakati, kutokuwa na mpango bora wa kurithisha madaraka, mpango wa kubakiza watumishi, pamoja na kuwa na ikama iliyoidhinishwa **(**Rejea **Kiambatisho Na. XIV).**

Mapungufu haya yanasababisha na kutokukubaliana baina ya wafanyakazi, hali inayoweza kuyaweka mashirika katika hatari ya migogoro na kuzuia uzalishaji na utendaji wa kazi.

**Ninapendekeza mashirika ya umma (a) Yahakikishe miongozo yote ya rasilimali watu kama vile mpango wa motisha, miundo ya shirika, na mipango ya urithishaji madaraka inaandaliwa na kuidhinishwa na Katibu Mkuu- Utumishi kabla ya utekelezaji. (b) Pia, mashirika ya umma yenye nyaraka zilizopitwa na wakati au zilizokosekana yahakikishe yanaharakisha mchakato wa kuziandaa na kuziwakilisha kwa ajili ya kupata idhini ili kuboresha usimamizi wa rasilimali watu, uhifadhi wa wafanyakazi na kuboresha ufanisi na uendeshaji.**

## 12.5 Wafanyakazi Walioajiriwa au Kukaimu Nafasi Bila Idhini ya Katibu Mkuu- Utumishi

Katika ukaguzi nilibaini kuwa mashirika ya umma matano yalitoa nafasi za ajira bila kuomba kibali kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Pia, nilibaini uwepo wa mashirika ya umma matano yaliyofanya uteuzi wa watumishi wake na kukaimu nafasi za usimamizi na uongozi bila kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Rejea **Jedwali Na. 35).**

**Jedwali Na. 35: Mashirika yaliyoajiri au Kuteua Wafanyakazi katika Nafasi za Kaimu Bila kupata idhini ya Katibu Mkuu- Utumishi**

| Na. | Jina la Shirika | Mambo ambayo hayakuidhinishwa na Katibu Mkuu-Utumishi |
|---|---|---|
| **Mashirika yaliyotoa ajira bila kupata idhini ya Katibu Mkuu(Utumishi)** | | |
| 1 | Kampuni ya Ndege Tanzania | Kuajiri wafanyakazi kwa Masharti ya kudumu 56 bila kibali |
| 2 | Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu | Kuajiri wafanyakazi wa mkataba 72 bila kibali |
| 3 | Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya | Kuajiri wafanyakazi wa mkataba 11 bila kibali |
| 4 | Kampuni ya Mkulazi | Kuajiri wafanyakazi 143 bila idhini na wafanyakazi 7 walibadilishwa kutoka mkataba hadi masharti ya kudumu bila kibali |
| 5 | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko | Kuajiri wafanyakazi wa mkataba 37 bila kibali |
| **Kutoidhinishwa kwa nafasi ya kaimu kwa kuanzishwa kwa kudumu** | | |
| 1 | Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania | Wafanyakazi wawili walikaimu bila kibali |
| 2 | Chuo kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa | Wafanyakazi 12 walikaimu bila kibali |
| 3 | Chuo Kikuu cha Dodoma | Wafanyakazi 11 walikaimu bila kibali |
| 4 | Shirika la Umeme Tanzania | Wafanyakazi 48 walikaimu bila kibali |
| 5 | Mamlaka ya Bandari Tanzania | Wafanyakazi 11 walikaimu bila kibali |

**Chanzo:** *Mapitio ya nyenzo pamoja na ripoti za rasilimali watu kwa mwaka 2023/24*

Hii ilitokana na kuwa na mpango duni wa urithishaji wa madaraka hali inayosababisha uhaba wa wafanyakazi ndani ya mashirika na kuilazimu Bodi ya wakurugenzi kuidhinisha ajira au uteuzi wa wafanyakazi katika nafasi za kukaimu bila idhini ya Katibu Mkuu (Utumishi). Vivyohivyo, hali hii inasababishwa na ucheleweshaji wa

uhakiki wa maafisa waliopendekezwa katika nyadhifa hizo, unaofanywa na mashirika husika kabla ya kuidhinisha nafasi hizo.

Kuajiri wafanyakazi bila idhini ya Katibu Mkuu (Utumishi) kunaweza kupelekea kuajiri wafanyakazi wasio na vigezo na kuleta upendeleo. Kwa kuwa baadhi ya wafanyakazi walikuwa katika masharti ya mikataba, huku wengine wakilipwa moja kwa moja na mashirika husika ambayo hayatumii mfumo wa Serikali, kama vile Kampuni ya Mkulazi na Kampuni ya Ndege Tanzania, posho za kukaimu na mishahara iliyolipwa kwa wafanyakazi hawa inaweza kuchukuliwa kama malipo yasiyostahili kwa kuwa hayakuidhinishwa na mamlaka husika.

**Ninapendekeza mashirika ya umma yahakikishe yanaandaa mpango mzuri wa kurithishana madaraka, vilevile yaandae mpango bora wa uteuzi pamoja na ajira ili kuhakikisha vibali kutoka kwa mamlaka husika vinaombwa kwa wakati ili kuepuka uhaba mkubwa wa wafanyakazi. Pia, mashirika yafanye kazi kwa karibu na mamlaka husika ili kuhakikisha kuwa mchakato wa uchunguzi unakamilika kwa wakati.**

## 12.6 Maafisa Waliokaimu Nafasi kwa Muda wa Zaidi ya Miezi Sita

Katika ripoti yangu ya mwaka 2022/23 niliripoti mashirika 11 yalikuwa na wafanyakazi 190 waliokuwa kwenye nafasi za kukaimu kwa kipindi kirefu. Katika ukaguzi huu nimeendelea kubaini wafanyakazi wanaokaimu ambapo mashirika 19 yalikuwa na wafanyakazi 135 waliokuwa wakikaimu nafasi kwa zaidi ya miezi sita, ambapo muda uliozidi kwa kipindi cha miezi sita ulikuwa kati ya mwezi mmoja hadi miezi 57. Hii ni kinyume na Agizo D.24 (3) la Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ambalo linataka watumishi wasikaimu nafasi kwa muda usiozidi miezi sita. Maelezo zaidi yanaoneshwa katika **Jedwali Na. 36.**

**Jedwali Na. 36: Maafisa waliokaimu katika nafasi zao kwa zaidi ya miezi sita**

| S/N | Jina la Shirika | Watumishi wanaokaimu | Miezi waliyokaimu |
|---|---|---|---|
| 1. | Kampuni ya Ndege Tanzania | 9 | 7 |
| 2. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha | 13 | 23 |
| 3. | Chuo cha Ufundi Arusha | 8 | 10 |
| 4. | Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika | 3 | 8 |
| 5. | Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam | 4 | 11 |
| 6. | Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro | 5 | 2-10 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 7. | Bohari Kuu ya Dawa | 14 | 5-15 |
| 8. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro | 12 | 57 |
| 9. | Taasisi ya Mifupa Muhimbili | 15 | 13 |
| 10. | Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila | 2 | 7 -10 |
| 11. | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 3 | 9-16 |
| 12. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma | 4 | 12 |
| 13. | Shirika la Nyumba la Taifa | 10 | 2-32 |
| 14. | Kampuni ya Ranchi za Taifa | 11 | 6 |
| 15. | Bodi ya Kahawa Tanzania | 2 | 10 - 26 |
| 16. | Mamlaka ya Elimu Tanzania | 3 | 4-8 |
| 17. | Bodi ya Nyama Tanzania | 5 | 40 |
| 18. | Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania | 2 | 14 |
| 19. | Chuo Kikuu cha Dodoma | 10 | 1 - 10 |
| | | 135 | |

**Chanzo:** *Barua ya uteuzi za mashirika ya umma kwa mwaka 2023/24*

Tatizo hili linachangiwa na kuchelewa kwa mchakato wa uhakiki wa maafisa waliopendekezwa katika nyadhifa hizo unaofanywa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kushindwa kuteua na kupandisha vyeo maafisa kwa wakati kunaweza kuathiri hamasa ya kufanya kazi, uwezo wa kufanya maamuzi, uwajibikaji, na hatimaye utendaji wa maafisa hao kwa jumla.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yashirikiane na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuharakisha uteuzi wa watumishi ambao wamekuwa wakikaimu kwa muda mrefu na kuteua watumishi wapya katika nafasi hizo endapo wataona maafisa hao wanaokaimu hawakidhi sifa za nyadhifa hizo.**

## 12.7 Maafisa Walioajiriwa au Kukaimu Nafasi Bila kuwa na Sifa Zinazohitajika

Nilibaini uwepo wa wafanyakazi 32 wanaofanya kazi au walioteuliwa kukaimu nafasi mbalimbali katika mashirika ya umma sita bila kuwa na sifa zinazohitajika kulingana na miundo iliyoidhinishwa ya mashirika husika (Rejea **Jedwali Na. 37).**

Hii ilisababishwa na ukosefu wa mpango wa urithishaji madaraka na ukosefu wa wafanyakazi wenye sifa za kushikilia nyadhifa hizo ndani ya mashirika husika. Kuteua wafanyakazi wasio na sifa kwa nafasi za usimamizi kunaweza kupunguza ufanisi wa kazi na kutoridhika kwa

wafanyakazi wenye sifa na waliohitimu lakini ambao hawajateuliwa kushika nafasi hizo.

**Jedwali Na. 37: Maafisa katika nafasi ya kaimu au walioajiriwa bila sifa**

| Na. | Jina la Shirika | Idadi |
|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza | 13 |
| 2 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu | 5 |
| 3 | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 1 |
| 4 | Shirika la Mawasiliano Tanzania | 1 |
| 5 | Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania | 10 |
| 6 | Kampuni ya Mkulazi | 2 |
| | JUMLA | 32 |

**Chanzo:** *Barua za Uteuzi wa nyazifa mbalimbali kwa mwaka 2023/24*

**Ninapendekeza mashirika husika yatekeleze mpango kamili wa urithishaji wa madaraka ili kutambua, kukuza, na kufundisha wafanyakazi wenye uwezo wa kushika nafasi za uongozi hali itakayohakikisha wafanyakazi wanaoteuliwa kushika nafasi hizo wanakuwa na ujuzi unaohitajika**

## 12.8 Upungufu wa Watumishi 7,479 katika Mashirika ya Umma 20

Nilibaini mashirika ya umma 20 yaliyokuwa na upungufu wa watumishi 7,479 sawa na asilimia 36 ya kiwango cha wafanyakazi kilichopendekezwa (Rejea **Jedwali 39**). Tatizo hili liliripotiwa pia katika ripoti zangu za nyuma za 2022/23, 2021/22 na 2020/21, ambapo kulikuwa na upungufu wa jumla wa watumishi 7,808 kwa mashirika ya umma 23, watumishi 4,547 kwa mashirika ya umma 29 na watumishi 8,356 kwa mashirika ya umma 29, mtawalia.

**Jedwali Na. 38: Upungufu wa watumishi 7,479 katika mashirika ya umma 20**

| Na. | Upungufu wa watumishi | Wanaohitajika | Waliopatikana | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi | 3250 | 1,523 | 1727 |
| 2. | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 4930 | 3,230 | 1,700 |
| 3. | Hifadhi za Taifa Tanzania | 4,469 | 2,940 | 1,504 |
| 4. | Chuo Kikuu cha Dodoma | 2074 | 1,508 | 566 |
| 5. | Taasisi ya Mifupa Muhimbili | 1,310 | 913 | 397 |
| 6. | Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini | 721 | 435 | 286 |
| 7. | Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania | 457 | 226 | 231 |
| 8. | Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo | 455 | 276 | 179 |
| 9. | Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere | 501 | 355 | 146 |
| 10. | Taasisi ya Elimu Tanzania | 360 | 216 | 144 |
| 11. | Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi | 359 | 223 | 136 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 12. | Kampuni ya Mkulazi | 508 | 385 | 123 |
| 13. | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira | 365 | 246 | 119 |
| 14. | Baraza la Mitihani la Tanzania | 455 | 343 | 112 |
| 15. | Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka | 165 | 130 | 35 |
| 16. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda | 45 | 20 | 25 |
| 17. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma/Ujiji | 72 | 54 | 18 |
| 18. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo | 30 | 14 | 16 |
| 19. | Mamlaka ya Maeneo Maalumu ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje | 51 | 43 | 8 |
| 20. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Sumbawanga | 53 | 46 | 7 |
| | **Jumla** | **20,630** | **13,126** | **7,479** |

**Chanzo:** *Taarifa za Watumishi wa mashirika ya umma kwa mwaka 2023/24*

Upungufu wa watumishi unatokana na ucheleweshaji wa kupata vibali vya ajira kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hali hii huathiri uwezo wa mashirika kutoa huduma bora na kufikia malengo yaliyopangwa.

**Ninarejea mapendekezo yangu kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu kuhakikisha utoaji wa vibali vya ajira kwa kadri inavyowezekana.**

## 12.9 Kuajiri Wafanyakazi wa Muda bila Kufuata Taratibu Rasmi za Ajira

Nilibaini jumla ya mashirika ya umma 11 yalitoa ajira za muda kwa vibarua 1065 bila kufuata utaratibu rasmi. Hii ni kinyume cha Kifungu 14(1)&(2) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano ya mwaka 2019, Sura ya 366 ambapo mashirika hayo yaliongezeka na kufika jumla ya mashirika 11 ikilinganishwa na mashirika manne ambayo yaliripotiwa katika ripoti yangu ya mwaka 2022/23 (Rejea **Jedwali Na. 39).**

Kutokuwa na utaratibu rasmi wa ajira za mkataba unaotambuliwa kunaweza kuhusishwa na ukosefu wa sera kamili za rasilimali watu na usimamizi usioridhisha katika kusimamia vibarua.

**Jedwali Na. 39: Mashirika ya umma yaliotoa ajira za muda mfupi bila kuwa na muongozo**

| Na. | Jina la Shirika | Changamoto iliyobainishwa |
|---|---|---|
| 1 | Kampuni ya Ndege Tanzania | Jumla ya shilingi milioni 358.52 kwa vibarua 43 bila kuwa na muongozo |

| | | |
|---|---|---|
| 2 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi | Watumishi 28 wanafanya kazi katika nafasi mbalimbali bila mkataba. |
| 3 | Bodi ya Usajili wa Makandarasi | Shilingi milioni 13.7 zililipwa kwa vibarua 21 kwa vibarua bila kuwa na muongozo. |
| 4 | Chuo cha Uhasibu Arusha | Shilingi bilioni 2.83 zinalipwa kwa vibarua bila mikataba |
| 5 | Kiwanda cha kuzalisha mashine na vipuli Kilimanjaro | Ukosefu wa mkataba na kazi kwa wafanyakazi wa kiwanda 18 |
| 6 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya | Shilingi milioni 70 zililipwa kwa wafanyakazi 346 wa kawaida bila taratibu rasmi na/au makubaliano |
| 7 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma | Shilingi milioni 420.07 zililipwa kama mshahara kwa wafanyakazi 100 wenye mikataba mbadala na mkataba ukaongezwa zaidi ya mara mbili |
| 8 | Baraza la Sanaa Tanzania | Kushindwa kutoa mikataba kwa wafanyakazi wa kujitolea kwa watumishi wa kujitolea 9 |
| 9 | Kampuni ya Sisalana | Kutohuishwa kwa mikataba kutoka kwa wafanyakazi 412 |
| 10 | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania | Wafanyakazi 2 walifanya kazi bilakuwa na mikataba mipya |
| 11 | Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania | ajira za muda mfupi zilitolewa bila kuwa na muongozo kwa vibarua 86 |

**Chanzo:** *Mapitio ya mikataba ya ajira kwa mwaka 2023/24*

Ukosefu wa taratibu za ajira ya vibarua kunayaweka mashirika kwenye hatari, ikiwa ni pamoja na madeni ya kisheria kwa mwajiri kutokana na ukosefu wa masharti ya mkataba yanayoweza kutekelezwa. Kukosekana kwa taratibu hizo,Wafanyakazi wa mkataba wa muda mfupi wanaweza wasitendewe haki hali inayoweza kusababisha kutoridhika, kushuka kwa morali ya kazi pamoja na kiwango kikubwa cha wafanyakazi kuondoka kazini.

**Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma husika yaanzishe na kutekeleza taratibu za ndani za kuajiri na kusimamia wafanyakazi ambao wanaajiriwa na mashirika kama vibarua.**

## 12.10 Kutokutumia Mifumo ya kielektroniki ya Serikali ya Usimamizi wa Rasilimali Watu ya HCMIS na PEPMIS

Waraka namba 1 wa Utumishi wa Umma wa mwaka 2021 uliagiza mashirika yote ya Serikali kuanza kutumia Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Rasilimali Watu) ambao mfumo huu unatumika kwa ajili ya usimamizi wa wafanyakazi wote, malipo, ajira, uhamisho pamoja na madai ya wafanyakazi. Vivyohivyo Waraka kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Rejea JA.

228/609/01/B.47 wa tarehe 3 Julai 2024) ulielekeza ofisi zote za Serikali kuzingatia matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Utendaji wa Watumishi wa Umma ambapo mfumo huu hutumika kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango kazi na idhini.

Licha yakuwepo kwa maelekezo hayo, nilibaidi jumla ya mashirika ya umma 26 hayakuzingatia utekelezaji wa mfumo wa HCMIS, wakati jumla ya mashirika nane hayakuzingatia matumizi ya mfumo wa PEPMIS (Rejea **Jedwali Na. 40**). Hali hii inaweza kuathiri ufanisi katika kuandaa mchakato wa mishahara, usimamizi wa wafanyakazi na kufanya tathmini ya utendaji wa mpango kazi wa wafanyakazi. Hii inapunguza uwazi, kuchelewesha mchakato wa maamuzi na kuongeza hatari za makosa katika usimamizi wa rasilimali watu na utendaji. Orodha ya mashirika ya umma ambayo hayakutumia mfumo wa HCMIS imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. XV**.

**Jedwali Na. 40: Mashirika ya Umma ambayo hayakutumia mfumo wa PEPMIS**

| Na. | Jina la Shirika |
|---|---|
| 1 | Benki ya Maendeleo ya TIB |
| 2 | Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania |
| 3 | Benki ya Biashara Tanzania |
| 4 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu |
| 5 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Same Mwanga |
| 6 | Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Kibaiolojia Tanzania |
| 7 | Kampuni ya Mbolea Tanzania |
| 8 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Ngara |

Chanzo: *Mapitio ya taarifa za kimfumo za rasilimali watu kwa mwaka 2023/24*

**Ninapendekeza kuwa mashirika yote ya umma yaliyobainishwa yaharakishe uendelezaji na utekelezaji wa mfumo huo wa taarifa za usimamizi wa rasilimali Watu (HCMIS na PEPMIS) ili kuboresha ufanisi, na kuongeza uwajibikaji katika shughuli za utumishi wa umma.**

13

# Usimamizi wa Kodi Katika Mashirika ya Umma




# SURA YA KUMI NA TATU

# USIMAMIZI WA KODI KATIKA MASHIRIKA YA UMMA

## 13.0 Utangulizi

Mashirika ya umma yanatakiwa kuzingatia sheria za kodi zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Sheria za kodi ni pamoja na Sheria ya Kodi ya Mapato (Sura ya 332), Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Sura ya 438) na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (Sura ya 148).

Sura hii inabainisha mapungufu na mapendekezo yanayohusiana na kutofuata sheria za kodi, ikiwa ni pamoja na malipo ya kodi ya zuio, malipo ya kodi ya makisio na makato na uwasilishaji wa kodi ya mapato ya ajira.

## 13.1 Kuchelewa kulipwa kwa Kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania shilingi bilioni 46.93

Ukaguzi ulibaini ucheleweshwaji wa kulipa kodi kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2023/24, nilibaini mashirika matano ya umma yalichelewa kulipa kodi kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania kiasi cha shilingi bilioni 46.93 ucheleweshaji huu ulikuwa kwa muda wa siku moja hadi 485 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 41**.

**Jedwali Na. 41: Ucheleweshaji wa kulipwa kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania**

| Na. | Jina la Shirika | Aina ya kodi | Kiasi (Sh.'000) | Siku zilizocheleweshwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya | Kodi ya zuio | 56,039 | 10-485 |
| 2 | Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa Tanzania (Shirika la Reli Tanzania) | Kodi ya zuio | 46,662,776 | 57-260 |
| 3 | Taasisi ya Elimu Tanzania | Kodi ya mapato yatokanayo na ajira | 101,337 | Zaidi ya siku 30 |
| 4 | Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu | Kodi ya mapato yatokanayo na ajira | 97,540 | 11-17 |
| 5 | Baraza la Ushauri la Watumia Huduma za Usafiri wa Anga | Kodi ya mapato yatokanayo na ajira | 14,552 | 1-36 |
| | **JUMLA** | | **46,932,246** | |

**Chanzo:** *Taarifa za fedha na vocha za malipo*

Licha ya kupungua kwa idadi ya mashirika ikilinganishwa na miaka iliyopita, kiasi cha kodi kilichocheleweshwa kimeongezeka. Katika mwaka wa fedha 2022/23, mashirika ya umma 12 yalichelewesha malipo ya kodi ya jumla ya shilingi bilioni 29.09 kwa kipindi cha kati ya siku 1 hadi 1,015. Vilevile, kwa mwaka wa fedha 2021/22, mashirika ya umma 18 yalichelewesha malipo ya kodi ya shilingi bilioni 5.09, kinyume na kifungu cha 84 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato (Sura ya 332), ambacho kinamtaka kila wakala wa kodi ya zuio kuwasilisha malipo kwa Kamishna wa Mamlaka ya Mapato ndani ya siku saba baada ya mwisho wa mwezi ambapo kodi ilizuiliwa.

Kuchelewa kuwasilisha kodi kulitokana na mashirika husika kushindwa kuzingatia matakwa ya sheria au kuelekeza fedha zilizopangwa kwa ajili ya kodi kwenye matumizi mengine.

Katika Taasisi ya Elimu Tanzania, ucheleweshaji ulisababishwa na matatizo yaliyojitokeza wakati wa kutumia mfumo wa kodi, matatizo hayo yaliwasilishwa kwenye dawati la msaada la Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ajili ya marekebisho. Aidha , deni la kodi ya mapato lililorithiwa kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tangu mwaka 2019 nalo liliathiri malipo ya kodi kwa wakati.

Kwa upande wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi, utengamanishi kati ya mfumo wa bajeti wa Serikali (PlanRep) na Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Utendaji Kazi na Rasilimali za Taasisi (ERMS) ulisababisha kuchelewa kupata bajeti iliyoidhinishwa ndani ya mfumo, ambayo baadaye ilichelewesha kuanza kwa malipo ikiwa ni pamoja na kodi.

Ucheleweshaji wa malipo ya kodi unaweza kupelekea Mamlaka ya Mapato Tanzania kutoza riba na adhabu.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yahakikishe yanalipa kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa wakati, ili kuepuka tozo ya riba na adhabu.**

## 13.2 Mashirika ya Umma Kutokulipa Kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania shilingi bilioni 9.65

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa mashirika ya umma 17 (sawa na asilimia 7) kati ya mashirika 217 yaliyokaguliwa hayakuwasilisha kodi mbalimbali zenye thamani ya shilingi bilioni 9.65 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka wa fedha 2023/24 kinyume na sheria za kodi.

Ingawa hali ya mashirika kulipa kodi imeimarika ikilinganishwa na miaka ya nyuma, tatizo la kutolipa kodi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania limekuwa likijirudia. Katika mwaka wa fedha 2022/23, mashirika 16 (asilimia 7) hayakulipa kodi zenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 33.45; na mwaka 2021/22 , mashirika ya umma 13 (sawa na asilimia 6) kati ya mashirika 203 yaliyokaguliwa hayakuwasilisha kodi mbalimbali za jumla ya shilingi bilioni 46.83 kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Kutowasilisha kodi kulisababishwa na changamoto za kifedha katika mashirika ya umma husika. Kutolipa kodi kunaweza kuongeza gharama kwa mashirika ya umma husika kutokana na adhabu zitakazotozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Kwa Kampuni ya STAMIGOLD, kutowasilishwa kwa kodi kulitokana na kutokuwepo kwa namba ya mlipa kodi kwa baadhi ya waajiriwa.

**Kiambatisho Na. XVI** kinatoa mchanganuo wa kodi mbalimbali ambazo hazikuwasilishwa kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania, zikiwemo Kodi ya Ongezeko la Thamani, kodi ya zuio, kodi ya mapato yatokanayo na ajira na kodi ya ujuzi na maendeleo.

**Ninapendekeza kuwa mashirika ya umma husika yahakikishe yanafuata sheria za kodi na kulipa kodi husika kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.**

## 13.3 Kufanya Malipo Bila Risiti za Kodi za Kielektroniki katika Mashirika ya Umma shilingi bilioni 4.14

Kanuni ya 28 ya Kanuni za risiti za Kielektroniki za Kodi ya Mapato za mwaka, 2012 inamtaka kila mnunuzi kudai na kuhifadhi risiti ya fedha au ankara katika milki yake. Pia, kanuni ya 21 hadi 25 ya kanuni hiyo zinaeleza kuwa mtu yeyote ambaye anashindwa kudai, kuhifadhi au kutoa risiti au ankara anafanya kosa la kisheria na anawajibika kulipa adhabu ya mara mbili ya kiasi cha kodi aliyokwepa.

Katika ukaguzi nilibaini kuwa mashirika ya umma 12 yalifanya malipo ya jumla ya shilingi bilioni 4.14 bila kuambatisha risiti za kielektroniki (Rejea **Jedwali Na. 42**). Hii inaonesha ongezeko la malipo ambayo hayakuambatishwa risiti za kielektroniki ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2022/23, ambapo mashirika tisa yalifanya malipo ya shilingi bilioni 2.17 bila kuambatisha risiti. Pia, katika mwaka wa fedha 2021/22, kulikuwa na malipo yenye thamani ya shilingi milioni 556.83

yaliyofanywa na mashirika ya umma 11 bila kuambatisha risiti za kielektroniki za kodi.

Kujirudia kwa malipo yasiyoambatishwa risiti za kielektroniki kwa mwaka wa fedha 2023/24 kunaonesha uhitaji mkubwa wa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa kanuni za risiti za kielektroniki za kodi ya mapato.

**Jedwali Na. 42: Malipo bila risiti za kodi za kielektroniki**

| Na | Jina la Shirika | Kiasi Sh. '000 |
|---|---|---|
| 1 | Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba | 1,776,510 |
| 2 | Baraza la Taifa la Ujenzi | 925,862 |
| 3 | Kampuni ya Mkulazi | 869,305 |
| 4 | Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania | 252,676 |
| 5 | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima | 95,904 |
| 6 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tukuyu | 61,314 |
| 7 | Kituo cha Uwekezaji APC | 33,425 |
| 8 | Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere | 32,978 |
| 9 | Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari | 32,525 |
| 10 | Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi | 26,484 |
| 11 | Shirika la Posta Tanzania | 24,601 |
| 12 | Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania | 10,185 |
| | **Jumla** | **4,141,767** |

**Chanzo:** *Taarifa za vocha za malipo za mashirika husika 2023/24*

Maoni yangu ni kuwa mashirika ya umma yanapaswa kuwa mfano katika kuzingatia na kufuata sheria za kodi hasa katika kutoa na kudai risiti za kielektroniki za kodi. Adhabu zinaweza kutozwa kwa mashirika ya umma husika kwa kushindwa kudai, kuhifadhi na kutoa risiti ya fedha au ankara katika milki yao. Aidha, kodi ya ongezeko la thamani kwenye ununuzi haiwezi kudaiwa bila risiti za kielektroniki za kodi, hivyo kuongeza gharama kwa mashirika ya umma husika. Vilevile, Serikali inapoteza mapato ambayo yangeweza kupokelewa kama risiti za kielektroniki za kodi zingetolewa.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yazingatie sheria na kanuni za kodi ya mapato kuhusu kudai na kuhifadhi risiti za kielektroniki za kodi.**

## 13.4 Kampuni ya Uzalishaji ya KMTC na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania Hazijasajiliwa kwa Ajili ya Kodi ya Ongezeko la Thamani

Kanuni ya 4 ya Kanuni za Kodi ya Ongezeko la Thamani, (Marekebisho), 2023 inahitaji Shirika la Serikali linalojihusisha na shughuli za kiuchumi, kusajiliwa kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani. Usajili kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani ni lazima kisheria kwa Shirika ambalo limefikia kiwango cha usajili kwa kuwa na mapato ya kuanzia kiasi cha shilingi milioni 200 au zaidi katika kipindi cha miezi 12 au kiwango cha shilingi milioni 100 au zaidi katika kipindi cha miezi sita iliyopita. Mashirika ya Serikali ambayo yanafanya shughuli za kiuchumi, yanatakiwa kusajiliwa bila kuangalia kama yamefikiwa kiasi cha mapato cha usajili.

Katika mwaka 2023/24, nilibaini kuwa Kampuni ya Uzalishaji ya KMTC na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania hazikuwa zimesajiliwa kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani. Kutokusajiliwa kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani kunasababisha mashirika haya kushindwa kudai kodi iliyolipwa kwenye manunuzi, hivyo kodi hiyo inakuwa sehemu ya gharama kwa mashirika hayo.

Aidha, kwa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania haikusajiliwa kwa sababu ya kuamini ni shirika la Serikali linalotoa huduma, hivyo kudhani kuwa halitakiwi kusajiliwa kwa ajili ya kodi ya ongezeko la thamani. Hata hivyo, mapitio ya sampuli ya miamala 15 yalionesha kuwa Mamlaka hiyo inalipa kodi ya ongezeko la thamani.

Kutofuata sheria zilizowekwa kunaweza kusababisha mashirika haya kutozwa riba na adhabu au kufungiwa kutoa huduma.

**Ninapendekeza kuwa Kampuni ya Uzalishaji ya KMTC na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania ifuatilie Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa ajili ya usajili wa kodi ya ongezeko la thamani.**

## 13.5 Kutokuwepo kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani katika Ankara ya Malipo ya Wasambazaji wa Bodi ya Korosho

Kifungu cha 86 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kinawataka wasambazaji kutoa hati ya madai iliyo sahihi, ambayo inaonesha, pamoja na mambo mengineyo, namba ya mlipa kodi, kiasi kinachotakiwa kulipwa na kiasi cha kodi ya ongezeko la thamani.

Bei za mikataba ya usambazaji wa viuatilifu kwa Bodi ya Korosho Tanzania kwa mwaka wa fedha 2022/23 ilijumuisha kodi ya ongezeko la thamani. Hata hivyo, licha ya mikataba hiyo kuonesha kipengele hicho, hati za madai ya jumla ya shilingi bilioni 89.20 zilizowasilishwa mwaka 2024 na wasambazaji kuhusiana na mikataba ya mwaka 2023 hazikuonesha kipengele cha kodi ya ongezeko la thamani, ambayo kwa ujumla ni shilingi bilioni 16.05. Kukosekana kwa kipengele cha kodi ya ongezeko la thamani kunahusishwa na menejimenti ya Bodi ya Korosho kukosa uthabiti wa usimamizi na ufuatiliaji kuhakikisha sheria za kodi zinafuatwa. Hali hii inasababisha Serikali kukosa mapato.

**Ninapendekeza kuwa Bodi ya Korosho Tanzania ihakikishe wasambazaji wote wanatoa hati ya madai yenye kipengele cha kodi ya ongezeko la thamani kama inavyotakiwa na mkataba. Zaidi, Bodi ya Korosho ikishirikiana na Mamlaka ya Kodi Tanzania ifuatilie na kuhakikisha Kodi ya ongezeko la thamani inalipwa na wasambazaji.**

# Mwenendo wa Benki Zinazomilikiwa na Serikali, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Taasisi Zingine za Kifedha





# SURA YA KUMI NA NNE

# MWENENDO WA BENKI ZINAZOMILIKIWA NA SERIKALI, MIFUKO YA HIFADHI YA JAMII NA TAASISI ZINGINE ZA KIFEDHA

## 14.0 Utangulizi

Benki na Mifuko ya Hifadhi za Jamii ina majukumu muhimu ya kiuchumi. Benki hutoa huduma muhimu za kifedha, kuchochea ukuaji wa uchumi, wakati Mifuko ya Hifadhi za Jamii hutoa ulinzi wa kifedha kupitia manufaa kwa wanachama kama vile pensheni na bima ya afya, mara nyingi huwekeza katika miradi ya kiuchumi ili kusaidia manufaa ya baadaye. Sura hii inaangazia Benki zinazomilikiwa na Serikali, Mifuko ya Hifadhi za Jamii, na Shirika la Bima la Taifa. Pia inajumuisha taasisi zinazohusika na masoko ya mitaji na dhamana nchini Tanzania, zikiwemo Dhamana ya Uwekezaji na Usimamizi Rasilimali Tanzania, Bodi ya Bima ya Amana, na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana.

### 14.1 Utendaji wa Benki za Serikali

Nilifanya Ukaguzi katika Benki ya Maendeleo ya TIB, Benki ya Azania, Benki ya Biashara Tanzania, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2024 na kubaini usimamizi duni wa mikopo, mapungufu katika mchakato wa tathmini za dhamana za mikopo, na kutokidhi matakwa ya Benki Kuu ya Tanzania, na mapungufu mengine kama yalivyoainishwa hapo chini :-

#### 14.1.1 Usimamizi Duni wa Dhamana za Mikopo Iliyotolewa ya shilingi bilioni 558.53

Ukaguzi wangu kuhusu usimamizi wa mikopo katika **Benki ya Maendeleo ya TIB** ulibaini mikopo ya shilingi bilioni 209.05 ilitolewa kwenye dhamana ambazo thamani zake za mauzo zilikuwa shilingi bilioni 52.06 na kupelekea tofauti ya shilingi bilioni 156.99 ambapo ni kinyume na Kifungu cha 29 cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha , Sura 342. Pia, nilibaini mikopo ya shilingi bilioni 19.63 ambayo bima ya dhamana zake zilikuwa zimeisha muda wake au zilikuwa hazijahuishwa ambapo ni Kinyume na Kanuni ya 54 (a) (vii) ya Mabenki na Taasisi za Fedha(Mikopo ya Maendeleo) ya mwaka 2021.

Katika **Benki ya Biashara Tanzania**, sikupatiwa ripoti za uthamini wa dhamana za mikopo 31 kati ya 51, yenye jumla ya shilingi bilioni 24.93. Aidha, nilibaini wateja 44 kati ya 50 ambao thamani ya dhamana za mikopo yao ilikuwa shilingi bilioni 407.49 kwenye orodha ya dhamana za mikopo, wakati jumla ya thamani ya dhamana hizo iliyoandikiswha kwenye majalada ya mikopo husika ilikuwa shilingi bilioni 419.93 na kupelekea tofauti ya shilingi bilioni 12.46.

Aidha, nilibaini mikopo sita ya jumla ya shilingi bilioni 20.31 ambayo dhamana zake hazikuwa na bima. Vile vile, dhamana za mikopo 13 ya shilingi bilioni 47.14 hazikufanyiwa uhakiki kikamilifu.

Katika **Benki ya Azania**, nilibaini utofauti wa shilingi bilioni 277.07 kati ya thamani ya mikopo ilivyooneshwa kwenye rejista ya dhamana na majalada ya mikopo halisi. Thamani kutoka kwenye rejista ilikuwa bilioni 786.27 wakati thamani kutoka kwenye majalada ya mikopo ilikuwa shilingi bilioni 509.20.

Mapungufo hayo yalitokana na usimamizi hafifu wa dhamana za mikopo na kutofakufanya usuluhishi kati ya taarifa za thamani halisi za dhamana na taarifa zilizoandikishwa kwenye majalada ya mikopo husika.

Nimebaini mapungufu kama vile kuwepo kwa taarifa za uthamini wa dhamana zisizohuishwa kwa wakati, taarifa za fedha zilizopitwa na wakati na hazijahuishwa ambazo zilitumika kupata mikopo.

Uwepo wa hati za dhamana zisizotosheleza au kukamilika zina hatarisha mikopo hiyo kwani benki inaweza kushindwa kurejesha mikopo endepo wakopaji watashindwa kulipa.

**Ninapendekeza Benki ya Azania, Benki ya Biashara Tanzania, na Benki ya** Maendeleo **ya TIB (a) zihakikishe dhamana zinakuwa na bima, (b) zihakikishe mikopo inakuwa na dhamana pamoja na kufanya uthaminishaji wa dhamana mara kwa mara ili kuomba nyonheza ya dhamana wakati thamani ya dhamana iliyotolewa inapokuwa chini ya kiwango kinachohitajika; na (c) Afisa Masuuli ambae hatatoa taarifa na nyaraka kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali anapaswa kuadhibiwa maana kufanya hivyo ni kinyume na Ibara ya 143(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.**

### 14.1.2 Kutofuata viwango vya Udhibiti Vilivyowekwa na Benki Kuu

Ukaguzi wangu wa utendaji wa **Benki ya Biashara Tanzania** ulibaini kuwa Benki ilikuwa ina utofauti wa viwango vya udhibiti vilivyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania. Mapitio zaidi ya ukaguzi yalibaini kuwa **Benki ya Biashara Tanzania** ilikuwa na uwiano wa mtaji wa asilimia 13.41 ambao ni chini ya uwiano unaohitajika wa asilimia 14.5. Pia, Benki ilikuwa na akaunti za amana za makampuni ya simu yanayotoa huduma za fedha zenye jumla ya shilingi bilioni 129.18 sawa na uwiano wa asilimia 97 ya mtaji mkuu dhidi ya uwiano unaohitajika wa asilimia 50. Aidha, uwiano wa gharama dhidi ya mapato ulikuwa

asilimia 76 dhidi ya kiwango kinachopaswa cha asilimia 55. **Jedwali Na. 43** linaonesha tofauti kati ya Benki ya Biashara na matakwa ya Benki Kuu ya Tanzania. Jambo hili limechangiwa na uhaba wa mtaji uliopelekea Benki kutokidhi viwango vilivyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania.

**Jedwali Na. 43: Maelezo ya utendaji wa Benki ya Biashara dhidi ya kiwango cha udhibiti cha Benki**

| Na | Aina | Kinachotakiwa na Benki Kuu ya Tanzania(Asilimia) | Kilichofikiwa na Benki ya Biashara Tanzania (Asilimia) | Tofauti ya uwiano katika asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Jumla ya Mtaji | 14.5 | 13.41 | 1.09 |
| 2 | Akaunti ya Amana | Akaunti ya Amana isizidi asilimia 50 ya mtaji | 97 | 47 |
| 3 | Uwiano wa gharama na mapato | 55 | 76.31 | 21.31 |

**Chanzo:** *Uchambuzi wa wakaguzi kuhusu utendaji wa Benki ya Biashara Tanzania 2024*

Benki ya Biashara Tanzania ilinifahamisha kuwa inashirikiana na wanahisa wake ili kuweza kuongeza mtaji mpya. Zaidi ya hayo, Benki inapanga kukusanya mtaji kupitia kuuza hisa ifikapo mwaka 2026 ambapo suala hili litatoa suluhisho la kudumu kwa changamoto ya mtaji wa Benki na hivyo kuboresha uwiano wa mtaji unaohitajika.

**Ninapendekeza Benki ya Biashara Tanzani (a) iwasiliane na wanahisa kuomba mtaji mpya ili benki ikidhi matakwa ya Benki Kuu; na (b) Benki ifanye utafiti wa kina ambao utakuwa msingi wa taarifa sahihi kwa ajili ya kufanya maamuzi ya kukusanya fedha kupitia kuuza hisa kwa umma.**

### 14.1.3 Viwango vya Utoshelevu wa Mtaji Visivyoridhisha kwa Benki ya Maendeleo ya TIB kwa kiasi cha shilingi bilioni 112.74

Kanuni ya 22(1) ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha za mwaka 2021 inaeleza kuwa taasisi ya fedha ya maendeleo itaanza kufanya kazi ikiwa wakati wote ina mtaji wa msingi usiopungua shilingi bilioni 200 au zaidi ya kiasi hicho.

Mapitio yangu yalibaini kuwa mtaji mkuu wa Benki ya Maendeleo TIB hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2024 ulikuwa shilingi bilioni 87.26 ambapo ni pungufu kwa shilingi bilioni 112.74 za mahitaji ya mtaji wa shilingi bilioni 200. Aidha, Benki ilieleza kuwa inafuatilia Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuongeza mtaji kuwa shilingi bilioni 200. Tarehe

3 Januari 2025 Msajili wa Hazina alimshauri Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha kukubali pendekezo la kuongeza mtaji wa shilingi bilioni 200.

Pia nilibaini kiasi cha shilingi bilioni 37 ambacho hakijalipwa tangu mwaka 2019 kutoka kwa Msajili wa Hazina ambapo ni kipindi cha miaka sita. Mwaka 2019 Msajili wa Hazina alitakiwa kulipa shilingi bilioni 37 kwa Benki ya Maendeleo ya TIB ikiwa ni kiasi ambacho Benki ya Maendeleo ya TIB ilikuwa ikiidai iliyokuwa Benki TIB Corporate ambayo ilisitisha shughuli zake na kuchukuliwa na Benki ya Biashara Tanzania. Hata hivyo, hadi nafanya ukaguzi wangu mnamo tarehe 5 Machi 2025 kiasi hicho kilikuwa bado hakijalipwa na Msajili wa Hazina.

Aidha, mapitio yangu yalibainisha kuwa hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2024, Benki iliripoti madeni yaliyoiva ya shilingi bilioni 183 wakati mali halisi ya mtaji ilikuwa pungufu kwa kiasi cha shiling bilioni 2.84 huku riba ya madeni yaliyoiva ikiwa imeongezeka kutoka shilingi bilioni 19.4 ya mwaka 2023 hadi shilingi bilioni 26.9 kwa mwaka 2024 ikiwa ni sawa na asilimia 39.

Ni maoni yangu kuwa Uwiano usiofaa wa utoshelevu wa mtaji unaleta hatari kwa Benki kupoteza sifa zake za kujiendesha, hali hii inaweza kusababisha Benki kuwekwa chini ya usimamizi wa Benki Kuu Tanzania. Kwa maana hiyo, kiasi cha shilingi bilioni 37 kinachodaiwa na Benki ya Maendeleo TIB kina umuhimu mkubwa wa kuboresha mtaji mkuu wa Benki.

**Ninapendekeza kuwa Serikali, kwa kushirikiana na wadau husika, itengeneze muongozo wa kimkakati wa kuboresha uimara wa kifedha na usimamizi wa benki za Serikali. Muongozo huu unapaswa kuzingatia uwepo wa muundo mzuri na wa muda mrefu wa upatikanaji wa fedha za kujiendesha, ambao utapunguza utegemezi na nyongeza za mara kwa mara za mtaji ili kuhakikisha uimara wa kifedha. Aidha, Muongozo huo unapaswa kuimarisha sera za usimamizi wa ukwasi ili kuepuka ukata wa fedha na kuongeza ustahimilivu dhidi ya hatari za kifedha. Vilevile, Muongozo uainishe viwango vya upimaji wa utendaji wa kifedha na uendeshaji ili kutathmini na kuboresha ufanisi, usimamizi, na uwajibikaji katika benki za Serikali. Kutekeleza njia hii ya kimkakati kutachangia kudumisha uhai na ufanisi wa benki za Serikali katika kukuza maendeleo ya kiuchumi ya taifa.**

### 14.1.4 Kutofikiwa kwa Upanuzi wa Wigo wa Lengo la Mpango wa Udhamini wa Mikopo kwa Wakulima Wadogo

Mpango wa Udhamini wa Mikopo kwa Wakulima Wadogo unalenga kuhamasisha benki nyingine kuboresha upatikanaji wa mikopo kwa wakulima wadogo ambao wanakabiliwa na changamoto za upatikanaji wa fedha ndani ya sekta ya fedha. Uwepo wa mikopo, utatoa fursa kwa wakulima wadogo kutumia mbinu za kisasa za kilimo ili kutengeneza ajira, kukuza akiba ya chakula na kubadilisha shughuli za kilimo kutoka kilimo cha kujikimu hadi cha kibiashara.

Ukaguzi wangu wa Mpango Kazi wa Mwaka 2024 wa **Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania** ulibaini kuwa benki ilipanga kusajili Taasisi tano mpya za Kifedha lakini iliweza kusajili taasisi tatu ambazo ni sawa na asilimia 60 ya lengo. Hali hii imechangiwa na taasisi mbili za kifedha zilizolengwa kutokukidhi vigezo na katika kukabiliana na hilo Benki ilianza majadiliano na taasisi nyingine za fedha. Ni maoni yangu kuwa ucheleweshaji wa kupanua wigo wa udhamini wa mikopo kwa wakulima wadogo unapelekea Benki kutotimiza jukumu lake la kusaidia wakulima wadogo kupata wigo mpana wa kuchagua taasisi za kifedha katika kukopa.

**Ninapendekeza kuwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ihakikishe kuwa taasisi mpya za Kifedha zinasajiliwa kwa idadi inayolengwa, ili kuharakisha upanuzi wa mpango wa uendelezaji wa mnyororo wa thamani unaofanywa kupitia Udhamini wa Mikopo kwa Wakulima Wadogo.**

### 14.1.5 Usimamizi duni katika Mfuko wa SELF wa Utoaji wa Mikopo kwa Wateja ya shilingi milioni 124.2

Tarehe 31 Desemba 2023, Mfuko wa SELF ulitoa mikopo inayoitwa **pamoja** ya shilingi milioni 79.2 kwa vikundi kwa riba ya asilimia 24 kwa mwaka kwa kiwango kisichobadilika, ambacho ni kinyume na kiwango kilichoidhinishwa cha asilimia 30 kama ilivyoainishwa katika Kiambatisho 16.22 cha Mwongozo wa Utaratibu wa Mikopo, 2023. Suala hili lilitokana na hitilafu ya mfumo kwa vile haikuwekwa fomula kwa ajili ya kukokotoa riba kwa kutumia njia ya kupunguza salio.

Aidha, ukaguzi wangu ulibaini tofauti kati ya mkataba wa mkopo wa tarehe 25 Januari 2022, na fomu ya maombi ya mkopo. Mkataba huo unaeleza kuwa lengo la mkopo huo ni upanuzi wa biashara ya vileo jijini Arusha huku fomu ya maombi ikionesha mkopo huo ni kwa ajili ya ukarabati wa maeneo ya biashara, ofisi na ununuzi wa samani. Hata hivyo, shilingi milioni 45 pekee ndizo zilitolewa kwa ajili ya ukarabati

wa majengo ya biashara na ununuzi wa samani, kinyume na masharti ya mkataba kati ya Mfuko wa SELF (mkopeshaji) na mkopaji. Mkopaji hakuweza kurejesha mkopo na alilipa awamu moja tu. Suala hilo limechangiwa na kutokukamilika kwa mapitio na ufuatiliaji wa mkopo ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa karibu wa mkopo huo.

Kushindwa kutoza kiwango cha riba kilichoidhinishwa kunaweza kuathiri faida ya mkopo na kupelekea kupunguza uzalishaji wa mapato. Aidha, uchambuzi duni wa maombi ya mikopo, tathmini duni ya viashiria vy hatari, udhibiti dhaifu wa tathmini ya dhamana, na ufuatiliaji usioridhisha baada ya kutolewa mikopo kunaongeza hatari ya mikopo chechefu na hasara inayoweza kutokea kwa Mfuko.

**Ninapendekeza Mfuko wa SELF uhakikishe taratibu za mapitio ya mkopo zinaimarishwa ili kujumuisha tathmini ya kina ya hatari, uthamini sahihi wa** dhamana**, na ufuatiliaji thabiti baada ya mikopo kutolewa ili kuepuka hatari ya mikopo chechefu. Aidha, riba zilizoidhinishwa zinapaswa kuingizwa kwenye mfumo kwa usahihi.**

### 14.1.6 Utendaji Usioridhisha wa TIB Rasilimali

**TIB Rasilimali** ilianzishwa awali kama Waendelezaji Mali na baadaye kubadilishwa kuwa wakala wa masoko ya mitaji. Kampuni imepewa leseni na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Soko la Hisa la Dar es Salaam na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kushughulikia huduma za udalali wa dhamana, ushauri wa uwekezaji, uthamini wa biashara na wakala wa bima.

TIB Rasilimali imeendelea kupata hasara baada ya kodi kwa zaidi ya miaka mitano, mwaka 2024 iliripoti hasara ya shilingi milioni 539.86 (2023: Hasara ilikuwa shilingi milioni 343.80). Pia, hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2024, madeni yalizidi jumla ya mali zake kwa shilingi bilioni 1.25, jambo linaloashiria uwepo wa ukata wa fedha. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, Kampuni ilikuwa imepata jumla ya hasara ya shilingi bilioni 3.62, na kupelekea kupunguza mtaji hadi kufikia mtaji hasi wa shilingi bilioni 1.25.

Kwa maoni yangu TIB Rasilimali haiwezi kushamiri kutokana na mwenendo wa kupata hasara ambayo imeiweka TIB Rasilimali katika hali ya hatari. Jambo hilo limechangiwa na ukosefu wa mtaji pamoja na kubadili aina ya uwekezaji ambapo uwekezaji umehama kutoka kwenye hisa zilizoorodheshwa kwenda dhamana zenye riba. **Jedwali Na. 44** linaonesha mwenendo wa hasara kwa kipindi cha miaka mitano.

**Jedwali Na. 44: Mwenendo wa hasara wa TIB Rasilimali kwa kipindi cha miaka mitano**

| Na | Mwanka wa Fedha | Faida au (Hasara) Sh '000 |
|---|---|---|
| 1 | 2020 | 700,150 |
| 2 | 2021 | 301,910 |
| 3 | 2022 | 456,040 |
| 4 | 2023 | 343,800 |
| 5 | 2024 | 539,860 |
| Jumla ya hasara hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2024 | | 3,628,711 |

**Chanzo***: Taarifa za fedha za Benki za 2020 hadi 2024*

Menejimenti iliniarifu kuwa inachukua hatua za kuboresha hali ya TIB Rasilimali kwa kuwa timu maalumu imeteuliwa kukagua na kutathmini shughuli zake na uhakiki utakapokamilika ripoti itakabidhiwa kwa Msajili wa Hazina.

**Ninapendekeza TIB Rasilimali iharakishe mchakato wa utafiti na matokeo ya** utafiti **yatumike kuandaa Mkakati wa kuiinua Benki kiuwezo, pamoja na kuangalia fursa ili kuanzisha vyanzo vingine vya mapato.**

## 14.2 Utendaji wa Mifuko ya Hifadhi za Jamii

Mapitio yangu ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi), na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi na Shirika la Bima la Taifa yalibaini usimamizi duni wa mikopo iliyotolewa, usimamizi duni wa uwekezaji, na utoaji huduma usioridhisha kwa walengwa. Ukaguzi wangu ulibaini mapungufu kama ilivyoainishwa hapa chini:

### 14.2.1 Kiasi Inachodaiwa Serikali cha shilingi trilioni 2.28 za Wanachama wa Zamani wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma

Katika ripoti yangu ya mwaka 2022/23, nilielezea mashaka yangu kuhusu deni la shilingi trilioni 2.28 linalohusiana na mafao ya watumishi waliokuwepo kabla ya mwaka 1999, ambalo lilirithiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa zamani (PSPF).

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) ulirithi jumla ya madeni ya Shilingi trilioni 4.46 kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa zamani. Mnamo Desemba 2021, Serikali ilitoa hati fungani maalumu ya shilingi trilioni 2.18 na kuahidi kulipa deni lililobaki la

shilingi trilioni 2.28 baada ya kukamilika kwa zoezi la uhakiki, ambalo lilipangwa kukamilika ifikapo tarehe 31 Machi 2024.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2023/24, uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma uliripoti kuwa Serikali bado inaendelea na uhakiki wa deni la shilingi trilioni 2.28 na kuthibitisha kuwa malipo ya deni hilo yatafanyika mara baada ya zoezi hilo kukamilika.

**Narudia pendekezo langu kuwa Serikali iharakishe zoezi la uhakiki na ikamilishe malipo ya deni la shilingi trilioni 2.28 la watumishi waliokuwepo kabla ya mwaka 1999. Kukamilika kwa malipo haya kutasaidia kuboresha kiwango cha ukwasi wa Mfuko hadi kufikia kiwango kilichopendekezwa cha asilimia 40, ikilinganishwa na kiwango cha sasa cha asilimia 36.40.**

### 14.2.2 Usimamizi Duni wa Mikopo na Michango ya Wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii

#### i) Kutorejesha kwa Mikopo ya muda Mrefu iliyotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa Serikali shilingi trilioni 1.29

Nimekuwa nikiripoti juu ya uwepo wa mikopo ambayo haijalipwa kwa muda mrefu iliyotolewa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa mashirika ya Serikali kwa miaka mitano mfululizo, hata hivyo, nilibaini uwepo wa mikopo mikubwa ambayo bado haijarejeshwa hali inayoathiri uwezo wa kifedha kwa Mifuko ya Hifadhi za Kijamii.

**Katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi**: Katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024, nilibaini mikopo ambayo ilikuwa haijarejeshwa ya shilingi trilioni 1.06, ikiwa imepungua kwa shilingi bilioni 437 (sawa na asilimia 29) ukilinganisha na deni la mwaka uliopita (2022/23 shilingi trilioni 1.50). Kupungua huko kulitokana na Serikali kutoa hati fungani maalumu zenye thamani ya shilingi bilioni 433.71 ili kulipia mikopo yake ya muda mrefu.

**Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma** ulikuwa na mikopo ambayo ilikuwa haijalipwa ya shilingi bilioni 231.40 sawa na mikopo ya mwaka uliopita (2022/23 shilingi bilioni 231.40) kutoka kwa mashirika ya umma 12. Mikopo hii haijalipwa kwa muda wa kuanzia mwaka mmoja hadi 17, na hivyo kuathiri uwezo wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kutimiza majukumu yao ya msingi kwa ufanisi.

**Ninarudia mapendekezo yangu ya awali kuwa (a) Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na mashirika ya Serikali ambayo yamekopa**

**kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ifanye mipango ya marejesho ya mikopo hiyo; na (b) Mifuko ya hifadhi za jamii iimarishe udhibiti kabla ya kutoa mikopo na kuendelea kufanya ufuatiliaji ili kuhakikisha mikopo inarejeshwa.**

### ii) Kutokuwa na Uhakika wa Kurejeshwa kwa Mkopo wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi Uliotolewa kwa Halmashauri ya Jiji la Dar-es-Salaam wa shilingi bilioni 15.91

Mwaka 2007, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi uliingia makubaliano na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kutoa mkopo wa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Biashara kiitwacho Machinga Complex. Hata hivyo, kiasi cha mkopo cha awali hakikutosha kukamilisha mradi huo, hivyo kuilazimu Halmashauri kusaini mikataba ya nyongeza mitatu yenye nyongeza ya shilingi bilioni 3.41 na kufanya jumla ya mkopo uliopata idhini kufikia shilingi bilioni 13.41. Hata hivyo ukaguzi wangu wa fedha zilizotolewa ulibaini kuwa jumla ya fedha zilizotolewa kama mkopo ni shilingi bilioni 15.91 huku zikizidi kiwango kilichoidhinishwa cha shilingi bilioni 13.41 na kupelekea ziada ya shilingi bilioni 2.50 ambapo hapakuwa na ushaidi wa idhini ya nyongeza ya mkopo huo.

Pia nilibaini kuwa Halimashauri ya Jiji la Dar es Salaam haikutoa dhamana ya Serikali wala hatimiliki ya ardhi ambayo iko kwa jina lake, kinyume na kifungu cha 3 cha Mkataba wa Mkopo ambacho kinasisitiza kuwa, mkopo utatolewa kwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam endapo halmashauri hiyo itapata Dhamana ya Serikali ya angalau asilimia 60 ili kuwa kama dhamana ya mkopo mkuu na riba na vile vile endapo itawasilisha hati miliki ya ardhi inayoonesha jina la Halmashauri.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi ulibainisha jumla ya mkopo wake ulikuwa umefikia bilioni 27.61, ukijumuisha mkopo mkuu na riba. Tathmini yangu ya Halmashauri kurejesha mkopo ilibaini kuwa, tangu mwaka 2009 Halmashauri ilikuwa imerejesha shilingi milioni 80 pekee, licha ya wajibu wa marejesho ulioanza mwaka huo kufuatia kipindi cha matazamio cha miaka miwili kuanzia 2007, kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 7 cha Mkataba. Mkopo huo ulitakiwa kulipwa kikamilifu kuanzia tarehe 1 Januari 2009 hadi tarehe 31 Desemba 2018. Hata hivyo, hakuna mpango wa ulipaji uliokubaliwa na pande zote mbili, licha ya muda wa kurejesha mkopo kupita.

Kutokuwepo kwa Dhamana ya Serikali, mpango uliokubaliwa na pande zote mbili wa ulipaji, na hati miliki ya ardhi vinaashiria mkopo huo kutokuwa na dhamana, na hivyo kusababisha hatari ya kushindwa kufanya marejesho ya mkopo huo.

**Ninapendekeza Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi; (a) Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ufanye maridhiano ya kina ili kukubaliana kuhusu ulipaji wa mkopo ambao bado unadaiwa katika Halmashauri ya Jiji la Dar-es-Salaam; (b) upate hati ya makubaliano kutoka kwa Halmashauri ya Jiji la Dar-es-Salaam kuonesha jinsi mkopo mkuu na riba utakavyolipwa kikamilifu kwa kufuata mpango wa marejesho ya mkopo huo; na (c) ufuatilia Dhamana ya Serikali na hatimiliki ili kuweza kulinda mkopo huo.**

### iii) Mapungufu katika Usimamizi wa Madai ya Michango ya Wanachama shilingi trilioni 1.18

Nilibaini Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi ilikuwa na kiasi inachodai kwa wanachama shilingi trilioni 1.06 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, huku mwaka wa fedha uliopita 2022/23 madai ya michango yalikuwa shilingi bilioni 710. Ukaguzi wangu zaidi ulibaini kuwa shilingi bilioni 582.63 (sawa na asilimia 55) kati ya shilingi trilioni 1.06 zilikuwa hazijalipwa kwa zaidi ya miezi 12.

Zaidi, ukaguzi ulibaini uwepo wa kiasi cha shilingi bilioni 63.98 ambacho kilikuwa hakijapokelewa kutoka kwa wadaiwa 14 kati ya 3712 wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (Rejea **Jedwali Na. 45**). Jambo hilo limesababishwa na usimamizi hafifu wa utekelezaji wa sheria ya pensheni. Kutokusanywa kwa michango kuna athiri ukwasi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

**Jedwali Na. 45: Orodha ya wadaiwa ambao michango yao haijawasilishwa**

| Na | Jina la Shirika | Kiasi cha Fedha Shs.'000 |
|---|---|---|
| 1 | Shirika la Reli la Tanzania na Zambia | 10,771,884 |
| 2 | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | 9,201,138 |
| 3 | SUMA JKT Guard Limited | 8,816,085 |
| 4 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | 8,406,302 |
| 5 | Shirika la Posta Tanzania | 5,350,051 |
| 6 | Shirika la Usafirishaji Dar es Salaam | 5,263,131 |
| 7 | Wakala wa Menejimenti ya UDA | 4,249,404 |
| 8 | Shirika la Taifa la Maendeleo | 1,221,958 |
| 9 | Idara ya Mahakama | 1,255,578 |

| | | |
|---|---|---|
| 10 | Shirika la Umeme Tanzania | 2,928,972 |
| 11 | Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania | 2,177,660 |
| 12 | Mamlaka ya Bandari Tanzania | 1,670,361 |
| 13 | Chuo cha Teofilo Kisanji | 1,353,827 |
| 14 | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi | 1,316,669 |
| **Jumla** | | **63,983,020** |

**Chanzo:** *Ripoti ya wadaiwa wa Mfuko ya tarehe 30 Juni 2024*

Pia nilibaini kuwa katika Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi kulikuwa na michango kutoka kwa wanachama ambayo haikuwa imekusanywa ya shilingi bilioni 56.48 ikilinganishwa na madeni ya mwaka uliopita 2022/23 ya shilingi bilioni 46.07. Ukaguzi wangu zaidi ulibaini kuwa shilingi bilioni 40.44 sawa na asilimia 87 kati ya shilingi bilioni 56.48 zilikuwa hazijalipwa kwa zaidi ya miezi 12.

Jambo hili limesababishwa na utekelezaji usioridhisha wa sheria ya pensheni. Kutokusanywa kwa michango inayostahiki kuna athiri ukwasi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

**Ninapendekeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Mfuko wa Taifa** wa **Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi waendelee kuwasiliana na wanachama na kuwahimiza kusaini hati za malipo ambazo zinajumuisha mpango wa malipo ya michango ambayo haijalipwa kwani mbinu hii itahakikisha ahadi ya wanachama kulipa madeni yao kwa utaratibu uliowekwa.**

### iv) Ukusanyaji Usioridhisha wa Kodi ya Pango katika Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi shilingi bilioni 19.57

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi ulikuwa na kodi ya pango inayodaiwa kiasi cha shilingi bilioni 23.87. Tathmini yangu ya ukaguzi kutoka katika ripoti ya madai ilibainisha kuwa shilingi bilioni 19.57 (sawa na asilimia 82) zilikuwa ni madai yenye umri wa zaidi ya miezi 12 wakati shilingi bilioni 4.30 yalikuwa na umri chini ya miezi 12. Mapitio ya nyaraka za madai yalithibitisha kuwa kati ya shilingi bilioni 23.87 kiasi cha shilingi bilioni 4.83 yanadaiwa mashirika ya Serikali huku shilingi bilioni 15.54 zikitokana na aidha watu waliofariki, kusitisha au kufungwa kwa biashara, wakati shilingi bilioni 3.50 zikitokana na wapangaji ambao bado wanaendelea na shughuli zao katika majengo ya mfuko.

Ninashaka na ulipwaji wa kodi ya jumla ya shilingi bilioni15.54 ambayo inadaiwa kutoka kwa wadaiwa ambao inaonesha ama wamefariki au

kufunga biashara. Hali hii inaashiria hatari ya kutokusanywa kwa kodi hiyo na inaonesha upungufu wa utaratibu wa ufuatiliaji. Zaidi ya hayo, sehemu kubwa ya michango hiyo inakosesha Mfuko fedha ambazo zingeweza kuwekezwa kwenye fursa zingine za kiuchumi.

**Ninapendekeza kuwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi uhakikishe vifungu katika mikataba ya ukodishaji vinatekelezeka na kuweka mikakati madhubuti na thabiti ya ukusanyaji ili kuhakikisha ukusanyaji wa kodi unafanyika kwa wakati.**

### 14.2.3 Upungufu wa Huduma Zinazotolewa kwa Wanachama wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi

#### (i) Ucheleweshaji wa Kushughulikia Madai kwa Walengwa kwa Zaidi ya siku 60 kutoka kwa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi Uliohusisha shilingi milioni 262.70

Nilipitia sampuli ya madai yapatayo 28 na kubaini madai 23 (sawa na asilimia 82) yalikuwa yamecheleweshwa kwa wastani wa siku 82, kinyume na Aya ya 4.0 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Madai ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, 2022 ambayo inataka mchakato wa uthibitishaji ukamilike ndani ya siku 30 kwa madai ya ajali na magonjwa, na siku 60 kwa madai ya kifo.

Zaidi ya hayo, mapitio yangu ya taarifa za fedha za Mfuko kwa mwaka wa fedha 2023/24 yalibaini ucheleweshaji mkubwa wa malipo ya mafao ya fidia ya wafanyakazi. Nilibaini uwepo wa wadai 22 wenye madai ya shilingi milioni 58.06 ambao madai yao yalibaki bila kulipwa kwa muda wa zaidi ya miezi 24 huku madai 148 ya shilingi milioni 204.64 yalikuwa yana zaidi ya miezi 12, jumla ya madai yote ya shilingi milioni 262.70 upembuzi wake ulizidi siku 30 zinazokubaliwa.

Suala hili limechangiwa na ucheleweshaji wa uwasilishaji nyaraka za madai zinazohitajika na ufuatiliaji duni wa Afisa anayehusika. Malipo yanayocheleweshwa huwanyima walengwa uwezo wa kupata fidia kwa wakati, jambo ambalo linaweza kusababisha matatizo ya kifedha kwa wafanyakazi na familia zao, na hivyo kuzidisha athari za kijamii na kiuchumi za wagonjwa na majeruhi walioumia kazini.

**Ninapendekeza Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi uimarishe na kuanzisha utaratibu thabiti ili kuhakikisha walengwa wanahudumiwa kwa wakati kwa kuboresha mchakato wa uthibitishaji wa ndani wa madai.**

### 14.2.4 Malipo ya Huduma za Bima ambayo Hayakukusanywa kutoka kwa Wanachama ya Jumla ya shilingi bilioni 66.46

Nilibaini kuwa Shirika la Bima la Taifa liliripoti madeni ya bima ambayo hayakulipwa ya shilingi bilioni 66.46 ikilinganishwa na shilingi bilioni 61.95 za mwaka 2022/23 hivyo kupelekea ongezeko la shilingi bilioni 4.51 sawa na asilimia 7.28. Ukaguzi ulibaini kuwa shilingi bilioni 41.45 (sawa na asilimia 62) zilikuwa hazijalipwa kwa zaidi ya miezi 12. Mapato ya jumla yanajumuisha shilingi bilioni 18.10 (sawa na asilimia 27) kutoka taasisi za Serikali na shilingi bilioni 48.35 (sawa na 73) kutoka kwa taasisi na watu binafsi. Aidha, Shirika la Bima la Taifa lilitoza ada za bima zenye thamani ya shilingi bilioni 39.24 kwa wateja binafsi na Serikali ambao walikuwa wanadaiwa shilingi 14.39, na kupelekea deni kufikia shilingi bilioni 53.63 hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024 kutoka kwa wateja waliokopeshwa bila kumaliza malipo yao ya awali.

Ucheleweshaji wa kukusanya michango inayopokelewa huathiri ukwasi na uwezo wa Mfuko wa Bima ya Taifa wa kutimiza ahadi zake za faida zinazoiva.

**Ninapendekeza Shirika la Bima la Taifa lifuatilie kwa karibu madeni ambayo hayajalipwa ili kuhakikisha ukusanyaji wake kwa wakati, jambo ambalo litaboresha mzunguko wa fedha na kutoa fursa kwa uwekezaji zaidi.**

## 14.3 Changamoto za Kiutendaji wa Kampuni Tanzu na Vitega Uchumi vya Mifuko ya Hifadhi za Jamii

Mifuko ya Hifadhi za Jamii inakabiliwa na changamoto za kiutendaji ambapo nimebain kuwepo kwa utendaji duni wa kampuni tanzu kutokana na uwekezaji wake. Kampuni tanzu hizo ni Pamoja na Kampuni ya Mkulazi, Kampuni ya Sisalana Tanzania, Kampuni ya Ubungo Plaza na Kampuni ya Miliki ya Msamvu.

### 14.3.1 Uwekezaji katika Kampuni Tanzu wa shilingi bilioni 161.53 ambao Hauzalishi Faida

Nilibaini kuwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma ulikuwa na vitega uchumi vinane vyenye thamani ya shilingi bilioni 161.53 ambavyo havikuleta faida yoyote kwa Mfuko kwa kipindi cha wastani wa kuanzia mwaka mmoja hadi miaka saba. Hali hii inakinzana na Kifungu cha 9 cha Mwongozo wa Uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya Benki Kuu, 2021 ambacho kinataka uwekezaji

wowote kuwa na faida zaidi ya ile inayoweza kupatikana endapo kiasi hicho kingewekwa kwenye amana za Serikali katika vipindi sawa.

Pia, nilibaini kuwa sera ya uwekezaji ya Mfuko haioneshi muongozo wa kujitoa kwenye uwekezaji pale itakapobainika uwekezaji huo hauna faida na manufaa kwa Mfuko. Kukosekana kwa mapato hayo kunatokana na Mfuko kuwekeza kwenye makampuni yanayoanza kufanya biashara, ambayo huchukua muda mrefu kuleta faida, hali inayoweza kusababisha upotevu wa fedha na kushindwa kurejesha mtaji uliowekezwa (Rejea **Jedwali Na. 46).**

**Jedwali Na. 46: Orodha ya vitega uchumi visivyozalisha mapato**

| Na | Jina la Kitega Uchumi | Aina ya uwekezaji | Tarehe ya uwekezaji | Jumla ya uwekezaji (Sh. '000) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kampuni ya Majengo ya Biashara ya Jiji la Mwanza | Kampuni tanzu | 22-Oktoba-17 | 72,000,000 |
| 2 | Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro | Kampuni tanzu | 22-Januari-20 | 59,960,100 |
| 3 | Kampuni ya Miliki ya Msamvu | Kampuni tanzu | 01-Mei-23 | 15,319,286 |
| 4 | Ranchi ya Nguru | Kampuni Mshirika | 31-Desemba-17 | 2,980,000 |
| 5 | Mamba Miyamba Ginger Co. Ltd | Kampuni Tanzu | 21-Juni-17 | 6,700,000 |
| 6 | Tanzania Mechantile Exchange | Kampuni Mshirika | 09-Aprili-20 | 1,000,000 |
| 7 | Kampuni ya Mponde | Kampuni Mshirika | 17-Mei-21 | 2,075,000 |
| 8 | Tanzania Pharmaceutical Industries | Hisa Zisizoorodheshwa | 16-Januari-17 | 1,500,000 |
| | | | **Jumla ya uwekezaji** | **161,534,386** |

**Chanzo**: *Orodha za uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2023/24*

Mfuko ulikiri uwepo wa ucheleweshwaji na changamoto katika uwezeshwaji wa kampuni tanzu hata hivyo, ulisisitiza juu ya manufaa ya muda mrefu ya kijamii na kiuchumi na kuahidi kuimarisha usimamizi wa karibu, kuweka mtaji mpya, na kuangalia biashara upya. Zaidi ya hapo walieleza kuwa baadhi ya miradi inakaribia kukamilika, huku mingine ikiwa inakaguliwa ili kufilisiwa au kujiondoa. Aidha walieleza kuwa Kampuni ya Msamvu ilianzishwa kwa ajili ya kuendesha kituo cha mabasi cha Msamvu mkoani Morogoro ambapo Mfuko unamiliki asilimia 60 ya hisa za kampuni hiyo huku asilimia 40 ikimilikiwa na Manispaa ya Morogoro. Hata hivyo, shughuli za kituo cha mabasi cha Msamvu zilikabidhiwa kwa Halmashauri ya Manispaa ya

Morogoro tarehe 1 Machi 2020 chini ya maelekezo ya Serikali kuwa Serikali itarejesha fedha hizo za Mfuko kama fidia. Hata hivyo, hadi tarehe 30 Juni 2024 hakuna fedha zilizokuwa zimerudishwa na Serikali.

**Ninapendekeza Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (a) uboreshe sera ya uwekezaji na ijumuishe mkakati wa Mfuko kujiondoa kwenye uwekezaji usiokuwa na tija, na (b) uendelee kufuatilia fidia kutoka serikalini kuhusiana na uwekezaji katika Kampuni ya Msamvu.**

### 14.3.2 Usimamizi Duni wa Uendeshaji na Uzalishaji katika Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi

Katika mwaka 2023/24, Malengo ya uzalishaji ya Kampuni ya Mkulazi hayakufikiwa kwa kiasi kikubwa. Kampuni ililenga kuzalisha tani 21,895 za sukari lakini ilizalisha tani 1,754 tu, na kusababisha upungufu wa tani 19,814 sawa na asilimia 92. Pia, Kampuni ililenga kuzalisha tani 7,888 za molasisi lakini ilizalisha tani 2,340 tu, hivyo tani 5,548 sawa na asilimia 50 hazikuzalishwa. Pia, Kampuni iliweza kusaga tani 42,928 tu kati ya 202,917 zilizolengwa, hivyo tani 159,989 sawa na asilimia 79 hazikusagwa. Vilevile, kampuni ilipanga kupanda hekta 624 za miwa lakini iliweza kupanda hekta 300 tu (pungufu ya asilimia 52 ya kilichopangwa).

Utunzaji duni wa mazao ulichangia kudorora, kwani ni hekta 7,595 tu ndizo zilitunzwa kati ya hekta 25,043 zilizopangwa sawa na upungufu wa asilimia 70 **(**Rejea **Jedwali Na. 47).**

**Jedwali Na. 47: Maelezo ya shughuli zilizopangwa dhidi ya utendaji halisi**

| Aina | Kilichopangwa | Utendaji halisi | Upungufu | Upungufu kwa asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Tani za uzarishaji wa sukari | 21,895 | 1,754 | 19,814 | 92 |
| Tani za uzalishaji ya molasisi | 7,888 | 2,340 | 5,548 | 50 |
| Tani za miwa iliyosagwa | 202,917 | 42,928 | 159,989 | 79 |
| Hekta za miwa iliyopandwa | 624 | 300 | 324 | 52 |
| Hekta za shamba lilishoghulikiwa | 25,043 | 7,595 | 17,450 | 70 |

**Chanzo**: *Ripoti ya utekelezaji wa mipango ya Kampuni ya Mkulazi ya 2023/24*

Pia nilibaini mapungufu katika uvunaji wa miwa, huku ukataji wa miwa ukicheleweshwa kwa zaidi ya miezi 12 inayotakiwa, na hivyo kusababisha miwa kukomaa kupita kiasi na kupungua kwa ubora wake

wa kuzalisha sukari. Baadhi ya mashamba yalivunwa kati ya miezi 13 na 32, na kusababisha hasara kubwa ya ubora na mavuno. Zaidi ya hayo, Kampuni ya Mkulazi haina sera rasmi ya mauzo au mkakati wa bei ya sukari na molasisi, na hivyo kuongeza hatari ya namna ya upangaji wa bei ya kuuza sukari.

Mapungufu haya yanatokana na uwiano mbaya kati ya shughuli za ununuzi na mahitaji ya uzalishaji, mipango isiyoridhisha ya usafirishaji na uwezo mdogo wa ghala za kuhifadhi bidhaa. Kushindwa kufikia malengo ya uzalishaji huathiri vibaya kuridhika kwa wateja kutokana na utendaji wa Kampuni na kupelekea kudhoofika kwa uthabiti wa kifedha kwa Kampuni huku kukiongeza gharama za uendeshaji.

**Ninapendekeza kuwa Kampuni ya Mkulazi; Ikamilishe haraka mkakati wa uuzaji wa bidhaa za miwa na uidhinishwe na Bodi ya Wakurugenzi kabla ya kuanza kutumika; Iimarishe uratibu wa ugavi kwa kuoanisha ratiba za uvunaji na mahitaji ya kiwandani; na Itekeleze mifumo ya hali ya juu ya ugavi, kama vile mfumo wa ufuatiliaji unaojulikana kama GPS, ili kupunguza ucheleweshaji.**

### 14.3.3 Kushindwa Kufikiwa kwa Malengo Yaliyopangwa Katika Mpango wa Biashara wa Kampuni ya Ubungo Plaza

Mpango wa Biashara wa Kampuni ya Ubungo Plaza uliweka malengo ya kuridhika kwa wateja kuwa asilimia 95 kwa kipindi cha mwaka 2019/2020 hadi 2022/23, lakini mafanikio halisi yalikuwa kati ya asilimia 67 hadi 75. Vile vile, lengo la kukodisha jengo liliwekwa kati ya asilimia 85 na 96, wakati upangaji halisi ulianzia asilimia 43 hadi 51. Aidha, mwaka 2023/24, mapato ya bajeti ya kampuni yalikadiriwa kuwa shilingi bilioni 4.59 huku mapato halisi yalikuwa shilingi bilioni 2.12, na kupelekea kutofikia lengo kwa shilingi bilioni 2.47 (sawa na asilimia 54). Jambo linalochangia kwa utendajikazi huu duni ni kiwango cha juu cha eneo la upangaji kuwa wazi kwa asilimia 43.51 na kupelekea kukodishwa kwa takribani kilomita za mraba zipatazo 25,489 ambazo zilibaki wazi kwa zaidi ya miaka mitatu.

Menejimenti ilieleza kuwa mchakato wa kumpata muwekezaji wa kuendesha hoteli uko katika hatua zake za mwisho, ikisubiri idhini ya bodi. Huku nafasi inayoendelea kuwa wazi bila wapangaji siyo tu inaathiri mapato ila pia  huongeza gharama za uendeshaji wa Kampuni ya Ubungo Plaza, ikiwa ni pamoja na matengenezo, huduma, na ulinzi. Hali hii inaathiri vibaya faida na uendelevu wa kampuni.

Napendekeza Kampuni ya Ubungo Plaza (a) iharakishe mchakato wa kuwashirikisha waendesha hoteli ili kuifanya Ubungo Plaza kuwa hai na kuingiza mapato kwa wanahisa; na (b) ianzishe kampeni ya promosheni ili kufikia wapangaji watarajiwa na hii inaweza kujumuisha kutangaza kwa njia ya kidijitali, kufanya kazi na Mawakala au kutoa motisha kwa kuingia makubaliano ya awali na wapangaji.

# Mapitio Katika Sekta ya Utalii



# SURA YA KUMI NA TANO

# MAPITIO KATIKA SEKTA YA UTALII

## 15.0 Utangulizi

Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuanzia mwaka 2021/22 hadi 2025/26 unatanabaisha kuwa Serikali imelenga kuongeza idadi ya watalii wanaokuja nchini kutoka watalii 1,527,230 waliokuja nchini mwaka 2019/20 hadi watalii 5,000,000 ifikapo mwaka 2025 ambao wanatarajiwa kuiingizia nchi Dola za Marekani zipatazo bilioni sita. Kwa mujibu wa Taarifa ya Takwimu ya Maliasili ya tarehe 31 Disemba 2024, watalii wa kimataifa walioingia nchini mwaka 2024 walikuwa 2,141,895 sawa na ongezeko la watalii 333,690 ikilinganishwa na watalii wa kimataifa wapatao 1,808,205 walioingia nchini mwaka 2023. Sekta ya utalii iliingiza Dola za Marekani bilioni 3.37 mwaka 2023 na Dola za Marekani bilioni 3.9 kwa mwaka 2024 kutoka kwa watalii wa kimataifa, ikiwa ni ongezeko la Dola za Marekani bilioni 0.53 (sawa na asilimia 16).

Sura hii inaangazia changamoto zinazoikabili Sekta ya Utalii, ikijumuisha Mamlaka ya Hifadhi za Taifa, inayosimamia hifadhi za taifa 21; Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro inayosimamia maeneo matatu ambayo ni Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro, Pori la Akiba la Poloreti pamoja na hifadhi ya kumbukumbu ya mambo kale ya Olduvai Gorge; na Bodi ya Utalii Tanzania ambayo imepewa jukumu la kutangaza, kukuza na kuendeleza masuala yote ya sekta ya utalii, nchini Tanzania.

Katika ukaguzi nilibaini kuwa Sekta ya Utalii inakabiliwa na changamoto zinazozorotesha mfumo wa ikolojia wa hifadhi za Taifa, na changamoto zinazozorotesha shughuli za utangazaji wa utalii. Changamoto hizo ni pamoja na miundombinu duni katika hifadhi za taifa, ufinyu wa bajeti za miradi ya maendeleo, kukosekana kwa huduma za mtandao wa intaneti kwa uhakika katika Hifadhi za Taifa, wananchi kuvamia maeneo ya Hifadhi za Taifa; kuota, kuenea na kusambaa kwa mimea vamizi; na uthibiti hafifu wa taka ngumu ndani ya Hifadhi za Taifa.

## 15.1 Ufinyu wa Bajeti ya Kujenga na Kuendeleza Miundombinu Ndani ya Hifadhi za Taifa

Katika ukaguzi wa usimamizi na uendelezaji wa miundombinu ya Hifadhi za Taifa nilibaini kuwa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa Tanzania ilipokea shilingi bilioni 1.06 kati ya shilingi bilioni 23.03 zilizoidhinishwa kwa ajili ya ujenzi na uendelezaji wa miundombinu ya hifadhi kwa mwaka wa fedha 2023/24. Kiasi cha shilingi bilioni

21.97 hakikutolewa ikiwa ni asilimia 95 ya bajeti iliyoidhinishwa, licha ya juhudi za Mamlaka kufuatilia kwa Serikali (Rejea **Jedwali Na. 48).**

**Jedwali Na. 48: Maelezo ya bajeti iliyoidhinishwa dhidi ya kilichotolewa na Serikali**

| Na. | Jina la Hifadhi ya Taifa | Kiasi cha bajeti Sh.'000 | Kiasi kilichotolewa Sh.'000 | Kiasi ambacho hakikutolewa Sh.'000 | Asilimia ya kiasi ambacho hakikutolewa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Serengeti | 4,063,752 | 750,066 | 3,313,686 | 82 |
| 2 | Katavi | 2,341,612 | 0 | 2,341,612 | 100 |
| 3 | Kilimanjaro | 2,948,454 | 0 | 2,948,454 | 100 |
| 4 | Manyara | 565,334 | 0 | 565,334 | 100 |
| 5 | Mikumi | 570,567 | 0 | 570,567 | 100 |
| 6 | Nyerere | 1,961,862 | 270,961 | 1,690,901 | 86 |
| 7 | Ruaha | 2,888,094 | 0 | 2,888,094 | 100 |
| 8 | Mkomazi | 857,072 | 0 | 857,072 | 100 |
| 9 | Burigi | 2,181,826 | 0 | 2,181,826 | 100 |
| 10 | Tarangire | 2,624,274 | 0 | 2,624,274 | 100 |
| 11 | Saadani | 448,384 | 0 | 448,384 | 100 |
| 12 | Arusha | 1,585,228 | 39,000 | 1,546,228 | 98 |
| | **Jumla** | **23,036,459** | **1,060,027** | **21,976,432** | **95** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa ya Mwaka wa Fedha 2023/24*

Ukosefu wa fedha za maendeleo ulisababisha kuchelewa kukamilika kwa miradi ya maendeleo 15 (Rejea **Jedwali Na. 49),** yenye thamani ya shilingi bilioni 14.12 inayotekelezwa na Hifadhi za Taifa 10, ucheleweshwaji huo ulianzia miezi 10 hadi 33.

**Jedwali Na. 49: Miradi iliyochelewa**

| Jina la Hifadhi ya Taifa | Jina la Mradi | Gharama kulingana na mkataba Sh '000 | Kiasi Kilicholipwa hadi Juni 2024 Sh. '000 |
|---|---|---|---|
| Serengeti | Ujenzi wa mageti changamani kwa ajili ya kukusanya mapato katika eneo la Machochwe na Kleins | 4,165,140 | 1,338,720 |
| Katavi | Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Ikuu | 564,820 | 147,660 |
| Mikumi | Ukarabati wa nyumba za wafanyakazi Kikoboga | 71,000 | 0 |
| Nyerere | Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi Kalulu | 164,450 | 64,080 |
| Ruaha | Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi Tungamalenga | 1,150,970 | 945,010 |
| Burigi-Chato | Ukarabati wa barabara kutoka madaraja 6 hadi Ruiza yenye kilomita 30 kwenye Hifadhi ya Burigi Chato | 218,060 | 74,060 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Arusha | Mradi wa Umeme wa Maji – malipo kwa mkandarasi na ununuzi na usimikaji wa kidhibiti mzigo cha kidijitali (digital load control) na kidhibiti joto (heater ballast load) | 550,680 | 0 |
| Tarangire | Ujenzi wa geti changamani kwa ajili ya kukusanya mapato katika eneo la Mamire, na Ujenzi wa daraja la Matete katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire | 5,119,890 | 3,404,800 |
| Saadani | Ujenzi wa choo cha umma katika ufukwe wa Saadani; Kukamilisha njia, mandhari na kasoro katika bweni la vijana; Ukarabati na matengenezo ya saketi za utalii na upanuzi wa eneo la kulia chakula na jikoni | 331,900 | 0 |
| Kilimanjaro | Ujenzi wa nyumba tatu za wageni katika eneo la kupumzika la Horombo | 1,790,020 | 1,665,920 |
| **Jumla** | | **14,126,930** | **7,640,250** |

***Chanzo:*** *Faili la miradi na uhakiki wake*

Aidha, nilifanya mapitio ya Mpango wa Mwaka wa Matengenezo ya barabara kwa mwaka wa fedha 2023/24 na kubaini Hifadhi za Taifa 12 zenye mtandao wa barabara wa kilomita 25,683.9. Hifadhi hizo ni Serengeti, Katavi, Ziwa Manyara, Mikumi, Nyerere, Ruaha, Burigi, Arusha, Tarangire, Mkomazi, Saadani na Kilimanjaro. Mamlaka ilipanga kufanya matengenezo ya kilomita 6,712.2 kati ya kilomita 25,683.9 hata hivyo iliweza kutengeneza kilometa 4,022 sawa na asilimia 60 ya lengo huku kilomita 2,690.2 (sawa na asilimia 40) hazikutengenezwa kutokana na kutopata fedha kutoka serikalini. Pamoja na kutotolewa kwa fedha za maendeleo, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 637.60 katika mwaka wa fedha 2023/24 kwaniaba ya Mamlaka ya Hifadhi za Taifa na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, ambapo shilingi bilioni 410.90 zilikusanywa kutoka Mamlaka ya Hifadhi za Taifa na shilingi bilioni 226.70 kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro.

Katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, tathmini yangu ya utekelezaji wa bajeti ya miundombinu kwa mwaka wa fedha 2023/24 ilibaini kuwa shilingi bilioni 28.61 ziliidhinishwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo ambayo ilijumuisha miradi nane, ikiwamo barabara, maji, vibanda vya walinzi na mageti ya kuingilia na kutoka. Hata hivyo, kiasi hicho hakikutolewa na Serikali.

Hali hii ikiendelea hivi, itasababisha kuzorota kwa miundombinu inayosaidia huduma za utalii, itaathiri ukuaji wa utalii, itatatiza utoaji wa huduma, na hatimaye kupunguza mapato kwa Serikali.

**Ninapendekeza Serikali izipe kipaumbele Hifadhi za Taifa na maeneo ya hifadhi kwa kuzipa fedha za kutosha zinazohitajika kusaidia shughuli za ujenzi na undelezaji wa miundombinu ya ndani ya Hifadhi za Taifa.**

## 15.2 Ufinyu wa Bajeti ya Kukuza na Kutangaza Utalii wa Ndani na Kimataifa

Mapitio yangu ya bajeti ya kukuza soko la utalii inayofanywa na Bodi ya Utalii Tanzania yalibainisha kuwa mwaka wa fedha 2023/24 bajeti ya Bodi ilikuwa shilingi bilioni 4.95 kwa ajili ya kukuza masoko ya ndani na nje ya Nchi. Hata hivyo, Serikali ilitoa shilingi bilioni 3.40 (sawa na asilimia 69) huku shilingi bilioni 1.55 hazikutolewa, sawa na asilimia 31.

Vilevile, nilibaini kuwa Bodi ya Utalii ilipanga kushiriki katika maonesho yapatayo 212 kwa ajili ya kutangaza utalii wa kimataifa na wa ndani kama sehemu ya mkakati wake wa masoko kwa vivutio vya utalii. Hata hivyo, kutokupatikana kwa fedha zote zilizoidhinishwa kwa lengo hilo kulipelekea Bodi ya Utalii kushiriki katika maonesho 103 sawa na asilimia 48 kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 50**.

**Jedwali Na. 50: Maelezo ya maonesho yaliyopangwa kufanyika na yaliyofanyika**

| Na | Malengo ya Mwaka 2023/24 | Mafanikio ya kilichofanyika | Asilimia ya mafanikio |
|---|---|---|---|
| 1 | Maonesho 40 ya kimataifa ya utangazaji wa utalii | Maonesho 20 kati ya 40 ndiyo yaliweza kufanyika | 50 |
| 2 | Maonesho 4 ya kimataifa ya utangazaji wa utalii wa uwindaji | Maonesho mawili kati ya manne ya utangazaji wa utalii wa uwindaji yaliweza kufanyika | 50 |
| 3 | Kampeni 36 za kutangaza utalii | Zilifanyika kampeni 13 kati ya 36 zilizopangwa | 36 |
| 4 | Maonesho 36 ya utangazaji wa utalii wa ndani | Yalifanyika maonesho 17 kati ya 36 ya kutangaza utalii wa ndani | 47 |
| 5 | Maonesho 12 ya Biashara ya Utalii wa Kitamaduni | Yalifanyika maonesho 10 kati ya 12 ya Biashara ya Utalii wa Kitamaduni | 83 |
| 6 | Mikutano, vivutio na maonesho yapatayo 75 | Mikutano, vivutio na maonesho 36 kati 75 yaliweza kufanyika | 48 |
| 7 | Kushiriki katika tafiti 4 za soko la utalii | Tafiti moja ilifanyika | 25 |
| 8 | Mikutano 5 ya wadau kuhusu maendeleo na utangazaji wa utalii | Mikutano minne 4 kati ya mitano ya wadau ilifanyika | 80 |

**Chanzo:** *Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Bodi ya Utalii Tanzania 2023/24*

Matumizi bora ya maonesho ya utalii wa kimataifa na ule wa ndani yana mchango mkubwa katika kutangaza vivutio vya utalii vya Tanzania na matokeo yake yanaweza kuongeza mapato ya Serikali na kuongeza watalii wanaokuja nchini.

**Ninapendekeza kuwa Bodi ya Utalii, kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, ifuatilie mara kwa mara Wizara ya Fedha ili kuhakikisha inatoa kwa wakati fedha zilizoidhinishwa za utangazaji wa utalii kwa maonesho yaliyopangwa.**

## 15.3 Changamoto za Mtandao wa Intaneti katika Hifadhi za Taifa Zinazoathiri Shughuli za Utalii

Nilibaini ucheleweshaji wa kutatua changamoto za mtandao wa intaneti kwenye Hifadhi za Taifa na kupelekea changamoto hizo kuchukua muda wa saa moja hadi 49 bila utatuzi hasa kwenye Hifadhi za Taifa za Serengeti, Mikumi na Saadani. Ucheleweshaji huu ulichangiwa zaidi na kutokuwepo kwa ufuatiliaji wa kutosha na kutokufanya malipo kwa wakati kwa watoahuduma.

Mtandao wa intaneti usiyo thabiti unaathiri uwezo wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa kufanya kazi kwa ufanisi na kuathiri taswira za watalii kutokana na kuchelewesha ukataji wa vibali vyao kwa ajili ya kuingia au kutoka hifadhini.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Hifadhi za Taifa ishirikiane na Wizara ya Fedha kuweka kipaumbele katika utoaji wa fedha kwa watoa huduma, kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa mtandao wa intaneti ili kusaidia ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za utalii.**

## 15.4 Uvamizi unaofanywa na Wananchi kwenye Mipaka na Maeneo Tenganishi ya Hifadhi za Taifa

Kifungu cha 74 cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ya mwaka 2022 kinakataza shughuli za binadamu, makazi au maendeleo ndani ya mita 500 kutoka maeneo ya hifadhi bila kibali cha Mkurugenzi wa Hifadhi za Taifa.

Nilibaini uvamizi mkubwa wa vijiji 54 vilivyo ndani ya hifadhi huku vijiji 163 viko ndani ya mita 500 ya mipaka ya hifadhi. Hifadhi hizo ni: Serengeti, Katavi, Ziwa Manyara, Mikumi, Nyerere, Ruaha, Burigi, Arusha, Tarangire, Kilimanjaro, Mkomazi, na Saadani. Uvamizi huu unatokana na kutofanyika tafiti ili kutathmini viwango vya uvamizi na

kuchelewa kuchukua hatua stahiki. Wananchi wa vijiji hivyo wanajishughulisha na shughuli zisizo za utalii kama vile kilimo, makazi ya watu, na ufugaji.

Kushindwa kudhibiti maeneo ya mipaka ya hifadhi husababisha uharibifu wa ikolojia, uchafuzi wa mazingira na kuchochea kuenea kwa mimea vamizi kunatarisha bayoanuwai na mfumo wa ikolojia. Pia, huongeza migogoro kati ya Serikali na jamii zinazovamia mipaka ya hifadhi.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (a) ifanye utafiti kwa hifadhi zote za taifa ili kuweza kubaini vijiji vilivyovamia hifadhi na vile ambavyo vimevamia mipaka ya maeneo ya hifadhi, (b) ishirikiane na Serikali kuvihamisha vijiji hivi kutoka katika maeneo ya hifadhi kwa gharama zao wenyewe, na (c) ibuni programu ya mafunzo kwa ajili ya kuendesha na kuelimisha jamii ili kuongeza uelewa wao kuhusiana na uhifadhi, ushirikiano na wadau, na matumizi mazuri ya ardhi.**

## 15.5 Usimamizi Hafifu wa Udhibiti wa Taka Ngumu Katika Hifadhi za Taifa

Lengo C-6-4 la Mpango Mkakati wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa wa mwaka 2022 hadi 2026 linataka asilimia 100 ya aina zote za taka zinazoingizwa na watalii au zinazozalishwa zinakusanywa na kutupwa ipasavyo kwenye maeneo yaliyoidhinishwa huku ikiwa ni takwa la kila mwaka.

Nilibaini kuwa Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara na Hifadhi ya Taifa ya Mikumi zilipanga kukusanya taka ngumu za kilo 3,264, hata hivyo, zilikusanya kilo 1,512 (sawa na asilimia 46 ya lengo lilokusudiwa), hali hii ilitokana na usimamizi hafifu wa mpango wa udhibiti taka ngumu, na ufinyu wa bajeti ambapo mwaka wa fedha 2023/24 bajeti ya Mamlaka ya usimamizi na ukusanyaji wa taka ngumu ilikuwa shilingi milioni 18.36 na kiasi kilichopokelewa ni shilingi milioni 10.77 na kiasi ambacho hakikutolewa ni shilingi milioni 7.59 sawa na asilimia 41.

Usimamizi duni wa taka ngumu katika Hifadhi za Taifa unachangia upotevu wa bayoanuwai, uharibifu wa mfumo wa ikolojia, na kuenea kwa magonjwa miongoni mwa wanyamapori.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Hifadhi za Taifa iweke mpango wa kina wa usimamizi wa taka ngumu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha inatenga fedha za kutosha kwa ajili ya usimamizi wa taka ngumu ndani Hifadhi za Taifa.**

## 15.6 Kusambaa na Kuongezeka kwa Kasi kwa Mimea Vamizi Zaidi ya Uwezo wa Hifadhi Kudhibiti

Licha ya kuripoti kwa miaka mitano mfululizo kuhusiana na mimea vamizi, suala hilo bado halijatatuliwa kutokana na kutokuwepo kwa hatua za kutosha za kukabiliana na hali hiyo. Katika mwaka wa fedha 2022/23 Mamlaka ya Hifadhi za Taifa ilipanga kung'oa na kuondoa mimea vamizi kutoka katika hekta zipatazo 3,384.22 katika Hifadhi 15, hata hivyo, Mamlaka ilifanikiwa kung'oa na kuondoa katika hekta 2,352.53 tu ya lengo lililopangwa (sawa na asilimia 69.50). Pia, Mamlaka ya Hifadhi za Taifa ilifanya utafiti kwenye hifadhi nyingine mbili za Kilimanjaro na Burigi-Chato na kubaini hekta 507.01 zilikuwa zimeathirika na mimea vamizi.

Huku mwaka wa fedha 2023/24 Mamlaka ililenga kungóa na kundoa mimea vamizi kutoka katika hekta zipatazo 16,734.3 lakini iliweza kungóa hekta 1,311.26 tu (sawa na asilimia 18 ya lengo), na kuacha hekta 15,423.04 (sawa na asilimia 72). Mimea vamizi huhatarisha mifumo ya ikolojia ya hifadhi kwani baadhi ni sumu, huondoa mimea asilia na malisho na pia mimea vamizi hailiwi na wanyamapori.

**Kwa hiyo, ninarudia pendekezo langu kuwa Serikali kutangaza tatizo la mimea vamizi kuwa suala la kitaifa na kuhakikisha wadau wa ngazi zote wanahusishwa ili kuchukua hatua za kuondoa, kudhibiti na kuzuia kuwapo kwa mimea hiyo ndani ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, katika hifadhi zingine za taifa, na katika maeneo mengine kote nchini.**

## 15.7 Maandalizi Hafifu ya Maeneo Teule ya Uwekezaji katika Kuvutia Wawekezaji

Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Hifadhi wa mwaka 2016 hadi 2026 unatoa mamlaka ya utambuzi na ugawaji wa maeneo kwa ajili ya malazi mbalimbali katika Hifadhi za Taifa.

Ukaguzi wangu wa taarifa za utendaji wa utalii za Mamlaka ya Hifadhi za Taifa za mwaka 2023/24 ulibaini kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mikumi ina maeneo 15 yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa nyumba za kulala wageni, kambi za kudumu, kambi za umma na kambi za msimu huku Hifadhi ya Ziwa Manyara ikiwa na maeneo ya aina hiyo yapatayo saba. Hata hivyo, maeneo 11 kati ya 15 ya Hifadhi ya Mikumi yamesalia wazi huku matatu tu yakiwa yameendelezwa na moja liko katika uendelezaji. Vile vile, katika Hifadhi ya Ziwa Manyara maeneo matatu ndiyo yana wawekezaji, huku maeneo manne yakisalia bila kuwa na wawekezaji.

Wakati wa ziara ya ukaguzi, niliona kuwa maeneo haya yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji yanakabiliwa na changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na barabara mbovu, ukosefu wa maji, na kupelekea yasiwe kivutio kwa wawekezaji. Hali hii inatokana na kutopewa vipaumbele vya kutosha katika kutumia fursa zilizopo na uhaba wa fedha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu.

Changamoto hizi za maeneo ya uwekezaji zisipopatiwa ufumbuzi, kuvutia wawekezaji kutabaki kuwa kugumu, na Serikali itaendelea kupoteza mapato.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Hifadhi za Taifa itoe kipaumbele katika uboreshaji wa maeneo ya uwekezaji yaliyoainishwa kwa kushughulikia mapungufu yaliyopo ya miundombinu na maji huku juhudi za kutangaza maeneo hayo zikiongezwa ili kuvutia wawekezaji.**

## 15.8 Usimamizi Hafifu wa Maeneo ya Urithi ya Engaruka, Mumba na Mapango ya Amboni kwa Madhumuni ya Kuvutia Watalii

Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro linasimamia maeneo manne ya urithi wa kitamaduni yaani Engaresero, Engaruka, Kimondo na Mapango ya Amboni ambayo ni mojawapo ya maeneo muhimu ya kiikolojia katika Afrika Mashariki.

Tathmini yangu ya utendaji wa maeneo haya ya kihistoria, ikiwa ni pamoja na usimamizi, mwonekano, na ufikiwaji, ulibaini kuwa Mamlaka imechukuwa jitihada kidogo za kutangaza na kuendeleza vivutio hivyo viweze kuvutia watalii. Aidha, miundombinu muhimu, kama vile barabara, maji, na miundombinu ya kuzuia mafuriko, bado haitoshelezi. Kutokana na hali hiyo, maeneo haya yaliweza kuingiza shilingi milioni 1.53 tu katika kipindi cha miaka mitatu (2021/22 hadi 2023/24), ambacho ni kiashiria tosha kwa kutopewa kipaumbele kwa maeneo hayo.

Kwa mujibu wa maelezo ya menejimenti, maeneo haya ya kitamaduni na mambo kale yalikabidhiwa kwa Mamlaka mwaka 2018 yakiwa hayana miundombinu muhimu ya kusaidia shughuli za utalii. Wakati baadhi ya maboresho yamefanyika, kama vile upatikanaji wa barabara na maji, kasi ya kuyaendeleza imekuwa ndogo kutokana na ufinyu wa bajeti. Aidha mkakati na mbinu zilizopangwa katika kutangaza vivutio hivi bado hazijatekelezwa na kupelekea maeneo hayo kutovutia mashirika yanayoshughulikia watalii na wadau wengine.

Pia, idadi ndogo ya watalii waliotembelea vivutio hivi kwa vile vilipata wageni wapatao 397 tu katika kipindi cha miaka mitano (tangu 2020 mpaka sasa) hivyo kuashiria kutotumika kwao, na hivyo kusababisha upotevu wa mapato na fursa za kiuchumi kwa jamii na wadau. Zaidi ya hayo, kushindwa kuendeleza na kukuza vivutio hivi kunazuia uhifadhi na uoneshaji wa umuhimu wao wa kihistoria na kitamaduni.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (a) itengeneze mkakati wa kina wa uuzaji na ukuzaji wa eneo la Engaruka, Mumba na Mapango ya Amboni utangazaji huo wa utalii utumie njia ya kidijitali, na kuwa na ushirikiano na mashirika yanayojihusisha na usafiri ili kuimarisha vivutio hivyo, na (b) iwekeze katika uboreshaji wa miundombinu, ikiwa ni pamoja na barabara, malazi na maji ili kuongeza taswira nzuri kwa wageni na kuvutia watalii zaidi.**

# Utendaji wa Mamlaka za Maji



# SURA YA KUMI NA SITA

# UTENDAJI WA MAMLAKA ZA MAJI

## 16.0 Utangulizi

Utendaji wa mamlaka za huduma za majisafi na usafi wa mazingira unapimwa kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa katika makubaliano baina ya mamlaka hizo na Wizara ya Maji, na kusimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji. Viashiria muhimu vya utendaji ni pamoja na kulinda maslahi ya wateja, uendelevu wa huduma za maji, uwezo mzuri wa kifedha wa mamlaka, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato, gharama za uendeshaji, uendelezaji wa miundombinu, uhimilivu na uendelezaji wa mazingira, usimamizi wa upotevu wa maji, pamoja na kuongeza na kupanua uwezo wa vyanzo vya maji.

Licha ya jitihada za Serikali za kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira, kumekuwepo na changamoto kadhaa ambazo zimeendelea kujitokeza. Sura hii imeeleza mapungufu katika utendaji wa mamlaka za huduma za maji na usafi wa mazingira 34 pamoja na masuala mengine yanayohusiana na utendaji wa mamlaka hizo za madaraja A na B, na mapendekezo ya kuboresha.

## 16.1 Changamoto katika Utekelezaji wa Miradi ya Maji

Miradi ya maji inayotekelezwa na mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira inaratibiwa na kufadhiliwa na Wizara ya Maji kupitia bajeti ya Serikali. Pia, mamlaka hizo hutumia mapato ya ndani pamoja na fedha kutoka kwa wafadhili katika utekelezaji wa miradi hiyo. Hata hivyo, tathmini yangu ya utekelezaji wa miradi ya maji imebaini mapungufu yafuatayo:

Kulikuwa na ucheleweshaji wa hadi siku 622 katika kukamilisha miradi ya maji katika mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira za Mwanza na Songea hadi kufikia tarehe 30 Juni 2024, kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 51.**

**Jedwali Na. 51: Miradi ya Maji Iliyocheleweshwa katika mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira Mwanza na Songea**

| Na. | Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira | Jina la Mradi | Gharama ya Mradi- Sh. '000 | Tarehe ya Kuanza Inatarajiwa | Tarehe ya Kukamilika Inatarajiwa | Asilimia ya ukamilishwaji | Kuchelewa kwa Kukamilisha (Siku) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mwanza | Upanuzi wa mtandao wa usambazaji wa maji Magu | 176,849 | 17/10/2022 | 17/10/2022 | 92 | 622 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | mabomba pamoja na viungio vyake, ikijumuisha uchimbaji wa mtaro, uwekaji na ujazaji udongo juu ya mabomba, na upimaji, Misungwi | 110,717 | 20/4/2022 | 1/5/2023 | 85 | 542 |
| | | Uboreshaji wa mtandao wa usambazaji maji Misungwi | 888,007 | 6/8/2022 | 6/6/2023 | 85 | 390 |
| 2 | Songea | Ujenzi wa Mradi wa Maji katika Subira | 1,168,863 | | 30/10/2023 | 40 | 330 |

**Chanzo:** *Taarifa za Utekelezaji wa Miradi katika mamlaka ya maji Mwanza na Songea*

- Miradi mitatu katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam ilichelewa kuanza kwa miezi tisa kutokana na kuchelewa kwa malipo ya awali kwa wakandarasi, kiasi cha shilingi bilioni 6.31. Mikataba hiyo ilisainiwa tarehe 15 Desemba 2023, na miradi iliyoathiriwa ni pamoja na: Ujenzi wa mradi wa usambazaji maji katika bandari kavu ya Kwala na eneo la viwanda la Kwala; Ujenzi wa bomba la usambazaji maji (630 HDPE) kutoka Kibada (Kigamboni) hadi Taasisi ya Uhasibu Tanzania na awamu ya kwanza ya mradi wa usambazaji maji kwa maeneo ya makazi ya viwanda vya 'TAMCO'na Lulanzi/Pangani.

- Katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi, nilibaini kutotekelezwa kwa miradi mitano(5) yenye thamani ya shilingi bilioni 23 iliyopangwa, kutokana na uhaba wa fedha. Miradi hiyo ni pamoja na: Mradi wa Maji katika eneno la Njoro ya Dhobi;ukarabati na ujenzi wa mabwawa ya kutibu maji taka katika eneo la Mabogini; mradi wa maji wa Karanga Darajani; na mradi wa maji katika eneo la Ngozi/Maji taka, Karanga , na miradi mingine ya maji kwa kata 12 - Moshi.

  Pia, katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga, nilibaini miradi miwili ya uboreshaji wa usambazaji wa maji katika mji wa Pangani, na ujenzi wa miundombinu ya maji, Madanga na Kimang'a, inayogharimu shilingi bilioni 1.38, imesimama kwa muda wa miezi kumi na nne kutoka mwezi Septemba 2023 mpaka muda wa ukaguzi mwezi Novemba 2024, ikiwa utekelezaji wa miradi hiyo umekamilika kwa asilimia 85 na 75, mtawalia. Hii ilitokana na upungufu wa fedha uliosababishwa na ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kutoka Wizara ya Maji.

- Pia, nilibaini, kuwa utekelezaji wa mradi wa maji taka wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe, wenye thamani ya shilingi

bilioni 1.24, umesimama kutokana na kuchelewa kumlipa mkandarasi malipo ya awali kwa muda wa siku 579, tarehe ya kukamilika kwa mradi ilisogezwa mbele hadi tarehe 1 Julai 2025, kutoka tarehe ya awali ya kukamilika (1 Machi 2023). Hata hivyo, mradi ulikuwa na maendeleo ya asilimia 6.7 tu hadi kufikia tarehe 22 Novemba 2024.

Aidha, nilibaini kuwa ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kutoka Wizara ya Maji na ukosefu wa vipaumbele katika matumizi ya fedha za ndani vinakwamisha utekelezaji wa miradi ya huduma za majisafi na usafi wa mazingira kwa wakati.

**Ninapendekeza Wizara ya Maji kutoa fedha kwa wakati ili kukamilisha miradi inayosubiriwa na kuimarisha huduma za maji na usafi wa mazingira. Pia, mamlaka za maji husika zinapaswa kuanzisha miradi baada ya kuhakikisha upatikanaji wa fedha na kufanya uthibitisho wa kina wa miradi ili kuepuka ucheleweshaji.**

## 16.2 Mapungufu katika Kushughulikia Malalamiko ya Wateja

Miongozo ya huduma kwa wateja katika mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira inaelekeza kuwa, malalamiko ya wateja yashughulikiwe ndani ya siku mbili hadi kumi. Hata hivyo, uhakiki wangu umebaini mapungufu katika utekelezaji, ambayo yamesababishwa na ufanisi mdogo wa mfumo wa kushughulikia malalamiko, ukosefu wa wafanyakazi wa kutosha, mifumo duni ya ufuatiliaji, na udhaifu katika udhibiti wa ndani—ikiwemo ukosefu wa uwajibikaji na kutobainishwa kwa majukumu.

Ukaguzi wangu ulibaini kucheleweshwa kutatuliwa kwa malalamiko, ambapo baadhi yake yalichukua hadi siku 342, kinyume na miongozo ya huduma kwa wateja, katika mamlaka za maji za Same, Babati na Moshi kama inavyooneshwa kwenye **Jedwali Na.52.**

**Jedwali Na. 52: Kucheleweshwa kwa Kutatuliwa kwa Malalamiko**

| Na | Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira | Idadi ya Malalamiko | Muda wa ucheleweshwaji (siku) |
|---|---|---|---|
| 1 | Same | 17 | 94 - 342 |
| 2 | Moshi | 2,422 | 2 - 139 |
| 3 | Babati | 19 | 6 - 68 |
| | | | |

**Chanzo**: *Daftari la Malalamiko la Mamlaka za Maji za Same, Moshi na Babati*

Katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha, nilibaini kukosekana kwa utatuzi wa malalamiko ya wateja kwa wakati, ambapo malalamiko 1,678 (asilimia 32) kati ya 5,159

yaliyopokelewa katika mwaka wa fedha 2023/24 hayakutatuliwa hadi mwisho wa mwaka. Hali hii ni ithibati ya kuwepo kwa mapungufu makubwa katika utoaji huduma.

Aidha, katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Dar es Salaam, nilibaini malalamiko yanayojirudia kuhusu makosa kwenye tozo za huduma za maji, usomaji wa mita usio sahihi, uvujaji wa maji, na usambazaji wa maji usio thabiti. Kiwango cha wastani cha malalamiko kwa mwezi ilikuwa 9,065, ikiwa na kiwango cha chini cha malalamiko 7,019 na cha juu cha malalamiko 11,493.

Mapungufu haya yanadhihirisha kutoridhika kwa wateja, kuharibu taswira nzuri za Mamlaka ya MajiSafi na Usafi wa Mazingira huduma zisizo za uhakika, na yanaweza kuathiri ukusanyaji wa mapato.

**Ninapendekeza mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira ziboreshe mifumo ya ufuatiliaji, ziwe na uwazi katika uwajibikaji, ziimarishe taratibu za uwasilishaji wa malalamiko kwa ngazi za juu, na ziboreshe rasilimali watu.**

## 16.3 Ucheleweshaji wa Uunganishaji wa Maji kwa Wateja Wapya

Ukaguzi wangu ulibaini ucheleweshaji mkubwa wa uunganishaji wa maji kwa wateja wapya katika mamlaka mbalimbali za maji, kinyume na sera zao na miongozo ya huduma kwa wateja, inayohitaji uunganishaji kufanyika ndani ya siku saba baada ya malipo.

Ucheleweshaji huu, katika baadhi ya mamlaka za maji ulifikia hadi siku 1,036, na hasa ulisababishwa na upungufu wa mita. **Jedwali Na. 53** linonesha ucheleweshaji wa uunganishaji wa maji katika mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira.

**Jedwali Na. 53: Ucheleweshaji wa Uunganishaji katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira**

| Na. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira | Idadi ya waombaji waliocheleweshwa kuunganishiwa maji | Ucheleweshaji (Siku) | Idadi ya Waombaji Wasioungani shwa hadi 30 Juni 2024 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Morogoro | 1,251 | 31-1036 | 3,203 |
| 2 | Babati | 1,429 | 8-736 | |
| 3 | Dar es Salaam | 35,125 | 16-368 | 751 |
| 4 | Mwanza | 3,965 | 10-394 | |
| 5 | Tanga | 1,405 | 9-331 | 22 |
| 6 | Mbeya | 16 | 28 | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Jumla | 43,175 | | 3,976 |

Chanzo: *Ripoti za Utendaji za mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira*

Katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam, utafiti kwa wateja 29,708 ulicheleweshwa kati ya siku 15 hadi 709. Aidha, wateja 12,367 hawakufanyiwa utafiti kabisa kwa muda wa kati ya siku 15 hadi 669, kinyume na utaratibu unaotaka utafiti kufanyika ndani ya siku 7 za kazi baada ya kupokea maombi ya mteja.
Katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro, maombi 1,426 ya uunganishaji mpya hayakufanyiwa utafiti kama ilivyoelekezwa katika miongozo.

Katika Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Ngara, hakukuwa na taarifa za uunganishaji wa mita. Nilibaini kuwa, kati ya wateja 115 waliolipa jumla ya shilingi milioni 20.24 kwa uunganishaji kwa wateja wapya, hakukuwa na taarifa kuhusu muda wa ufungaji wa mita ili kuthibitisha muda wa uunganishaji.

Ucheleweshaji huu unaonesha udhaifu katika utoaji wa huduma, ambao unaathiri uunganishaji wa mita, na hivyo kuna haja ya kuboresha upangaji wa rasilimali, kuboresha taratibu, na kufuata kwa makini miongozo ya utoaji huduma.

**Ninapendekeza kuwa Mamlaka ziwe na akiba ya kutosha ya mita za maji na vifaa kutokana na matarajio sahihi ya mahitaji. Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam na Morogoro ziboreshe ufanisi wa tafiti, wakati Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Ngara inapaswa kuanzisha mfumo wa kufuatilia muda wa ufungaji wa mita ili kuhakikisha uwajibikaji.**

## 16.4 Kutokuwa na Miundombinu ya Usafi wa Mazingira katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira

Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019 kinaamuru Mamlaka kutoa huduma za usafi wa mazingira, ikijumuisha ukusanyaji, usafishaji, na uondoshaji wa maji taka.

Ukaguzi wangu ulibaini mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira 11 kati ya 34 hazijaanza au zimechelewa kujenga miundombinu ya usafi wa mazingira kutokana na ukosefu wa fedha. Kukosekana kwa miundombinu sahihi kunatishia afya ya umma, kuathiri mazingira, kusababisha adhabu za kisheria, na kuzorotesha hali ya maisha, hasa katika jamii hatarishi. Mamlaka hizi za Maji ni pamoja na: Karatu, Makambako, Mtwara, Bariadi, Bukoba, Kahama, Kyela, Shinyanga, Babati, Njombe na Ngara.

- **Kyela-Kasumulu**; Mpango wa Kila Mwaka wa Utekelezaji na Ripoti za Utekelezaji haijaonesha ujumuishaji wa huduma za usafi wa mazingira katika shughuli zake.

- **Njombe na Bukoba**: Ujenzi wa eneo la ustahimilivu wa majitaka, ambayo mikataba yao iliingiwa Mei 2023 na Julai 2022, ulisitishwa kutokana na ucheleweshaji wa utoaji wa fedha.

- **Ngara**: Mipango ya biashara na kimkakati ya Mamlaka za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya Taifa (NWSSA) wa mwaka 2022 hadi 2026 na 2020/21 hadi 2025/26 mtawalia haioneshi shughuli zozote zinazohusiana na ujenzi wa kituo cha kusafisha na kutibu maji taka na hakuna kituo kilichopo kwa sasa.

**Ninapendekeza Mamlaka za Maji husika, kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, kutilia mkazo kupata fedha ili kuhakikisha kukamilika kwa wakati kwa miradi ya miundombinu ya usafi wa mazingira.**

## 16.5 Kushindwa Kukidhi Mahitaji ya Maji katika Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira

Licha ya kusimamiwa na kupewa mamlaka kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Mwaka 2019 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Mamlaka za Maji zinaendelea kukabiliwa na upungufu wa maji yanayohitajika kila siku. Changamoto hii inatokana na ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi, ukosefu wa fedha za kutosha kutoka Wizara ya Maji, pamoja na changamoto za kiutendaji, ikiwa ni pamoja na kukatika kwa umeme, hitilafu katika mitambo mikubwa, na ufanisi duni wa pampu za maji.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, niliripoti upungufu wa maji yanayohitajika kila siku unazozikabili mamlaka za maji, ambapo Mamlaka 31 zilikuwa na upungufu wa kati ya asilimia 8 na 80 ya mahitaji ya kila siku. Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2023/24, nilibaini Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira 27 kati ya 34 zilipata upungufu mkubwa wa maji, uliokadiriwa kuwa kati ya asilimia 30 na 77 ya mahitaji yao, kama inavyooneshwa kwa kina katika **Kiambatisho Na. XVII.**

Licha ya tatizo hili kuripotiwa hapo awali, bado halijapatiwa suluhisho la kudumu, hali inayosababisha usumbufu wa huduma, ongezeko la hatari za kiafya, kuongezeka kwa gharama za uendeshaji, na kupungua kwa uaminifu wa Mamlaka za Maji kwa wateja wake. **Kielelezo Na. IV** na **Kiambatisho Na. XVII** kinaonesha mwenendo wa mahitaji ya maji ya kila siku kulinganisha na uzalishaji wake katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

**Kielelezo Na. IV: Wastani wa Mahitaji ya Maji dhidi ya Uzalishaji katika Ujazo kwa Siku**




**Chanzo**: *Ripoti za Utendaji za mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira*

**Ninaendelea kusisitiza mapendekezo yangu kwa Serikali, kupitia Wizara ya Maji, kuhakikisha ongezeko la uzalishaji wa maji na kuboresha ugavi wake kwa kutoa fedha kwa wakati na kusimamia miradi inayoendelea kwa ufanisi. Aidha, mamlaka za maji zinapaswa kuboresha ufanisi wa uzalishaji na kupunguza changamoto za kiutendaji kwa kutekeleza mfumo wa nishati mbadala na kushughulikia kwa wakati masuala muhimu ya matengenezo ya mitambo.**

## 16.6 Kuendelea kwa Upotevu wa Mapato Kunakotokana na Upotevu wa Maji shilingi bilioni 182.21

Upotevu wa maji ni kipimo muhimu cha ufanisi na utendaji wa Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira, kwani hupima maji yanayopotea kabla ya kuwafikia watumiaji. Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imeweka kikomo cha upotevu kuwa asilimia 20, lakini kiwango cha upotevu kinaendelea kuwa juu kutokana na uchakavu wa miundombinu, uvujaji, na miunganisho isiyo halali.

Nimekuwa nikiripoti mara kwa mara kuhusu tatizo hili, nikitoa pendekezo kwa Serikali kufanya tathmini ya miundombinu ya maji ya Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira na kutekeleza hatua madhubuti za kuboresha usimamizi. Upotevu wa maji hauleti tu hasara za kifedha kutokana na maji yasiyopimiwa, bali pia huathiri uendeshaji wa huduma na kuongeza gharama za uzalishaji.

Ingawa katika mwaka wa fedha 2023/24, nilibaini uboreshaji ikilinganishwa na 2022/23, Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira

29 (ikilinganishwa na 30 mwaka 2022/23) bado zilizidi kikomo cha asilimia 20, huku viwango vya upotevu wa maji vikiwa kati ya asilimia 21 hadi 49 kama ilivyooneshwa katika **Kiambatisho Na. XVIII, na** wastani wa upotevu wa maji umeoneshwa kwenye **Kielelezo Na. V.**

Jumla ya upotevu wa maji kwa mwaka 2023/24 ilikuwa shilingi bilioni 182.21, ikilinganishwa na shilingi bilioni 162.25 mwaka 2022/23.

**Kielelezo Na. V: Uchambuzi wa Mwenendo wa Upotevu wa Maji**




**Chanzo:** *Ripoti za Utendaji za Mwaka za Mamlaka za Maji*

**Ninapendekeza Serikali ichukue hatua kufanya tathmini ya miundombinu ya maji ya mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira na kutekeleza mikakati mahsusi ya kuboresha usimamizi wake, kuimarisha utambuzi na udhibiti wa uvujaji, na kupunguza upotevu wa maji.**

## 16.7 Ongezeko la Madai ya Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira shilingi bilioni 149.71

Ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato, Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira zinatekeleza sera ya mkopo inayohitaji malipo ya bili ndani ya mwezi na kusitisha huduma kwa wateja wanaoshindwa kulipa bili zao ndani ya siku 90. Hata hivyo, licha ya hatua hizi, madai yaliyoko nje ya muda wa mkopo yameendelea kuongezeka. Ufanisi mdogo katika ukusanyaji wa madai umeathiri ukwasi wa mamlaka za maji, hali inayoweza kusababisha changamoto za kifedha katika kutekeleza majukumu ya kiutendaji.

Mapitio yangu ya Mamlaka za Maji 34 yalionesha ongezeko la wateja wanaodaiwa kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo, kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. VI.**

**Kielelezo Na. VI: Mwenendo wa Madai ya Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira**




**Chanzo:** *Taarifa za fedha za mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira*

Katika mwaka wa fedha 2023/24, mamlaka 34 zilikuwa na madai ya shilingi bilioni 149.71, kutoka shilingi bilioni 138.64 mwaka 2022/23, kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na. XIX**.

Ongezeko hili linasababishwa na kutolipwa kwa bili za huduma za maji na usafi wa mazingira ambazo hazijalipwa kutoka kwa taasisi za Serikali, mashirika ya umma, na wateja binafsi.

Mamlaka 11 zinazoongoza kwa madai yasiyolipwa ambazo ni Kahama-Shinyanga, Arusha, Tanga, Tabora, Iringa, Mtwara, Sumbawanga, Bariadi, Same Mwanga, Kyela, na Mpanda ambazo ongezeko ni zaidi ya asilimia 20.

**Ninapendekeza kuwa mamlaka za maji ziimarishe ukusanyaji wa madeni kwa kutekeleza sheria kali za malipo, kutilia mkazo ukusanyaji wa madeni kutoka kwa mashirika ya Serikali, na kuimarisha utekelezaji wa sera za kusitisha huduma kwa wadaiwa sugu. Aidha, mamlaka za maji zichunguze matumizi ya mita za maji kabla ya malipo kwa wadaiwa sugu ili kuzuia ongezeko la madai.**

17

# Tathmini ya Utendaji wa Taasisi Za Mafunzo, Utafiti na Elimu ya Juu



# SURA YA KUMI NA SABA

# TATHMINI YA UTENDAJI WA TAASISI ZA MAFUNZO, UTAFITI NA ELIMU YA JUU

## 17.0 Utangulizi

Taasisi za elimu ya juu, mafunzo na utafiti zina mchango mkubwa katika utafiti na uvumbuzi, ukuzaji wa ujuzi, ukuaji wa maarifa binafsi na ya kijamii na ukuaji wa kiuchumi. Taasisi hizi zinajumuisha vyuo vikuu, vyuo vya ufundi, vituo vya utafiti, mashirika ya mafunzo ya ufundi, bodi ya mikopo ya wanafunzi, mamlaka za elimu na maendeleo ya teknolojia.

Sura hii inaangazia changamoto na mapungufu yanayozuia taasisi hizi kufikia malengo yake makuu, ikiwa ni pamoja na: udahili mdogo wa wanafunzi; uhaba wa miradi ya utafiti, uhaba wa huduma za ushauri na kozi fupi; miundombinu isiyotosheleza; na uhaba wa zana na vifaa vya kufundishia. Pia kuna ongezeko la utegemezi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa Serikali. Mapungufu haya yamefafanuliwa katika aya zinazofuata hapa chini.

## 17.1 Upungufu katika Utafiti na Ushauri Elekezi katika Taasisi za Kitaaluma

Utafiti na ushauri ni moja ya malengo muhimu ya taasisi za elimu ya juu, yanayochangia kukuza maarifa, kupata suluhisho halisia, kuongeza ujuzi, kuchagiza utungaji wa sera, na kukuza uchumi. Katika ukaguzi wa kazi za utafiti na ushauri kwa taasisi za elimu ya juu nilibaini kasoro zifuatazo;

- Katika **Chuo cha Usafirishaji cha Taifa**, nilibaini kuwa, sera yake ya utafiti, ushauri na uchapishaji ya mwaka 2022 haijaonesha idadi ya tafiti na machapisho inayotakiwa kwa kila mhadhiri kulingana na madaraja na ngazi zao za kitaaluma yaani, mhadhiri msaidizi/mhadhiri/mhadhiri mwandamizi ili kupima utendaji kwa ufanisi. Nilibaini kuwa chuo kilichapisha machapisho 34, kufanya tafiti sita na kazi za ushauri mbili. Hata hivyo, hakuna ushahidi kuwa kamati ya utafiti, ushauri, na uchapishaji ilifanya mikutano katika mwaka wa masomo wa 2023/24 ili kupitia na kuidhinisha kazi za kitaaluma, ingawa inapaswa kukutana kila robo mwaka. Hii inasababishwa na mapungufu katika sera ambayo haijaonesha idadi ya tafiti, ushauri na machapisho yanayopaswa kufanywa na wakufunzi, pamoja na uhaba wa fedha.

  **Ninapendekeza Chuo cha Usafirishaji cha Taifa (a) kiainishe bayana idadi inayotarajiwa kutoka kwa kila mhadhiri kwa tafiti, machapisho na kazi za ushauri zinazotakiwa kwa kila mwaka wa masomo, (b) kamati ya utafiti na uchapishaji izingatie mikutano ya**

**kila robo mwaka, na (c) kitenge fedha za kutosha kusaidia utafiti na ushauri.**

- Katika **Chuo Kikuu Mzumbe,** nilibaini kuchelewa kuanzishwa kwa ofisi ya utafiti na ushauri pamoja na mifumo ya kisasa na madhubuti ya usimamizi wa taarifa, kinyume na Sera ya Utafiti na Ubunifu ya mwaka 2020, ambapo ni miaka mitatu tangu kuazishwa kwa Sera. Hii inasababishwa na usimamizi duni wa mikakati ya utekelezaji, na hivyo kusababisha uwezekano wa kurudi nyuma katika mipango ya kimkakati na malengo ya muda mrefu yanayohusiana na utafiti na uvumbuzi. Pia, inazuia uwezo wa kubaini mwenendo, kufuatilia maendeleo, na kutathmini ufanisi wa shughuli za utafiti na ushauri.

  **Ninapendekeza kuwa Chuo Kikuu Mzumbe kianzishe ofisi ya utafiti na ushauri pamoja na kuanzisha mifumo ya kisasa ya usimamizi wa taarifa za utafiti na ushauri.**

- **Utendaji Duni wa Huduma za Ushauri na Kozi za muda Mfupi**
  Katika ukaguzi wa utendaji wa huduma za ushauri katika taasisi za elimu ya juu, nilibaini utendaji duni wa kozi za ushauri na kozi fupi katika taasisi za elimu ya juu nne kama inavyoelezwa kwenye **Jedwali Na.54** hapa chini.

**Jedwali Na. 54: Ushauri na kozi fupi Halisi dhidi ya Lengo la Kila Mwaka**

| Na | Jina la Shirika | Maelezo | Malengo | Uhalisia | Tofauti katika asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Chuo cha Uhasibu Arusha | Kozi fupi | 111 | 40 | 36 |
| 2 | Chuo Kikuu cha Dodoma | Kozi fupi | 33 | 9 | 27 |
| 3 | Chuo Kikuu Mzumbe | Kozi fupi na huduma za Ushauri | 60 | 15 | 25 |
| 4 | Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam | Huduma za Ushauri | 7 | 1 | 14 |

**Chanzo:** Ripoti za kitaaluma

Hii inasababishwa na ushiriki duni wa wafanyakazi wa kitaaluma katika ushauri na ukosefu wa mkakati ya kuongeza kozi za kitaaluma.

**Ninapendekeza mashirika ya umma husika yatengeneze mikakati ya kuongeza idadi ya huduma za ushauri na mkakati wa kuongeza kozi za taaluma.**

## 17.2 Upungufu wa Vifaa na Miundombinu ya Kufundishia katika Taasisi za Elimu ya Juu

### 17.2.1 Upungufu wa Miundombinu ya Madarasa katika Chuo cha Usafirishaji cha Taifa

Katika ukaguzi na tathmini ya uwezo wa madarasa katika Chuo cha Usafirishaji cha Taifa nilibaini kuwa taasisi hiyo kwa sasa ina jumla ya madarasa 53 yenye uwezo wa wanafunzi 6,568. Hii ni sawa na uwiano wa darasa kwa wanafunzi wa 1:302, uwiano ambao unazidi Mwongozo wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (Viwango vya Ubora vya Kitaaluma vya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ya mwaka 2010, Kiambatisho 1), ambao unatoa kiwango cha wanafunzi 100 kwa darasa moja kubwa. Hii inatokana na mkakati duni wa kukusanya fedha za kupanua majengo. Msongamano kwenye madarasa yaliyopo unaweza kuathiri mazingira ya kujifunzia, kupunguza ushiriki wa wanafunzi, na kudhoofisha uwezo wa wahadhiri kudhibiti na kufundisha vikundi vikubwa vya wanafunzi.

**Ninapendekeza Chuo cha Usafirishaji cha Taifa kitafute fedha kwa ajili ya kuongeza miundombinu yake, ikiwemo madarasa, ili kukidhi viwango vinavyohitajika. Zaidi ya hayo, taasisi inapaswa kuwekeza katika mafunzo kwa njia ya mtandao kwa kuboresha matumizi ya majukwaa ya kujifunza kwa njia ya Kidijitali na kutumia mbinu za kujifunza za mseto ili kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi madarasani.**

### 17.2.2 Kukosekana kwa Vifaa vya Kufundishia katika Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Katika ukaguzi wangu katika vituo vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi nilivyochagua, ambavyo ni pamoja na Shinyanga-ngazi ya mkoa, Mpanda-ngazi ya kati, Ruangwa-ngazi ya wilaya, Chato-ngazi ya wilaya, Kagera-ngazi ya mkoa, Pwani-ngazi ya mkoa, Kagera-ngazi ya kati, Dakawa-ngazi ya kati, Mikumi-ngazi ya kati, Shinyanga-ngazi ya kati na Ruangwa-ngazi ya kati, nilibaini kuwa vituo hivyo vilikuwa na; vifaa vilivyopitwa na wakati katika ufundi wa mavazi na usanifu wa mambo ya ndani, kubuni kwa msaada wa kompyuta, na ubunifu wa kushona kwa mashine ya kidijitali ambao hauendani tena na viwango vya sasa vya tasnia; uhaba wa vifaa muhimu vya mafunzo; na uhaba au kuwepo kwa magari mabovu yanayotumika katika utoaji wa kozi za udereva. Hii inachangiwa na ukosefu wa mkakati katika ununuzi wa zana za mafunzo, na kipaumbele kidogo kwa kozi zilizoathirika zaidi, pamoja na uhaba wa fedha. Ukosefu na hali ya kupitwa na wakati ya zana hizi, kunapunguza ubora na viwango vya elimu, na kusababisha uzalishaji wa wahitimu wasio na umahiri wa kutosha.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kuhakikisha upatikanaji wa zana na vifaa vya kutosha katika karakana ili kuzalisha nguvu kazi inayokidhi mahitaji ya soko la ajira la ndani.**

### 17.2.3 Ukosefu wa Vifaa katika Jengo la Maabara la Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania

Katika tathmini yangu ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania nilibaini kuwa jengo jipya la maabara huko Sota, Mara lililojengwa na kukamilika miaka miwili iliyopita hadi kufikia tarehe 30 June 2024. Hata hivyo, maabara haitumiki na haijawa na vifaa vya maabara kwa ajili ya utafiti wa kisayansi na majaribio kama ilivyokusudiwa. Hali hii inatokana na ukosefu wa fedha za kutosha na utumiaji usiofaa wa rasilimali zilizopo za taasisi, jambo linalosababisha kukosekana kwa fursa za utafiti na maendeleo ya uvuvi.

**Ninapendekeza Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania iandae mpango wa kununua na kufunga vifaa muhimu ili kuwezesha maabara kuweza kufanya kazi kamilifu ya utafiti kikamilifu.**

## 17.3 Kutokuwa na Ufanisi Katika Usimamizi wa Mafunzo

### 17.3.1 Kiwango Hafifu cha Uwiano wa Wahadhiri kwa Wanafunzi

Katika tathmini ya uwiano wa walimu kwa wanafunzi katika taasisi 22 za elimu ya juu nilibaini uwiano wa wanafunzi na walimu hauendani na viwango vya uwiano halisi na vinavyokubalika.

Hii inasababishwa na upungufu wa idadi ya walimu, na kwa maoni yangu, uwiano usiofaa wa walimu kwa wanafunzi unaweza kuhatarisha ubora wa elimu. Taarifa za taasis hizo imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. XX.**

**Ninapendekeza taasisi za elimu ya juu husika (a) zidahili wanafunzi kulingana na uwezo wao; na (b) zishirikiane na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kupata kibali cha kuajiri idadi inayohitajika ya walimu wenye sifa zinazohitajika ili kufikia uwiano wa walimu na wanafunzi uliowekwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.**

### 17.3.2 Utoaji wa Programu zisizo na Ithibati, Kuchelewa katika Utekelezaji wa Programu zenye Ithibati na Kufanya Kazi Bila Mitaala Halali

Katika mapitio yangu nilibaini kuwa taasisi 43 za kielimu zinatoa programu bila kuthibitishwa na Tume ya Vyuo Vikuu ya Tanzania kinyume na viwango na miongozo ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania

kwa Elimu ya Vyuo Vikuu nchini Tanzania ya mwaka 2019 au zinatoa programu bila kuthibitishwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kinyume na Kanuni za Ithibati na Utambuzi za Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi za mwaka 2001.

Hii inatokana na mipango hafifu na michakato duni ya taasisi kuhakikisha maandalizi ya wakati na kupitia upya mitaala kabla ya kumalizika muda wake, na upungufu wa wafanyakazi wenye sifa za kitaaluma zinazohitajika kuendesha programu. Kuna hatari kuwa baadhi ya wahitimu wanaweza kupoteza fursa za ajira kutokana na kusoma kozi ambazo hazijathibitishwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Taarifa kuhusu taasisi hizo imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. XXI**.

**Ninapendekeza kuwa taasisi husika za elimu ya juu zihakikishe kuwa programu zote zimeidhinishwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania au Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.**

### 17.3.3 Kuchelewa Kuhuisha Mitaala katika Chuo Kikuu cha Dodoma

Katika ukaguzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma nilibaini programu 27 za shahada ya kwanza na programu 12 za shahada ya uzamili zilichelewa kuhuishwa kwa zaidi ya mwaka mmoja kinyume na Kifungu 2.6.1 cha viwango na Miongozo ya Elimu ya Vyuo Vikuu Tanzania, ya mwaka 2019 iliyotolewa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, inayotaka mapitio ya programu zilizothibitishwa kufanywa baada ya miaka miwili ya mzunguko wa utoaji. Hii ilitokana na upungufu wa bajeti na ufuatiliaji duni. Kucheleweshwa kwa mapitio kunaweza kusababisha mitaala kupitwa na wakati, hivyo kushindwa kuakisi mabadiliko ya karibuni katika fani husika, jambo linaloweza kuathiri ufanisi wa wahitimu katika soko la ajira

**Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Dodoma kihakikishe kinahuisha programu ili ziendane na miongozo ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania kwani hili litahakikisha kuwa maudhui ya programu za kitaaluma yana maana, na yanaendana na viwango na mwelekeo wa sasa wa sekta.**

### 17.3.4 Kushindwa Kufikia Malengo ya Udahili wa Wanafunzi Wanaojiunga na Taasisi za Elimu ya Juu

Katika ukaguzi nilibaini udahili duni wa wanafunzi katika taasisi za elimu ya juu, ambapo kilikuwa chini ya lengo kwa hadi asilimia 69, ikilinganishwa na mwaka uliopita ambapo kiwango cha juu cha kutofikia lengo kilifika asilimia 31. Hali hii ilitokana na upungufu wa rasilimali, ikiwa ni pamoja na uhaba wa walimu, miundombinu duni, ukosefu wa vifaa na zana, baadhi ya programu kukosa soko, pamoja

na upatikanaji mdogo wa mikopo ya elimu ya juu kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Kwa mfano, katika mwaka wa fedha wa 2023/24, ni asilimia 70 tu ya wanafunzi wapya waliweza kupata elimu ya juu kwa ufadhili wa Bodi ya Mikopo. Jumla ya wanafunzi wapya 79,133 walipewa mikopo kati ya 113,574 waliostahiki. Katika tathmini yangu, wanafunzi waliostahiki lakini hawakupata mikopo wanaweza kukumbana na changamoto za kifedha zinazoweza kuathiri upatikanaji wao wa elimu ya juu, jambo ambalo linapunguza fursa za kitaaluma na kuathiri matarajio yao ya baadaye. Aidha, upungufu wa miundombinu na walimu unachangia kupungua kwa udahili

**Jedwali Na. 55: Upungufu wa udahili wa wanafunzi**

| Na. | Jina la Shirika | Malengo | Uhalisia | Tofauti | Tofauti katika asilimia |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia | 150 | 46 | 104 | 69 |
| 2 | Chuo cha Sukari cha Taifa | 700 | 478 | 222 | 31 |
| 3 | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima | 5,000 | 3,500 | 1500 | 30 |
| 4 | Chuo Kikuu cha Dodoma | 14,241 | 10,815 | 3,426 | 24 |
| 5 | Chuo Kikuu Huria cha Tanzania | 21,000 | 16,311 | 4,689 | 22 |
| 6 | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | 32,273 | 27,535 | 4,738 | 14 |
| 7 | Chuo cha Ufundi Arusha | 4,752 | 4,112 | 640 | 13 |
| 8 | Chuo cha Ustawi wa Jamii | 6,300 | 5,457 | 843 | 13 |
| 9 | Chuo cha Elimu ya Biashara | 25,000 | 22,263 | 2,737 | 11 |
| 10 | Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini | 16,036 | 14,582 | 1,454 | 9 |
| 11 | Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine | 19,450 | 17,660 | 1,790 | 9 |
| 12 | Chuo cha Usimamizi wa Fedha | 16,500 | 15,323 | 1,177 | 7 |
| 13 | Chuo Kikuu Ardhi | 6876 | 6516 | 360 | 5 |

**Chanzo:** *Ripoti ya Takwimu; Mpango mkakati; na Data ya Usajili wa Mwaka 2023/24, Mkataba wa Utendaji na Hazina*

**Ninapendekeza kuwa taasisi za elimu ya juu zihakikishe zinatekeleza malengo ya udahili yaliyopangwa kwa kuboresha miundombinu na kuongeza idadi ya wafanyakazi wa kitaaluma, na Serikali ihakikishe inatenga fedha za kutosha kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kuongeza wanufaika wa mikopo na uandikishaji.**

## 17.4 Utendaji Duni wa Taasisi za Elimu

### 17.4.1 Kuongezeka kwa Utegemezi kutoka Serikalini katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi ya Elimu ya Juu

Katika ukaguzi na tathmini ya vyanzo vya fedha vya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa kipindi cha miaka mitano (2019/20 hadi 2023/24), nilibaini kuwa Bodi inategemea kwa kiwango kikubwa marejesho ya mikopo na fedha kutoka kwa Serikali kama chanzo kikuu cha ufadhili wake.

Katika kipindi hicho, ufadhili wa mikopo umeongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2019/20 hadi asilimia 73 mwaka 2023/24. Michango ya Serikali imeongezeka kutoka shilingi bilioni 255.62 mwaka 2019/20 hadi shilingi bilioni 469.67 mwaka 2023/24, ongezeko la asilimia 84. Hata hivyo, marejesho ya mikopo yamepungua kwa asilimia 7, kutoka shilingi bilioni 190.72 hadi shilingi bilioni 176.61 katika kipindi husika.

Wakati mahitaji ya mikopo kwa wanafunzi yameongezeka, marejesho ya mikopo hayajatosha kukidhi ongezeko la mahitaji ya mikopo kwa wanafunzi. Utegemezi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa msaada wa Serikali unasababishwa na kasi ndogo ya urejeshaji wa mikopo inayotokana na kutokuwekeza fedha zake katika kuzalisha mapato kusaidia shughuli zake ikiwa ni miongoni mwa malengo ya Bodi na kupunguza utegemezi kwa ufadhili wa Serikali na ongezeko la mahitaji ya mikopo kutoka kwa wanafunzi.

Endapo ufadhili wa Serikali utapungua kunaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa uwezo wa Bodi wa kutoa mikopo na kukidhi mahitaji ya wanafunzi.

**Ninapendekeza kuwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ianzishe na kutekeleza mikakati ya vyanzo mbadala vya fedha ambavyo vitasaidia uzalishaji wa fedha na kupunguza utegemezi wa Bodi kwa Serikali. Pia, itengeneze na kutekeleza mikakati madhubuti ya kuongeza urejeshaji wa mikopo kama vile kuimarisha juhudi za ukusanyaji wa madeni na kuboresha motisha za urejeshaji wa mikopo.**

### 17.4.2 Mafunzo Hafifu kwa Mitaala ya Elimu na Mafunzo yenye Ujuzi Inayofanywa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Mapitio yangu ya utekelezaji wa mafunzo ya mtaala wa elimu na mafunzo yenye ujuzi kwa elimu na mafunzo ya ufundi stadi yalibaini kuwa taasisi 265 (Taasisi binafsi 176 na Taasisi za Umma 89) kati ya ya taasisi 323 hazikupata mafunzo kuhusu mtaala wa elimu na mafunzo yenye ujuzi hadi mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Hii inatokana na upungufu wa bajeti pamoja na ukosefu wa ufuatiliaji

na tathmini ya utekelezaji wa kozi ya mtaala wa elimu na mafunzo yenye ujuzi. Kushindwa kutekeleza mafunzo ya mtaala wa elimu na mafunzo yenye ujuzi kunaathiri uwasilishaji wa maarifa kutoka kwa walimu kwenda kwa wanafunzi.

**Ninapendekeza Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi lihakikishe mafunzo kuhusu mitaala ya elimu na mafunzo yenye ujuzi yanatolewa kwa taasisi husika.**

### 17.4.3 Udahili wa Wanafunzi Wapya Bila Idhini kwa Taasisi 12 na Uendeshaji wa Vituo 43 bila Kupata Usajili kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Katika ukaguzi nilibaini kuwa Vituo 43 vya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi havikusajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Kati ya vituo hivyo, vituo 15 vilianza kufanya kazi wakati bado viko katika hatua za maandalizi kinyume na Kanuni ya 17(1 na 2) ya Kanuni za Usajili wa Taasisi za Ufundi za mwaka 2001.

Vilevile, nilibaini kuwa taasisi 12 za ufundi ziliendela na udahili wa wanafunzi licha ya kusitishiwa udahili wa wanafunzi wapya au kushushwa hadhi na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Hii ni kinyume na Kifungu 5(1) cha Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi Sura 129. Hali hii inahatarisha ubora wa elimu na ujuzi kwa wahitimu.

**Jedwali Na. 56:Taasisi zilizositishwa na kushushwa hadhi**

| Na | Chuo/Shule/Taasisi | Maelekezo ya Baraza |
|---|---|---|
| 1 | Taasisi ya Sayansi ya Afya na Teknolojia ya Apple Valley | Kusitisha udahili. |
| 2 | Taasisi ya Sayansi ya Afya na Sayansi Shirikishi ya Jelly's Mwanza | |
| 3 | Taasisi ya Sayansi ya Afya na Sayansi Shirikishi ya St. Alvin - Morogoro." | |
| 4 | Chuo cha Ufundi Zoom Polytechnic, Bukoba | |
| 5 | Chuo cha Sayansi ya Afya na Sayansi Shirikishi cha Top One - Songea. | Kushushwa Hadhi hadi Hatua ya Maandalizi na Kusitisha Udahili. |
| 6 | Chuo cha Sayansi ya Afya na Sayansi Shirikishi cha Mtwara | |
| 7 | Chuo cha Kumbukumbu ya Kilenzi cha Sayansi ya Afya na Sayansi Shirikishi (KIMCHAS)-Dar es Salaam | |
| 8 | Chuo cha Sayansi ya Afya na Sayansi Shirikishi cha Jiji la Ilala (ICCoHAS)- Dar es Salaam. | |
| 9 | Taasisi ya Sayansi ya Afya na Sayansi Shirikishi ya Kilimanjaro (KIHAS) - Dar Es Salaam. | |
| 10 | Taasisi ya Kilimanjaro-Dar Es Salaam | |
| 11 | Chuo cha Biashara cha Afrika Mashariki - Dar es Salaam. | |
| 12 | Chuo cha Bima na Ulinzi wa Jamii cha Afrika - Dar es Salaam. | |

Sababu kuu za matatizo haya ni ucheleweshaji katika kukamilisha ukaguzi wa miundombinu unaohitajika kwa usajili kamili na ufuatiliaji duni, na uhifadhi wa kumbukumbu za maagizo ya kusitisha udahili kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Ukiukwaji huu unapelekea taasisi kuandikisha wanafunzi bila miundombinu, rasilimali, au wafanyakazi wenye sifa za kutosha, jambo ambalo linaweza kuathiri ubora na ujuzi wa wahitimu.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi iharakishe usajili kamili wa vituo vyake kutoka kwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi. Pia, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi liimarishe ufuatiliaji na uhifadhi wa kumbukumbu za maagizo ya kusitisha udahili.**

### 17.4.4 Ukosefu wa Mkakati wa Kina wa Uendelezaji wa Shamba la Kibiashara la Kilimo katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine

Mapitio yangu yalibaini kuwa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine hakina mkakati wa kina kwa shamba lake la biashara la kilimo kama kituo bora cha kuzalisha mapato ya kilimo, kutoa mafunzo ya ujuzi wa vitendo, kufanya utafiti, na kuandaa maonesho kwa umma kama ilivyoainishwa kwenye Sera na Miongozo ya Maendeleo ya Mashamba ya Mwaka 2006. Zaidi ya hayo, shamba la kibiashara halikuwa na mpango wa biashara na ulinganifu na idara ya kilimo.

Nilibaini kuwa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kilikuwa na mpango wa kulima ekari 500 za mkonge katika shamba la kibiashara lakini kililima ekari 200 pekee kwa gharama ya uwekezaji ya shilingi milioni 102.50 huku ekari 300 zikiwa bado hazijalimwa. Chuo kilivuna mkonge lakini kiliuza malighafi badala ya nyuzi zilizochakatwa kinyume na matarajio ya Hati ya Dhana. Mauzo yaliyotarajiwa ya shilingi milioni 470 kwa kipindi cha miaka minne yalitofautiana kwa kiasi kikubwa na mapato halisi ya shilingi milioni 4, ikiwa ni pungufu kwa shilingi milioni 466 sawa na asilimia 99 ya mauzo ya mradi.

Hii inatokana na ukosefu wa mikakati ya upanuzi wa shamba la kibiashara, kutokuwepo kwa mpango wa biashara na mgao duni wa bajeti kwa shamba hilo. Kutokutumika kikamilifu kwa shamba la kibiashara kunakikosesha chuo kikuu mapato ambayo yangeweza kusaidia chuo kujitegemea kifedha. Pia kunaharibu taswira ya chuo

kikuu hasa kwa wadau wa sekta ya kilimo wanaotegemea kujifunza kutoka kwa Chuo Kikuu hicho.

**Ninapendekeza kuwa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kiandae mkakati wa kina wa kibiashara kwa shamba lake la kilimo, ukiwemo mpango wa biashara unaolenga kukuza shughuli za shamba. Mkakati huu unapaswa kuainisha hatua muhimu, kuweka malengo wazi na yanayoweza kupimika, pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa bora kwa mafunzo ya vitendo, utafiti, na maonesho kwa umma.**

### 17.4.5 Kutokurejeshwa kwa Mikopo ya Wanafunzi kwa Wanafunzi Wasiodahiliwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Mapitio yangu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kuhusu udhibiti wa usimamizi wa mikopo ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, yalionesha kuwa Chuo kilikusanya mikopo yenye jumla ya shilingi milioni 94.49 kwa wanafunzi 194 ambao hapo awali walisajiliwa lakini baadaye usajili wao ulifutwa kwa sababu mbalimbali

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hakikurejesha fedha za wanafunzi wasiosajiliwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kama inavyotakiwa na kifungu cha 7.9.2 (iv) cha Mwongozo wa Utoaji Mikopo kinachotaka fedha ambazo hazijasainiwa na mwanafunzi zirejeshwe kwa Bodi ndani ya siku 30.

Hali hii inatokana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutohakiki kwa wakati mikopo ya wanafunzi isiyotiwa saini ambayo inapaswa kurejeshwa ndani ya siku 30.

Kutokufuata miongozo ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kunaweza kusababisha matumizi yasiyokusudiwa ya fedha, na hivyo kutengeneza madeni kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa wanafunzi ambao walifutiwa usajili.

**Ninapendekeza Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kifanye uhakiki wa mikopo ya wanafunzi dhidi ya wanafunzi waliosajiliwa kwa kila semista ili kuhakikisha fedha za wanafunzi wasiosajiliwa na fedha zozote za ziada zinarejeshwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa wakati.**

### 17.4.6 Udhibiti Duni wa Utambuzi katika Uhariri wa Matokeo ya Mitihani kwenye Mfumo wa Taarifa za Usajili wa Wanafunzi na Mfumo wa Usimamizi wa Wanafunzi

Nilikagua michakato ya usimamizi wa tathmini za wanafunzi na matokeo ya mitihani katika Mfumo wa Taarifa za Usajili wa Wanafunzi (ARIS3) na Mfumo wa Usimamizi wa Wanafunzi (ISMS), ili kutathmini upatikanaji wake na uwezekano wa kukaguliwa na wasimamizi kubaini mabadiliko yasiyoidhinishwa.

Nilibaini kanzidata haikuwa na uwezo wa kutunza kumbukumbu za mienendo na shughuli za watumiaji na hivyo kuzuia kugundua kwa urahisi endapo watafanya mabadiliko yasiyoidhinishwa kwenye mifumo. Hii inatokana na kutokuzingatia kwa kiwango cha kutosha kwa usalama na usimamizi wa rekodi katika mfumo wa usimamizi wa kanzidata. Ukosefu wa rekodi za kanzidata unazuia uchunguzi na uoanishaji wa vyanzo vya mienendo isiyofaa na shughuli zisizoidhinishwa ndani mfumo.

**Ninapendekeza mashirika husika yaimarishe uwezo wa mifumo ili kutunza rekodi za kanzidata na kuweza kunasa taarifa zote muhimu za kanzidata za mifumo yote ya matumizi na yaandae ripoti maalumu inayojumuisha mabadiliko yote ya matokeo ya mitihani kwa ajili ya usimamizi ulio bora, uadilifu wa data na udhibiti wa ubora.**

# Ufanisi wa Mamlaka za Udhibiti Katika Kutekeleza Majukumu yao



## SURA YA KUMI NA NANE

# UFANISI WA MAMLAKA ZA UDHIBITI KATIKA KUTEKELEZA MAJUKUMU YAO

## 18.0 Utangulizi

Serikali imekuwa ikisimamia utoaji wa huduma, uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa kwa kutumia mashirika ya udhibiti 57. Mashirika haya yamekuwa yakitunga sera, miongozo na kanuni na kuzisimamia ili kuhakikisha usawa, kuzuia unyonyaji, kuzuia ushindani usiosawa, kulinda mazingira, kudumisha ubora wa viwango, na kuongeza imani kwa wawekezaji.

Katika ukaguzi wa mwaka uliopita 2022/23, nilibaini usimamizi na matumizi hafifu ya teknolojia, usimamizi na udhibiti hafifu wa waliofutiwa vibali/leseni, kutofanyika tafiti za kutosha kubaini mapungufu ya kiudhibiti, na kuwepo kwa vipengele vinavyozuia ushindani katika mikataba ya uwakala wa ununuzi wa magari ambavyo vinazuia fursa ya kupunguza gharama za kununua moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji.

Kwa mwaka wa fedha 2023/24, nimebaini udhaifu katika kusimamia na kutekeleza hatua za kiudhibiti na kinidhamu kwa wanaokiuka taratibu za udhibiti, udhaifu katika matumizi ya teknolojia ili kuboresha utoaji wa huduma kwa njia za kisasa, kuwepo kwa michakato isioyoridhisha katika utoaji na usimamizi wa leseni, na udhaifu wa Bodi za mazao katika kusimamia mazao ya biashara, kama ilivyoainishwa katika aya zinazofuata:-

## 18.1 Udhaifu katika Kusimamia Hatua za Kiudhibiti

Nimeendelea kubaini kuwa baadhi ya mashirika yameonesha udhaifu katika kusimamia hatua za kiudhibiti kwa wanaoukiuka kanuni, miongozo na taratibu za udhibiti katika sekta, kama nilivyoripoti katika taarifa yangu ya mwaka uliopita 2022/23. Kwa kiwango kikubwa, hali hii inasababishwa na kukosekana kwa mifumo thabiti, yenye ufanisi na yenye uhalisia katika kusimamia utekelezaji wa hatua za kiudhibiti kama ilivyoainishwa hapa chini;

(i) **Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji** haidhibiti bei ya gesi asilia kwa makampuni yenye mikataba ya uzalishaji wa gesi iliyoingiwa kabla ya Sheria ya Mafuta na Gesi ya Mwaka 2015. Hivyo, watumiaji wa huduma ya gesi kutoka katika makampuni hayo wanaweza wasilindwe na nguvu za udhibiti za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kwa kuwa imedhibitiwa na kifungu cha 260 (3) cha Sheria ya Gesi na Petroli ya mwaka 2015. Sheria hiyo inaruhusu vipengele vyote vya leseni zilizotolewa ama mikataba iliyoingiwa

kabla ya sheria hiyo kuanza, kuendelea kutumika bila kuathiriwa na uwepo wa sheria hiyo, katika shughuli zao za kuzalisha ama kusambaza gesi ama bidhaa za petroli.

Pia, nilibaini Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji haikutoza asilimia 20 ikiwa ni adhabu ya kuchelewesha matokeo ya vipimo, kwa makampuni ya upimaji yaliyopewa zabuni ya kutoa huduma za upimaji kwa bidhaa zinazotokana na petroli. Ucheleweshwaji ulikuwa wa kati ya kipindi cha siku 15 hadi 25 kinyume na muda wa kipindi cha siku tano uliowekwa katika mikataba ya makubaliano ya utoaji wa huduma za upimaji. Ucheleweshwaji huu unaweza kutoa mianya kwa baadhi ya wafanyabiashara kuuza bidhaa za petroli ambazo hazikidhi viwango vilivyowekwa, kabla hatua za kiudhibiti kuchukuliwa. Kuna uwezekano kuwa, wakati Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji inajiandaa kuanza mchakato wa kuchukua hatua za kiudhibiti, bidhaa zisizokidhi viwango huuzwa na kuletwa zingine, hali inayoweza kusababisha ugumu katika kuchukua hatua kwa wakati kwa bidhaa zisizo na ubora.

Hali hii inasababishwa na udhaifu katika kuchukua hatua za kiudhibiti dhidi ya ucheleweshwaji, na kusababisha uwezekano wa kusambaza bidhaa za petroli zisizo na ubora unaotakiwa.

Pia nilibaini **Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji** haikutoza adhabu kwa makampuni sita ambayo yalijenga vituo vya petroli bila kupata kibali cha Mamlaka, hali inayokinzana na matakwa ya kisheria yanayotaka mtu ama kampuni yeyote yenye lengo la kujenga vituo vya mafuta na gesi lazima kuomba na kupata kibali kutoka kwa Mamlaka. Mianya ama mapungufu katika kusimamia utekelezaji wa sheria, unaweza kuruhusu ujenzi holela wa vituo vya mafuta na gesi hali inayoongeza hatari ya usalama na uharibifu ama majanga kwenye mazingira kama vile moto au milipuko, uharibifu wa udongo na uchafuzi wa maji unaoweza kuhatarisha maisha ya wafanyakazi wa vituo hivyo, jamii na mazingira kwa ujumla. Pia, tozo za adhabu zinazotozwa, kwa mfano shilingi milioni 20 kwa makampuni makubwa ya mafuta na gesi, ni ndogo na haziwezi kuzifanya kampuni hizo kuogopa kukiuka sheria, kwa kuwa zinaweza kulipa kwa urahisi na kuendelea na biashara bila kuathirika. Hii inasababishwa na mapungufu katika usimamizi wa utozaji wa adhabu na mapungufu ya ufuatiliaji wa ukiukwaji wa kanuni na taratibu za uendeshaji katika sekta ya mafuta na gesi.

**Ninapendekeza kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (a) kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na makampuni ya Mafuta na Gesi, ichakate namna ya kuchukua hatua za kubadilisha ama kuboresha vipengele Sheria ya Gesi na Petroli, ili kuvihuisha**

**na uhalisia wa muundo na uendeshaji wa sasa wa shughuli za gesi na mafuta, (b) ichukue hatua za kiudhibiti kwa ukamilifu kwa mujibu wa vipengele vya mikataba, kwa watoa huduma wa vipimo wanaochelewesha majibu ya vipimo; na kupanua wigo wa watoa huduma za upimaji ili kupunguza utegemezi kwa watoa huduma waliopo na kuongeza kasi ya upimaji na utoaji wa majibu, na (c) iimarishe usimamizi wa uchukuaji hatua za kiudhibiti na kuboresha ufuatiliaji wa kubaini ukiukwaji wa ujenzi wa vituo vya mafuta na gesi, kwa kutoza faini kubwa, kuweka vikwazo na kuziweka wazi kampuni zinazokiuka matakwa ya kisheria; na kuchukua hatua za haraka zenye ufanisi kwa wanaokiuka sheria ili kuimarisha uaminifu, nidhamu na kuondosha ukiukwaji wa sheria.**

(ii) **Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania** haikuchukua hatua stahiki dhidi ya makampuni ya bima yanayofanya biashara yakiwa na dhamana ya chini ya asilimia 50 ya mitaji yao, kinyume na matakwa ya kanuni ya 20(1) ya kanuni za bima za mwaka 2009. Makampuni mawili ya bima na kampuni moja ya "*re – insurance*" yalibainika kuwa na dosari hiyo. Hii inasababishwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kutochukua hatua stahiki za kuhakikisha sheria na kanuni za bima za eneo hili, zinafuatwa kikamilifu. Hali hii inawaweka waliolipia bima katika hatari ya kutolipwa madai yao ya bima, endapo kampuni ya bima inafilisika au kushindwa kujiendesha.

**Ninapendekeza kuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania iimarishe ufuatiliaji na uchukuaji wa hatua stahiki ili kuhakikisha makapuni yote ya bima yanafuata kwa ukamilifu matakwa ya sheria na kanuni za bima, hasa kwenye dhamana za mitaji**

(iii) **Bodi ya Usajili wa Wakandarasi**, kupitia mfuko wa kusaidia wakandarasi, ilidhamini wakandarasi 30 jumla ya shilingi bilioni 1 waliokuwa wanadaiwa tozo za adhabu na ada mbalimbali, ambazo walitakiwa kulipa kabla ya kupewa msaada wa kifedha kutoka katika mfuko huo. Hii ni kinyume na matakwa ya kanuni ya 23.3(a) ya kanuni za fedha za Bodi ya Usajili wa Makandarasi na Muongozo wa Mfuko wa Kusaidia Wakandarasi uliotolewa na Bodi ya Usajili wa Wakandarasi. Hali hii inasababishwa na kukosekana kwa uthabiti wa mifumo ya udhibiti katika kuhakiki ada na tozo za adhabu ambazo hazijalipwa, kabla ya kutoa msaada wa udhamini wa fedha kwa wakandarasi husika, hali inayoondoa au kupunguza imani juu ya uadilifu katika mchakato wa kutoa msaada wa fedha kwa wakandarasi na kuzuia uvunjwaji wa sheria na kanuni. Mfuko wa Kusaidia Wakandarasi ulianzishwa kwa lengo la kutoa msaada wa kifedha kwa wakandarasi wa ndani ya nchi, ili kuwawezesha kutekeleza mikataba au kandarasi

walizopata, kuwawezesha kuimarika kiuchumi, na kushindana na wakandarasi wa kimataifa

**Ninapendekeza kuwa Bodi ya Usajili wa wakandarasi iweke mfumo thabiti wa kudhibiti, kuhakiki kielektroniki na kubaini wakandarasi ambao bado hawajalipa ada na tozo za adhabu, kabla ya kutoa msaada wa kifedha kwa wakandarasi hao.**

(iv) **Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli** haukutoza riba ya asilimia 10 kwa malipo yaliyocheleweshwa kulipwa na makampuni ya mafuta na gesi kwa mikataba ya vitalu vya Nyuni, Ruvu na Kilosa. Riba hiyo iliwekwa ili kudhibiti ucheleweshwaji wa malipo kutoka kwa makampuni hayo. Kwa mfano, nilibaini Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli haikutoza riba ya asilimia 10 kwenye jumla ya shilingi bilioni 2.12 zilizochelewa kulipwa na makampuni makubwa ya mafuta, na wala haikuzijumuisha kwenye hati za madai zilizotumwa kwa makampuni hayo, kinyume na ilivyoelekezwa na kanuni ya 14(1) za Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli za mwaka 2019. Hivyo, **Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli** imepoteza fursa ya kukusanya kiasi cha shilingi milioni 212.15 mbacho hakikutozwa kama riba na kukosa ufanisi wa kuhakikisha makampuni yanafuata sheria na kanuni. Hali ambayo imesababishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli kutokuwa thabiti katika kusimamia utekelezaji wa kanuni.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli ifanye uhakiki wa madai yake kwa makampuni ya mafuta na gesi mara kwa mara, na ihakikishe inatoza riba ya asilimia 10 kwa malipo yaliyochelewa, kwa maslahi mapana ya umma.**

(v) **Bodi ya Udhibiti wa Stakabadhi Ghalani** haina kanuni zinazoelekeza hatua za kuchukua kwa kukabiliana na uwasilishaji pungufu wa bidhaa pamoja na kuwepo kwa kifungu cha sheria katika Sheria ya Stakabadhi za Ghala, kinachokabiliana na hali ya kutokuwepo kwa bidhaa kwenye maghala na kumuwajibisha muendeshaji wa ghala. Hali hii inasababishwa na kuwepo kwa sheria na kanuni zilizopitwa na wakati, na inasabisha ombwe na hatua zisizo na usawa katika kushughulikia uwasilishaji pungufu wa bidhaa na kusababisha migogoro, ucheleweshaji wa fidia au hasara kubwa kwa wadau wanaoathirika. Nilibaini kuwepo kwa malalamiko kwa wanunuzi kupokea bidhaa pungufu kutoka kwa waendeshaji wa maghala, hakuna utaratibu wa kikanuni na hatua za kuchukua kukabiliana na hali hiyo.

**Ninapendekeza Bodi ya Udhibiti wa Stakabadhi Ghalani kushirikiana na wadau ili kuweka utaratibu na miongozo ya wazi kudhibiti uwasilishaji pungufu wa bidhaa, na kuanzisha mchakato wa kuhuisha sheria na kanuni za kudhibiti hali hiyo.**

## 18.2 Mamlaka za Udhibiti Kushindwa kutumia Teknolojia Kikamilifu katika Kuboresha na Kuongeza Ufanisi wa Kutekeleza Majukumu ya Kiudhibiti

Katika ukaguzi, nilibaini baadhi ya Mamlaka za Udhibiti hazikuwa zimetumia fursa ya matumizi ya teknolojia kikamilifu katika kuboresha na kuongeza ufanisi wa kutekeleza majukumu yao, kama ilivyofafanuliwa hapa chini;

(i) **Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli** haijaweka mfumo wa kielektroniki wa kutoa na kufuatilia uhalali wa leseni, wala kufuatilia makampuni ya uzalishaji wa bidhaa za petroli na mauzo ili kuhakikisha usahihi wa bili. Badala yake, Mamlaka imekuwa ikitegemea taarifa zilizowasilishwa na wazalishaji hao, taarifa ambazo hazitoshi kuhakiki usahihi na ukamilifu wa takwimu zilizowasilishwa na makampuni hayo. Hii inasababishwa na kutowekeza vya kutosha katika kuweka mifumo ya kielektroniki na kutokuwepo kwa mpango mkakati toshelevu katika kuchochea ufanisi wa utendaji kazi na kufuatilia ufuataji wa sheria.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli iweke kipaumbele katika kuweka na kutumia mfumo wa kielektroniki wenye muunganisho wa kutosha na mifumo mingine husika ya Serikali, ili kusimamia utoaji wa leseni na kufuatilia shughuli za wakandarasi, ikiwemo ufuatiliaji wa moja kwa moja wa uzalishaji wa kila siku wa bidhaa za mafuta na mauzo.**

(ii) **Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji** haijatengamanisha mifumo yake ya kielektroniki na mashirika yanayokusanya mapato ya tozo au taarifa kwa niaba yake, kutokana na kutokuwepo na kutekelezwa kwa mpango mkakati wa Mamlaka wa utengamanishi wa mifumo yake ya kielektroniki. Hali hii inazuia Mamlaka kuwa na udhibiti wa taarifa kutoka kwa mashirika yanayoshirikiana na Mamlaka. Kwa mfano, Mamlaka haiwezi kupata taarifa za moja kwa moja za bidhaa za petroli kutoka nje ya nchi hadi taarifa hizo zotolewe na Wakala wa ununuzi Mafuta kwa Pamoja au Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari kwa ajili ya kufuatilia au kuhakiki/kufanya ulinganishi wa bidhaa hizo. Badala yake, Mamlaka inategemea taarifa kutoka kwa Wakala wa Vipimo kuwasilisha taarifa hizo kwa mfumo wa “excel”. Utegemezi huu unaipa Mamlaka

changamoto mbalimbali hasa katika usuluhishi wa takwimu za bidhaa za petroli, kukosa taarifa kwa wakati, na ugumu wa kutambua shehena/kiwango halisi na utumiaji hapa nchini. Pia, Mamlaka haina mbadala zaidi ya kulitegemea Shirika la Umeme Tanzania katika kupata mgao wake wa asilimia moja ya mauzo ya umeme, kwasababu mfumo wa "EPICOR 10" unaotumiwa na Mamlaka haujatengamanishwa na mfumo wa uuzaji wa umeme (LUKU) unaotumiwa na Shirika la Umeme Tanzania.

**Napendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ianzishe utengamanishi wa mifumo yake ya kielektroniki na Wakala wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja,Wakala wa Vipimo, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari na Shirika la Umeme Tanzania ili kuboresha mtiririko wa taarifa na kuwezesha upatikanaji wa takwimu zinazoaminika, kuwezesha kupatikana kwa taarifa muhimu kwa wakati, kuboresha usahihi wa takwimu za kiwango/shehena ya bidhaa za petroli na matumizi yake nchini, na kuwezesha ufuatiliaji na usimamizi wa taarifa za uwekaji wa mafuta katika maeneo maalumu.**

**(iii)** **Bodi ya Tumbaku Tanzania** haitumii fursa ya uwepo wa mfumo wa e-Mrejesho katika kuboresha mawasiliano na wadau wa Tumbaku, ili kuwawezesha kutuma, kufuatilia, na kupokea mrejesho wa maswali, malalamiko, na mapendekezo kwa njia ya mtandao na simu. Kutotumia mfumo huu ni kinyume na matakwa ya kanuni ya 40(b) ya Kanuni za Jumla za Serikali Mtandao za mwaka 2020. Hali hii inasababishwa na Bodi ya Tumbaku kutochukua hatua za kutenga fedha na kufanya mafunzo kwa watumishi wake kwa matumizi yenye ufanisi ya mifumo. Bodi inapoteza fursa za kuboresha huduma zake kwa kutumia mifumo na ufanisi wa kupokea na kushughulikia malalamiko kutoka kwa wadau wake.

**Ninapendekeza Bodi ya Tumbaku Tanzania ijiunge na kutumia mfumo wa e-Mrejesho katika kushughulika na utoaji wa huduma kwa wateja wake.**

**(iv)** Nimebaini **Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania** haitumii Mfumo wa Taarifa za Mbolea wa Kielekroniki (FIS) katika ufungashaji wa mbolea, uendeshaji wa maabara na uteketezaji wa mbolea, licha ya mfumo huo kuwa na uwezo wa kufanya kazi hizo na unaendelea kufanyiwa majaribio tangu mwezi Septemba 2023. Pia nilibaini mfumo wa Taarifa za Mbolea wa Kielekroniki unatumika katika usajiri wa mbolea, lakini haujatengamanishwa na mfumo wa kidijitali wa usambazaji na malipo ya mbolea ya ruzuku unaotumiwa katika mauzo

na usambazaji wa mbolea. Hili inasabishwa na Mamlaka kutochukua hatua za kutosha kuboresha uendeshaji wa shughuli zake kidigitali kupitia mfumo wa Taarifa za Mbolea wa Kielektroniki.

Kutotumia mfumo wa Taarifa za Mbolea wa Kielektroniki na kushindwa kuutengamanisha na mfumo wa kidijitali wa usambazaji na malipo ya mbolea ya ruzuku, unaiweka Mamlaka katika hatari ya kushindwa kudhibiti na kusimamia kikamilifu masuala ya mbolea na kutoa mianya ya mbolea zisizosajiliwa kuuzwa kwenye programu ya mbolea ya ruzuku.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania ichukue hatua kikamilifu kuhakikisha mfumo wa Taarifa za Mbolea wa Kielektroniki unatumika kikamilifu, na unatengamanishwa na mifumo mingine muhimu, ili kuwezesha ufanisi katika kudhibiti na kusimamia masuala ya mbolea.**

## 18.3 Mamlaka za Udhibiti Kukosa Ufanisi katika Utoaji na Usimamizi wa Leseni

Utoaji wa lesini unaziwezesha Mamlaka za Udhibiti kuhakikisha kuwa waliokidhi vigezo tu ndiyo wanapewa leseni za kutoa huduma ama kusambaza bidhaa ambazo Mamlaka hizo zinasimamia. Pia, utoaji leseni unazipa Mamlaka za Udhibiti nguvu ya kulinda maslahi ya umma kwa kuwa utoaji wa huduma na bidhaa unafanywa na waliokidhi vigezo tu na kuwa Mamlaka zinapata fursa ya kuwawajibisha watoa huduma au wasambazaji wa bidhaa endapo wataenda kinyume. Hata hivyo, nimebaini kukosekana kwa ufanisi katika mchakato wa utoaji au usimamizi wa leseni kwa Mamlaka za udhibiti tatu, kama ilivyoainishwa hapa chini;

**Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli** haijatekeleza mpango mkakati wa utoaji wa leseni uliopangwa kutekelezwa tangu mwaka 2023, kutokana na kusubiri kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi. Mpango ambao unalenga kukuza uwekezaji wa vitalu vya gesi na mafuta vilivyogunduliwa. Kuchelewa huku kunakwamisha uwezo wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu kukuza na kusimamia fursa za utoaji wa leseni, na kusababisha kupotea kwa fursa za uwekezaji na kupunguza ukuaji wa sekta ya mafuta na gesi.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli kuongeza kasi ya mchakato wa kupitia na kupitisha mpango mkakati wa utoaji wa leseni na kuhakikisha unatekelezwa**

Nilibaini kuwa **Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji** haifuatilii kwa ukamilifu leseni za muda mfupi zilizotolewa kwa kampuni nne za uzalishaji wa umeme, kutokana na kutokuwepo kwa muongozo wa kusimamia leseni za aina hii. Kampuni hizi hazijaleta taarifa za mwaka wala kutoa taarifa za utekelezaji za shughuli zinazohusiana na leseni hizi, na ujenzi wa vituo, hali ambayo ingeiwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kuchukua hatua za kiudhibiti kutokana na masharti ya leseni hizo. Hii siyo tu inazuia wawekezaji muhimu kutotumia maeneo bora ya uwekezaji wa ufuaji wa umeme, pia inaathiri tathmini ya usimamizi wa utekelezaji na viwango vya ubora, usalama, afya na mazingira, ambavyo baadaye vinaweza kuathiri ufuaji na uzalishaji wa umeme.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji kuweka na kutekeleza muongozo wa kusimamia utekelezaji wa leseni za muda mfupi zilizotolewa ili kutathmini maendeleo ya utendaji wa wawekezaji katika ujenzi wa vituo vya kuzalishia umeme**

Katika **Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania** nilibaini ucheleweshaji wa kati ya miezi mitano hadi 14, wa utoaji wa leseni kwa wadau 27 wa sekta ya bima. Ucheleweshaji huu ulitokana na kukosekana kwa ufanisi wa matumizi ya mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao kwa maombi ya leseni na kukosekana kwa takwimu za muda wa maombi yalipofanyika kwa ajili ya ufuatiliaji kubaini tarehe ya tangu maombi yalipofanyika na tarehe ambayo maombi yaliwasilishwa rasmi kwa ajili ya kupitishwa. Hali hii inaweza kukatisha tamaa waombaji wa leseni na inaweza kuzuia utii wa sheria na kuzuia juhudi za kukuza ukuaji wa sekta ya bima. Pia nilibaini watoa huduma za bima 132 wanaoendelea kutoa huduma za bima huku leseni zao zikiwa zimekwisha muda wake, lakini Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania haikuchukua hatua za kiudhibiti. Haya yanatokana na mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao na mfumo wa TIRAMIS kuruhusu watoa huduma za bima kuendelea na huduma bila kuwa na leseni.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania kusanidi mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao na mfumo wa TIRAMIS ili iwe na ufanisi katika kunasa na kufuatilia muda wa mchakato kutoa leseni, na umma ueleweshwe juu ya matumizi ya mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao**

## 18.4 Mapungufu ya Bodi za Mazao katika Usimamizi wa Mazao ya Biashara

Mazao ya Biashara yanajumuisha kahawa, korosho, pamba, mkonge, tumbaku, miwa, pareto na chai. Kila zao linasimamiwa na bodi ya zao husika ambayo huchochea ukuaji wa kilimo cha zao hilo na kusimamia masuala ya zao husika kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo. Pia, usimamizi wa mazao ya biashara unajumuisha uhusiano na mashirika mengine ya Serikali ambayo yanasimamia masuala ya upatikanaji wa mbolea na viatilifu. Katika ukaguzi, nilibaini mambo mahususi na ya jumla ambayo yanaathiri bodi ustawi wa mazao ya biashara pamoja na bodi za mazao husika kama ilivyoelezwa hapa chini;

### 18.4.1 Uwezekano wa Kukwama kwa Upanuzi wa Maeneo Mapya ya Kilimo cha Kahawa kutokana na Vikwazo Vilivyowekwa katika Mkataba wa Ulaya wa Kuzuia Uharibifu wa Misitu

Kwa mujibu wa Mpango Mkakati wa kuendeleza zao la kahawa wa mwaka 2021 hadi 2025, Bodi ya Kahawa Tanzania ililenga kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa hadi kufikia tani 300,000 (MT) kwa mwaka, ifikapo mwaka 2025, kwa kuongeza kiwango cha uzalishaji kwa heka na kuongeza maeneo mapya ya mashamba ya kahawa. Lakini, kipengele cha 225 cha Mkataba wa Ulaya wa Kuzuia Uharibifu wa Misitu, mkataba ambao Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Ulaya wa kuzuia uharibifu wa misitu, kinapendekeza hatua za kisheria zinazotaka uchunguzi kuwa unafanyika, uchunguzi ambao unaweza kupelekea kuwekewa vikwazo vya kutouza kahawa katika soko la Ulaya, endapo itabainika kuwa uharibifu wa misitu unatokana na shughuli za uzalishaji za kilimo. Hii inatokana na msisitizo mkali uliowekwa katika kusimamia na kuzingatia matakwa ya Mkataba huo, ambao malengo yake mama ni kuzuia uharibifu wa misitu na uoto wa asili. Uzingatiaji na utekelezaji wa matakwa ya Mkataba huo, kwa namna nyingine unazuia jitihada za Bodi ya Kahawa Tanzania na wakulima wa kahawa kuanzisha mashamba mapya ya kahawa kutoka katika maeneo ya misitu ambayo yanafaa kwa kilimo cha kahawa, licha ya Tanzania kama nchi kuwa na maeneo makubwa ambayo yanafaa kwa shughuli za kilimo.

**Ninapendekeza kuwa Bodi ya Kahawa Tanzania itumie mbinu bora na endelevu za kilimo kwa kutumia njia za kilimo ambazo hazikinzani na kanuni za kimataifa ili kupata soko katika masoko muhimu ya kimataifa, kuepuka vikwazo na kuwa na maeneo mbadala mbalimbali kwa kilimo cha kahawa. Hii iende sambamba na kuongeza ufanisi wa mavuno ya kahawa kwa kutumia mbinu bora za kilimo ili kuongeza ufanisi wa uzalishaji katika maeneo yaliyopo yanayolimwa kahawa kwa sasa.**

### 18.4.2 Utekelezaji Duni wa Mkakati wa Kuimarisha Bei ya Kahawa

Bodi ya Kahawa Tanzania haijafikia lengo lake la kimkakati la kuimarisha bei ya kahawa lililoainishwa katika Mpango Mkakati wake wa mwaka 2020/21 hadi 2024/25 Sehemu A, sambamba na utekeleaji wa kifungu cha 5(1) (c) cha Sheria ya Sekta ya Kahawa ya mwaka 2001. Hii ilitokana na uamuzi wa Wizara ya Kilimo kuchukua jukumu la kuimarisha bei za mazao sokoni kwa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo uliopewa jukumu la kusimamia uimarishaji wa bei za mazao kwa mazao yote ya biashara, ikiwemo zao la kahawa. Hata hivyo, Mfuko huo haujaanza kazi zake hadi sasa na Bodi ya Kahawa haijachukua hatua mbadala kushughulikia kuyumba yumba kwa bei ya kahawa sokoni, hali ambayo kwa kiasi kikubwa inaathiri uzalishaji wa zao la kahawa na sekta nzima ya kahawa kwa ujumla. Mpango Mkakati wa Bodi ya Kahawa ulilenga kusimamia na kudhibiti masuala yanayoathiri bei ya kahawa ili kuwa na udhibiti juu ya ubora wa kahawa na bei.

**Ninapendekeza kuwa Bodi ya Kahawa Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, ihakikishe mahitaji ya sekta ya kahawa yanajumuishwa na kuzingatiwa kikamilifu katika Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo. Pia, Bodi iwe na mpango mbadala wa hatua za kuchukua kuimarisha bei ya kahawa endapo Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo utaendelea kuchelewa kuanza kutekeleza majukumu yake.**

### 18.4.3 Uratibu Duni kati ya Bodi za Mazao, Halmashauri za Wilaya na Wadau Wengine

Bodi za mazao hazijihusishi moja kwa moja katika kilimo cha mazao bali huratibu na husimamia kilimo na biashara ya mazao wanayoyasimamia. Bodi za mazao zinaweka mazingira wezeshi ya kukuza uzalishaji, ubora, na ufanisi wa mavuno ya mazao ya biashara ambayo wanayasimamia ili kupata faida za kiuchumi na kuwa na athari chanya kwa wakulima na uchumi wa nchi kwa ujumla. Kilimo na uzalishaji wa mazao unafanywa na wakulima na makampuni ya kilimo katika maeneo yaliyo katika utawala wa Halmashauri za Wilaya, na kwa kuwezeshwa na wadau wengine katika sekta ya kilimo kama vile Vyama vya Ushirika vya Kilimo na Masoko na wauzaji na wasambazaji wa mbolea na viuatilifu. Hivyo, ufanisi wa uratibu wa shughuli za kilimo na wadau wa kilimo ni muhimu sana.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini Bodi za Mazao ambazo zilikuwa na mapungufu katika kuratibu shughuli za kilimo na biashara za mazao wanayayoyasimamia, kama ilivyoelezwa hapa chini;

Bodi ya Kahawa Tanzania na Bodi ya Pamba Tanzania hazijaweka makubaliano rasmi na wadau muhimu, jambo linalodhoofisha uwajibikaji na utekelezaji wa kisheria katika shughuli zao.

Bodi ya Kahawa Tanzania haina makubaliano ya ushirikiano na Halmashauri za Wilaya kunakolimwa kahawa katika mkoa wa Kagera, licha ya kuwa Bodi inakusanya ada za mauzo ya kahawa kwa niaba ya Halmashauri hizo na kuzitoza asilimia 1.5 ya ada hizo ikiwa ni kamisheni ya Bodi. Ushirikiano na utaratibu unaotumiwa sasa kati ya Bodi ya Kahawa na Halmashauri hizo unafanywa bila makubaliano ya kimaandishi na yenye mashiko kisheria, unazorotesha uwajibikaji na kukwamisha kuchukuliwa hatua za kisheria endapo kuna makosa ama kutofautiana kwa pande hizo.**Bodi ya Pamba Tanzania** haijaingia makubaliano na Vyama vya Ushirika vya Kilimo na Masoko katika usambazaji wa pembejeo za zao la pamba kwa wakulima, kinyume na kifungu cha 3(1) (d) cha Sheria ya Boadi ya Pamba ya mwaka 2001. Kwa mwaka wa fedha 2023/24 Bodi ilisambaza pembejeo za pamba zenye thamani ya shilingi bilioni 71.79 ukilinganisha na shilingi bilioni 75.38 mwaka 2022/23, na shilingi bilioni 74.39 mwaka 2021/22.

Nilibaini kuwepo kwa dosari katika usimamizi wa pembejeo za kilimo cha pamba katika vyama vya ushirika 10 vilivyochaguliwa kwa sampuli, ambapo fomu 30 kati ya fomu 50 za usambazaji wa pembejeo nilizopitia zilikuwa na dosari kama vile wakulima kusaini kwa niaba ya wengine, wakulima kupokea pembejeo bila kukiri kupokea, kukosekana kwa saini za watumishi wa mamlaka za Serikali za mitaa, kutofautiana kwa takwimu za viwango vya pembejeo kati ya pembejeo zilizopokelewa na AMCOS na takwimu za maghala ya kuhifadhia pembejeo, na ugawaji wa pembejeo kwa wakulima bila kuzingatia ukubwa wa mashamba ya wakulima.

Kutokuwepo kwa makubaliano ya kimaandishi kunaweza kupunguza uwajibikaji na kukwamisha hatua za kisheria endapo kutatokea migogoro, ubadhilifu au matumizi mabaya ya pembejeo kwa Vyama vya Ushirika vya Kilimo na Masoko.

**Ninapendekeza (a) Bodi ya Kahawa Tanzania iweke makubaliano thabiti ya kimaandishi kati yake na halmashauri za wilaya inazofanyanazo kazi na kuweka bayana masharti na misingi ya makubaliano hayo kwa upana wa utekelezaji wa majukumu yake na (b) Bodi ya Pamba Tanzania iweke makubaliano thabiti ya kimaandishi kati yake na Vyama vya Ushirika vya Kilimo na Masoko.**

**Bodi ya Korosho Tanzania** ilishindwa kuratibu utunzaji na upatikanaji wa nyaraka kutoka Vyama vya Ushirika vya Kilimo na Masoko na wakulima wa Korosho kuhusiana na usambazaji wa pembejeo za korosho zilizotokana na rukuzu ya Serikali kwa miaka miwili mfululizo zenye jumla ya shilingi bilioni 69.68 (shilingi bilioni 40 kwa mwaka 2023/24 na shilingi bilioni 29 kwa mwaka 2022/23), usambazaji ambao ulisimamiwa na Vyama vya Ushirika vya Kilimo na Masoko kwa niaba ya Bodi ya Korosho, katika juhudi za kukuza sekta ya korosho. Licha ya Bodi ya Korosho kutoa muongozo wa usambazaji mwezi Mei 2022, nilibaini kutokuwepo kwa ushahidi wa wakulima kukiri kupokea pembejeo hizo. Kwa mfano, taarifa kutoka kwa wasambazaji wakuu TANECU na RUNALI iliyoorodhesha majina ya wakulima kutoka vyama 62 vya msingi (AMCOS) ilitolewa, lakini haikuonesha namba za simu za wakulima wala kiasi cha viuatilifu walichopokea. Aidha, wasambazaji wengine wakuu kama MAMCU, Lindi Mwamboa, TAMCU na CORECU hawakuwa na orodha ya wanufaika , wazabuni sita kuzidisha bei ya viuatilifu shilingi bilioni 2.79 , wazabuni kutolipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) shilingi bilioni 16.06 , na kukosekana kwa ushahidi wa viuatilifu vilivyorudishwa vyenye thamani ya shilingi milioni 810.

Nilibaini kuwa, dosari hizi zilisababishwa na uratibu na ufuatiliaji duni wa Bodi ya Korosho Tanzania katika kuhakikisha muongozo wa usambazaji unafuatwa ili kudhibiti ubadhilifu. Hivyo, kwa sasa nimeshindwa kutoa maoni juu ya uhalali wa usambazaji uliofanyika na kama tija na thamani ya fedha za Serikali imepatikana, hadi pale nyaraka na ushahidi wa usambazaji uliofanywa zitakapowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na uhakiki.

**Ninapendekeza Bodi ya Korosho Tanzania, ianzishe na kutekeleza hatua stahiki na toshelevu katika kusimamia, kudhibiti na kufuatilia fedha za pembejeo za kilimo na kutunza ushahidi kwa ajili ya Mamlaka zingine kuhakiki.**

### 18.4.4 Uwezo Mdogo wa Uzalishaji wa Mbolea Nchini, Hali Inayopelekea Utegemezi Mkubwa wa Uagizaji kutoka Nje

Katika ukaguzi wa **Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania**, nilibaini kuwa, kwa miaka minne mfululizo, kiwango cha uzalishaji wa mbolea nchini kimekuwa kikiongezeka, lakini kwa kasi ndogo. Kwa mwaka wa fedha 2023/24, ni asimilia 17 tu ya mbolea yote iliyosambazwa, ilizalishwa hapa nchini (Rejea **Jedwali Na. 57**). Kwa hali hii, uagizaji wa mbolea kutoka nje hauepukiki. Hali hii inasababishwa na uwekezaji usiotosheleza katika uzalishaji wa pembejeo za kilimo hapa nchini. Hata hivyo, Serikali imeweka mipango na mikakati ya kuwashirikisha wawekezaji zaidi kuja kuweka hapa nchini na kuna

viwanda vinne vikubwa ambavyo tayari vipo na endapo vitaanza uzalishaji kikamilifu, vitaweza kukidhi mahitaji ya mbolea ya ndani

**Jedwali Na. 57: Mwenendo wa uzalishaji mbolea nchini dhidi ya uagizaji kutoka nje ya nchi 2020/21 -2023/24**

| Na. | Mwaka | Mbolea iliyozalishwa nchini (MT) | Mbolea iliyongizwa kutoka nje ya nchi (MT) | Jumla ya mbolea iliyosambazwa nchini (MT) | Asilimia za mbolea iliyozalishwa nchini |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2020/21 | 42,695 | 504,122 | 546,817 | 7.81 |
| 2 | 2021/22 | 62,724 | 379,927 | 442,651 | 14.17 |
| 3 | 2022/23 | 84,646 | 824,085 | 908,731 | 9.31 |
| 4 | 2023/24 | 158,628 | 728,758 | 887,386 | 17.88 |

**Chanzo***: Taarifa za mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja kutoka nje kwa kipindi cha mwaka 2020/21-2023/24.*

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania ishirikiane na Serikali kuweka mikakati ambayo itakuza mnyororo himilivu na mseto wa upatikanaji wa mbolea. Hii inajumuisha uwekezaji katika viwanda vya ndani ya nchi, utafiti na uendelezaji wa teknolojia ya mbolea, pamoja na sera ambazo zinawezesha mbinu himilivu za kilimo.**

### 18.4.5 Haja ya Kutathmini Upya Utekelezekaji wa Ununuzi wa Mbolea kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja

**Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania** ilianzisha mbinu ya kununua mbolea kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja kwa kuzingatia kanuni ya 7(1) ya Kanuni za Mbolea (Ununuzi wa Pamoja) za mwaka 2017, kwa lengo la kufaidika na faida za ununuzi wa kiwango kikubwa na kutoa fursa kwa wakulima kupata mbolea zenye ubora kwa bei nafuu.

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwa, ununuzi wa mbolea kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja haukuwa na ufanisi. Uchanganuzi wa kikaguzi ulibaini kuwa, kwa miaka minne mfululizo kuanzia mwaka 2020/21 hadi 2023/24, Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja ulitumika mara moja tu mwaka 2022/23 ambapo tani 48,530 zilinunuliwa sawa na asilimia 2 ya mbolea yote iliyonunuliwa kutoka nje, tani 2,388,362, kwa kipindi hicho cha miaka minne (Rejea **Jedwali Na. 58).**

Pia nilibaini kuwa, ni mbolea aina ya UREA na DAP tu ndizo walau zilinunuliwa kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja. Aina zingine za mbolea kama vile Calcium Ammonia Nitrate (CAN), Ammonium Sulphate (SA), NPK na zingine ambazo Mamlaka ingezitangaza kwa mamlaka yake, hazijawahi kununuliwa kwa Mfumo wa Ununuzi wa

Pamoja. Kwa kuwa kiwango kilichonunuliwa kwa Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja ni kidogo, hapakuwa na manufaa makubwa ya matumizi ya mfumo huo.

**Jedwali Na. 58: Mwenendo wa ununuaji mbolea kutoka nje kwa Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja kwa miaka minne**

| Na. | Mwaka | Aina ya mbolea iliyonunuliwa kwa Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja (MT) | | Jumla ya mbolea iliyonunuliwa kwa Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja (MT) | Jumla ya mbolea iliyonunuliwa nje ya Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja (MT) | Jumla ya mbolea iliyonunuliwa kutoka nje (MT) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | UREA | DAP | | | |
| 1 | 2020/21 | 33,948 (Ilifutwa) | 21,016 (Ilifutwa) | 0 | 504,122 | 504,122 |
| 2 | 2021/22 | Iliruhusiwa kutokutumia mfumo wa pamoja | Iliruhusiwa kutokutumia mfumo wa pamoja | 0 | 379,927 | 379,927 |
| 3 | 2022/23 | 27,670 | 20,860 | 48,530 | 775,555 | 824,085 |
| 4 | 2023/24 | 0 | 0 | 0 | 728,758 | 728,758 |
| | **Jumla** | **27,670** | **20,860** | **48,530** | **2,388,362** | **2,436,892** |

**Chanzo**: *Taarifa za mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja kutoka nje kwa kipindi cha mwaka 2020/21-2023/24*

Kasoro nilizozibaini zinasababishwa na wafanyabiashara wa mbolea kukwepa kuingia gharama za ziada zinazotokana na Dhamana za benki na Barua za Mkopo (LC) kwa shehena za mbolea wanazotaka kuingiza nchini kwa njia ya Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja ulioanishwa kwenye kanuni. Pia, tofauti na ilivyo kwa UREA na DAP, mahitaji ya wakulima kwa aina zingine za mbolea yanakuwa chini ya kiwango cha chini cha tani 15,000 kinachohitajika kufikiwa ili kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja. Hivyo, faida iliyokusudiwa za ununuzi wa pamoja na kupunguza bei za mbolea, hazifikiwi.

**Ninapendekeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania kwa kushirikia na Wizara ya Kilimo na wadau wengine, kutathmini upya uhalisia wa ununuzi wa mbolea kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja, na kuweka mfumo halisia wa kununua mbolea kutoka nje. Pia, wakulima waelimishwe juu ya matumizi ya aina zingine za mbolea tofauti na UREA na DAP.**

19

# Utendaji wa Mashirika ya Umma Katika Sekta ya Afya



## SURA YA KUMI NA TISA

## UTENDAJI WA MASHIRIKA YA UMMA KATIKA SEKTA YA AFYA

### 19.0 Utangulizi

Ukaguzi wa utendaji katika huduma za afya hutathmini ubora wa huduma, utayari wa kutoa huduma na minyororo ya usambazaji wa dawa. Ukaguzi huu pia umetathmini gharama zilizoingiwa na hospitali kwa wagonjwa wa msamaha, uwepo wa dawa zilizokwisha muda au zinazokaribia kuisha muda wake, madeni ya Mfuko wa Bima ya Afya yaliyokataliwa. Tathmini hii inalenga kuboresha huduma katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, na Bohari Kuu ya Dawa.

### 19.1 Gharama Kubwa Iliyoingiwa na Hospitali ya Muhimbili kutokana na Wagonjwa wa Msamaha - shilingi bilioni 17.84

Kanuni Namba 6.3.1 ya Kanuni na Taratibu za Uhasibu za Hospitali ya Taifa Muhimbili za mwaka 2022, inaitaka Hospitali kutoa msamaha kwa mujibu wa sera ya msamaha ya Serikali na sera ya msamaha wa Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Nilibaini Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila ilitumia shilingi bilioni 3.93 kwa wagonjwa wa msamaha kwa mwaka wa fedha 2023/24, ikiwa ni ongezeko la shilingi milioni 58.28 kutoka shilingi bilioni 3.87 kwa mwaka wa fedha 2022/23. Vile vile, Hospitali ya Taifa Muhimbili ilitumia shilingi bilioni 13.91 kwa wagonjwa wa msamaha kwa mwaka wa fedha 2023/24, ikipungua kwa shilingi bilioni 4.88 kutoka shilingi bilioni 18.80 kwa mwaka wa fedha 2022/23. Gharama za wagonjwa wa msamaha kwa Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila zimechukua asilimia 8 ya bajeti ya hospitali kwa mwaka 2023/24 kwa mashirika yote mawili, ikionesha changamoto ya fedha.

Katika ukaguzi, nilibaini kuwa sera ya Afya ya Taifa haikuweka wazi kama hospitali zinatakiwa kudai na kurejeshewa gharama zilizotumika katika kuwatibu wagonjwa wa msamaha. Hali hii inaleta changamoto ya namna ambavyo gharama zilizoingiwa na hospitali kwenye matibabu ya wagonjwa wa msamaha zitarejeshwa, kwa kuwa gharama hizi zinaathiri utendaji wa hospitali.

**Ninapendekeza Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Taifa Muhimbili -Mloganzila wawasiliane na Wizara ya Afya (a) kuweka mwongozo wa jinsi gharama za matibabu ya wagonjwa wa msamaha zitakavyorejeshwa**

### 19.2 Uwepo wa Dawa ziliokwisha na zinazo Karibia Kuisha Muda Wake wa Matumizi za shilingi bilioni 9.29

Wakati wa ukaguzi, nilibaini kuwepo wa dawa za kawaida na maalumu zilizokwisha muda wake katika Bohari Kuu ya Dawa, zenye thamani ya shilingi bilioni 4.18 kwa mwaka wa fedha 2023/24, ambapo kiwango hicho

kilipungua kwa shilingi bilioni 7.56 kutoka shilingi bilioni 11.74 katika mwaka wa fedha 2020/21.

Pia, katika Bohari Kuu ya Dawa nilibaini uwepo wa dawa zenye thamani ya shilingi bilioni 4.86 zilizobakiza muda wa mwezi mmoja hadi miezi sita kabla ya kumalizika kwa muda wake wa matumizi. Dawa hizi bado zilikuwa hazikutolewa bure wala kutolewa kwa punguzo la bei kinyume na Mwongozo wa Usimamizi wa Dawa na Vifaa tiba Ghalani, ambao unaelekeza dawa zilizobakiza kuanzia mwezi mmoja hadi miezi mitatu kabla ya kumalizika kwa muda wake wa matumizi zitolewe bure zikiambatana na barua inayoeleza zitatumiwa kabla ya kumalizika muda huo, na pia zilizobakiza muda wa miezi minne hadi sita kabla ya kumalizika muda wake, zitolewe kwa punguzo la bei au bure baada ya kupata idhini kutoka kwa menejimenti.

Nilibaini kuwa dawa zilizokuwa zimebaki kwenye maghala mwishoni mwa mwaka wa fedha 2023/24 ambazo muda wa matumizi ulishapita ni asilimia 2 ya jumla ya dawa zilizopo ghalani, hali inayoashiria upotevu wa fedha na kukosekana kwa ufanisi.

Vilevile, katika mwaka wa fedha 2023/24 nilibaini Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, ilikuwa na dawa zenye thamani ya shilingi milioni 107.91 zilizoisha muda wa matumizi. Aidha, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, dawa zilizoisha muda wake zilikuwa na thamani ya shilingi milioni 156.74.

Dawa zilizokwisha muda katika Bohari Kuu ya Dawa zilisababishwa na makisio duni yanayopelekea kukisia mahitaji ya wateja yasiyo na uhalisia, uwepo wa bidhaa zisizotumika, zinazotumika polepole na bidhaa zilizopitwa na wakati na kutozingatia ratiba za wasambazaji wa bidhaa. Katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila, baadhi ya vitendanishi viliisha muda wa matumizi kwa sababu ya kuharibika kwa mashine maalumu isiyoweza kutengenezeka kirahisi na pia haiwezi kutumika kwenye vituo vya afya vingine. Kwa upande wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, bidhaa zinazotumika kwenye mashine za matibabu ya kibingwa haziwezi kutumika sehemu nyingine, hivyo kupelekea kupitwa na wakati.

Dawa zilizoisha muda wa matumizi siyo tu hutumia nafasi kwenye ghala lakini pia huongeza hatari ya kuzorota zaidi, na kusababisha changamoto za uendeshaji.

**Ninapendekeza (a) Bohari Kuu ya Dawa iimarishe mchakato wake wa makisio ya mahitaji kwa kutumia taarifa ya matumizi ya hospitali ya wakati halisi ili kufanya maamuzi ya ununuzi yanayotokana na taarifa sahihi na kupunguza bidhaa zinazotumika polepole au bidhaa za ziada; na (b) Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila ziharakishe utupaji salama wa dawa zilizokwisha muda wake kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali.**

## 19.3 Madai ya Hospitali Yaliyokataliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya shilingi bilioni 11.23

Wakati wa ukaguzi wangu wa mwaka 2023/24, nilibaini Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulikataa jumla ya madai ya shilingi bilioni 11.23 (asilimia 16 ya madai yote ya shilingi bilioni 68.25) kutoka hospitali mbili za umma zinazooneshwa kwenye **Jedwali Na. 59**. Mwenendo unaonesha kumekuwa na ongezeko la kukataliwa kwa madai ambapo mwaka 2020/21 madai ya shilingi bilioni 3.87 sawa na asilimia 7 ya madai yalikataliwa. Mwaka 2021/22 jumla ya madai ya shilingi bilioni 8.84 sawa na asilimia 10 ya madai yalikataliwa na mwaka 2022/23 madai ya shilingi bilioni 11.83 sawa na asilimia 15 ya madai yalikataliwa.

Sababu kuu za kukataliwa ni kutozingatia bei ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, ubadilishaji wa bidhaa ya huduma, dozi isiyofaa na kiasi, ada za kumuona daktari ambazo hazitumiki, kutofanya uhakiki sahihi wa madai kabla ya kuwasilishwa.

**Jedwali Na. 59: Madai ya bima ya afya yaliyokataliwa na Mfuko wa Taifa wa Bima wa Afya**

| Na. | Jina la Shirika | Kipindi | Jumla ya Kiasi Kilichotozwa | Kiasi kilichokataliwa | Asilimia iliyokataliwa |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Sh. '000 | | |
| 1 | Hospitali ya Taifa Muhimbili | Julai 23 mpaka Juni 24 | 46,835,087 | 7,372,424 | 16 |
| 2 | Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mloganzila | Julai 23 mpaka Juni 24 | 21,418,361 | 3,862,512 | 18 |
| | **Jumla** | | **68,253,448** | **11,234,936** | **16** |

**Chanzo**: *Uchambuzi wa Hati za madai za Mfuko wa Bima ya Afya*

Ukwasi ya mashirika haya unaweza kuathiriwa sana kutokana na kukataliwa kwa madai kunakosababisha upotevu wa fedha.

**Ninarudia tena mapendekezo yangu kuwa Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila zianzishe utaratibu wa kupitia upya sababu zote za madai kukataliwa na kutoa mrejesho kwa wakati kwa maafisa wanaohusika na sehemu zinazoshughulikia utoaji wa huduma za afya ili kuzuia au kupunguza kurudia kwa tatizo katika siku zijazo.**

## 19.4 Kuimarisha Uendelevu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Kuongeza Wigo wa Uanachama

Kulingana na utendaji wa kifedha wa mwaka 2023/24, uendelevu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umeimarika kwa kiasi kikubwa, kama inavyothibitishwa na faida ya shilingi bilioni 75.51, ikilinganishwa na hasara kubwa za shilingi bilioni 214.14 na shilingi bilioni 205.95 zilizopatikana katika miaka ya fedha 2022/23 na 2021/22, mtawalia.

Mfuko umeshuhudia ukuaji wa michango ya wanachama kwa shilingi bilioni 66.59 sawa na asilimia 10.5, ikiongezeka kutoka shilingi bilioni 633.51 mwaka 2022/23 mpaka shilingi bilioni 700.10 mwaka 2023/24, sambamba na kupungua kwa matumizi zinazohusiana na wanachama kwa shilingi bilioni 166.08 sawa na asilimia 21.5, yakipungua kutoka shilingi bilioni 771.68 mpaka shilingi bilioni 605.59 ndani ya kipindi hicho. Hii imepelekea kupata faida kutokana na kuhudumia mwanachama ya shilingi bilioni 94.50 ikilinganishwa na hasara kutokana na kuhudumia mwanachama ya shilingi bilioni 109.77 kwa mwaka 2022/23 na shilingi bilioni 121.67 katika mwaka wa fedha 2021/22.

Hata hivyo, uendelevu wa muda mrefu wa Mfuko bado unazuiliwa na kutokuwa na uwezo wa kufikia usajili wa wanachama waliolengwa. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulisajili wanachama 570,800 pekee, sawa na asilimia 78 ya lengo lake la mwaka la wanachama 731,796, hasa kutokana na mikakati isiyotosheleza ya kuwafikia wananchi waliopo katika sekta binafsi.

Kushindwa kufikia malengo ya kusajili wanachama kunadhoofisha uwezo wa Mfuko kupanua wigo wake wa kuweza kutoa huduma na kupata mapato.

**Ninapongeza juhudi za Serikali na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa uboreshaji mkubwa wa utendaji wa kifedha na hatua zilizochukuliwa ili kuimarisha uendelevu wa Mfuko. Hata hivyo, ili kuimarisha zaidi uendelevu wa muda mrefu, ninapendekeza Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uongeze mipango yake ya kuwafikia wananchi ili kuboresha uelewa na kuongeza usajili, hasa katika sekta binafsi.**

## 19.5 Ucheleweshaji wa Malipo Unaofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

Kifungu cha 28 cha Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Sura ya 395 kinasema kuwa madai yoyote ya fedha ya mtoa huduma ya afya yatalipwa ndani ya siku 60 baada ya madai hayo kuwasilishwa kwenye mfuko wa Bima ya Afya. Jumla ya madai 58,937 yalichakatwa kuanzia Julai 2023 hadi Juni 2024 na jumla ya kiasi kilicholipwa ni shilingi bilioni 650.42.

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulilipa asilimia 55 ya madai 58,937 yenye thamani ya shilingi bilioni 416.08 zaidi ya siku 60. Mapitio ya kina ya muda wa madai yalionesha ucheleweshaji mkubwa katika ofisi mbalimbali za mfuko, ambapo ucheleweshaji mkubwa zaidi ulionekana ofisi ya Dodoma, ikiwa ni ucheleweshaji wa wastani wa siku 122.

Malipo kwa watoa huduma za afya yanacheleweshwa nje ya muda wa makubaliano kutokana na ufinyu wa fedha unaotokana na ucheleweshaji wa michango inayotakiwa kuwasilishwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kila mwezi.

Ucheleweshaji wa malipo unaweza kupelekea changamoto ya kifedha kwa watoa huduma ya afya, hivyo kuathiri utoaji wa huduma yenye ubora na kwa wakati kwa wanufaika wa Mfuko.

**Ninapendekeza kuwa Mfuko wa Bima ya Afya uweke mkakati wa kuhakikisha michango inawasilishwa kwa wakati kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kuwezesha kulipa madai ya watoahuduma.**

## 19.6 Bohari Kuu ya Dawa Kushindwa Kutimiza Oda za Dawa na Vifaa Tiba Zinazowasilishwa na watoa Huduma wa Afya

Utekelezaji wa Oda unapimwa kwa asilimia za oda ambazo Bohari Kuu ya Dawa inaweza kuzitekeleza na inaonesha uwezo wa Bohari kuweza kukidhi mahitaji ya wateja. Hili ni moja ya malengo katika mpango mkakati wa Bohari Kuu ya Dawa wa mwaka 2021-2026 wa kuweza kutekeleza oda za dawa na vifaa tiba kwa asilimia 90 ifikapo Juni 2026, ambapo lengo kwa mwaka 2023/24 lilikuwa uwezo wa kutekeleza asilimia 90 ya oda.

Bohari Kuu ya Dawa ilipokea jumla ya oda 114,966,729 kutoka kwenye hospitali za rufaa, za mikoa na vituo vya afya, ambapo ilitekeleza oda 90,769,925 sawa na asilimia 79 na kushindwa kutekeleza oda 24,196,804 sawa na asilimia 21. Tathmini inaonesha kuna kuimarika kwa hali ya utekelezaji wa oda ikilinganishwa na miaka miwili iliyopita, ambapo mwaka 2022/23, Bohari ilipokea jumla ya oda 105,646,079 na kuweza kutekeleza asilimia 76 na kwa mwaka 2021/22 Bohari ilitekeleza asilimia 33 tu ya oda.

Uchambuzi wangu zaidi wa hospitali zilizoagiza vifaa tiba na dawa kutoka Bohari Kuu ya Dawa ulibaini kuwa hospitali saba ziliagiza vifaa tiba na dawa zenye thamani ya shilingi bilioni 14.15 kutoka Bohari Kuu ya Dawa. Hata hivyo, Bohari Kuu ya Dawa iliwasilisha vifaa tiba na dawa zenye thamani ya shilingi bilioni 6.10 na kutoa cheti cha kuishiwa bidhaa zenye thamani ya shilingi bilioni 8.04 sawa na asilimia 57. Kushindwa kutekeleza oda kunatokana na makisio yasiyo halisi ya mahitaji ya wateja. Pia, kunasababishwa na ukata kutokana na deni ambalo Bohari Kuu ya Dawa inaidai Serikali. Taarifa kuhusu oda ambazo Bohari Kuu ya Dawa ilishindwa kutekeleza imeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 60.**

**Jedwali Na. 60:Oda za Hospitali zilizoshindwa Kutekelezwa na Bohari Kuu ya Dawa**

| Na | Jina la Hospitali | Oda Sh. '000 | Oda iliyopokelewa Sh. '000 | Oda ambazo hazijatekelezwa Sh. '000 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Hospitali ya Kanda ya Rufaa Chato | 1,525,913 | 342,711 | 1,183,202 |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Geita | 887,358 | 411,105 | 476,253 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Iringa | 2,582,134 | 2,000,227 | 581,907 |
| 4 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Maweni | 2,976,024 | 594,862 | 2,381,162 |
| 5 | Hospitali ya Mirembe | 2,851,338 | 1,342,090 | 1,509,248 |
| 6 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Shinyanga | 1,606,890 | 689,562 | 917,328 |
| 7 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Singida | 1,721,219 | 721,178 | 1,000,041 |
| **Jumla** | | **14,150,876** | **6,101,735** | **8,049,141** |

**Chanzo:** *Oda na Hati ya Madai Zilizowasilishwa Bohari Kuu ya Dawa*

Zaidi, nilibaini kuwa oda za mauzo 10 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.17, kati ya oda 18 zilizochanguliwa kwa sampuli, zilichelewa kutekelezwa kwa siku kati ya 289 hadi 935.

Uhaba wa Dawa na vifaa tiba unapelekea hospitali kushindwa kutoa matibabu kwa wakati, jambo linalosabisha kuchelewa kwa huduma. Hali hii inaweza kuathiri hali za wagonjwa na pia kupelekea kununua vifaa tiba na Dawa kutoka kwa wasambazaji wengine kwa bei kubwa.

**Ninapendekeza Bohari Kuu ya Dawa ishirikiane na Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha kuhakikisha fedha zinatolewa kwa wakati kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na dawa na kuhakikisha kuwa deni la Bohari Kuu ya Dawa linalipwa na Serikali ili kuongeza ukwasi wa Bohari Kuu ya Dawa.**

## 19.7 Kiwanda cha Dawa cha Keko Kufanya Mauzo kwa Mkopo Bila Mikataba

Kipengele cha 5.1 na 5.2 cha Taratibu za Uendeshaji wa Mauzo za Kiwanda cha Dawa cha Keko, za mwaka 2023, kinataka mauzo yote yanayofanyika kwa Mkopo kwa Wateja yafanyike kwa njia ya mkataba. Katika ukaguzi wa Kiwanda cha Dawa cha Keko nilibaini mauzo yaliyofanyika mwaka 2023 na 2024 ya shilingi bilioni 4.58 na shilingi bilioni 4.39 mtawalia, yalifanyika kwa wateja bila ya kuwa na mkataba.

Hii ilitokana na kutofuata sheria za ndani zinazosimamia mauzo. Mauzo yanayofanyika bila ya mkataba yanaweza kupelekea kiwanda hicho kushindwa kurejesha fedha za bidhaa zilizouzwa kwa mkopo kwa wateja.

**Ninapendekeza kuwa Kiwanda cha Dawa cha Keko kihakikishe mauzo yote yanayofanyika kwa wateja, yanafanyika kwa njia ya mkataba.**

## 19.8 Kusuasua kwa Uzalishaji wa Dawa katika Kiwanda cha Dawa cha Keko

Kiwanda cha Dawa Keko kina idara ya uzalishaji yenye maeneo mawili ambayo ni eneo la uzalishaji dawa aina ya penicillin na eneo la uzalishaji wa dawa ambazo siyo penicillin ambayo huzalisha Kapsuli na vidonge mtawalia.

Wakati wa ukaguzi wangu kwa mwaka 2024 nilibaini kiwanda hicho kilifanya uzalishaji wa dawa chini ya kiwango kilichopangwa kufikiwa, kwa miaka mitatu mfululizo ambapo uzalishaji ulikuwa asilimia 40, 66 na 40 kwa mwaka 2021/22, 2022/23 na 2023/24 mtawalia. Taarifa kuhusu uzalishaji huo imeoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. XXII**.

Uzalishaji wa kiwango cha chini ya lengo ulisababishwa na kutopatikana kwa malighafi kutokana na kutokuwa na mtaji wa kutosha wa kufanya kazi, kuharibika kwa mashine na kukatika kwa umeme.

Uzalishaji wa dawa chini ya kiwango unapelekea kutokukidhi mahitaji ya wateja na kukosa mapato.

**Ninapendekeza Kiwanda cha Dawa Keko kiweke na kutekeleza mikakati thabiti ya kuimarisha mtaji utakaowezesha upatikanaji wa fedha za kununua malighafi na kuongeza uzalishaji.**

## 19.9 Kiwanda Cha Dawa Keko Kutozingatia Njia Bora za Uzalishaji wa Dawa

Kanuni ya 7 (1) na (2) ya Vyakula, Dawa na Vipodozi Tanzania (Utaratibu Bora wa Utengenezaji) za mwaka 2018 inaitaka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania kutoa cheti kwa kiwanda ambacho kimetimiza mahitaji yanayohitajika ya Utaratibu Bora wa Utengenezaji na cheti kitakuwa halali kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mapitio yangu ya ripoti ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania ya Mei 2023 yalibaini kuwa Kiwanda Cha Dawa Keko hakikuzingatia mahitaji ya chini ya Mwongozo wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania wa "Utaratibu Bora wa Utengenezaji".

Mapitio zaidi ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Utaratibu Bora wa Utengenezaji yaliyotolewa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba kwenda kwa Kiwanda cha Dawa Keko yalibaini kiwanda kiliweza kufanyia kazi mapendekezo 29 sawa na asilimia 59 kati ya mapendekezo 49 ambayo yaligawanywa kwa umuhimu, ukubwa na udogo.

Hii imesababishwa na; Uwepo wa teknolojia ya zamani ya mashine na vifaa vinavyosababisha kutokuwepo kwa ufanisi wa uzalishaji; Idadi ndogo ya wafanyakazi wa kiufundi katika Kiwanda; na Ukosefu wa mtaji wa kufanya kazi kwa ajili ya kununua malighafi.

Hali hii ya kufuata utaratibu usioendana na Utaratibu Bora wa Utengenezaji huweza kusababisha kushindwa kupenya katika soko pana.

**Ninapendekeza kuwa Kiwanda Cha Dawa Keko kihakikishe (a) kinaajiri idadi ya kutosha ya wafanyikazi wa kiufundi ili kutekeleza majukumu ya uzalishaji kwa mujibu wa Utaratibu Bora wa Utengenezaji, (b) kibadilishe mashine na vifaa vya zamani na kuwekwa mashine na vifaa vyenye teknolojia ya kisasa ili kuhakikisha ufanisi wa uzalishaji kulingana na Utaratibu Bora wa Utengenezaji; na (c) kishirikiane na Wizara ya Fedha juu ya kuboresha mtaji wa kiwanda ili kuwezesha ununuzi wa malighafi na vifaa vya kisasa vya uzalishaji.**

# Ufanisi Katika Sekta ya Madini, Gesi na Mafuta



# SURA YA ISHIRINI

# UFANISI KATIKA SEKTA YA MADINI, GESI NA MAFUTA

## 20.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea usimamizi wa sekta za madini, mafuta, na gesi, ikizingatia usawa wa rasilimali, uzingatiaji wa mazingira, na uwazi wa mapato. Sekta hii inajumuisha wadau wakuu kama Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Shirika la Umeme Tanzania, Kampuni ya Gesi Tanzania, Shirika la Madini la Taifa, Kampuni ya STAMIGOLD, Shirika la Taifa la Maendeleo, Tume ya Madini, Wizara ya Madini, na Wizara ya Nishati.

Uchambuzi huu unalenga kuwapa watunga sera, wasimamizi, na wadau, mbinu za kimkakati zinazohitajika ili kuimarisha ukuaji endelevu na maendeleo ya sekta ya madini, gesi na mafuta nchini. Uchambuzi huu umebaini changamoto mbalimbali zinazoathiri utendaji wa jumla wa sekta ya madini, gesi na mafuta.

## 20.1 Kasi Ndogo ya Utekelezaji wa Mradi wa Kuzalisha Magadi katika Eneo la Engaruka

Mradi wa Magadi wa Engaruka, kama ulivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, unalenga kujenga kiwanda cha uzalishaji wa tani milioni 10 za magadi kwa mwaka ifikapo 2025. Mradi huu, unaotekelezwa na Shirika la Maendeleo ya Taifa, kwa sasa uko katika hatua za awali za upatikanaji wa leseni za uchimbaji na ulipaji wa fidia kwa jamii zilizoathirika. Upembuzi yakinifu, uliokamilika mwaka 2019, ulilenga kurahisisha uwekezaji na hatua ya ujenzi. Hata hivyo, kasi imekuwa ndogo sana tangu wakati huo.

Ucheleweshaji huu unatokana na kuchukua muda mrefu wa kupata leseni za uchimbaji kulikotokana na ukata wa fedha za kulipa fidia kwa wananchi waliothirika. Licha ya tathmini ya fidia kukamilika Januari 2024, ambapo shilingi bilioni 14.48 zilitengwa kwa ajili ya mamlaka nne za Serikali za mitaa na wananchi 595 waliothirika, hadi tarehe ya ukaguzi wa 14 Oktoba 2024, hakuna malipo yoyote yaliyokuwa yamefanyika licha ya fedha kutoka hazina kutolewa mwezi Mei 2024.

Ucheleweshaji huu unakiuka kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Utwaaji wa Ardhi Sura ya 118 na unasababishwa na ucheleweshaji wa utoaji wa fedha za Serikali. Hali hii inaathiri maendeleo ya mradi, na kusababisha ucheleweshaji wa kukamilika kwa mradi mzima.

Kwa kuzingatia hali ya sasa ya mradi, nina wasiwasi kuwa mradi huu uko hatarini kutokamilika kwa mwaka 2025 kama ilivyoainishwa

katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa, jambo ambalo linaweza kuchelewesha manufaa ya kiuchumi yanayotarajiwa.

**Ninapendekeza Shirika la Maendeleo ya Taifa liweke kipaumbele suala la malipo ya fidia, pamoja na kupata leseni za uchimbaji. Pia, litekeleze mpango wa kuharakisha mradi kwa kuweka ratiba yenye muda maalumu ili kupunguza ucheleweshaji zaidi na kuhakikisha mradi unasonga mbele kwa wakati.**

## 20.2 Ucheleweshaji wa Uanzishwaji wa Mradi wa Chuma Liganga

Mradi wa chuma Liganga ni miongoni mwa miradi ya kimkakati inayolenga kuimarisha uchumi wa viwanda wa Tanzania kwa kuanzisha sekta za msingi zitakazosaidia sekta nyingine katika mnyororo wa thamani. Mradi huu unakadiriwa kuzalisha mapato ya zaidi ya dola za Marekani bilioni 1.2 kila mwaka kutokana na uzalishaji wa madini ya chuma, titani, vanadium, na sulfati ya alumini.

Mradi huu ulianzishwa mwaka 2011 chini ya Mkataba wa Ubia kati ya Shirika la Maendeleo ya Taifa na Kampuni Mshirika. Ingawa hatua ya awali ya kutambua rasilimali ilikamilika ndani ya miezi 36 hadi mwaka 2014, hatua zilizofuata za uendelezaji wa mgodi na ujenzi wa kiwanda cha kuyeyusha madini ya chuma bado hazijakamilika kutokana na kuchelewa kwa majadiliano na changamoto za kisheria.

Licha ya mapendekezo yangu ya awali katika mwaka wa fedha 2020/21 kuhusu kuhakikisha utekelezaji wa mradi huu, hakuna maendeleo yaliyofanyika. Ingawa fidia kubwa imelipwa kwa watu waliothirika na mradi, bado kuna majadiliano kuhusu motisha za kampuni mshirika kama vile msamaha wa ushuru wa bidhaa, ushuru wa forodha, na kodi ya ongezeko la thamani kwa vifaa vya ujenzi wa Mradi, jambo linalochelewesha utekelezaji wa mradi.

Sheria ya Uwekezaji, Sura ya 38 ya mwaka 2002, inataka motisha hizi zichapishwe kwenye Gazeti la Serikali, jambo ambalo bado halijafanyika. Zaidi ya hayo, kati ya motisha 29 zilizopendekezwa, 19 zinakabiliwa na changamoto za utekelezaji kutokana na kukinzana kwa sheria za kitaifa, ikiwemo Sheria ya Fedha ya 2015 na Sheria ya Madini ya 2017, ambazo ziliwekwa ili kulinda rasilimali za taifa.

Ingawa tathmini ya athari za mazingira imefanyika na watu waliothirika wamelipwa fidia, kutokuwepo kwa makubaliano kati ya

Serikali na mwekezaji kumeufanya mradi kusimama. Matokeo yake, faida kubwa za kiuchumi, kama vile ajira na ukuaji wa viwanda, hazijapatikana.

Ucheleweshaji huu wa muda mrefu katika utekelezaji wa mradi umesababisha kupoteza fursa za ajira na kuzuia maendeleo ya viwanda nchini Tanzania. Mradi huu ulitarajiwa kuchochea ukuaji wa sekta zinazotegemea chuma, hivyo ucheleweshaji wake unaweza kuongeza gharama za utekelezaji na kupoteza fursa za kiuchumi.

**Ninapendekeza shirika la Maendeleo ya Taifa, kupitia Wizara ya Viwanda, liharakishe majadiliano na mwekezaji ili kufikia makubaliano ya mwisho, Lihakikishe utekelezaji wa mradi unafuata mifumo sahihi ya kisheria, na lifuatilie kwa karibu na kutatua changamoto za kisheria kwa wakati ili kuzuia ucheleweshaji zaidi na kufungua fursa zote za kiuchumi za mradi wa chuma Liganga.**

## 20.3 Kutotatuliwa kwa Mgogoro wa Umiliki wa Hisa katika Kampuni ya TANCOAL Energy na Kutokulipwa kwa Kodi ya Mauzo ya Hisa

Kampuni ya TANCOAL Energy inamilikiwa na kampuni mbili kwa ubia ambapo kampuni ya Intra Energy Tanzania Limited (IETL) inamiliki asilimia 70 na Shirika la Taifa la Maendeleo linamiliki asilimia 30. Kampuni ya Intra Energy Coorporation (IEC), ambayo ni kampuni mama ya IETL, iliuza hisa ilizokuwa inazimiliki IETL kwenye kampuni ya TANCOAL Energy, kwa Kampuni ya Uchimbaji ya Mirambo bila idhini ya Shirika la Taifa la Maendeleo kinyume na mkataba wa makubaliano ya umiliki kati ya kampuni ya IETL na NDC. Ili kupata ufumbuzi wa suala hili, Shirika la Taifa la Maendeleo na mshirika wake wa ubia (IETL) walikubaliana kupitia upya mkataba wa ubia huo, lakini mchakato huo umekumbwa na ucheleweshaji kwa sababu mshirika wa ubia hajaweza kusaini hati ya nyongeza (Addendum) tangu Julai 2023. IETL imeeleza kuwa haikuweza kusaini hati hiyo kwa sababu ilikuwa inatarajia kipengele kinachohusu Leseni za Utafiti kijumuishwe, kwani Tume ya Madini ilikataa kuzitoa leseni hizo kwa Kampuni ya TANCOAL Energy. Kwa mujibu wa Sheria ya Madini (Sura 123) na kanuni zake, muda wa juu kabisa wa kushikilia Leseni ya Utafiti ni miaka tisa (9), na baada ya muda huo, leseni hurudishwa serikalini. IETL iliorodhesha leseni hizo kuwa ni PL11156/2017, PL7391/11, PL8999/13, PL11086/2016, na PL13996/2019. Pia, IETL ilisisitiza kuwa kipengele hicho kiongezwe kwenye hati ya nyongeza kabla ya kuendelea na kusaini mkataba huo. Hali hii imesababisha ucheleweshaji wa mchakato wa utatuzi

wa mgogoro na kuathiri ufanisi wa uendeshaji wa Kampuni ya TANCOAL Energy.

Kampuni ya TANCOAL Energy imekuwa ikifanya vibaya kifedha na haijawahi kutengeneza faida tangu kuanzishwa kwake, hali ambayo imesababisha Serikali, kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo, kutopata mgao wa faida. Kufikia tarehe 30 Juni 2024, Kampuni ya TANCOAL Energy ilikuwa inadaiwa na Shirika jumla ya Shilingi bilioni 11.21 kama ada za usimamizi ambazo hazijalipwa, huku malipo ya mwisho yakifanyika Januari 2021, jambo ambalo limeendelea kudhoofisha hali ya kifedha ya Shirika.

kutokutekelezwa ipasavyo kwa mchakato wa uhamishaji wa hisa kumesababisha kutolipwa kwa Kodi ya mauzo ya Hisa (Capital Gains Tax) yanayotokana na makubaliano ya mauzo ya hisa yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 2. Mkataba huo ulieleza kuwa malipo yafanyike kwa awamu mbili sawa, ambapo malipo ya kwanza yalipokelewa na IEC mwaka 2021. Hata hivyo, kodi hiyo haijalipwa, jambo ambalo linahatarisha hali ya kisheria na kifedha ya Kampuni ya TANCOAL energy, huku IEC kushindwa kulipa kodi hiyo kukiwa kumesababisha upotevu wa mapato kwa Serikali. Changamoto hizi za kifedha na utawala zinatishia uendelevu wa ubia huu.

**Ninapendekeza Shirika la Taifa la Maendeleo lishirikiane na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda, na Biashara ili kuharakisha utatuzi wa mgogoro wa umiliki wa hisa na kuhakikisha ada za usimamizi zinazodaiwa zinalipwa. Pia, Shirika lifanye kazi kwa karibu na Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kubaini na kukusanya Kodi ya Ongezeko la Mtaji inayotokana na uhamishaji wa hisa. Kuimarisha mfumo wa utawala ndani ya Mkataba wa Ubia ili kuzuia migogoro ya aina hii kutokea siku zijazo.**

## 20.4 Utekelezaji wa Miradi Mitano bila Kufanya Upembuzi Yakinifu na Shirika La Madini la Taifa

Katika ukaguzi wa utekelezaji wa miradi, nilibaini kuwa Shirika la Madini la Taifa iliwekeza katika miradi mitano bila kufanya upembuzi yakinifu, kinyume na kifungu cha 2.2.1 na 3.1 cha Miongozo ya Uwekezaji ya Shirika ya mwaka 2020. Miradi hiyo muhimu ni pamoja na Mwanza Gold Refinery, Buckreef Gold Mine, STAMIGOLD Biharamulo Gold Mine, Mundarara Ruby Mines, na kiwanda cha kusafisha chumvi Lindi, ambavyo vilianza kazi bila kufanyiwa tathmini yakinifu (Rejea **Jedwali Na. 61).**

**Jedwali Na. 61: Miradi ambayo upembuzi yakinifu haukufanyika**

| Na. | Mradi | Mwaka kuanza |
|---|---|---|
| 1. | Mradi wa Kusafisha Dhahabu Mwanza | 2020 |
| 2. | Mgodi wa Dhahabu wa Buckreef | 2011 |
| 3. | Mgodi wa Dhahabu wa STAMIGOLD | 2014 |
| 4. | Migodi ya Ruby Mundarara | 2018 |
| 5. | Kiwanda Cha kusafisha Chumvi - Lindi | 2024 |

**Chanzo:** *Nyaraka za uwekezaji na mafaili ya miradi*

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa kutofanyika kwa upembuzi yakinifu kulisababishwa na usimamizi duni, jambo ambalo lilidhoofisha uwezo wa kutathmini uhalisia wa miradi na hatari zake. Bila kufanya tathmini sahihi, uwekezaji unaweza kushindwa kufikia matarajio, na hivyo kusababisha hasara za kifedha na matumizi yasiyo na ufanisi.

**Ninapendekeza Shirika la Madini la Taifa lifanye upembuzi yakinifu wa miradi inayoendelea ili kutathmini utendaji, kutambua changamoto zisizotarajiwa, na kutumia uzoefu uliopatikana kwa ajili ya uwekezaji wa miradi katika siku zijazo.**

## 20.5 Ucheleweshaji wa Kukamilika kwa Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Ngozi wa Megawati 30 Unaotekelezwa na Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania

Nishati ya umeme wa jotoardhi ni chanzo cha nishati kinachoweza kuzalisha umeme kwa kutumia joto kutoka ndani ya ardhi. Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania ina jukumu la kutafiti, kuchimba na kutumia rasilimali za jotoardhi kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na matumizi ya moja kwa moja. Kampuni inalenga kutoa huduma za kuaminika na bora za maendeleo ya nishati ya jotoardhi ili kusaidia dira ya maendeleo ya taifa.

Katika ukaguzi wangu wa ripoti ya maendeleo ya Mradi wa Ngozi, ripoti ya mkandarasi mshauri, na ziara ya moja kwa moja kwenye eneo la mradi nilibaini kuwa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania ilishindwa kukamilisha Mradi wa Ngozi kulingana na Mpango Mkakati wa Kampuni wa mwaka 2017 hadi 2042 na maelezo ya dhana ya Mradi wa Umeme wa Jotoardhi wa Ngozi. Mpango huo ulikuwa kuzalisha megawati 30 ifikapo mwaka 2023 kama sehemu ya uzalishaji wa jumla ya Megawati 200 ifikapo mwaka 2025, huku muda wa utekelezaji wa mradi ukiwa miaka saba kuanzia mwaka 2015 hadi 2022 na kukamilika kabisa kwa megawati 600 ifikapo mwaka 2042 kwa gharama inayokadiriwa kuwa dola za Marekani milioni 150. Hadi sasa, mradi wa Ngozi uko katika hatua ya uchimbaji

wa visima vidogo vya uchunguzi ili kuthibitisha uwepo wa rasilimali za jotoardhi.

Halikadhalika, nilibaini kuwa mradi huu umekuwa nyuma kwa miezi 27 hadi wakati wa ukaguzi wa tarehe 20 Machi 2024, na nyuma kwa miezi 37 kwa kukamilika kwa mkataba wa mkandarasi mshauri (nyongeza ya kwanza ya miezi 17 na nyongeza ya pili ya miezi 20). Hii ni sawa na asilimia 53.15 ya kazi iliyokamilika huku asilimia 47.85 ikiwa bado haijatekelezwa.

Uchelewashaji wa mradi umesababishwa na changamoto za ununuzi, ikiwa ni pamoja na waombaji kutokuwa na mwitikio na michakato ya zabuni iliyochukua muda mrefu. Matokeo ya ucheleweshaji huu yanaweza kuongeza gharama za mradi na kuathiri upatikanaji wa mchanganyiko wa nishati kwa wakati unaotarajiwa.

**Ninapendekeza kuwa Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi Tanzania itumie mbinu sahihi za ununuzi ili kuhakikisha ufanisi, uokoaji wa gharama, na tija. Pia ihakikishe utekelezaji wa uchimbaji, uendelezaji wa miundombinu, na ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme unafanyika kwa wakati ili kuepuka ucheleweshaji zaidi na ongezeko la gharama.**

## 20.6 Ufanisi Duni wa Uendeshaji wa Kampuni ya STAMIGOLD kutokana na Mitambo Kusimama Muda Mrefu

Sura ya 3 ya Mkakati wa Biashara wa kampuni ya STAMIGOLD wa mwaka 2022/23 hadi 2026/27 inasisitiza upatikanaji na matumizi ya vifaa kama vipimo muhimu vya ufanisi wa mitambo. Hata hivyo, katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2023/24 nilibaini kuwa mitambo muhimu ilisalia bila kufanya kazi kwa muda mrefu. Mzunguko wa usagaji mawe ulisimama kwa saa 4,843.47, Kinu cha kusagia mawe kilisimama kwa saa 1,846.77, Kifaa cha Kutenganisha chembechembe ndogo za dhahabu kutoka kwenye mchanga (Knelson Concentrator) ilisimama kwa saa 743.21, Hii ni sawa na asilimia 55, asilimia 21, na asilimia 8 ya muda wote unaohitajika wa uendeshaji kwa mwaka mzima (masaa 8,760 kwa kila kifaa).

Aidha, nilitembelea eneo la mgodi tarehe 15 Agosti 2024 na kuthibitisha kuwa kiwanda kilikuwa hakifanyi kazi kwa siku tatu mfululizo kutokana na ukosefu wa malighafi za uchakataji.

Matatizo ya mara kwa mara ya kusimama kwa mitambo kutokana na upungufu wa vipuri, hitilafu za umeme, na ukosefu wa mawe ya

madini kwa ajili ya uchakataji yameathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi wa uzalishaji, na kusababisha ucheleweshaji usiopangwa wa kiutendaji. Kusimama kwa mitambo kwa muda mrefu kunaongeza gharama zisizo badilika kuendana na uzalishaji kama vile mishahara na mafuta, na kuathiri utumiaji wa rasilimali na ufanisi wa gharama kwa ujumla.

**Ninapendekeza kampuni ya STAMIGOLD itekeleze mkakati madhubuti wa matengenezo ili kupunguza muda wa kusimama kwa mitambo usiopangwa na kuongeza ufanisi wa kiwanda**

## 20.7 Kiwango Kikubwa cha Sumu katika Mabaki ya Kiwanda cha Uchakataji cha Kampuni ya STAMIGOLD

Viwango vya Usimamizi wa Taasisi ya Kimataifa ya Kemikali ya Sianidi ya mwaka 2021 vinaweka kikomo cha mkusanyiko wa Sianidi kuwa chembechembe 50 kwa milioni kwa uchakataji na mabaki ya uchimbaji, na sehemu 1 kwa milioni (ppm) kwa maji yanayotiririshwa nje ili kuhakikisha usalama wa mazingira.

Wakati wa ziara yangu katika kiwanda cha Kampuni ya STAMIGOLD tarehe 15 Agosti 2024, nilibaini kuwa kiwanda hakifanyi mchakato wa kupunguza kemikali ya Sianaidi. Uchunguzi zaidi wa takwimu za hali ya hewa na mchakato wa uzalishaji kutoka kiwandani ulionesha kuwa viwango vya Sianidi vilikuwa juu kwa mwaka mzima, vikivuka mara kwa mara kikomo salama cha chembechembe 50 kwa milioni (ppm), huku kiwango cha wastani kikiwa chembechembe 87.5 kwa milioni (ppm). Hali hii imesababishwa na kutokufanya kazi kwa mfumo wa kupunguza sumu, jambo ambalo linaweza kusababisha uchafuzi wa mazingira na kuleta madhara kwa mifumo ya ikolojia ya eneo husika.

**Ninapendekeza, Kampuni ya STAMIGOLD itengeneze mfumo wa kupunguza sumu ya Sianidi, na ifanye ufatiliaji wa mara kwa mara wa viwango vya Sianidi ili kuhakikisha viwango vinakaa katika kiwango kinachokubalika kwa usalama wa mazingira.**

## 20.8 Utendaji Duni wa Mkandarasi katika Uendeshaji wa Migodi ya STAMIGOLD

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Kampuni ya STAMIGOLD iliingia mkataba na Mkandarasi  kwa ajili ya shughuli za uchimbaji madini kupitia mkataba Na. PA/125/SBM/2022-23 wa tarehe 21 Februari 2023. Mapitio yangu ya ripoti zote za kila robo mwaka za uchimbaji madini kwa mwaka wa fedha 2023/24 yalionesha muda mwingi wa kusimama kwa vifaa, ambapo tinganga halikufanya kazi kwa asilimia

55 ya muda, Mitambo ya kuchimbia haikupatikana kwa asilimia 64, na Greda halikupatikana kwa asilimia 63. Hali hii imeathiri malengo ya uendeshaji kwa mwaka 2023/24.

Pia, ziara ya ukaguzi niliyoifanya tarehe 15 Agosti 2024 katika mgodi ilibaini kuwa; kusitishwa kwa uzalishaji wa madini kwa siku nne kutokana na hitilafu za vifaa; Kiwanda kikiwa na gari moja la kuchimba lenye hitilafu; na Kuwepo kwa shughuli chache za udhibiti wa ubora na ulipuaji wa miamba.

Utendaji wa uchimbaji madini haukufikia malengo yaliyopangwa, ambapo, Uzalishaji wa madini ulikuwa chini kwa asilimia 44, Uhamishaji wa mabaki ya mgodi ulikuwa chini kwa asilimia 22, na Jumla ya uhamishaji wa malighafi ulikuwa chini kwa asilimia 24.

Hali hii imesababishwa na usimamizi duni wa mkataba, jambo ambalo linaweza kusababisha kupungua kwa uzalishaji, kutofikiwa kwa malengo, na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji. Taarifa zaidi zinaoneshwa katika **Jedwali Na. 62**.

**Jedwali Na. 62: Utendaji Duni wa Mkandarasi wa Uchimbaji Madini**

| Kigezo | Uhalisia | Lengo | Tofauti (Kiasi) | Tofauti (asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| Madini (tani) | 306,759 | 543,060 | 236,301 | 44 |
| Mabaki (tani) | 4,722,378 | 6,037,338 | 1,314,960 | 22 |
| Ubora wa madini (g/t) | 0.90 | 1.03 | 0.14 | 13 |
| Jumla ya wakia (oz) | 8,944 | 18,046 | 9,102 | 50 |
| **Jumla ya malighafi iliyohamishwa (tani)** | **5,029,136** | **6,580,399** | **1,551,263** | **24** |

**Chanzo**: *Uchambuzi wa mkaguzi kutoka ripoti za utendaji wa uchimbaji madini za kila robo mwaka 2023/24*

**Ninapendekeza kuwa Kampuni ya STAMIGOLD iimarishe usimamizi wa mkataba ili kupunguza muda wa kusimama kwa vifaa kwa kupitia matengenezo madhubuti na ukarabati wa haraka.**

## 20.9 Kutokuwepo kwa Sera ya Kitaifa ya Kufanikisha Uwekezaji wa Ndani Kwenye Teknolojia za Madini

Katika ukaguzi wangu katika utekelezaji wa Kanuni za ushirikishwaji wa wazawa za mwaka 2018, nilibaini kuwa Tume ya Madini bado haijatekeleza jukumu lake la kuandaa Sera ya Kitaifa ya Kufanikisha Uwekezaji wa Ndani Kwenye Teknolojia za Madini. Hili linaonesha

ukosefu wa juhudi za kuendeleza na kuchapisha sera hiyo, kinyume na matakwa ya Kanuni ya 25(1) na (2) za Kanuni za Madini (ushirikishwaji wa wazawa) za mwaka 2018.

Kushindwa kuanzisha sera hii kunaleta changamoto katika kufanikisha malengo ya ushirikishwaji wa wazawa kwa sababu husababisha ukosefu wa ufafanuzi na utatuzi wa matatizo, kutokuwepo kwa suluhisho madhubuti, na ukosefu wa miongozo rasmi ya utekelezaji.

**Ninapendekeza Tume ya Madini iongeze kasi ya uundaji na uchapishaji wa sera hiyo ili kuhakikisha uzingatiaji wa kanuni na kuimarisha uwekezaji wa ndani Kwenye Teknolojia za Madini**

## 20.10 Uwiano Usioridhisha wa Malipo ya Mishahara kati ya Wafanyakazi Wazawa na Wageni katika Sekta ya Madini

Kanuni ya Madini ya ushirikishwaji wa wazawa za mwaka 2018 zinazitaka kampuni kutoa kipaumbele kwa kuajiri watanzania wenye sifa zinazostahili na kuandaa mipango madhubuti ya ajira kwa wenyeji na malipo ya haki. Vilevile, Mkataba wa Shirika la Kazi Duniani Na. 100 unahakikisha usawa wa malipo kati ya wanaume na wanawake kwa kazi yenye thamani sawa, na hivyo kuhakikisha sera zisizo na ubaguzi katika mishahara. Tanzania, kama nchi iliyotia saini mkataba huu, inapaswa kutekeleza sera za malipo ya haki bila kujali utaifa au jinsia.

Uchambuzi wangu wa kampuni kubwa za madini nchini Tanzania, ikiwemo Bulyanhulu, Kampuni ya Uchimbaji Madini Geita (GGM), na Kampuni ya Makaa ya Mawe ya Ruvuma (Ruvuma Coal), umebaini tofauti kubwa ya mishahara kati ya wafanyakazi wazawa na wale wa nje, kinyume na matakwa ya kanuni hizi. Maelezo zaidi nimeainisha katika **Jedwali Na. 63**.

**Jedwali Na. 63: Asilimia ya Wafanyakazi wa Kitanzania dhidi ya Wageni katika Malipo ya Mishahara**

| Na | Jina la Kampuni | Asilimia ya Idadi ya wafanyakazi | | Asilimiaya malipo ya mshahara | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wafanyakazi wazawa | wafanyakazi wa kigeni | wafanyakazi wazawa | wafanyakazi wa kigeni |
| 1 | Bulyanhulu | 94 | 6 | 51 | 49 |
| 2 | GGM | 97 | 3 | 87 | 13 |
| 3 | Ruvuma Coal | 99 | 1 | 94 | 6 |

***Chanzo:*** *Taarifa za Uwezeshaji wa Wenyeji kutoka kwa Kampuni za Madini, 2023*

Takwimu zinaonesha kuwa licha ya wafanyakazi wa Kitanzania kuwa sehemu kubwa ya nguvu kazi katika kampuni hizi, mgawanyo wa mishahara unaonesha kuwa wafanyakazi wa kigeni wanapokea sehemu kubwa ya malipo ya jumla. Kwa mfano, Bulyanhulu, wafanyakazi wa kigeni ni asilimia 6 tu ya wafanyakazi wote lakini wanapokea asilimia 49 ya jumla ya malipo ya mishahara. Hii inaashiria pengo kubwa ambalo huenda linatokana na wafanyakazi wa kigeni kushikilia nafasi za juu za uongozi au kazi maalumu zinazolipwa vizuri.

Hali hii inasababishwa na ukosefu wa utekelezaji wa sera za usawa wa mishahara. Pengo hili la mishahara linaweza kuwa matokeo ya wafanyakazi wa kigeni kushikilia nafasi za kipekee au za uongozi, jambo linaloonesha upungufu wa mifumo ya kuhakikisha malipo ya haki kwa kazi zinazofanana.

Kutokuwepo kwa usawa huu kuna athari za kijamii na kiuchumi, kwani malipo ya chini kwa Watanzania yanapunguza uthabiti wao wa kifedha, uwezo wao wa kupata huduma muhimu, na ukuaji wao wa kitaaluma. Aidha, sehemu kubwa ya malipo ya mishahara kuelekezwa kwa wafanyakazi wa kigeni ni upotevu wa kiuchumi kwa nchi, kwani fedha hizi hazizunguki ndani ya jamii za watanzania.

**Ninapendekeza Tume ya Madini isimamie utekelezaji wa kanuni za ushirikishwaji wa wazawa kwa ufanisi, iandae miongozo ya usawa wa mishahara, na ifanye tathmini huru za kuhakikisha usawa wa malipo huku ikihamasisha uhamishaji wa ujuzi na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Kitanzania.**

### 20.11 Ukosefu wa Hatua Stahiki za Kukabili Mmomonyoko wa Udongo Kando ya Bomba la Gesi Asilia

Wakati wa ziara yangu na mapitio ya Taarifa ya eneo lililoathirika na Mmomonyoko wa Udongo katika Ulongoni B, Mto Msimbazi ya tarehe 2 Januari 2024, ilibainika kuwa Kampuni ya Gesi Tanzania haijachukua hatua za kutosha kushughulikia mmomonyoko mkubwa wa udongo kando ya njia ya bomba la gesi katika eneo la ulongoni Dar es Salaam tangu tarehe 27 Novemba 2023.

Hali hii ilisababisha sehemu ya bomba yenye urefu wa mita 80 (bomba la gesi la Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na SONGAS) kubaki wazi, kinyume na Kanuni ya 58 ya Kanuni za Petroli (Gesi Asilia) (Shughuli za Usafirishaji na Usambazaji) za mwaka 2018 ambazo zinahitaji bomba la gesi wakati wote kuwa chini ya ardhi

kati ya mita 0.8, 1.1 au 1.4 kutokana na sehemu bomba linapopita kama ilivyopitishwa na Shirika la Viwango Tanzania.

Mmomonyoko huu ulisababishwa na maji yanayotiririka kutokana kutoka bonde la mto Msimbazi kipindi cha mvua. Licha ya juhudi za awali kama mapitio ya makisio ya Gharama za ujenzi na michoro ya ujenzi, bado hakukuwa na makubaliano kati ya Kampuni ya Gesi Tanzania na SONGAS kuanza ukarabati. Kutochukua hatua za haraka kunaweka bomba katika hatari, kwani kukaa wazi kwa muda mrefu kunadhoofisha mifumo yake ya ulinzi.

**Ninapendekeza Kampuni ya Gesi Tanzania iweke kipaumbele katika kufanikisha makubaliano hayo na kuanza matengenezo mara moja. Kuchelewa matengenezo kunahatarisha usalama wa bomba la gesi la mafuta.**

## 20.12 Ukarabati Duni wa Vituo vya Kudhibiti  Kutu katika Bomba la Gesi

Mnamo tarehe 14 Septemba 2024 nilitembelea maeneo ya Ulongoni hadi Tegeta, Dar es Salaam kwa ajili ya ukaguzi wa bomba la gesi. Pia, nilipitia taarifa ya ukaguzi wa ndani kuhusu shughuli za uwendeshaj wa bomba la gesi kwa mwaka 2023/24 katik Kampuni ya Gesi Tanzania. Ukaguzi ulibaini upungufu mkubwa katika ukarabati wa vituo vya kudhibiti kutu katika bomba la gesi. Mapungufu yaliyobainishwa ni pamoja na kutokuwepo kwa vifuniko vy juu katika baadhi ya vituo, uwepo wa nyaya zilizokatika na vituo vilivyoshika kutu, hali iliyotoka na uharibufu wa makusudi na matumizi ya vifapande vya chuma vinavyoshika kutu kwa haraka.

Hali hii inadhoofisha mfumo wa kudhibiti kutu na kuongeza uwezekano wa bomba kuchakaa na kushindwa kufanya kazi ipasavyo. Menejimenti ya Kampuni ya Gesi Tanzania ilikiri kuwepo kwa mapungufu hayo. Hivyo Kampuni imeanzisha mradi chini ya zabuni Na. TR24/001/2024/2025/W/11 wa kurekebisha mapungu yaliyobainika, na wanatarajia kukamilisha mradi huo ifikapo mwezi Juni 2025. Hata hivyo, nilibaini kuwa Kampuni ya Gesi Tanzania haijaanza kutekeleza mradi huo.

**Ninapendekeza Kampuni ya Gesi Tanzania ichukue hatua ya kubadilisha vituo vya udhibiti kutu vilivyopo, na kutumia vifaa visivyoshika kutu ili kuongeza uimara wa bomba na kupunguza ukarabati wa mara kwa mara.**

## 20.13 Kutofanya Usafi Ndani ya Bomba la Gesi kwa Zaidi ya Miaka 10

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Kampuni ya Gesi Tanzania haijafanya usafi ndani ya bomba tangu bomba la gesi lilipoanza kufanya kazi mwaka 2015, kinyume na Kanuni ya 74(1) ya Kanuni za Petroli (Gesi Asilia) (Shughuli za Usafirishaji na Usambazaji) za mwaka 2018 ambayo inataka kuwa mmiliki wa leseni ahakikishe kuwa uso wa ndani wa bomba linalosafirisha kimiminika unalindwa dhidi ya kutu.

Kutofanya usafi kunazidisha hatari ya kutu kutokana na uchafu unaojikusanya, maji, na mabaki ndani ya bomba. Ingawa Kampuni ya Gesi Tanzania imepanga kuutekeleza usafi huo kati ya Aprili na Mei 2025, bado hakuna mpango wa matengenezo wa maalumu ulioainishwa.

Aidha, Kampuni ya Gesi Tanzania inategemea uchujaji wa vichungi (filter) pekee kwa ajili ya kugundua kutu, ambavyo havina uwezo wa kushughulikia mambo mengine muhimu kama vile mkusanyiko wa maji ndani ya bomba.

**Ninapendekeza Kampuni ya Gesi Tanzania ianzishe mpango madhubuti wa matengenezo na kutumia mbinu mbalimbali za udhibiti wa kutu ili kuimarisha uimara wa bomba.**

## 20.14 Upungufu katika Urekebishaji wa Mita za Usomaji wa Gesi

Kampuni ya Gesi haijafanya marekebisho sahihi ya mita za usomaji wa gesi, kinyume na Kanuni ya 38 (j) ya Kanuni za Petroli (Gesi Asilia) (Shughuli za Usafirishaji na Usambazaji) za mwaka 2018, inayohitaji mita za gesi kupimwa mara kwa mara ili kuhakikisha usahihi wake.

Kwa kawaida, mita za gesi zinapaswa kupimwa kila baada ya miezi sita hadi miaka mitano, kulingana na viwango vya vifaa na miongozo ya sekta.

Mapitio ya taarifa za utendaji za mwaka 2023/24 na vyeti vya upimaji yalionesha kuwa mita za gesi 16 zilizofungwa kati ya mwaka 2017 na 2019 hazijapimwa, huku zinapaswa kuwa zimepimwa. Mita hizi zipo katika maeneo ya viwanda na mitambo ya kuzalisha umeme.

Ukosefu wa usmimazi wa kuhakikisha mita za gesi zinapimwa kwa wakati kunathiri usahihi wa kiasi cha gesi kinacho sambazwa. Suala hili linaweza kuathiri ufanisi wa uendeshaji na ukosefu wa usahihi wa vipimo vya gesi.

**Ninapendekeza Kampuni ya Gesi ianzishe mpango ili kuhakikisha mita za gesi zinapimwa. Pia, ihakikishe inazingatia ratiba hiyo ili kufuata viwango vya sekta na kuboresha usahihi wa vipimo.**

## 20.15 Kasi Isiyoridhisha ya Uwekezaji katika Vituo vya Kujaza Gesi Asilia

Kati ya mwaka 2020 na Juni 2024, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania lilikubali maombi ya kampuni 35 za kuanzisha vituo vya kujaza Gesi Asilia. Hata hivyo, katika mapitio yangu, nilibaini kuwa ni vituo vitatu tu vilivyofanikiwa kuanzishwa, wakati kampuni nyingine 32 zilikutana na changamoto kama vile ucheleweshaji wa kupata vibali vya kisheria kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, kutokuwepo kwa uhakika kuhusu bei ya gesi kutokana na mabadiliko ya thamani ya sarafu, na ugumu katika kupata ardhi inayofaa.

Vilevile, upanuzi mdogo wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia umeleta changamoto katika kufikia maeneo mengi, hali inayozuia matumizi ya gesi kwa wingi. Kampuni hizo ziko katika mchakato wa kukamilisha Makubaliano ya uuzaji wa Gesi (GSA) au bado ziko kwenye hatua za ujenzi, wakati zingine zimepiga hatua ndogo au hazijafanikiwa tangu kupata kibali.

Utekelezaji wa kusuasua kwa vituo vya kujaza gesi asilia kunapunguza upatikanaji wa nishati hii nafuu kwa umma. Ucheleweshaji huu unazuia akiba kwa watumiaji na kupunguza fursa za kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika katika uagizaji wa mafuta kutoka nje, jambo linaloathiri vibaya uwiano wa malipo ya nje ya nchi. Zaidi ya hayo, kushindwa kwa Shirika kuharakisha uanzishwaji wa vituo vya CNG kunazuia maendeleo yanayotarajiwa katika sekta hii na mchango wake katika nishati mbadala.

**Ninapendekeza kuwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania lishirikiane na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ili kuharakisha mchakato wa utoaji vibali na kuanzisha miongozo ya bei ili kupunguza wasiwasi unaosababishwa na mabadiliko ya thamani ya sarafu. Zaidi ya hayo, menejimenti ya shirika inapaswa kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara wa kampuni zilizokubaliwa ili kutathmini maendeleo, kushughulikia vikwazo katika utekelezaji, na kuhakikisha upanuzi wa kutosha wa miundombinu ya gesi ili kusaidia upokeaji wa gesi kwa wingi.**

### 20.16 Kusuasua kwa Uanzishwaji wa Mfuko wa Fedha Zitakazotumika Kurejesha Mazingira ya Awali pindi Miradi ya Sekta ya Gesi Itakapofikia Ukomo

Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 inahitaji kuanzishwa wa Mfuko wa Fedha zitakazotumika kurejesha mazingira ya awali pindi Miradi ya Sekta ya gesi Iiakapofikia ukomo. Fedha za Mfuko huo zinapaswa kuhifadhiwa kupitia akaunti ya Escrow inayosimamiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Kampuni husika.

Katika ukaguzi wangu wa ripoti ya ukaguzi wa ndani ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli na kumbukumbu za kikao cha robo ya nne kwa mwaka wa kifedha 2023/24, kuhusu uwasilishaji wa Mpango kazi na bajeti ya Mwaka 2023/24, nilibaini kuwa dola za Marekani 705,000 kwa mwaka 2023 na dola za Marekani 200,000 kwa mwaka 2024 zilikuwa zimeidhinishwa kwa ajili hiyo kutoka kwa kampuni ya Maurel & Prom (M&P) kwa eneo la Mnazi Bay.

Licha ya idhini hii, fedha hizi hazikuwekwa kwenye Mfuko na kampuni husika kwani akaunti ya escrow inayohusika bado haijafunguliwa na pande husika (yaani Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli na kampuni husika). Ucheleweshaji huu ulisababishwa na kutoweka kipaumbele katika utekelezaji, jambo ambalo limekwamisha utekelezaji wa masharti ya kisheria.

Kutokuwepo kwa mfuko huo kunahatarisha utekelezaji wa shughuli za kurejesha mazingira ya awali kwa wakati, na huenda kukaongeza hatari za kifedha na mazingira. Niliona kuwa kwa sasa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli imeanzisha Kamati ya Mfuko kulingana na kifungu cha 188(8) cha Sheria ya Mafuta Sura ya 392, ambayo miongoni mwa majukumu yake, itasimamia na kuanzisha Mfuko huo kwa eneo la leseni ya Mnazi Bay.

**Ninapendekeza kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli iweke kipaumbele katika kuanzisha mfuko huu na kuimarisha uangalizi ili kuhakikisha kuwa waendeshaji wanachangia fedha zilizothibitishwa kama sheria inavyotaka.**

### 20.17 Tofauti ya Taarifa za Usomaji wa Mita za Gesi zaidi ya Kiwango Kinachokubalika cha Asilimia Moja na Shirika la Umeme Tanzania

Ukaguzi wangu katika Shirika la Umeme Tanzania ulibaini tofauti kubwa katika taarifa za usomaji wa mita za gesi ambazo zinavuka kiwango kinachokubalika cha asilimia 1 kama ilivyoainishwa katika

makubaliano ya udhibiti na kimkataba. Tofauti hizi, zilizobainika zinaashiria uwezekano wa kutokuwepo kwa usahihi katika mita za kupimia gesi. Baadhi ya matukio yalionesha mita kuu kusajili usomaji wa juu kuliko mita ya ukaguzi, ikiashiria uwezekano wa hitilafu katika mita hizo.

Aidha, baadhi ya vituo kama vile Mtwara II na Ubungo III havina mita za ukaguzi, hali inayofanya iwe vigumu kupima tofauti hizo kwa usahihi. Sababu kuu za changamoto hizi ni ukosefu wa upangaji wa marekebisho ya mara kwa mara na usimamizi duni wa kushughulikia tofauti hizo kama inavyotakiwa katika makubaliano.

**Jedwali Na. 64: Maelezo ya Tofauti Zilizozidi Kiwango Kinachokubalika cha asilimia 1**

| MWEZI | Taarifa za usomaji Mita | Taarifa za usomaji Mita za Ukaguzi | Tofauti ya usomaji wa mita | Asilimia ya utofauti |
|---|---|---|---|---|
| Somanga- Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania | | | | |
| **Julai,2023** | 246,365.73 | 234,649.00 | 11,716.73 | 5 |
| **Septemba,2023** | 268,677.53 | 260,332.00 | 8,345.53 | 3 |
| **Oktoba,2023** | 314,992.56 | 306,609.00 | 8,383.56 | 3 |
| **Novemba,2023** | 238,293.39 | 230,148.00 | 8,145.39 | 3 |
| **Desemba,2023** | 246,050.25 | 241,865.00 | 4,185.25 | 3 |
| **Januari,2024** | 243,945.75 | 217,982.00 | 25,963.75 | 11 |
| **Februari,2024** | 271,795.00 | 173,580.00 | 98,215.00 | 36 |
| **Machi,2024** | 298,547.00 | 53,886.00 | 244,661.00 | 82 |
| **Mei,2024** | 40,375.99 | 25,724.00 | 14,651.99 | 36 |
| **Juni,2024** | 235,851.75 | 229,706.00 | 6,145.75 | 3 |
| Kinyerezi I - Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania | | | | |
| **Januari, 2024** | 42,253,218.00 | 34,990,610.00 | 7,262,608.00 | 17 |
| Tegeta- PAET/ Shirika la Maendeleo la Petroli | | | | |
| **Julai,2023** | 5,470,716.41 | 5,377,490.00 | 93,226.41 | 2 |

**Chanzo***: Taarifai za Uzalishaji 2023/24*

Kutokuwepo kwa usahihi katika taarifa za usomaji wa mita kunahatarisha masuala ya kifedha, ikiwa ni pamoja na uwezekano wa malipo kupita kiasi katika ununuzi wa gesi.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania lifanye usulihishi wa taarifa za usomaji wa mita kila mwezi na wauzaji kwa tofauti zinazozidi kiwango kinachokubalika. Vilevile, marekebisho ya mita yanapaswa kufanyika mara kwa mara ili kuhakikisha upimaji sahihi. Aidha, Shirika linatakiwa lihakikishe uwekaji wa mita za ukaguzi katika maeneo yote muhimu, yakiwemo Mtwara II na Ubungo III ili kuimarisha ufuatiliaji na ulinganifu wa masharti ya mikataba na kanuni.**

### 20.18 Kuongezeka kwa Matumizi ya Gesi Kupita Kiwango Kinachokubalika katika Shirika la Umeme Tanzania

Uzalishaji wa umeme kwa kutumia mitambo ya gesi ni mojawapo ya vyanzo vikuu vya nishati katika gridi ya taifa. Gharama ya ununuzi wa gesi ni sehemu kubwa ya gharama za uendeshaji wa Shirika la Umeme Tanzania, ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/24, gharama hiyo ilifikia shilingi bilioni 763.54, sawa na asilimia 35 ya shilingi trilioni 2.15 ambazo ni gharama za uendeshaji kwa mwaka husika.

Tofauti inayokubalika ya matumizi ya gesi kwa kila kWh (MMBtu/kWh) inategemea aina ya injini ya gesi, hali ya uendeshaji, na viwango vya sekta. Kwa ujumla, kiwango kinachokubalika cha tofauti ya matumizi ya gesi ni kati ya Asilimia ±5 hadi asilimia ±10 ya matumizi ya kiwango rejea.

Ukaguzi wangu ulibaini ongezeko la matumizi ya gesi kupita kiwango kinachokubalika, jambo ambalo linaathiri gharama za uzalishaji wa umeme. Mapitio ya ripoti za uzalishaji za mwaka 2023/24 yalionesha upungufu wa ufanisi katika matumizi ya gesi kwenye mitambo mbalimbali, ambapo baadhi ya mitambo ilizidi kiwango cha matumizi ya msingi au kiwango rejea kwa zaidi ya asilimia 10 hadi 20. Ongezeko hili limechangiwa na mambo kama vile changamoto za matengenezo, na halijoto, ambapo vyote vinasababisha kupungua kwa ufanisi wa mitambo.

Kutokuwepo kwa tafiti za kina ili kubaini chanzo halisi cha tatizo, kama vile mabadiliko ya thamani ya kalori ya gesi na uchakavu wa injini, kumezidisha hali hii. Matokeo yake, matumizi makubwa ya gesi yamesababisha kuongezeka kwa gharama za uzalishaji, hivyo kuathiri utendaji wa kifedha kwa ujumla.

**Jedwali Na. 65: Asilimia ya Kuongezeka kwa Matumizi kutoka Kiwango rejea au msingi**

| Mwezi /mtambo | Ubungo 2 | Ubungo 3 | Kinyerezi 1 Upanuzi | Kinyerezi 2 | Ubungo 1 | Tegeta | Mtwarali Gasi | Somanga |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya kiwango rejea kilichoainishwa mmBTU/Kwh** | **0.0108** | **0.0095** | **0.0097** | **0.0073** | **0.0082** | **0.0078** | **0.0110** | **0.0113** |
| **Julai-23** | -2.12 | 13.6 | 2.7 | 17.3 | 10.9 | 11.5 | -9.8 | 0.3 |
| **Agosti-23** | -1.68 | 13.3 | 3.62 | 17.9 | 12 | 13.1 | -9.8 | 0.4 |
| **Septemba-23** | -1.6 | 12.3 | 2.1 | 19.3 | 10.9 | 11.0 | 9.1 | 2.7 |
| **Oktoba-23** | -1.3 | 17.8 | 1.9 | 18.5 | 10.8 | 13.3 | -5.7 | 0.7 |
| **Novemba-23** | -0.6 | 13.6 | 1.0 | 17.2 | 9.7 | 11.7 | -8.9 | --2.8 |
| **Disemba-23** | 0.2 | 13.9 | 1.6 | 20.1 | 9.8 | 13.4 | -8.6 | 1.7 |
| **Januari-24** | -0.3 | 16.5 | 0.8 | 17.2 | 10.5 | 14.1 | 7.4 | 1.9 |
| **Februari-24** | -0.4 | 13.2 | 0.6 | 21.6 | 10.6 | 13.9 | -8.6 | 3.1 |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Machi-24 | -5.7 | 10.1 | 1.9 | 19.3 | 11.0 | -42.2 | -7.4 | 0.8 |
| Aprili-24 | -1.4 | 15.2 | 2.7 | 17.8 | 9.7 | 13.2 | -2.1 | -12.3 |
| Mei-24 | -1.3 | 9.9 | 2.6 | 18.2 | 10.8 | -8.3 | -3.3 | 3.0 |
| Juni-24 | -1.4 | 18.0 | 3.3 | 18.8 | 11.2 | 5.1 | -4.1 | -7.6 |

**Chanzo:** *Ripoti ya matumizi ya mafuta 2023/24 na kiwango cha rejea*

Aidha nilibaini pia utofauti katika usomaji wa mita za gesi, ambapo tofauti hizo zimezidi kiwango kinachokubalika cha Asilimia 1 kama ilivyoainishwa kwenye mikataba na wasambazaji wa gesi. Ukaguzi wangu ulibaini mita za ukaguzi zilionesha thamani tofauti ikilinganishwa na mita kuu, huku baadhi ya tofauti zikifikia zaidi ya asilimia 80.

Aidha, baadhi ya maeneo hayakuwa na mita za ukaguzi, hali iliyozuia uthibitishaji wa tofauti hizo. Kutokuwepo kwa mita za kiuthibiti na kushindwa kushughulikia tofauti kwa wakati unaofaa kunazidisha hatari ya bili kubwa na malipo ya ziada yasiyo sahihi.

**Ninapendekeza Shirika la Umeme Tanzania lichukue hatua za haraka, ikiwa ni pamoja usuluhishi wa kila mwezi kati ya Shirika na wasambazaji, kuhakiki mita za gesi mara kwa mara, na kuweka mita za ukaguzi katika maeneo yote yanayokosa vifaa hivyo ili kuhakikisha usahihi wa ankara.**

**Kiambatisho Na. I: Hati za ukaguzi na mahitimisho ya uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake na sheria ya bajeti na kanuni zake kwa mwaka wa fedha 2023/24**

| Na. | Jina la shirika | Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya bajeti na kanuni zake |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kampuni ya Ndege Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 2. | Kituo cha Uwekezaji APC | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 3. | Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 4. | Chuo Kikuu Ardhi | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 5. | Jumuiya ya Wahitimu Chuo Kikuu Ardhi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 6. | Kampuni ya Ushauri Elekezi wa Mazingira Jengekwa ya Chuo Kikuu Ardhi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 7. | Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 8. | Chuo cha Ufundi Arusha | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 9. | Kampuni ya Uzalishaji na Ushauri Elekezi ya Chuo cha Ufundi Arusha | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 10. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 11. | Benki ya Azania | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 12. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 13. | Benki Kuu ya Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 14. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bariadi | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 15. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bukoba | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 16. | Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 17. | Bodi ya Korosho Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 18. | Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 19. | Chuo cha Diplomasia | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 20. | Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 21. | Chuo cha Elimu ya Biashara | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 22. | Bodi ya Usajili wa Makandarasi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |

| Na. | Jina la shirika | Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya bajeti na kanuni zake |
|---|---|---|---|---|
| 23. | Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 24. | Ofisi ya Hakimiliki Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 25. | Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Pamba | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 26. | Chuo cha Tekinolojia Dar es Salaam | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 27. | Kampuni ya Chuo cha Tekinolojia Dar es Salaam | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 28. | Chuo cha Ubaharia Dar es Salaam | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 29. | Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 30. | Kampuni ya Uchapishaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 31. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 32. | Bodi ya Bima ya Amana | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 33. | Taasisi ya Ushauri Elekezi ya Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 34. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 35. | Kampuni ya Ujenzi na Matengenezo ya Usafirishaji na Usambazaji wa Umeme | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 36. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 37. | Bodi ya Usajili wa Wahandisi | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 38. | Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 39. | Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 40. | Mfuko wa Faida | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 41. | Tume ya Ushindani | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 42. | Baraza la Ushindani | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 43. | Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 44. | Kampuni ya Gesi Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 45. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Geita | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 46. | Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 47. | Kampuni ya Nyumba na Mafao | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 48. | Chuo cha Uhasibu Arusha | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |

| Na. | Jina la shirika | Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya bajeti na kanuni zake |
|---|---|---|---|---|
| 49. | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 50. | Chuo cha Usimamizi wa Fedha | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 51. | Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 52. | Chuo cha Ustawi wa Jamii | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 53. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Iringa | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 54. | Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 55. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama - Shinyanga | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 56. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kahama | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 57. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 58. | Shirika la Masoko ya Kariakoo | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 59. | Kiwanda cha Dawa cha Keko | Yenye shaka | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 60. | Kituo cha Elimu Kibaha | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 61. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kigoma | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 62. | Kampuni ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 63. | Kampuni ya Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Kilimanjaro | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 64. | Kampuni ya Uzalishaji ya KMTC | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 65. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Kyela - Kasumulu | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 66. | Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 67. | Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 68. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 69. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Makambako | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 70. | Kitengo cha Usimamizi wa Hifadhi za Bahari | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 71. | Kampuni ya Huduma za Meli | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 72. | Mfuko wa Elimu na Mafunzo ya Bahari | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |

| Na. | Jina la shirika | Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya bajeti na kanuni zake |
|---|---|---|---|---|
| 73. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 74. | Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 75. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 76. | Kampuni ya MCB | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 77. | Bohari Kuu ya Dawa | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 78. | Kampuni ya Mkulazi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 79. | Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 80. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 81. | Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 82. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Moshi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 83. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 84. | Kampuni ya Miliki ya Msamvu | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 85. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 86. | Hospitali ya Taifa Muhimbili | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 87. | Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 88. | Taasisi ya Mifupa Muhimbili | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 89. | Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 90. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 91. | Taasisi ya Ushauri Elekezi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 92. | Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 93. | Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 94. | Kampuni ya Majengo ya Biashara ya Jiji la Mwanza | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 95. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 96. | Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori, Mweka | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 97. | Chuo Kikuu Mzumbe | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |

| Na. | Jina la shirika | Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya bajeti na kanuni zake |
|---|---|---|---|---|
| 98. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Namtumbo | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 99. | Baraza la Sanaa Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 100. | Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 101. | Ofisi ya Taifa ya Takwimu | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 102. | Baraza la Taifa la Ujenzi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 103. | Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 104. | Shirika la Taifa la Maendeleo | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 105. | Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 106. | Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 107. | Baraza la Mitihani la Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 108. | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 109. | Shirika la Nyumba la Taifa | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 110. | Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Dawa | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |
| 111. | Chuo cha Usafirishaji cha Taifa | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 112. | Shirika la Bima la Taifa | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 113. | Baraza la Kiswahili la Taifa | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 114. | Makumbusho ya Taifa la Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 115. | Kampuni ya Ranchi za Taifa | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 116. | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii kwa Sekta Binafsi | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 117. | Baraza la Michezo Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 118. | Chuo cha Sukari cha Taifa | Yenye shaka | Limekidhi | Limekidhi |
| 119. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Ngara | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 120. | Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 121. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Njombe | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 122. | Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Nzega | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
| 123. | Taasisi ya Saratani ya Ocean Road | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 124. | Chuo Kikuu Huria cha Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi na baadhi ya mapungufu | Limekidhi |

| Na. | Jina la shirika | Hati ya ukaguzi wa taarifa za kifedha | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya ununuzi na kanuni zake | Hitimisho kuhusu uzingatiaji wa sheria ya bajeti na kanuni zake |
|---|---|---|---|---|
| 125. | Tasisi ya Ushauri Elekezi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 126. | Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 127. | Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi Tanzania | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 128. | Kampuni ya Uwekezaji ya PPF na DCC | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 129. | Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni za Umma | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi |
| 130. | Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma | Inayoridhisha | Limekidhi | Limekidhi na baadhi ya mapungufu |
